# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

### Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 17 Mei, 2021

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya

Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea, Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Maswali tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Bryceson Magessa Tumaini Mbunge wa Busanda sasa aulize swali lake.

Na. 243

### Uhitaji wa Vituo vya Afya katika Jimbo la Busanda

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italipatia Jimbo la Busanda Vituo vya Afya hususan Tarafa ya Butundu na Tarafa ya Busanda?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Jimbo la Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Busanda katika Wilaya ya Geita lina Vituo vya Afya vitano ambapo vituo vya Afya vitatu vya Nyarugusu, Kashishi na Bukoli vipo katika Tarafa ya Busanda na Vituo vya Afya viwili vya Chikobe na Katoro vipo katika Tarafa ya Butundwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendelea kuboresha huduma za afya katika Wilaya ya Geita kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019 hadi 2019/2020 Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Geita shilingi bilioni 2.8 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Geita; shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Katoro na shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Nyarugusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu na shilingi milioni 500 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika Hospitali ya Wilaya ya Geita. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.9 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Geita na Hospitali ya Katoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri ya Wilaya ya Geita imetengewa shilingi milioni 200 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma manne ya zahanati, yakiwemo maboma ya Zahanati za Lubanda na Bujura katika Jimbo la Busanda. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ya Wilaya ya Geita imetengewa fedha shilingi milioni 375 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya Isulwabutundwe na shilingi milioni 375 kwa ajili kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya Butobela.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya huduma za afya katika Jimbo la Busanda, ikiwemo kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bryceson Magessa, swali la nyongeza.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, majibu haya yaliyotoka ni ya Wilaya ya Geita, nami maswali yangu yalikuwa yanaelekea Jimbo la Busanda. Kwa hiyo, nilipokee tu kwa sababu Jimbo la Busanda liko ndani ya Wilaya ya Geita, lakini mgawanyo wake inawezekana

Wilaya ya Geita usiwe ule ambao tunautarajia kuupata kule Busanda.

Swali langu la kwanza la nyongeza: Je, Serikali ina mpango gani; kwa sababu sasa hivi kuna ramani mpya ya vituo vya afya na vituo vingi vinavyotajwa vina ramani ya zamani ikionekana wazi kwamba kuna upungufu mkubwa wa wodi za wanaume na wodi za wanawake: Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya hivi vituo vya afya vijengwe kwa ramani hii mpya ya sasa? *(Makofi)*

Swali la pili; pamoja na vituo vilivyotajwa, kuna upungufu mkubwa sana wa uimarishaji wa upatikanaji wa dawa kwenye vituo hivyo: Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba vituo hivi sasa vinaweza kuwahudumia wananchi na upatikanaji wa dawa ukawa kama uliokuwa unapatikana awali; kwa sababu, kwa miaka miwili sasa wananchi wana vituo vya afya lakini hawapati dawa kwa ajili ya kuwahudumia? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Swali la kwanza Mheshimiwa Mbunge alilokuwa anahitaji kufahamu ni juu ya ramani ambazo zimekuwa zikitolewa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwenye ujenzi wa vituo vya afya kwamba, wakati mwingine haziendani na mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kikubwa ambacho naweza nikamwambia Mheshimiwa Mbunge, zile ramani zilizoletwa katika maeneo husika ni *minimum standards*. Maboresho yanaweza yakafanyika kulingana na maeneo husikwa. Kwa hiyo, endapo kutakuwa na hitaji fulani, watu wa eneo husika wanaweza kufanya maboresho pamoja ikiwemo kuijulisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI, nasi tutawapa ruhusa hiyo ili kuhakikisha hivyo vituo vinajengwa kulingana na mahitaji husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili amezungumzia kwamba, tumekuwa na vituo lakini bado mahitaji ya dawa hayapatikani vya kutosha. Jambo hili nafikiri karibu Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Jinsia, Wazee na Watoto tumekuwa tukilijadili hili kila wakati na tumekuwa tukilitolea ufafanuzi. Kikubwa, wote tunafahamu kwamba, mahitaji kama bima za afya, fedha ambazo wananchi wanatoa pale pale, lakini kwa hivi karibuni Serikali imeongeza bajeti kubwa kwenye madawa na usimamizi wake mzuri. Kwa hiyo, tutaendelea kuongeza dawa katika vituo vyetu na tutaongeza vile vile usimamizi ili ziweze kuwafikia walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii. Kwa kuwa, Mkoa wa Kilimanjaro asilimia 40 ni Wilaya ya Same; na kwa kuwa Wilaya ya Same ina majimbo mawili; na Wilaya nzima ina Hospitali ya Wilaya moja: Je, Serikali haioni kwamba lile eneo ni kubwa sana, sasa upande wa Mashariki nao wapate japo Hospitali ya Wilaya moja? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, sera yetu ya sasa ni kwamba kila Halmashauri ya Wilaya ipate hospitali yenye hadhi ya wilaya na ndio maana kwenye bajeti hata ya mwaka huu ambayo tumeipitisha mwaka 2021/2022 Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuhakikisha hata zile Halmashauri ambazo hazikuwa na hospitali za Halmashauri tutazijenga mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili alilolileta hapa ni wazo kwamba angalau jimbo kwa imbo

liweze kupata lakini tutaendelea kuzingatia kuleta huduma bora za afya katika maeneo yote ikiwemo kujenga vituo vya afya na zahanati kuhakikisha huduma zinawafikia walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lengo la kwanza ni kuhakikisha kwamba tunamaliza kwanza Halmashauri zote halafu maombi mengine tutakuja kuyazingatia kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sawa. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki.

Na. 244

**Serikali Kuunga Mkono Kushiriki katika Ujenzi wa Zahanati na Vituo vya Afya**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaunga mkono juhudi za wananchi katika ujenzi wa Zahanati na Vituo vya Afya Kata za Arumeru Mashariki.

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuunga mkono jitihada za wananchi katika Halmashauri zote nchini kwa kutoa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya

miundombinu ya afya kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Meru shilingi milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha maboma ya Zahanati za Ngabobo, Shishtoni na Mikungani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha maboma ya Zahanati za Ngejisosia, Imbaseni na Msitu wa Mbogo.

Vilevile katika mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri kupitia mapato yake ya ndani imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Maroroni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kushirikiana na wananchi kuboresha miundombinu ya afya ikiwemo maboma ya zahanati na vituo vya afya kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini bado niseme kwamba Arumeru Mashariki kuna shida nyingi sana hususan katika sekta ya afya. Wananchi wanahangaika sana kujijengea zahanati wenyewe, mimi mwenyewe tangu nianze harakati za kurudisha jimbo kwenye jengo, nimezunguka kwenye jimbo kushoto, kulia, kusini, magharibi, kaskazini kuhakikisha kwamba, wananchi wanajua kwamba tunahangaika nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana nami kwamba Wabunge hatupitwi na changizo lolote jimboni, kwa hiyo, kila zanahati inayojengwa kila kituo cha afya kinachojengwa Mbunge anahusika.

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali Mheshimiwa.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali, je, ni lini Serikali itaingilia kati ujenzi wa Zahanati iliyoko Katiti, Zahanati ya Kolila, Zahanati ya Zengon, Zahanati ya Majengo na sehemu nyingine nyingi jimboni. *(Makofi)*

Pili, je, Waziri yuko tayari kuambatana na mimi baada ya Kikao hiki cha Bajeti tukakague aone ninalolizungumza hapa kama ni la kweli au la? Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ambalo Mheshimiwa Mbunge amejaribu kulieleza ili Serikali iweze kutoa ufafanuzi, ni kwa namna gani Serikali inatoa mchango katika maeneo ambayo wananchi wamekuwa wakianzisha ujenzi, hususan wa maboma ya afya; na ameainisha baadhi ya maeneo ikiwemo Kikatiti, Kolila na maeneo mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwa kuzingatia hilo, ndiyo maana Serikali katika mwaka huu wa fedha tumeamua kutenga shilingi milioni 150 mpaka 200 kwenye kila jimbo ili kwenda kusaidia kumalizia zahanati ambazo zimeanzishwa na wananchi. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya hivyo kulingana na fedha tunazopata na tutaendelea kuzingatia mchango mkubwa ambao unatolewa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali dogo la pili la nyongeza lilikuwa, kama niko tayari kuongozana naye Mheshimiwa Mbunge; nimhakikishie, nipo tayari na nitaifanya hiyo kazi kwa uaminifu mkubwa. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa.

Na. 245

**Kuongeza Fedha TARURA - Ngorongoro**

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA (K.n.y. MHE. CATHERINE V. MAGIGE)** aliuliza:-

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka wa kuongeza bajeti ya *TARURA* Wilayani Ngorongoro ili kukabiliana na uharibifu wa barabara uliotokana na mvua kubwa zilizonyesha msimu wa mwaka 2019 na 2020?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto ya uharibifu wa miundombinu ya barabara inayotokana na mvua kubwa zilizonyesha msimu wa mwaka 2019 na 2020, Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro katika mwaka wa fedha 2019/2020, ulifanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 94.4, vivuko 15 na daraja moja kwa gharama ya shilingi bilioni 1.08. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2021, Serikali imeipatia *TARURA* Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro shilingi milioni 917.64 kati ya shilingi bilioni 1.05 zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 sambamba na matengenezo ya kawaida, Serikali iliipatia *TARURA* Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro shilingi milioni 276.68 kwa ajili ya matengenezo ya dharura katika

barabara zilizoharibiwa na mvua. Barabara zilizotengenezwa ni pamoja na kipande chenye urefu wa kilomita 1.2 na makalavati manne katika barabara ya Oldonyowas - Ormania mpaka Pipaya, ujenzi wa makalavati manne na madrifti matano katika barabara ya Mdito – Digodigo – Oldonyosambu na matengenezo ya kipande chenye urefu wa kilomita 1.5 na drifti moja katika barabara za Ormania mpaka Oldonyorock.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 shilingi bilioni 1.04 zimetengwa kwa ajili ya matengenenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 105, mifereji yenye urefu wa kilomita 1.1 na makalavati 30. Serikali itaendelea kuongeza fedha zinazotengwa kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya barabara kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza, lakini pia nitumie fursa hii kuishauri Serikali kwamba, kwa kuwa barabara zetu za vijijini haziachi kuharibiwa na mvua kila wakati, nashauri kila Wilaya ambayo haina mtambo wa kutengeneza barabara, wapewe mtambo ili kuweza kunusuru barabara hizi badala ya kungojea makandarasi wapatikane ndipo barabara zifanyiwe *repair*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza. Kuna mkandarasi anaitwa *Balcon Construction Tanzania Ltd*. ambaye amepewa *contract* ya shilingi 115,357,520/= kutengeneza barabara ya kwenda Kitongoji cha Esokonem mlimani Gelai kwenye Kata ya Gelailumbwa, ambaye ametelekeza barabara, baada ya kuiharibu barabara hiyo ambayo imetengenezwa kwa nguvu ya wananchi na kutifua mawe makubwa kiasi kwamba haipitiki tena. Tangu mwezi wa Kumi na Moja mwaka 2020 barabara hiyo imesimama,

haipitiki. Naomba Serikali iseme neno kuhusu hilo: Je. Serikali itamchukulia hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kuna barabara za mitaa ya Mji Mdogo wa Longido na ambazo zilikuwa ni sehemu ya ahadi ya Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, kutoka pale kwa *DC* kwenda Makao Makuu ya wakazi wa Halmashauri ya Longido, ambayo imejengwa kwa kiwango cha lami na tangu mwezi wa Kumi na Moja mwaka 2020 kazi imesimama kwa sababu mkandarasi hajalipwa *certificate* ambayo amewasilisha; je, Serikali itatimiza lini takwa lake la kumlipa mkandarasi huyo ili kazi imalizike? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID ERNEST SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge amejaribu kuitaka Serikali tueleze ni hatua gani tutachukua kwa Mkandarasi ambaye ameitelekeza barabara aliyoitaja iliyopo jimboni kwake. Kwa kuwa taarifa hizi ndio nazipata hapa, naomba niiagize *TARURA* Makao Makuu kwa kushirikiana na Mkoa wa Arusha waweze kutuletea taarifa haraka iwezekanavyo ili sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI tujue ni hatua gani tutachukua. Endapo itabainika kwamba Mkandarasi huyo ametelekeza barabara basi tutamnyang'anya hiyo *contract* na tutatangaza upya ili tupate mkandarasi mwingine atakayemalizia hiyo barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ahadi ambayo ilitolewa na Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli ya barabara kutoka *DC* kwenda Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Longido eneo hilo ambalo ametaja Mheshimiwa Mbunge, kazi hiyo imesimama na amesema sababu ya

kusimama ni yule Mkandarasi kutokulipwa fedha. Naomba hili nilifuatilie ili tuone ni hatua gani ambazo ofisi zetu zimekuwa zinachukua kwa sababu mpaka Mkandarasi labda hajalipwa maana yake kutakuwa labda wana-*process* zile *certificates* ambazo amekuwa amezileta katika Ofisi ya Rais TAMISEMI. Kwa hiyo naomba nilifuatilie ili tuweze kui-*fast truck* na kuirahisisha ili waweze kulipwa na hiyo barabara iweze kukamilika. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justine Nyamoga swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kata ya Udekwa, Kata ya Ukwega, Kata ya Kimara na Kata ya Idete hazina mawasiliano kabisa kutokana na mvua ambazo zimeharibu kabisa barabara.

Je, Serikali ipo tayari kutoa fedha za dharura kwa ajili ya barabara ya kata hizi ambazo zina mazao mengi ili ziweze kutengenezwa na wananchi waweze kuendelea na shughuli zao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Raism TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID ERNEST SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameomba fedha za dharura katika barabara ambazo ameziainisha hapa. Nimwambie tu moja ya kazi kubwa na nzuri ambayo imefanywa na *TARURA* katika kipindi hiki ni pamoja na kupeleka fedha za dharura katika maeneo yote ambayo yalikuwa yemeathirika sana na mvua kubwa ambazo zilikuwa zimenyesha. Pamoja na fedha ndogo ambayo tunayo kwa sababu katika fedha za dharura ambayo tunayo kwa mwaka huu ambayo unakwisha ni kama

bilioni 12 ambazo tulikwenda kuziainisha katika yale maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ameainisha maeneo hayo, niseme tu kabisa Ofisi ya Rais, TAMISEMI itapitia hayo maeneo na ione kama kuna udharura wa haraka kabisa ili tuweze kupeleka fedha na hizo barabara ziweze kupitika. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na swali la Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 246

**Mpango wa Kupambana na Uvuvi Haramu Nchini**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kupambana na tishio la uvuvi haramu nchini?

(b) Je, ni meli ngapi zilikamatwa nchini tokea mwaka 2015 - 2020 kwa kosa la uvuvi haramu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupambana na tishio la uvuvi haramu, Serikali imeandaa Mkakati wa Ulinzi na Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi ambapo katika mpango huo ushirikishwaji wa jamii katika kusimamia na kulinda rasilimali za uvuvi kupitia Halmashauri, Serikali za Vijiji

na Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi utaimarishwa. Aidha, kupitia mkakati huo, Serikali itaendelea kutoa elimu kuhusu athari za uvuvi haramu kwa mazingira, jamii na uchumi. Vilevile Serikali itaendelea kuimarisha Mashirikiano ya Kikanda na Kimataifa kwa kushirikiana na nchi mbalimbali zikiwemo Nchi za *SADC* katika kuzuia uvuvi haramu usioratibiwa na kuripotiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bahari Kuu, Serikali inao mfumo wa kufuatilia mienendo ya meli zote za uvuvi. Katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2015-2020, meli moja ya uvuvi haramu ilikamatwa Bahari Kuu na kufunguliwa mashtaka, ambapo Mahakama iliamuru mmiliki wa meli hiyo kulipa jumla ya shilingi bilioni moja au kufungwa jela miaka 20.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis swali la nyongeza.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yake mazuri kwenye swali langu la msingi. Sasa ningeomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Serikali ina mkakati wa kukuza uchumi wa bluu, je, Wizara yake ina mpango gani wa kutoa elimu ya teknolojia kwa wavuvi wa Bara na Visiwani ili kukuza uchumi wao na pato la Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa kuwa Serikali tayari imeagiza meli nane, nne Bara na nne Zanzibar. Je, Serikali au Wizara ina mpango gani wa kutoa elimu kwa maofisa hao watakaohudumia meli hizo pamoja na ajira kwa vijana ambao ajira sasa hivi ni ngumu na meli hizo zitasaidia? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa

Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, msimamo na mkakati wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ni juu ya kutumia vyema fursa ya uchumi wa bluu. Katika kutekeleza jambo hilo Serikali ya Awamu ya Sita imejipanga vyema kuhakikisha kwamba teknolojia ndiyo itakayotuongoza ili tuweze kutumia vyema rasilimali zilizopo katika bahari yetu lakini vilevile na maziwa makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, teknolojia hii ni pamoja na kuwasidia wavuvi waweze kutumia vifaa vya kisasa vitakavyowafikisha katika maeneo yenye samaki kwa urahisi na kwa kutumia gharama nafuu. Vifaa hivi, hivi sasa Wizara ipo katika mkakati wa kuhakikisha kwamba tunajipanga vyema watumie *GPS,* mvuvi anapotoka pwani anapokwenda baharini, awe tayari anazo taarifa za wapi samaki wanapatikana ili hiyo iweze kumsaidia kuweza kufanya *timing* ya muda, lakini vile vile hata mafuta atakayoyatumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili analotaka kujua ni juu ya mkakati wa Serikali kwenye kuutumia uchumi huu wa bluu kutoa elimu na ajira kwa vijana na akinamama. Serikali zote mbili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutambua umuhimu wa uchumi wa bluu, meli nane kama alivyotaja zitanunuliwa nne kwa upande wa Zanzibar na nne kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa kufanya hivyo Mashirika yetu makubwa mawili ya *ZAFICO* na *TAFICO* yanafufuliwa na yatanunua meli mbili kwa kuanzia katika mwaka wa fedha huu 2021/2022. *ZAFICO* kwa maana ya Zanzibar *Fisheries Corporation* itanunua meli mbili na *TAFICO* itanunua meli mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa zitapatikana ajira kwa vijana wa Kitanzania ambao pia watapewa elimu ya kuweza kujiandaa na fursa hiyo kubwa. Zaidi ya hapo tunao mpango wa maendeleo ya kilimo kwa maana *Agricultural Sector*

*Development Program* II itakwenda sambamba na kutengeneza na kuwaandaa vijana wetu ikiwa ni pamoja na shughuli nzima za ufugaji wa samaki katika maeneo ya bahari, tunaita kwa lugha la kitaalam *Mariculture*. Zaidi ya vijana 1,000 kule Zanzibar na akinamama zaidi ya 15,000 watanufaika na mradi huu wa *AFDP.* Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kutuunga mkono na wananchi wajipange vyema kuhakikisha tunatumia fursa hii ya uchumi wa bluu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Kunti Yussuf Majala, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 247

**Changamoto ya Maji – Mji wa Chemba**

**MHE. KUNTI Y. MAJALA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua changamoto kubwa ya maji inayowakabili wananchi wa Mji wa Chemba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer* Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kunti Yussuf Majala, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya huduma ya maji inayowakabili wananchi wa Mji wa Chemba ambapo kwa sasa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama ni chini ya asilimia 50. Katika kutatua changamoto ya huduma ya maji katika mji huo, Serikali ina mpango wa muda mfupi na mpango wa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika katika mpango wa muda mfupi, kazi zilizopangwa kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika mji huo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ni pamoja na ujenzi wa matanki mawili ya kukusanya maji ya ukubwa wa lita 50,000, nyumba ya mitambo ya kusukuma maji, ununuzi na ufungaji wa pampu nne (4), ununuzi na ulazaji wa mabomba ya umbali wa kilometa 11.6. Kukamilika kwa kazi hizo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka wastani wa lita 50,000 kwa siku hadi lita 320,000 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa mpango wa muda mrefu, Serikali ilipata mkopo kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya *Exim* India jumla ya Dola za Marekani millioni 500 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika miji 28 nchini ukiwemo Mji wa Chemba. Maeneo yatakayonufaika katika utekelezaji wa Mradi huo ni pamoja na Paranga, Makamala, Kambi ya Nyasa, Gwandi, Chambalo na Chemba yenyewe. Ujenzi unatarajiwa kuanza wakati wowote katika mwaka huu wa fedha 2020/2021 na umepangwa kutekelezwa kwa miezi 24.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; suala la mradi huu wa Dola za Kimarekani milioni 500 ni mradi ambao umekuwa wa kila siku tunaendelea kusimuliwa, kuandikiwa kwenye vitabu, lakini utekelezaji wake hauleti tija kwa Watanzania. Kama Waziri alivyosema kwamba mradi huu ndio ulitarajiwa kwenda kukidhi maji kwa wananchi wa Wilaya ya Chemba ukiwemo Mji wa Chemba. Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya visima viwili ambavyo vimechimbwa mwaka 2017 lakini mpaka leo visima vile havijafungwa *pump* wala miundombinu yoyote haijaweza kutekelezwa? Lini Serikali itatoa fedha ili kwenda kukamilisha huo mradi wa visima hivyo viwili ambavyo vimechimbwa mwaka 2017 na mpaka sasa ni miaka minne? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Wilaya ya Chemba tunatarajia kupata maji ya kutosha kutokana na mradi mkubwa wa Bwawa la Farkwa, lakini bwawa hilo si tu kwa Wilaya ya Chemba bali litasaidia pia kupunguza adha ya maji kwenye Jiji la Dodoma, Wilaya ya Bahi na Wilaya ya Chamwino. Natamani kusikia kauli ya Serikali, ni lini mradi huu utakwenda kuanza rasmi kwa sababu hata kwenye bajeti ya maji hakujatengwa fedha za kwenda kuanzisha huu mradi badala yake tunasubiri fedha za wafadhili. Kwa hiyo nataka nijue Serikali ni lini inaenda kuanza Mradi wa Farkwa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer* Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kunti Majala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipende kumpongeza Mheshimiwa Kunti, amekuwa ni mfuatiliaji mzuri pamoja na kwamba ni mjumbe katika Kamati yetu ya Maji, amekuwa na mchango mkubwa, lakini vilevile nipende pia kumpongeza kwa sababu ana mahusiano mazuri na Mbunge wa Jimbo, wamekuwa wakifuatilia kwa pamoja masuala haya. Sisi kama Wizara tumesema kwamba Chemba maji lazima yaje. Pamoja na kwamba kuna visima hivi viwili vilichimbwa mwaka 2017, lakini mwezi Machi, 2021 tumeongeza kuchimba visima vinne, ili visima vile vinne vya mwaka huu tunakuja sasa kutengeneza mtandao wa usambazaji maji kuelekea kwenye vituo vya uchotaji maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili anaongelea Bwawa la Farkwa. Hili bwawa ni juzi tu Mheshimiwa Waziri ametoka kuliongelea kama moja ya mikakati ya kuhakikisha maji Chemba yanafika. Pamoja na hilo tuna Mradi mkubwa wa Ziwa Victoria ambao pia Chemba utafika. Kwa hiyo bwawa hili litakwenda sambamba na mradi huu mkakati wa Ziwa Victoria. Tuendelea kuvuta subira, tumetoka mbali tunakokwenda ni karibu, maji Chemba yanakuja bombani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza niipongeza Wizara ya Maji kwa kazi wanayoifanya, lakini naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Kutokana na ongezeko la watu kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Makete, hasa hasa Makete Mjini tuna uhitaji mkubwa wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Mradi wa Maji wa kutoka Kitulo, Isapulano kwenda Iwawa Makete Mjini ili kuongeza upatikanaji wa maji kutokana na kwamba tayari kama halmashauri tulishawasilisha andiko letu la mradi wa bilioni 3.1 kwenye Wizara? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Festo Sanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli andiko hili tumeshalipokea pale Wizarani na mipango ya kuona namna gani ya utekelezaji itaweza kufanyika tayari pia tunashughulikia. Pia nipende kumpongeza sana Mheshimiwa Festo Sanga amekuwa ni mfualitiaji mzuri wa miradi hii yote, yeye mwenyewe amefuatilia na sasa hivi tumeshampelekea Mradi wa Maji wa Lupila milioni 100, lakini vile vile tumempelekea Mradi wa Maji wa Bulongwa milioni 100. Yote haya ni matunda ya yeye kuwasemea vyema wananchi wake. Hivyo sisi kama Wizara hatutakuwa kikwazo kwa Mheshimiwa Sanga na kwa wote anaowawakilisha, tutahakikisha na mradi huu wa bilioni 3.0 nao tunakuja katika utekelezaji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Keneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi, sasa aulize swali lake.

Na. 248

**Ujenzi wa Mabwawa ya Maji – Dodoma**

**MHE. KENETH E. NOLLO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga mabwawa makubwa ambayo yatahifadhi maji ya mvua ili yaweze kutumika kwa shughuli za kibinadamu, kilimo na mifugo katika Mkoa wa Dodoma ambao umekuwa haupati mvua za kutosha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Keneth Ernest Nollo, Mbunge wa Jimbo la Bahi, kama ifuatavyo:-

Mheshmiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuboresha huduma ya maji kwa wananchi wa Dodoma, katika mwaka 2020/2021, Serikali imekamilisha usanifu kwa ajili ya kukarabati Bwawa la Chikopelo lililopo umbali wa kilomita 70 kutoka Bahi Mjini ili kuongeza upatikanaji wa maji katika vijiji sita ikiwemo Mji wa Bahi na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la Kidoka litakalohudumia vijiji saba ikiwemo Mji wa Chemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati na ujenzi wa mabwawa hayo unatarajiwa kufanyika katika mwaka 2021/2022, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa malambo sita katika Vijiji vya Mpamwata, Uwekela, Kambia, Nyasa, Kolema Kuu, Kidoka na Palanga katika Wilaya za Bahi na Chemba.

Mheshmiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali ina mpango wa kujenga bwawa la kimkakati katika Kata ya Farkwa ambapo mpaka sasa usanifu umekamilika na ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaotakiwa kupisha eneo la mradi wa ujenzi wa bwawa hilo umefanyika kwa asilimia 99. Bwawa hilo lenye

mita za ujazo milioni 470 linatarajiwa kujengwa kwa awamu kutegemea na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Dodoma, Serikali imechimba visima visima nane na kukarabati visima vitatu vya zamani. Kazi ya ufungaji wa miundombinu inaendelea na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2021.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Keneth Nollo, swali la nyongeza.

**MHE. KENETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, swali langu la msingi ilikuwa ni kwamba Mkoa wa Dodoma unapata mvua kidogo lakini kumekuwa na upotevu mkubwa wa maji kipindi mvua inavyokuwa inanyesha.

Lengo la swali langu ni je, Serikali ina programu gani mahsusi, acha hii ya kudonoa donoa, programu mahsusi ya kuanza kukinga maji ambayo yanapotea kwa kiasi kikubwa kwa miaka nenda rudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; tunajenga reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza. Lakini, mradi huu ni mkubwa unapita kwenye mabonde na mito mingi. Je, Serikali kupitia Wizara ya Fedha, Kilimo na Wizara ya Ujenzi haioni kwamba tuongeze sehemu ya mradi ule kwa ajili sasa ya kuweka mabwawa na kutengeneza upatikanaji wa maji kwa ajili ya kilimo badala ya fedha nyingi zinajenga kwenye reli lakini mradi ule hauna *pact* ambayo ingeweza kusaidia kwenye Sekta ya Kilimo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mpango mahsusi wa Serikali kutumia maji ya mvua kama nilivyoelekeza, tuna mpango wa kuchimba mabwawa ambayo yataweza kuvuna yale maji na yatasambazwa kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ni kuhusiana na ujenzi wa reli ya kisasa. Pamoja na kwamba hii ni nje ya Wizara yangu nipende tu kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba reli hii ni ya thamani kubwa sana na ni ya manufaa makubwa kwa wananchi hivyo, kila suala lina mkakati wake na umuhimu wake. Masuala ya mabwawa kuongezwa, sisi kama Wizara ya Maji tutashughulikia. Licha ya kwamba mradi huo wa reli manufaa yake yataendelea kuzingatiwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda sana. Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Mbali na mkakati wa Serikali katika jibu lake la msingi la kuchimba mabwawa na marambo. Jimbo la Bunda Mjini limekuwa na changamoto sana ya ukarabati wa marambo.

Sasa ni lini Serikali mtatukarabati Rambo la Nyabehu, Kinyambwiga na Gushigwamara ili sasa wananchi wa maeneo hayo wapate huduma ya maji vile vile mifugo iweze kupata huduma ya maji. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa mabwawa na marambo kwa ajili ya mifugo, sisi kama Wizara tunaendelea kukarabati awamu kwa awamu kadri fedha inavyopatikana. Hivyo, pia kwa suala hili la Bunda Mjini, Bwawa la Nyabehu, Kinyambwiga pamoja na hilo lingine yote yapo katika mkakati wa Serikali kuona kwamba yanarudi katika hali bora. Hivyo, nipende kukupongeza Mheshimiwa Esther kwa kufuatilia na uongeze ushirikiano na Mbunge wa Jimbo ili mambo yakae sawa zaidi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Khatib Said Haji Mbunge wa

Konde swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa.

Na. 249

**Kukabiliana na Manabii na Waganga Matapeli**

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA K.n.y. MHE. KHATIB SAID HAJI** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kukabiliana na Waganga wapiga ramli chonganishi na Manabii wa uongo wanaodanganya na kutapeli wananchi kila siku?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khatibu Said Haji Mbunge wa Jimbo le Konde kutoka Mkoa wa Kaskazini Pemba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi ina jukumu la kulinda watu na mali zao na kuleta amani na utulivu miongoni mwa jamii ikiwa ni pamoja na kuzuia na kupambana na uhalifu wa aina yoyote ile ili usitokee. Katika kutekeleza majukumu hayo operesheni na misako ya mara kwa mara imekuwa ikifanyika katika kuwakamata waganga wapiga ramli chonganishi na manabii wa uongo wanaodanganya na kuwatapeli wananchi na kuwaletea hasara kubwa na mfarakano katika jamii kwa kuwachukulia hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2020 jumla ya wapiga ramli chonganishi 57 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani na kesi zao zipo katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nichukue fursa hii kuwatahadharisha wananchi kujiepusha na waganga wapiga ramli chonganishi na manabii wa uwongo kwani matendo yao husababisha hasara, mfarakano na vifo katika jamii. Pia tuendelee kujitokeza bila uoga kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi kuhusu vitendo hivyo viovu ili hatua stahiki zichukuliwe kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa swali la nyongeza.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Lakini, hata hivyo ningependa kujua kuna mfano gani kwa waganga hao wa ramli chonganishi na manabii wa uongo hatua ambazo wamechukuliwa baada ya kupatikana na kadhia hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, je, Serikali haioni sasa wakati umefika wa wale manabii ambao wanadai wanao uwezo wa kuwafufua waliokufa ili kukaa nao kwa karibu ili kuweza kuwafufua wapendwa wetu. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza je ni mfano gani wowote ambao uliowahi kuchukuliwa hatua wa hawa waganga matapeli na Manabii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Khalifa atarejea kwenye jibu langu la msingi ni kwamba mpaka kufika kipindi cha mwaka 2020 jumla ya kesi 57 za waganga chonganishi na wengine tayari zimesharipotiwa kwasababu ili kesi iwe kesi kwanza iwe *reported.* Kwa hiyo, kikubwa nimwambie kwamba zipo kesi ambazo zimeshafika kwenye ofisi yetu au zimeshafika Mahakamani, tayari zimo katika mchakato wa kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine nimwambie kwamba hili jambo ni jambo amablo linahitaji utulivu wa kukaa tukafanya utafiti na takwimu za kutosha ili tukilileta hapa tuliseme kwa mujibu wa uhalisia lilivyo. Kikubwa ni kwamba zipo kesi ambazo zimeshakuwa *reported.* Kuna kesi ilijitokeza Mkoa wa Njombe, yupo kijana aliambiwa na babu yake ili uwe Tajiri na huo utajiri tupate mimi na wewe basi lazima uwe unawaua watoto mpaka wafike idadi fulani. Mwisho wa siku ile kesi ikaripotiwa na tukamshtaki huyo mtu kwa kosa la mauaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kesi imejitokeza Misungwi huko ya mtu mmoja aliambiwa na mganga hivyo hivyo tapeli ili mimi na wewe tuwe matajiri hakikisha unawaua wanawake halafu unatembea nao. Lengo na madhumuni tuwe matajiri. Hii kesi imeletwa na tumeichukulia hatua kwa hivyo. Kikubwa niseme kwamba hizi kesi zipo kwa zile ambazo zimeripotiwa na hatua za kisheria kwa mujibu wa taratibu zinachukuliwa na majibu yatapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali jingine lilikuwa linauliza je, hakuna haja ya kukaa sasa na hawa wafufuaji ili tuweze kuwafufua wapendwa wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, imani ya kibinadamu inaamini na ndivyo ilivyo kwamba mwenye uwezo wa kuondosha na kurejesha, yaani kufanya mtu akaondoka, akafa ni Mwenyezi Mungu peke yake. Ndiyo maana ilifika wakati tukawa tunasema kwamba kama kutakuwa kuna watu wa namna hii kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge, tuko tayari kukaa nao tuwaeleweshe, tuwafahamishe ili wafike wakati wasije wakazua migogoro katika jamii. Kwasababu anaweza akatokezea mtu akasema mimi nina uwezo wa kufufua, akachukua pesa za watu. Mwisho mtu akazikwa akafa akasahauliwa. Mwisho wa siku migogoro katika jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa nimwambie tuko tayari kukaa na hao watu ili tujue namna ya kuwaelimisha kuwaeleza kwamba mwenye uwezo wa kufufua na

kuondosha mtu kwa maana ya kufa ni Mwenyezi Mungu *Subhana Wataalah.* Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tujitahidi kujizuia hasa kujadili mambo ya imani. Yanaleta changamoto kwasababu wako watu wanaamini akiumwa akiombewa anapona. Na nchi hii ina uhuru wa kuabudu. Nchi haina dini lakini watu wanao uhuru wa kuamini.

Nadhani hoja ya msingi ilikuwa kwenye, kwasababu hata vitabu vya dini vinasema wako Manabii wa uongo. Sina uhakika kama Serikali mnao uwezo wa kuwatambua wapi ni wa uongo, wapi ni wa ukweli. Sina hakika na hilo kwamba mtaweza sasa kuwatafuta. Wapiga ramli, sawa ni suala lingine. Lakini mambo ya imani yataleta changamoto kidogo tukiliweka kwa namna ambayo humu ndani tunataka kuliweka. Wale wananchi ambao wana imani yao huko basi pengine kuna watu wao waliofufuliwa, mimi sijui! Hamna ndugu yangu aliyefufuliwa lakini huenda wapo na nisingependa Bunge letu lifike mahali ambapo tunataka kuanza kujadili imani za watu humu ndani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 250

**Ukosefu wa Huduma za Kipolisi Maeneo ya Pembezoni**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza:-

Je, serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya huduma ya kipolisi katika maeneo ya pembezoni mwa miji ikiwemo na mkoa wa Dar es Salaam?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga Mbunge Wa Viti Maalum kutoka mkoa wa Dar es Salaam, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi inatekeleza mpango wa Askari Polisi kata /shehia katika kata zote 3956 na shehia 335 za Tanzania, ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2021 jumla ya askari 3963 wameshapangwa kwenye kata/shehia zikiwemo kata zilizopo pembezoni mwa Mkoa wa Dar es Salaam na maeneo mengine kwa lengo la kutoa huduma za kipolisi pembezoni kuliko na idadi kubwa ya watu na huduma ya vituo vya polisi ipo mbali, lengo ni kushirikiana na wananchi katika ulinzi na kupunguza uhalifu katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa baadhi ya maeneo huduma za polisi ziko mbali, Jeshi la Polisi kupitia mpango wa askari kata limekuwa likishirikiana na walinzi wa jadi ikiwemo sungusungu ili kupambana na kutatua uhalifu huo. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga swali la nyongeza.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Pamoja na majibu hayo, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa usalama ni jambo muhimu sana kwenye jamii yetu, je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia magofu ambayo yamejengwa na wananchi hususan maeneo ya pembezoni mwa miji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kutokana na changamoto ya kiusalama hasa maeneo ya pembezoni mwa miji je, Serikali imeandaa utaratibu gani au ina mpango gani wa kupeleka magari ya doria hasa nyakati za usiku kwenye maeneo ambayo hayana vituo vya polisi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza sasa maboma?

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa kazi kubwa ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inawapelekea wananchi huduma ya ulinzi na usalama karibu ya maeneo yao. Hiyo ni sehemu ya wajibu kabisa. Lakini na wananchi nao wanafika wakati wanakuwa wanao wajibu kwa kushirikiana na viongozi mbalimbali kusaidia sasa kuona namna ambavyo nao wanajisaidia kujikaribishia hizo huduma kwa kushirikiana na Serikali. Kikubwa tu nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge. Tutajitahidi katika bajeti ijayo tutakapopanga mipango yetu basi tutajitahidi katika maeneo haya ya pembezoni hasa katika mkoa huu basi baadhi ya maeneo hayo tuyape kipaumbele ili tuone namna bora ambayo wananchi wanaweza wakafikishiwa hizo huduma kama ambavyo maeneo mengine yanafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini je, kutokana na changamoto hii Serikali sasa ina mpango gani katika kupeleka magari haya kwa ajili ya kufanya doria. Mpango upo, kama ambavyo tumefanya katika mikoa na wilaya na vituo vingine na maeneo mengine na hapa katika maeneo hayo ambayo Mheshimiwa ameyakusudia au ameyataja tunao mpango wa kupeleka magari hayo kufanya doria ili sasa wananchi na wao waweze kupata huduma hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa ambacho tumekifanya huko, tayari tuna mfumo au tuna utaratibu wa ulinzi shirikishi ambao askari polisi/Jeshi la Polisi wanashirikiana na raia/ jamii katika kuhakikisha kwamba maeneo ya wananchi yanapata huduma ya ulinzi kama maeneo mengine. Kikubwa nimwambie Mheshimiwa asiwe na wasiwasi, atulie awe na Subira. Mambo mazuri yanakuja maana kazi inaendelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Wilaya ya Ngara ina changamoto ya uhaba wa askari na Wilaya hii inapakana na nchi jirani za Rwanda na Burundi. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka askari wakutosha ili wananchi waweze kulindwa na mali zao? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, tuna mpango gani sasa wa kupeleka askari ama ulinzi katika maeneo ambayo ameyataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, narejea tena kusema kwamba wajibu na jukumu la Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kupitia Jeshi la Polisi ni kuhakikisha kwamba maeneo yote yanapata huduma ya ulinzi na usalama ili wananchi waishi kwa amani. Ikiwa pana watu wageni, ndani ya Tanzania hii lakini wajibu wetu ni kupeleka. Nimtoe hofu, asiwe na wasiwasi, maeneo hayo kwa kuwa amehisi kwamba yana upungufu wa ulinzi, tunayachukua na tunapeleka ulinzi ili wananchi na wao waweze kuishi kwa amani na wapate huduma za ulinzi na usalama. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tuelekee Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Augustine Vuma Holle, Mbunge wa Kasulu Vijijini sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

Na. 251

**Ujenzi wa Barabara ya Kasulu - Uvinza**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE K.n.y. MHE. VUMA A. HOLLE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Kasulu - Uvinza kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Eng. Msongwe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Vuma Holle, Mbunge wa Kasulu Vijijini kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza ujenzi wa barabara ya Kasulu – Uvinza yenye urefu wa kilometa 65.9 kwa kiwango cha lami ambapo kilometa 8.9 kutoka Kasulu njiapanda ya Kanyani ni sehemu ya mradi wa barabara ya Kidakhawe – Kasulu yenye urefu wa kilometa 63 ambayo ujenzi wake kwa kiwango la lami umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, wakati Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa sehemu ya njia panda ya Kanyani hadi Uvinza, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali kila mwaka ili iweze kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 barabara hii imetengewa jumla ya shilingi milioni 1,887.9 kwa ajili ya matengenezo mbalimbali. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kipande cha barabara ya kutoka Uvinza hadi Malagarasi, kilometa 48, Serikali iliahidi kukijenga kwa msaada wa pesa za Falme za Kiarabu. Tangu mwaka juzi, 2019 Serikali imekuwa ikisema kwamba kipande

hicho kitajengwa kwa pesa hizo za msaada wa Falme za Kiarabu:-

Je, ni lini sasa Serikali itajenga kipande hicho cha kutoka Uvinza hadi Malagarasi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Malagarasi hadi Uvinza yenye urefu wa takribani kilometa 53 ni kati ya barabara kuu ambayo inaunganisha Mkoa wa Kigoma na Tabora. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hiyo fedha ipo na muda wowote, hata kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha huu, itatangazwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami ili sasa tuweze kukamilisha barabara kwa kiwango cha lami kutoka Kigoma – Malagarasi – Kaliuwa – Urambo – Tabora hadi Dodoma. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Robert Maboto, swali la nyongeza.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Halmashauri ya Mji wa Bunda ni makutano kati ya barabara itokayo Ukerewe – Mwanza – Simiyu kwenda Sirari – Tarime – Musoma kuja Mwanza na Serengeti kuja Mwanza:-

Je, ni lini Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi itaweka taa za barabarani za kuongoza magari ili kupunguza ajali zinazotokea eneo hilo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, kwa sasa barabara zote zinazojengwa na

zinazopita kwenye miji, katika mikataba lazima watengeneze barabara katika miji. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mpango upo sasa wa *TANROADS* kuhakikisha kwamba sehemu zote za miji ambazo zilikuwa hazina barabara za kuongozea magari kama alivyosema, wafanye usanifu ili tupate gharama yake na tuweze kuweka taa za kuongozea magari, hasa maeneo ambayo yana magari mengi. Kwa hiyo, *study* hiyo inaendelea. Naamini Bunda itakuwa ni sehemu ya wanufaika. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, swali la nyongeza.

**MHE. ANTHONY P. MAVUNDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ubovu wa Barabara ya Ihumwa – Hombolo unaleta adha kubwa kwa wananchi wa Chahwa, Ipala na Hombolo yenyewe na hivyo kuongeza gharama za usafiri: Je, ni lini sasa Serikali itakuwa tayari kutekeleza mpango wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kuanzia Ihumwa mpaka Hombolo ili kuwaondolea adha wananchi hawa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Eng.* Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni azma ya Serikali kujenga barabara zote kwa kiwango cha lami, lakini suala hili linafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Barabara ya Ihumwa – Hombolo hadi Mayamaya yenye urefu wa takribani kama kilometa 7.3 ni ya kiwango cha changarawe na kama fedha itapatikana, itajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba muda wote inapitika ili wananchi wa eneo hilo ikiwa ni pamoja na wanafunzi na wafanyakazi wa Chuo cha Hombolo wasiweze kupata taabu. Kwa hiyo, tumetenga fedha kwa matengenezo ya muda na

kuhakikisha kwamba maeneo yote yale korofi yanatengenezwa ili kusiwe na changamoto ya usafiri na usafirishaji kwa barabara hiyo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabungem tumalizie swali la mwisho. Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, sasa aulize swali lake.

Na. 252

**Fidia kwa Wananchi wa Eneo la Idofi**

**MHE. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Je, ni lini Wananchi wa Idofi watalipwa fidia baada ya maeneo yao kuchukuliwa na Serikali kwa ajili ya kujenga Mradi wa Idofi One Stop Centre?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza miradi ya ujenzi wa vituo vya pamoja vya ukaguzi wa magari ya mizigo *(One Stop Inspection Station)* katika shoroba mbalimbali za barabara nchini, ikiwemo ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi Makambako katika eneo la Idofi.

Lengo la ujenzi wa vituo hivyo ni kupunguza vikwazo visivyo vya kiforodha kwa wasafirishaji wa nchi za *SADC* na *EAC* wanaotumia barabara zetu. Vituo hivyo vitakapokamilika vitakuwa na Ofisi ya Polisi, *TRA*, Afya, Uhamiaji na Vituo vya Mizani katika eneo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kituo cha Makambako hadi kufikia Aprili, 2021 jumla ya shilingi 870,182,049 zimelipwa kwa wananchi 39 kati ya 275 wanaopisha ujenzi wa mradi huo. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta jumla ya shilingi 3,758,635,767 ili kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi 236 waliosalia. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa wananchi wale wamesubiri kulipwa fidia kwa muda mrefu; na kwa kuwa, hawawezi kuendeleza kufanya shughuli yoyote katika maeneo yaliyozuiliwa, wanapata shida katika nyumba zao, hawawezi kuongeza kitu: Je, sasa Serikali imejipangaje; ni lini itawalipa fedha zilizobakia ili waweze kupisha ujenzi wa mradi huu wa *One Stop Centre? (Makofi)*

Swali la pili; kwa sababu fedha za kujenga mradi huu zilishatengwa na zipo; nilipofuatilia fedha hizi zipo: sasa ni lini mradi huu ambao una manufaa makubwa kwa wananchi wa Makambako utaanza kujengwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia fidia kwa wananchi wake wa Jimbo lake la Makambako.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mradi huu una maslahi makubwa na mapana kwa nchi yetu na kwa uchumi wa nchi yetu hasa kwa wasafirishaji upande wa *SADC* na *East Africa Community,* hata hivyo, fedha hizi ni za *World Bank.* Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imelipa uzito, litafanyiwa kazi mapema iwezekanavyo tulipe fidia kwa

wananchi hawa ili wapishe kazi ya ujenzi ifanyike na huduma ya uchukuzi iweze kuboreshwa katika Wizara yetu ya Ujenzi na Uchukuzi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa maswali kutoka kwa Wabunge, lakini pia majibu kutoka kwa Serikali. Nitaleta kwenu matangazo tuliyonayo kwa siku ya leo.

Tutaanza na tangazo linalohusu Kukaimu Nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni. Kama mnavyomwona Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi amekaa ile sehemu kuashiria kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hayupo Bungeni, naye ndiye atakayekuwa anakaimu hiyo nafasi mpaka Mheshimiwa Waziri Mkuu atakaporejea Bungeni. Kwa hiyo, atakuwa anakaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni mbalimbali ambao wako Bungeni siku ya leo:-

Kwanza ni wageni watatu wa Mheshimiwa Spika ambao ni Wabunge kutoka nchini Zimbabwe, hawa ni Mheshimiwa Pupurai Togarepi, karibu sana. Yupo pia Ndugu Evance Gorogodo, karibu sana. Yupo pia Ndugu Theresia Msendo, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ni wageni wa Mheshimiwa Spika kutoka Zimbabwe na tutaonana nao hapo baadaye. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Mhandisi Dkt. Leonard Chamuriho ambaye ni Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi. Hawa ni Mhandisi Joseph Malongo ambaye ni Katibu Mkuu, Ujenzi, karibu sana. Tunaye pia Ndugu Gabriel Migire ambaye ni Katibu Mkuu, Uchukuzi, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Mhandisi Aron Kisaka ambaye ni Mkurugenzi wa Huduma za Uchukuzi, karibu sana. Tunaye pia

Mhandisi Patrick Mfugale ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS),* karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, makofi hayo kwa Mhandisi Mfugale yanaashiria mambo mawili; moja, ni matumaini katika hii bajeti itakayosomwa leo, lakini la pili, ni kazi nzuri anayoifanya. Kwa hiyo, tunakushukuru sana Mhandisi Mfugale. Pia yuko Ndugu Erick Hamissi ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA),* karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri bado anao wageni wengine ambao ni Mwenyekiti wa Bodi ya *TMA;* Dkt. Buruhani Nyenzi, karibu sana. Yupo pia Mtendaji Mkuu wa *TEMESA,* Mhandisi Japhet Maselle, karibu sana. Yupo pia Mtendaji Mkuu wa *TBA, Architect* David Kandolo, karibu sana. Wapo pia watendaji watano kutoka Kanisa Kuu la Roho Mtakatifu Anglikana Dodoma Dayosisi ya *Central Tanganyika* wakiongozwa na Mchungaji Kiongozi Kenneth Sabdean, karibuni sana. Ugeni wa Mheshimiwa Waziri huo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge. Wageni 35 wa Waheshimiwa Wabunge wafuatao: Mheshimiwa William Ole-Nasha ambaye ni Naibu Waziri Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, Mheshimiwa Daniel Awack, Mheshimiwa Noah Lemburis, ambao ni wana-*Club* ya Sekretarieti ya Utumishi wa Umma kutoka Chuo cha Mipango cha Jijini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Yakin Lingato. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 33 wa Mwenyekiti wa Tawi la Simba Bunge Mheshimiwa Rashid Shangazi. Wageni hawa ni wa Mheshimiwa Shangazi pamoja na Waheshimiwa Wabunge wapenzi wa *Simba Sports Club* ambao ni msafara wa timu ya Simba ya Wanawake *(Simba Queens)* wakiongozwa na Mjumbe wa Bodi, Ndugu Asha Baraka. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hamjamaliza makofi hayo, timu hii ni mabingwa wa soka la wanawake nchini kwa miaka miwili mfululizo. Jana wamewafunga timu ya wanawake ya Baobao ya hapa Dodoma goli moja kwa sifuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimemwona Mheshimiwa Tarimba alikuwa anapiga makofi, lakini naona Wabunge wengine hasa wapenzi wa Yanga wanaonesha kwamba *Kaiza Chiefs* iliifunga Simba magoli manne; lakini sasa Waheshimiwa Wabunge... *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kweli wamefungwa hao! *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuwe tunakumbuka fadhila kwa sababu, pamoja na hayo Yanga wanapelekwa kwenda kucheza huko nje kwa sababu ya Simba kufanya vizuri. Kwa hiyo, sisi Wana-Yanga tungekuwa tunawapongeza Simba na tunawaombea heri kwa sababu ndio wanaotufanya tupande ndege kwenda nje ya nchi. Naamini hilo na Mheshimiwa Tarimba anakubaliananalo kabisa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wageni sita kutoka Jukwaa la Ndoto Ajira ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake wakiongozwa na Mratibu Ndugu Edward Msumo. Karibuni sana vijana wetu mjifunze namna Bunge linavyofanya kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge na hili ni tangazo la upimaji.

Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, tangazo la muhimu sana hili. Waheshimiwa Wabunge tusikilizane!

Kuna tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge ambalo linahusu zoezi la upimaji na ushauri wa afya linaloratibiwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Kutakuwa na zoezi la upimaji

na ushauri wa afya litakaloratibiwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa Waheshimiwa Wabunge, Watumishi na familia zao kuanzia leo tarehe 17/05/2021 mpaka tarehe 29/05/2021.

Huduma zitakazotolewa ni kama ifuatavyo:-

(i) Upimaji wa magonjwa ya ndani;
(ii) Upimaji wa magonjwa ya mfumo wa upumuaji;
(iii) Uchunguzi wa magonjwa ya mifupa na ajali; na
(iv) Uchunguzi wa magonjwa ya akina mama na masuala ya uzazi.

Waheshimiwa Wabunge zoezi hili linashirikisha Madaktari Bingwa kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Madaktari hawa wanatoka Taasisi ya Mifupa Moi, lakini pia Taasisi ya Magonjwa ya Moyo *JKCI.* Kwa hiyo, kipindi hiki ambacho Mheshimiwa Spika amewaleta hawa madaktari, ni muhimu tukaangalie afya zetu ili tuweze kuwatumikia wananchi vizuri. Pia siyo sisi peke yetu na familia zetu na watumishi wote wanakaribishwa kwa ajili ya zoezi hilo, nami nawatakia kila la heri.

Hapa sijaona; kuna kitu hakijatajwa, kile ambacho Wabunge walikuwa wanachangia sana wiki iliyopita, kwamba, tuwashawishi wanaume wakapime. Sasa hapa naona hakijawekwa, lakini nataka kuamini kipimo hicho kipo ili tuanze kwa kuwashawishi Wabunge wanaume humu ndani kwenda kupima. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ambao wanakaa karibu na mwanaume yeyote wahakikishe huyo mwanaume anaenda kupima ili tuijue afya yake.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Kipimo gani?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge baada ya matangazo hayo tutaendelea na shughuli zilizo mbele yetu. Katibu!

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Chamuriho aje awasilishe hoja ya Wizara yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na kupitisha Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi wa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii kwa ajili ya kushiriki katika katika Mkutano wa Bunge lako ili kujadili utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Ujenzi - Fungu 98 na Uchukuzi - Fungu 92 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na kujadili Mipango ya Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Sekta hizo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuapishwa kuwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Watanzania wana imani na matumaini makubwa naye na chini ya uongozi wake nchi yetu itapiga hatua kubwa zaidi za maendeleo. Nampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hatimaye kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunaamini kuwa ozoefu wake katika uongozi utakuwa chachu katika

kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nampongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na makini, akiwa Msimamizi Mkuu wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa naomba kutoa pole kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwako wewe binafsi na Bunge lako Tukufu na Watanzania wote kwa ujumla kwa msiba mkubwa wa Taifa letu kwa kuondokewa na mpendwa wetu na kipenzi cha Watanzania, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyeaga dunia tarehe 17 Machi, 2021. Tunaendelea kumwomba Mwenyezi Mungu ampe pumziko la milele. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba kutoa pole zangu kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondokewa na Rais Mstaafu Awamu wa Tatu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Benjamin William Mkapa na aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad na Balozi Mhandisi John William Herbert Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba nitoe pole nyingi kwako Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na Wapendwa wetu Mheshimwa Martha Jachi Umbulla, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara na Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Justus Nditiye, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambwe. Mwenyezi Mungu awape pumziko la milele. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikupongeze na kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wa

Kamati ya Kudumu ya Bunge, Katibu wa Bunge, Watendaji wa Ofisi ya Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano ninaoendelea kuupata wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa mbalimbali kuhusu Wizara ninayoisimamia. Napenda kuwahakikishia kuwa Wizara yangu itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika ili kufikia malengo ya kisekta na Kitaifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini na Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki. Nakiri kuwa Wizara imenufaika sana na umahiri, umakini na ushirikiano wa Kamati hiyo katika kuchambua kushauri na kufuatilia maendeleo ya Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hii yamezingatiwa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuwasilisha hotuba hii, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango kwa hotuba zao zilizotangulia. Hotuba hizo zimeeleza kwa ujumla maendeleo ya Sekta za Kijamii na Kiuchumi kwa mwaka 2020/2021 na Mwelekeo wa mwaka 2021/2022. Nawashukuru na kuwapongeza pia Mawaziri wote waliowasilisha hotuba zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha hotuba yangu ambayo imejikita katika utekelezaji wa Mipango ya Bajeti ya Wizara Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021, pamoja na Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara yangu kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Ujenzi; katika mwaka wa fedha 2020/2021, Sekta ya Ujenzi imetengewa

jumla ya Sh.38,774,425,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi Aprili, 2021 asilimia 71.2 ya fedha zilizoidhinishwa zilikuwa zimetolewa na Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kwa upande wa miradi ya maendeleo katika mwaka 2020/2021, Sekta ya Ujenzi ilitengewa shilingi 1,557,586,788,000 kiasi hicho kinajumlishwa fedha za ndani, fedha za nje na fedha za Mfuko wa Barabara. Hadi Aprili, 2021, fedha zilizopokelewa ni asilimia 67.2 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; Miradi ya Barabara na Madaraja; katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* ilipanga kutekeleza miradi ya barabara kuu inayohusisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 455.75 kwa kiwango cha lami; ujenzi wa madaraja 11; pamoja na ukarabati wa Kilometa 25 kwa kiwango cha lami. Hadi kufikia Aprili, 2021, jumla ya kilometa 423.11 za barabara kuu zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya kilometa 5.5 za barabara kuu zimekarabatiwa kwa kiwango cha lami. Aidha, utekelezaji wa mipango ya madaraja umekamilika kwa asilimia 36.36 ya mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa barabara za mikoa; katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara kupitia *TANROADS* ilijipanga kujenga kwa kiwango la lami barabara zenye urefu wa kilometa 64.72 ambazo kilometa 41.31 zilipangwa kujengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na kilometa 23.41 zilipangwa kujengwa kwa kutumia Mfuko wa Barabara. Aidha, kilometa 1,005.33 zilipangwa kukarabatiwa kwa kiwango cha changarawe ambapo kati ya hizo kilometa 589.31na madaraja 24 yalipangwa kukarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na kilometa 416.2 na madaraja 27 yalipangwa kukarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2021, jumla ya kilometa 23.88 za barabara za mikoa zilijengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya kilometa 428.44 zilifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe. Aidha, utekelezaji wa miradi ya madaraja umekamilika kwa asilimia 23.14.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa madaraja makubwa umeendelea ambapo hadi Aprili, 2021, miradi iliyokamilika ni pamoja na ujenzi wa Daraja la Sibiti, Daraja la Magufuli kule Kilombero, Daraja la Momba, Daraja la Mlalakuwa, Daraja la Magara, Daraja la Lukuledi na Daraja la Mara. Miradi mingine iliyokamilika ni usanifu wa kina wa Daraja la Simiyu, Daraja la Mitomoni na Daraja la Sanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Benki ya Dunia imeonesha nia ya kugharamia ujenzi wa Daraja la Simiyu kupitia Mpango wake wa *Lake Victoria Transport Programme*. Miradi mingine mikubwa ya madaraja inayoendelea ni pamoja na ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi, Daraja Jipya la Wami, Daraja jipya la *Selander*, Daraja la Gerezani na ujenzi wa sehemu ya juu wa Daraja la Ruhuhu ambalo ujenzi wa msingi na nguzo umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia *TANROADS* iliendelea na kazi ya kudhibiti uzito wa magari kwa mujibu wa Sheria ya Afrika Mashariki na Udhibiti wa Uzito wa Magari ya mwaka 2016 na Kanuni zake za mwaka 2017 kwa kutumia jumla ya mizani 85. Hadi kufikia Aprili, 2021, magari 4,465,261 yalikuwa yamepimwa ambapo kati ya hayo, magari 34,135 yalikuwa yamezidisha uzito zaidi ya asilimia tano ya uzito unaoruhusiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa miradi ya Barabara na Madaraja umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba aya ya 18 hadi aya 105.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vivuko na Majengo ya Serikali; katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania *(TEMESA)* iliendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa maegesho ya vivuko. Hadi Aprili, 2021, upanuzi wa jengo la abiria katika maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni Jijini Dar es Salaam ulikuwa katika hatua za mwisho. Vilevile, ujenzi wa miundombinu jengo la abiria, ofisi na uzio katika vituo kumi vya vivuko viko katika hatua mbalimbali za

manunuzi. Ukarabati wa maegesho wa vituo vingine vinne vya Vivuko Bugolora - Ukara, Rugezi - Kisorya, Nyakarilo - Kome na Kigongo – Busisi umekamilika na maegesho ya Iramba – Majita yapo katika hatua za manunuzi. Aidha, maegesho ya Kayenzi - Kanyinga na Muleba – Ikuza yapo katika hatua ya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi ya ununuzi wa vivuko, hatua iliyofikiwa hadi kufikia Aprili, 2021 ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa Vivuko vipya vya Nyamisati – Mafia, Chato - Nkome na Bugolora - Ukara. Aidha, ujenzi wa Kivuko kipya cha Kisorya – Rugezi na ununuzi wa *fiber* boti mpya moja kwa ajili ya Kivuko cha Utete – Mkongo upo katika hatua za manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania *TBA* iliendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali. Hadi Aprili, 2021, kazi za ujenzi wa nyumba tano za Majaji katika Mikoa ya Kilimanjaro, Shinyanga, Mtwara, Dar es Salaam na Tabora zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, ujenzi wa nyumba za makazi ya Magomeni Kota umefikia asilimia 94. Vile vile, ukarabati wa nyumba za viongozi, watumishi wa umma unaendelea ukiwa katika hatua za ukamilishaji. Utekelezaji wa miradi ya Vivuko na Majengo umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba aya 106 hadi aya ya 110.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwanja vya Ndege; katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara kupitia *TANROADS* imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya ndege mbalimbali nchini ikiwemo Viwanja vya Ndege vya Kigoma, Songwe, Tabora, Shinyanga, Sumbawanga, Mwanza, Arusha, na Bukoba. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ukarabati wa njia za kutua na kuruka ndege, uwekaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege, ujenzi wa majengo ya uchunguzi wa hali ya hewa, majengo ya abiria na kazi nyingine zinazohusiana na kuweka mazingira salama kwa abiria na ndege. Utekelezaji wa miradi

ya Viwanja vya Ndege umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu aya ya 114 hadi aya ya 128.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Mfuko wa Barabara; katika mwaka wa fedha 2020/2021, Mfuko wa Barabara ulitarajia kukusanya jumla ya shilingi 916,780,529,000 kwa ajili ya kugharamia kazi za matengenezo na maendeleo ya barabara. Kati ya fedha hizo, shilingi 641,746,370,000 zilikuwa kwa ajili ya kugharamia kazi za matengenezo na maendeleo ya barabara za Kitaifa.

Aidha, shilingi 275,034,159,000 zilitengwa kwa ajili ya kugharamia kazi za matengenezo na maendeleo ya barabara za Wilaya kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Hadi Aprili, 2021 Bodi imekusanya na kugawanya jumla ya shilingi 716,813,813,708, sawa na asilimia 78.19 ya bajeti ya mwaka. Utendaji wa Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Ujenzi umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba kuanzia aya ya 129 hadi aya ya 155.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uchukuzi; Bajeti ya Matumizi ya Kawaida; katika bajeti ya mwaka 2020/2021, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa shilingi 90,790,199,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Aprili, 2021, fedha za Matumizi ya Kawaida zilizotolewa kwa Sekta ya Uchukuzi na Taasisi zake ni asilimia 81.78 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Maendeleo; katika mwaka wa fedha 2020/2021, Sekta ya Uchukuzi ilitengewa jumla ya shilingi 3,062,148,630,000 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2021 jumla ya fedha zilizotolewa ni asilimia 55.7 ya bajeti iliyoidhinishiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; Udhibiti wa Usafiri kwa Njia ya Barabara; Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini *(LATRA)* imeendelea kusimamia na kudhibiti usafiri katika sekta ndogo za reli, barabara na usafiri wa anga. Aidha, Mamlaka imeendelea kufuatilia mwenendo wa mabasi ya masafa marefu ili kuimarisha shughuli za udhibiti wakati wote na

mahali popote vyombo hivi vilipo. Hadi Aprili, 2021, jumla ya mabasi 5,386 na vichwa vya treni vitano vilikuwa vimeunganishwa kwenye mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya uunganishaji wa mabasi kwenye mfumo wa tiketi za kielektroniki inaendelea. Hadi sasa jumla ya mabasi 2,194 kati ya mabasi 5,386 sawa na asilimia 40 ya mabasi yote yanayotoa huduma za usafiri mikoani yameunganishwa katika mfumo wa tiketi mtandao. Utendaji katika udhibiti wa usafiri kwa njia ya barabara katika mwaka 2020/2021 umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba aya ya 159 hadi aya ya 164.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Reli Tanzania *(TRC)*; Shirika hili limeendelea kusimamia, kuboresha na kuendeleza miundombinu na huduma za usafiri wa reli yenye jumla ya kilometa 2,706 kwa ajili ya kuhudumia Nchi jirani za Burundi, Rwanda, Uganda na Kenya. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, *TRC* ilisafirisha tani za mizigo 257,602 ikilinganishwa na tani 249,960 zilizosafirishwa kipindi kama hicho mwaka 2019/2020.

Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya abiria wa masafa marefu 333,696 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 369,638 waliosafirishwa kipindi kama hicho katika mwaka 2019/2020. Sababu za upungufu huu ni athari za mlipuko wa *COVID19* na kufungwa kwa njia kutokana matengenezo na ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, Serikali imeendelea kusimamia ujenzi wa reli ya Dar es Salaam hadi Mwanza kwa kiwango cha *Standard Gauge*. Ujenzi wa reli ya katika kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro umekamilika kwa asilimia 91 na kuhusu kipande cha reli kutoka Morogoro hadi Makutupora, ujenzi unaendelea na umekamilika kwa asilimia 60.2.

Aidha, kazi za ujenzi wa mfumo wa umeme katika Mradi wa *SGR* imekamilika kwa asilimia 100 kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro na asilimia 35.62 kwa kipande cha Morogoro hadi Makutupora.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Tarehe 8 Januari 2021, Serikali kupitia *TRC* ilisaini Mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya Mwanza-Isaka. Malipo ya awali ya ujenzi wa kipande hiki ya Shilingi bilioni 376.44 yamefanyika Aprili, 2021. Kazi ya ujenzi inatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Mei, 2021 na sasa Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya ujenzi ikiwemo uletaji wa mitambo. Serikali inaendelea na majadiliano na Taasisi za fedha na Washirika wa Maendeleo mbalimbali waliooneshа nia ya kugharamia ujenzi wa reli ya *SGR,* vipande vya reli ambavyo vimebaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ununuzi wa vifaa vya uendeshaji wa Reli ya *SGR*, Mkataba wa ununuzi wa vichwa viwili vya treni za umeme pamoja na mabehewa 30 ulisainiwa Oktoba, 2020. Majaribio ya kwanza ya Reli ya *SGR* yamepangwa kufanyika Agosti, 2021. Utekelezaji wa miradi ya reli ya Kati kupitia *TRC* umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba aya ya 168 hadi aya 177.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Reli ya *TAZARA;* huduma za kusafirisha abiria na mizigo kwa njia ya reli kati ya Dar es Salaam, Tanzania hadi New Kapiri Mposhi, Zambia zimeendelea kutolewa na Mamlaka ya Reli ya *TAZARA.* Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, *TAZARA* ilisafirisha jumla ya tani 167,242 za mizigo ikilinganishwa na tani 148,681 zilizosafirishwa kwa kipindi kama hicho 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko hili limechangiwa na kuanza kufanya kazi kwa injini saba zilizofungwa vipuri vipya vilivyonunuliwa na Serikali pamoja na matengenezo ya njia ya reli hasa kwenye maeneo korofi. Treni hizi kwa sasa zinafanya safari kati ya Dar es Salaam na Mbeya kwa upande wa Tanzania na kati ya Nakonde na New Kapiri Mposhi kwa upande wa Zambia. Utekelezaji wa miradi ya reli ya *TAZARA* umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba aya ya 178 hadi 182.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa Huduma za Usafiri kwa njia ya Maji; Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania *(TASAC)* imeendelea kudhibiti ulinzi na usalama wa vyombo vya usafiri kwa njia ya maji na kudhibiti uchafuzi

wa mazingira majini utokanao na shughuli za usafiri kwa njia ya maji. Pia, Shirika limeendeleza na kupanua huduma za sekta ya usafiri kwa njia ya maji, kudhibiti huduma za bandari na usafiri kwa njia ya maji na kuhimiza ufanisi, uchumi na ushindani katika biashara ya Uwakala wa Meli. Aidha, *TASAC* imeendelea kufanya kazi za uwakala wa meli ikiwa ni pamoja na kulinda maslahi mapana ya Taifa. Utendaji katika udhibiti wa usafiri kwa njia ya maji kwa mwaka 2020/2021 umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba aya ya 183 hadi 188.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Uchukuzi katika Maziwa; Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL)* imeendelea kutoa huduma ya usafiri wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu ya Tanganyika, Victoria na Nyasa. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, Kampuni ilisafirisha jumla ya abiria 220,122 ikilinganishwa na abiria 55,053 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa abiria kumetokana na kuanza kutoa huduma kwa meli mbili za New Victoria Hapa Kazi Tu na New Butiama Hapa Kazi Tu baada ya kufanyiwa ukarabati mkubwa na kuanza kutoa huduma katika Ziwa Victoria mwezi Agosti, 2020. Utendaji huu uliiwezesha *MSCL* kukusanya jumla ya shilingi bilioni 3.58 ikilinganishwa na Shilingi milioni 897.86 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *MSCL* imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa meli moja mpya ya kubeba abiria na mizigo pamoja na chelezo katika Ziwa Victoria. Aidha, *MSCL* imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa meli katika Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria pamoja na ujenzi wa meli mpya ya mizigo katika Bahari ya Hindi. Hadi kufikia Aprili, 2021, Ujenzi wa Meli mpya *MV* Mwanza Hapa Kazi Tu yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo ulikamilika kwa asilimia 69.5 na utakamilika Disemba, 2021. Utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa meli mpya na ukarabati wa meli zilizopo katika Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba aya ya 191 hadi 193.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Bandari, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania - TPA imeendelea kumiliki Bandari za Mwambao na za Maziwa katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, *TPA* ilihudumia shehena ya tani za mapato milioni 9.97 ikilinganishwa na shehena ya tani za mapato milioni 10.42 iliyohudumiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2019/2020.

Aidha, jumla ya magari 107,869 yalipakuliwa katika Bandari ya Dar es Salaam ikilinganishwa na magari 125,758 yaliyopakuliwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2019/2020. Sababu za kushuka kwa utendaji huu ni pamoja na athari za mlipuko wa UVIKO-19 uliosababisha mdodoro wa shughuli za usafirishaji kwa njia ya maji duniani pamoja na uchache wa vifaa na mitambo ya kuhudumia shehena bandarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia *TPA* inaendelea na uboreshaji wa bandari ya Mwambao ya Bandari ya Hindi za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Pamoja na bandari zilizoko kwenye maziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa. Kuhusu ujenzi wa Gati la kupokelea mafuta kutoka Uganda lililoko eneo la Chongoleani, Tanga maandalizi ya ujenzi wa Gati hilo yanaendelea wakati majadiliano ya utekelezaji wa mradi huu baina ya Tanzania na Uganda yakiwa yanaendelea kukamilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi ya uboreshaji wa bandari zilizopo kwenye mwambao wa bahari ya hindi na maziwa makuu umeonyeshwa katika kitabu cha hotuba aya 194 hadi 201.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa huduma za usafiri wa anga, viwanja vya ndege, masuala ya kiusalama na kiuchumi katika usafiri wa anga na utoaji wa huduma za uongozaji ndege umeendelea kufanywa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga - *TCAA*. Mamlaka hii pia imeendelea kudhibiti Viwanja vya Ndege vinavyomilikiwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa *(TANAPA),* Wizara ya Maliasili na Utalii, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Sekta Binafsi. Lengo ni kuimarisha

utoaji huduma, kukuza utalii nchini na kuendelea kuhakikisha utekelezaji wa Sheria na Kanuni za uendeshaji wa Viwanja vya Ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, idadi ya abiria wanaotumia usafiri wa anga imepungua hadi kufikia abiria 2,495,379 ikilinganishwa na abiria 4,423,732 waliotumia usafiri huo katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2019/2020. Sababu za kupungua kwa abiria wanaosafiri ndani na nje ya nchi ni mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO 19 ambapo nchi nyingi zilifunga na kuzuia safari za anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Viwanja vya Ndege Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)* imeendelea kutoa huduma kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya Usafiri wa Anga. Mamlaka hii ina jukumu la kusimamia, kuendesha na kuendeleza viwanja vya ndege 59 vinavyomilikiwa na Serikali isipokuwa vile vilivyo chini ya Mamlaka za Hifadhi, Halmashauri, Jeshi na Taasisi binafsi. Katika utekelezaji wa majukumu yake, *TAA* imeendelea kusimamia shughuli za uendeshaji wa Jengo jipya la Tatu la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji na uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro - *KIA* umeendelea kusimamiwa na Kampuni ya Kuendeleza Viwanja vya Ndege vya Kilimanjaro - *KADCO*. Kampuni hii imeendelea kuhakikisha kuwa inahudumia mizigo inayohitaji ubaridi ili kuvutia biashara na usafirishaji wa mizigo mbalimbali kama vile mbogamboga, matunda na maua kupitia kiwanja cha ndege cha Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Usafiri wa Anga Kampuni ya Ndege ya Tanzania - *ATCL* imeendelea kutoa huduma za kusafirisha abiria na mizigo ndani na nje ya Tanzania. katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, Serikali ilinunua ndege mbili aina ya A220-300 na ndege moja aina ya Dash 8 Q400. Utengenezaji wa Ndege hizo haukukamilika

kwa muda uliopangwa kutokana na athari za mlipuko wa UVIKO-19 uliosababisha viwanda kusimamisha uzalishaji. Kati ya ndege hizo, ndege moja aina ya Dash 8 Q400 inatarajiwa kuwasili nchini kabla ya Juni, 2021 na ndege nyingine mbili aina za *Airbus* (A220-300) zinatarajiwa kuwasili nchini mwezi Agosti 2021 na Oktoba, 2021. Maelezo kuhusu utendaji katika usafiri na uchukuzi kwa njia ya anga kwa mwaka 2021 yametolewa katika kitabu cha hotuba aya ya 202 hadi 224.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Hali ya Hewa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania imeendelea kusimamia, kudhibiti na kuratibu utoaji wa huduma za hali ya hewa hapa nchini. Utoaji wa huduma za hali ya hewa hapa nchini umeendelea kuwa bora ambapo usahihi wa utabiri umefikia asilimia 87.9. Kiwango hiki ni juu ya kiwango kinachokubalika na Shirika la Hali ya Hewa Duniani ambacho ni asilimia 70. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, kazi ya ufungaji wa rada ya hali ya hewa huko Mtwara ilikamilika na kukabidhiwa Disemba, 2020. Aidha, malipo ya ununuzi wa Rada mbili za hali ya hewa zitakazofungwa Mbeya na Kigoma zimekamilika kwa asilimia 90 na utengenezaji uko katika hatua za mwisho. Utekelezaji wa miradi ya huduma hii ya hali ya hewa umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba Aya ya 225 hadi 227.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi za Mafunzo utekelezaji wa majukumu ya Taasisi za Mafunzo zinazosimamiwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba kuanzia Aya ya 228 hadi Aya ya 240.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zinazoikabili Wizara katika kutekelezaji majukumu yake, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imekabiliwa na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo na mikakati ya kukabiliana nazo imeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba Ukurasa wa 129 hadi wa 136.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara kwa Mwaka 2021/

2022. Wizara imeandaa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2021/2022 kwa kuzingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Ujenzi Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Sekta ya Ujenzi (Fungu 98) imetengewa jumla ya shilingi 1,627,244,274,200.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekta ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2021/22 ni Shilingi 38,540,787,000.00. Aidha, Sekta ya Ujenzi imetengewa jumla ya Shilingi 1,588,703,487,200.00 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mgawanyo wa fedha za maendeleo kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama ilivyoonyeshwa katika Viambatisho Na.1 na Na. 2 vya Hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fedha za Mfuko Wa Barabara katika mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya shilingi 635,849,127,200.00 kutoka Mfuko wa Barabara zimetengwa kwa ajili ya kufanya kazi za matengenezo na ukarabati wa barabara kuu na za mikoa. Kati ya fedha hizo, *TANROADS* imetengewa shilingi 567,342,742,235.00 kwa ajili ya matengenezo ya barabara na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imetengewa shilingi 63,038,082,471.00 kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara za mikoa, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara, ukarabati na ununuzi wa vivuko, usalama barabarani pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hiyo. Aidha, shilingi 5,468,302,494.00 zitatumika kugharamia uendeshaji wa Bodi ya Mfuko wa Barabara. Mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi zimeonyeshwa katika Viambatisho Na. 3 na 4. Aidha, mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo umeoneshwa katika Viambatisho Na. 5, 5A - 5D.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uchukuzi katika mwaka wa fedha 2021/2022, Sekta ya Uchukuzi (Fungu 62) imetengewa jumla ya shilingi 2,120,049,821,000.00 kwa ajili ya

Matumizi ya Kawaida na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 91,743,411,000.00 zimetengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 2,028,306,410,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyooneshwa katika Kiambatisho Na. 6. Mchanganuo wa miradi inakayotekelezwa kwa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na Fedha za vyanzo vya ndani vya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba kuanzia Aya ya 410 hadi Aya ya 423 pamoja na Aya 425 hadi Aya ya 426 kwa Taasisi ambazo ziko chini ya Sekta ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani napenda kuwashukuru wananchi na wadau mbalimbali hasa sekta binafsi kwa ushirikiano wao katika kutekeleza malengo ya Sekta zetu. Shukurani za pekee ziwaendee Waheshimiwa wabunge wenzangu kwa michango yao ambayo imechangia katika kuimarisha huduma zitolewazo na Wizara. Naomba waendelee na moyo huo ili tuweze kuendeleza Wizara hii ambayo ni muhimu katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukurani zangu hazitakuwa kamili bila kuwashukuru Viongozi wenzangu katika Wizara nikianzia na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Msongwe Kasekenya (Mb.) na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara (Mb.); Makatibu Wakuu Mhandisi Joseph Kizito Malongo (Ujenzi) na Bwana Gabriel Joseph Migire (Uchukuzi). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawashukuru Wakuu wa Idara, Viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, Watumishi na Wataalamu wote wa Wizara kwa kujituma katika kusimamia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara. Naomba waendelee na juhudi hizo katika kipindi kijacho ili tuweze kutekeleza malengo Wizara na ya Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, washirika mbalimbali wa Maendeleo wamekuwa wakichangia katika maendeleo ya Programu na Mipango mbalimbali ya Wizara. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwatambua Washirika hao wa Maendeleo ambao ni pamoja na Shirika la Kimataifa la Usafiri kwa njia ya Maji *(IMO),* Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga *(ICAO),* Shirika la Hali ya Hewa Duniani *(WMO),* Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA), OPEC Fund*, Umoja wa Nchi za Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (World Bank), Japan kupitia (*JICA*), Korea Kusini kupitia(KOICA), *Abu Dhabi Fund*, Ujerumani kupitia(KfW), Uingereza kupitia(*DFID*), Uholanzi kupitia(ORIO), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Kuwait (KFAED), Uturuki *HSBC*, *TMEA*, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za *SADC*, Nchi za Urusi, Afrika Kusini, Uingereza, Marekani, Uholanzi, Japan, India, China, Denmark, Norway, Ubelgiji, Ujerumani, Taasisi za fedha za *CRDB, NSSF, PSSSF* na *TIB*, Asasi zisizokuwa za Kiserikali; Sekta Binafsi pamoja na wengine wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nakushukuru tena wewe binafsi na Mheshimiwa Spika hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara.

Muhtasari wa maombi ya fedha za Wizara katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 3,747,294,095,200.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,627,244,274,200.00 ni kwa ajili ya Sekta ya Ujenzi na shilingi 2,120,049,821,000.00 ni kwa ajili ya Sekta ya Uchukuzi. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa zimeonyeshwa katika kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Hotuba hii nimeambatisha Miradi ya Wizara inayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2021 ambacho ni Kiambatisho Na. 1-6 ikiwa ni pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa katika kutekeleza Miradi hiyo. Naomba kitabu kizima cha Hotuba yangu ya bajeti pamoja na viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI, MHESHIMIWA MHANDISI DKT. LEONARD MADARAKA CHAMURIHO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## A. UTANGULIZI

***1. Mheshimiwa Spika***, baada ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuchambua Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, na Mwenyekiti wa Kamati hiyo kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2020/21. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/22.

***2. Mheshimiwa Spika***, nianze kwa unyenyekevu mkubwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehma, kwa afya njema na uzima aliotujaalia.

***3. Mheshimiwa Spika***, naomba kuchukua fursa hii, kwa masikitiko makubwa, kuungana na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kutoa pole kwako wewe binafsi, Bunge lako Tukufu na watanzania wote kwa ujumla kufuatia kifo cha mpendwa wetu Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kilichotokea tarehe 17 Machi, 2021. Hakika tutamkumbuka shujaa huyu wa Afrika kwa uzalendo, ujasiri, vita dhidi ya ufisadi na uongozi 4 wake mahiri ulioacha alama kubwa kwa Taifa letu na Afrika kwa ujumla. Kipekee kwa Wizara ninayoiongoza, tumepata pigo kubwa kwani Hayati Magufuli alitumia kipindi kirefu cha uongozi wake akiiongoza Sekta ya Ujenzi kwa mafanikio makubwa. Ninaendelea kumuomba Mwenyezi Mungu ampe pumziko la milele, Amina.

***4. Mheshimiwa Spika,*** Taifa letu lilipata pigo lingine kubwa kwa kuondokewa na viongozi wa kitaifa. Kipekee natoa pole kwa kifo cha Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Hayati Maalim Seif atakumbukwa kwa kuhimiza amani, mshikamano na umoja wa kitaifa nchini. Mwenyezi Mungu amrehem, Amina. Aidha, nitoe pole kwa familia ya Hayati Mhandisi Balozi John William Herbert Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Tutamkumbuka kwa wema wake, uadilifu, hekima, maarifa na uchapaji kazi uliotukuka. Bwana alitoa na Bwana ametwaa, Jina lake lihimidiwe.

***5. Mheshimiwa Spika,*** sambamba na salamu hizo nichukue fursa hii kutoa mkono wa pole kwa Bunge lako Tukufu kufuatia vifo vya Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliofariki tangu kuzinduliwa kwa Bunge hili ambao ni Mhandisi Atashasta Justus Nditiye, aliyekuwa Mbunge wa jimbo la Muhambwe na Martha Jachi Umbulla, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum mkoa wa Manyara. Tutaendelea kuienzi michango yao katika ustawi na maendeleo ya majimbo waliyotoka na Taifa kwa ujumla. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi. Amina.

***6. Mheshimiwa Spika*****,** nichukue fursa hii kwa kipekee kumpongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuapishwa kushika nafasi hiyo ya juu kabisa ya uongozi wa nchi yetu. Ingawa ameanza uongozi wake katika mazingira ya wimbi la simanzi ya msiba wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kipindi kifupi alichokaa madarakani ameonesha dhahiri kuwa *ANATOSHA*. Hatuna shaka na utendaji wake, umakini, ujasiri, maarifa, uwajibikaji pamoja na uongozi wake uliotukuka. Tunamtakia kila la kheri Rais wetu huyu katika uongozi wake na kumuomba Mwenyezi Mungu azidi kumpa afya njema, hekima na maarifa kwa ajili ya kuiongoza nchi yetu. Aidha, ninampongeza Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango kwa kuteuliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hatimaye kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu, kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Awamu hii ya Sita. Tunaamini kuwa uzoefu wake katika uongozi

utakuwa chachu katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake. Vilevile, ninampongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na makini, akiwa msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali hapa Bungeni.

***7. Mheshimiwa Spika****,* kwa heshima kubwa nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Rais kwa imani kubwa aliyokuwa nayo juu yangu na kuniteua kuwa Waziri katika Serikali yake. Ninaahidi kuwa nitaitumikia nafasi hii nikiongozwa na falsafa ya kutanguliza mbele maslahi ya Taifa na nitatumia uzoefu wangu wa muda mrefu katika sekta ninazoziongoza ili ***kazi iendelee.***

***8. Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla kwa kuchaguliwa na wananchi kuingia katika Bunge hili Tukufu. Aidha, nikupongeze wewe binafsi Mhe. Spika, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Kamati za Bunge kwa namna mnavyolisimamia na kuliongoza Bunge letu Tukufu ili litimize jukumu lake la kuisimamia Serikali.

***9. Mheshimiwa Spika,*** niishukuru pia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na Mhe. Seleman Moshi Kakoso (Mb), Mbunge wa Mpanda Vijijini na Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Anne Kilango Malecela (Mb), Mbunge wa Same Mashariki. Uchambuzi wao wa Taarifa ya Utekelezaji wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/21 na Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/22 umetusaidia kwa kiasi kikubwa kuandaa Bajeti ya Wizara kwa ubora zaidi. Tutaendelea kupokea maoni na ushauri wao na kuufanyia kazi kwa kadri inavyowezekana.

***10. Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kuwasilisha Hotuba yangu, nitumie nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango kwa hotuba zao ambazo zimefafanua utendaji wa Serikali kwa mwaka 2020/21 na mwelekeo kwa mwaka 2021/22. Vilevile,

nawapongeza Mawaziri wote waliowasilisha hotuba zao kabla yangu.

## B. MAJUKUMU YA WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

***11. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inajumuisha Sekta mbili ambazo ni Sekta ya Ujenzi na Sekta ya Uchukuzi.

***12. Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya msingi ya Sekta ya Ujenzi ni kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ujenzi (2003) pamoja na Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani (2009); ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara, madaraja na vivuko; ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya viwanja vya ndege; ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali; usimamizi wa masuala ya ufundi na umeme; usimamizi wa shughuli za ukandarasi, uhandisi, ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi; usimamizi wa maabara na vifaa vya ujenzi; usimamizi wa masuala ya usalama barabarani na mazingira katika Sekta; uboreshaji, utendaji na uendelezaji wa watumishi wa Sekta pamoja na usimamizi wa majukumu ya taasisi zilizo chini ya Sekta.

***13. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Sekta ya Uchukuzi, majukumu yake ni kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uchukuzi ya mwaka 2003; ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya reli na bandari; usafiri na usafirishaji kwa njia ya anga, reli na bandari; utoaji wa leseni za usafirishaji; usalama katika usafirishaji; usimamizi wa huduma za hali ya hewa; kuendeleza rasilimaliwatu na kusimamia Taasisi na Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Sekta ya Uchukuzi.

***14. Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa kuwasilisha hotuba yangu ambayo inaonesha Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2020/21. Aidha, Hotuba hii itafafanua Mpango na Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2021/22.

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

### C.1 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KISEKTA

***15. Mheshimiwa Spika***, katika sehemu hii, nitaeleza kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/21 nikianzia na Sekta ya Ujenzi ikifuatiwa na Sekta ya Uchukuzi.

### C.1.1 SEKTA YA UJENZI
**Bajeti ya Matumizi ya Kawaida**

***16. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara (Ujenzi) ilitengewa jumla ya Shilingi **38,774,425,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi **36,420,026,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake na Shilingi **2,354,399,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi zake.

Hadi Aprili, 2021 jumla ya **Shilingi 27,607,504,049.69,** sawa na asilimia **71.2** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zilikuwa zimetolewa na HAZINA kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 25,645,504,883.19** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi na **Shilingi 1,961,999,166.50** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi zake.

**Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

***17. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa miradi ya maendeleo, katika mwaka wa fedha 2020/21, Sekta ya Ujenzi ilitengewa **Shilingi 1,577,586,781,000.00**. Kiasi hicho kinajumuisha **Shilingi 1,252,222,598,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 325,364,183,000.00** fedha za nje. Fedha za ndani zilijumuisha fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Funds) **Shilingi 610,476,228,000.00** na fedha za Mfuko wa Barabara **Shilingi 641,746,370,000.00.** Hadi Aprili, 2021 fedha zilizopokelewa ni **Shilingi 1,060,741,508,270.64** sawa na asilimia **67.2** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/21. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 768,538,345,231.27** ni fedha za ndani na **Shilingi 292,203,163,039.37** ni fedha za nje. Fedha za ndani zilizopokelewa zinajumuisha **Shilingi 266,768,675,670.96** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi 501,769,669,560.31** kutoka Mfuko wa Barabara.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**

**Miradi ya Barabara na Madaraja**

***18. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ilipanga kutekeleza miradi ya barabara kuu inayohusisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa **kilometa 455.75** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja **11** pamoja na ukarabati wa **kilometa 25** kwa kiwango cha lami. Hadi kufikia Aprili, 2021, jumla ya **kilometa 423.11** za barabara kuu zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya **kilometa 5.5** za barabara kuu zimekarabatiwa kwa kiwango cha lami. Aidha, utekelezaji wa miradi ya madaraja umekamilika kwa asilimia **36.36** ya mpango.

***19. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa barabara za mikoa, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara kupitia TANROADS ilipanga kujenga kwa kiwango cha lami barabara zenye urefu wa **kilometa 64.72** ambapo **kilometa 41.31** zilipangwa kujengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 23.41** zilipangwa kujengwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Aidha, **kilometa 1,005.33** zilipangwa kukarabatiwa kwa kiwango cha changarawe ambapo kati ya hizo, **kilometa 589.31** na madaraja **24** yalipangwa kukarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 416.2** na madaraja **27** yalipangwa kujengwa/ kukarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Hadi Aprili, 2021 jumla ya kilometa **23.88** za barabara za mikoa zilijengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya kilometa **428.44** zilifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe. Aidha, utekelezaji wa miradi ya madaraja umekamilika kwa asilimia **23.14** ya mpango. Utekelezaji wa miradi uliathiriwa na kuchelewa kupatikana kwa misamaha ya Kodi ya Ongezeko

la Thamani (VAT). Hata hivyo, Wizara ya Fedha na Mipango imeandaa Mfumo utakaorahisisha upatikanaji wa misamaha hiyo ya kodi.

***20. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, Wizara ilipanga kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa ambayo yanahusisha matengenezo ya kawaida (routine and recurrent maintenance) kwa kilometa **34,268.29,** matengenezo ya muda maalum kilometa **4,886.67** matengenezo ya sehemu korofi kilometa **743.49** na matengenezo ya madaraja **3,390.** Mpango huu pia unajumuisha shughuli za udhibiti wa uzito wa magari na ulinzi wa hifadhi za barabara, kazi za dharura pamoja na mradi wa matengenezo ya barabara kwa mikataba ya muda mrefu. Hadi Aprili, 2021 utekelezaji wa matengenezo katika barabara kuu na za mikoa ulikuwa umekamilika kwa asilimia **30.**

***21. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TANROADS iliendelea na kazi ya kudhibiti uzito wa magari kwa mujibu wa Sheria ya Afrika Mashariki ya Udhibiti wa Uzito wa Magari ya Mwaka 2016 na Kanuni zake za mwaka 2017 kwa kutumia jumla ya mizani **85**. Aidha, kati ya hiyo, mizani **63** ni ya kudumu na **22** ni inayohamishika. Kati ya mizani ya kudumu, mizani **13** ni ile inayopima uzito wakati magari yakiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion- WIM). Hadi kufikia Aprili, 2021, magari **4,465,261** yalikuwa yamepimwa ambapo kati ya hayo, magari **34,135,** sawa na asilimia **0.76** yalikuwa yamezidisha uzito zaidi ya asilimia tano (5) ya uzito unaoruhusiwa. Magari yaliyobainika kuzidisha uzio yameongezeka kwa asilimia 0.1 ikilinganishwa na mwaka 2019/20 kutokana na kuimarika kwa mfumo wa udhibiti wa uzito wa magari Jumla ya **Shilingi 3,683,000,000.00** zilikusanywa kutokana na tozo ya uharibifu wa barabara. Katika kuongeza uwazi na uwajibikaji na hivyo kupunguza mianya ya rushwa, Wizara imeweka mifumo ya kamera katika mizani 13 na inaendelea kuweka mifumo hiyo katika mizani 42 nchi nzima. Aidha, Wizara inaendelea na utoaji wa vibali vya usafirishaji barabarani wa mizigo maalum nchini. Hadi Aprili, 2021 jumla ya **Shilingi 3,416,812,534.00** zilikusanywa kutokana na tozo ya upitishaji wa mizigo maalum.

***22. Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa miradi ya barabara kwa mwaka 2020/21 ni kama ifuatavyo:

***23. Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2021, mkataba wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa **Barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe (km 74),** ulikuwa umesainiwa. Aidha, fedha za mradi huu ‘ mara baada ya Mhandisi Mshauri anayefanya kazi hii kuwasilisha hati za malipo.

***24. Mheshimiwa Spika,*** upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa **Barabara ya Mtwara – Newala – Masasi (km 210)** umekamilika. Aidha, Serikali imekamilisha ujenzi wa sehemu ya ***Mtwara – Mnivata (km 50).*** Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) wameonesha nia ya kugharamia ujenzi wa sehemu iliyobaki ya ***Mnivata – Tandahimba – Newala – Masasi (km160)***. Wataalam kutoka AfDB wakishirikiana na wataalam wa ndani wanaendelea na maandalizi ya mradi huu.

***25. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Likuyufusi – Mkenda (km 10)**, hadi kufikia Aprili, 2021, taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi wa barabara hii zinaendelea.

***26. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa **Barabara ya Nachingwea – Liwale (km 130),** hadi kufikia Aprili, 2021, rasimu ya taarifa ya upembuzi yakinifu imewasilishwa na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kuitolea maoni.

***27. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere (km 11),** hadi Aprili, 2021, usanifu wa kina umekamilika na taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi wa barabara hii zinaendelea.

***28. Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa **Barabara ya TAMCO – Vikawe – Mapinga (km 24)** unafanyika kwa awamu. Hadi Aprili 2021, kilometa 2.9 zimekamilika na ujenzi wa mita 600 unaendelea. Aidha, taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa kilometa 1.33 zinaendelea.

***29. Mheshimiwa Spika,*** kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa **Barabara ya Makofia – Mlandizi (km 36.7)** zimekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi.

***30. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Musoma – Makojo – Busekela** (km 92), hadi kufikia Aprili, 2021, ujenzi wa barabara hii unaendelea kwa sehemu ya ***Suguti – Kusenyi (km 5)*** ambapo umefikia asilimia 65.

***31. Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa **Barabara ya Kongwa Jct – Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 98)** unafanyika kwa awamu. Hadi Aprili, 2021, mradi huu unaendelea na ujenzi wa kilometa 5 umefikia asilimia 55.

***32. Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa **Barabara ya Muhutwe – Kamachumu – Muleba (km 54)** unafanyika kwa awamu. Hadi Aprili, 2021, mradi huu unaendelea na kilometa 29 zimekamilika kwa kiwango cha lami.

***33. Mheshimiwa Spika,*** kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa **Barabara ya Iringa – Ruaha National Park (km 104**) zimekamilika. Aidha, Benki ya Dunia imeonesha nia ya kugharimia ujenzi wa barabara hii. Wataalam kutoka Benki wakishirikiana na wataalam wa ndani wanaendelea na maandalizi ya mradi huu.

***34. Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa **Barabara ya Muheza – Amani (km 36)** unafanyika kwa awamu. Hadi Aprili, 2021, kazi za ujenzi wa kilometa 7 zinaendelea na zimefikia asilimia 60.

***35. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ukarabati kwa kiwango cha lami wa **Barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200),** hadi kufikia Aprili, 2021, mapitio ya usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara hii yamekamilika. Aidha, Benki ya Dunia imeonesha nia ya kugharamia ujenzi wa barabara hii. Wataalam wa Benki ya Dunia wakishirikiana na wataalam wa ndani wanaendelea na maandalizi ya mradi.

***36. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Kibaoni – Majimoto – Muze – Kilyamatundu (km 189)** hadi kufikia Aprili 2021, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya ***Kibaoni – Majimoto – Inyonga (km 152)*** na ***Ntendo – Muze – Kilyamatundu (km 200)*** kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, taratibu za kutangaza zabuni kwa ajili ya ujenzi wa kilometa 25 kati ya Ntendo na Muze zinaendelea.

***37. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa **Daraja la Kigongo – Busisi (J.P. Magufuli) na Barabara Unganishi** unaendelea na hadi Aprili, 2021, ujenzi wa daraja umefikia asilimia 27. Aidha, usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa **Daraja la Mzinga** na **Daraja la Ugalla,** umekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa madaraja haya. Vilevile, ujenzi wa **Daraja la Kitengule na Barabara za Maingilio (km 18)** unaendelea ambapo hadi Aprili, ujenzi wa daraja hili umefikia asilimia 62. Kuhusu **Daraja Jipya la Wami,** kazi za ujenzi zinaendelea na zimefikia asilimia 50.

***38. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Morogoro – Dodoma Pamoja na Daraja la Mkundi,** hadi kufikia Aprili, 2021 hatua ya manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ziko katika hatua ya mwisho. Aidha, katika **Barabara ya Njombe – Makete – Isyonje (km 157.4)**, hadi kufikia Aprili 2021, ujenzi wa barabara ***Njombe – Moronga (km 53.9)*** kwa kiwango cha lami umekamilika. Kwa sehemu ya ***Moronga – Makete (km 53.5)*** kazi za ujenzi zinaendelea na zimefikia asilimia 65.2. Aidha, taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi wa kilometa 25 za sehemu ya ***Isyonje – Makete (km 50)*** zinaendelea.

***39. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105),** hadi kufikia Aprili, 2021 kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika na maboresho ya taarifa ya uthamini kwa ajili fidia yalikuwa katika hatua ya mwisho kukamilika.

***40. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 145)**, hadi kufikia Aprili 2021, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya ***Masasi – Nachingwea – Ruangwa – Nanganga (km 145)*** umekamilika. Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Nanganga – Ruangwa (km 53.2) katika barabara ya ***Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 100)*** unaendelea na Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa sehemu ya ***Masasi – Nachingwea (km 45)***.

***41. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Mpemba – Isongole,** hadi kufikia Aprili 2021, ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya ***Mpemba – Isongole (km 51.2)*** ulikuwa umekamilika na ujenzi wa daraja la Songwe unaendelea. Aidha, Serikali inaendelea na maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya ***Ruanda – Iyula – Nyimbili (km 21)*** na ***Katumbasongwe – Kasumulu – Ngana – Ileje (km 90.1)*** kwa kiwango cha lami.

***42. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge (km 174.5),** hadi kufikia Aprili 2021, ujenzi wa barabara ya ***Tanga – Pangani (km 50)*** unaendelea na umefikia asilimia 7. Aidha, utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa ***Daraja la Pangani*** na barabara ya ***Pangani – Mkange (km 124.5)*** uko katika hatua za mwisho za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi.

***43. Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa **Barabara ya Kisarawe – Maneromango (km 54)** unafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi Aprili 2021, kilometa 18 zimekamilika na ujenzi wa kilometa 1.8 unaendelea. Aidha, kilometa 1.33 zipo katika hatua za mwisho za manunuzi.

***44. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Geita – Bulyanhulu – Kahama (km 174),** hadi kufikia Aprili 2021, taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi wa sehemu ya ***Geita – Bulyanhulu Jct (km 58.3), Bulyanhulu Jct – Kahama (km 61.7)*** na ***Uyogo – Nyamilagano – Nyandekwa – Kahama (km 54)*** zilikuwa zinaendelea.

***45. Mheshimiwa Spika,*** kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa **Barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50)** imekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa **Barabara ya Geita – Nzera (km 54)** umekamilika na taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi zinaendelea.

***46. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Arusha – Moshi – Himo – Holili (km 199.51)**, hadi kufikia Aprili 2021, ujenzi wa sehemu ya ***Sakina – Tengeru Section na Barabara ya Mzunguko ya Arusha (km 56.51)*** ulikuwa umekamilika. Kwa sehemu ya ***Tengeru – Moshi – Himo na Mizani ya Himo (km 105)***, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara hii imekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha za ukarabati wa barabara hii. Aidha, ujenzi wa barabara ya ***Kijenge – Usa River (Nelson Mandela AIST) (km 20)*** unafanyika kwa awamu ambapo kilometa 18 zimekamilika kwa kiwango cha lami. Taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi wa barabara ya ***Mianzini – Ngaramtoni (km 18)*** zinaendelea.

***47. Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa ujenzi wa **Barabara za Kuelekea Kwenye Mradi wa Kufua Umeme Katika Maporomoko ya Mto Rufiji (Access Roads to Rufiji Hydropower Project),** hadi Aprili, 2021, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya ***Bigwa – Matombo – Mvuha (km 70)*** imekamilika. Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ukarabati wa barabara hii kwa kiwango cha changarawe zipo katika hatua za mwisho. Serikali itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami kwa awamu. Taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Bigwa – Kisaki zinaendelea. Aidha, katika mradi wa ***Maneromango – Vikumburu – Mloka (km 100),*** taratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa kilometa 10 kwa kiwango cha changarawe upo katika hatua za mwisho. Vilevile, taratibu za manunuzi ya kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya ***Ubena Zomozi – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 178)*** zinaendelea. Aidha, barabara ya ***Kibiti – Mloka – Mtemele – Rufiji*** imekabidhiwa rasmi kwa Mkandarasi Mkubwa wa mradi

wa Julius Nyerere Hyropower Project (JNHP) kwa ajili ya matengenezo kwa kipindi chote cha mradi huo hadi utakapokamilika.

***48. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro – Dodoma (km 152.30),** hadi kufikia Aprili 2021, utekelezaji wa mradi wa ***Mlandizi – Chalinze (km 44)*** unaendelea ambapo taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea. Aidha ujenzi wa barabara ya ***Kwa Mathiasi (Morogoro Road) – Msangani (km 8.3***) ulikuwa unaendelea.

***49. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (km 118.10),** Serikali inaendelea kutafuta fedha za ukarabati wa sehemu ya ***Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (Tegeta – Bagamoyo Section) (km 46.9)*** na ujenzi wa barabara ya ***Mbegani – Bagamoyo (km 7.2)*** kwa kiwango cha lami.

***50. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Usagara – Geita – Buzirayombo – Kyamyorwa (km 110)**, kazi za ujenzi zimekamilika kwa barabara ya ***Uyovu – Bwanga – Biharamulo (Lot 1 and Lot 2) (km 110)*** sehemu ya ***Uyovu – Bwanga (km 45)*** na ***Bwanga – Biharamulo (km 67).*** Aidha, kuhusu **Barabara ya Nyakahura – Kumubuga – Rulenge – Kabanga Nickel Road (km 141),** hadi kufikia Aprili 2021, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya ***Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba*** na ***Kumubuga – Rulenge – Kabanga Nickel (km 141)*** umekamilika. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

***51. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 389.7),** miradi iliyokamilika ni ujenzi wa ***Daraja la Kikwete (Malagarasi), Kidahwe – Uvinza (km 76.6), Tabora – Ndono (km 42)***, ***Ndono – Urambo (km 51.98), Kaliua – Kazilambwa (km 56)*** na ***Urambo – Kaliua (km 28).*** Aidha**,** hadi Aprili, 2021 taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya ***Uvinza –***

***Malagarasi (km 51.1)*** kwa kiwango cha lami zilikuwa zinaendelea. Vilevile na Mkandarasi wa sehemu ya ***Kazilambwa – Chagu (km 36)*** ameshaleta vifaa na mitambo kwa ajili ya ujenzi katika eneo la kufanyia kazi na utekelezaji umefikia asilimia 2.5.

***52. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Ifakara – Kihansi – Mlimba – Madeke – Kibena (km 150),** hadi kufikia Aprili 2021, taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi wa barabara sehemu ya ***Ifakara – Kihansi (km 50), Lupembe – Madeke (km 50)*** na ***Kibena – Lupembe (km 50)*** zilikuwa zinasubiri upatikanaji wa fedha. Aidha, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa **Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389**) imekamilika. Taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi wa barabara hii kwa sehemu ya Mbulu hadi Hydom zinaendelea.

***53. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga /Bomang'ombe – Sanya Juu (km 84.80),** kazi za ujenzi kwa mradi huu zimekamilika kwa sehemu ya ***Sanya Juu – Kamwanga (Sehemu ya Sanya Juu – Alerai, km 32)*** na ***KIA – Mererani (km 26.0)***. Aidha, ujenzi unaendelea kwa kiwango cha lami kwa sehemu za ***Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km 16)*** na ***Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8).***

***54. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Tukuyu – Mbambo – Katumba (km 60.6),** ujenzi wa barabara ya ***Bujesi – Mbambo (km 26)*** unaendelea kutekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi Aprili, 2021 kilometa 10 za barabara zimekamilika na ujenzi wa kilometa 10 kwenye barabara hii unaendelea. Vilevile, ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometa 7 barabara ya ***Tukuyu – Mbambo (km 34.6)*** ulikuwa unaendelea. Aidha, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya ***Mbambo – Ipinda (km 19.7)*** zinaendelea.

***55. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa **Barabara ya Dodoma – Manyoni (km 127) na Barabara ya Mchepuo Kuingia Manyoni**

**Mjini (km 4.8)** unahusisha ujenzi wa ***Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Muhalala (Manyoni)*** ambapo utekelezaji wa mradi huu umesimama kutokana na changamoto za kimkataba. Hadi ujenzi wa Kituo unasimama ulikuwa umefikia asilimia 50.1. Aidha, ununuzi wa ***Mizani ya Nala – Dodoma*** (Weigh in Motion – WIM) umekamilika.

***56. Mheshimiwa Spika,*** **Barabara ya Tabora – Mambali – Bukene – Itobo** (km 114) itajengwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi kufikia Aprili 2021, maandalizi ya ujenzi wa barabara hii yalikuwa yanaendelea. Aidha, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa **Barabara ya Namanyere – Katongoro – New Kipili Port (km 64.8)** ilikuwa inaendelea.

***57. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Dumila – Kilosa – Mikumi (km 119),** sehemu ya ***Dumila – Rudewa (km 45)*** imekamilika kujengwa na kwa sehemu ya ***Rudewa – Kilosa (km 24)*** unaendelea. Hadi kufikia Aprili 2021, utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 67 ambapo kilometa 10 zimekamilika kwa kiwango cha lami. Aidha, ujenzi wa ***Mizani ya Kupima Uzito wa Magari Yakiwa kwenye Mwendo (Weigh in Motion – WIM) ya Dakawa*** umekamilika na mizani inafanya kazi. Maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya ***Kilosa – Ulaya – Mikumi (km 50)*** yalikuwa yanaendelea.

***58. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 162),** ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami umekamilika kwa sehemu ya ***Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112.0).*** Aidha, taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi wa sehemu ya ***Matai – Kasesya (km 50)*** zinaendelea.

***59. Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa mradi wa **Ujenzi wa Madaraja Makubwa** umeendelea ambapo hadi Aprili, 2021, miradi iliyokamilika ni ujenzi wa Daraja la Sibiti, Daraja la Magufuli, Daraja la Ruhuhu, Daraja la Momba, Daraja la Mlalakuwa, Daraja la Magara, Daraja la Lukuledi na Daraja la Mara. Miradi mingine iliyokamilika ni Usanifu wa kina wa

daraja la Simiyu, Daraja la Mitomoni na Daraja la Sanza. Aidha, Benki ya Dunia imeonesha nia ya kugharamia ujenzi wa daraja la Simiyu kupitia Mpango wa 'Lake Victoria Transport Programme'. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa Daraja la Kiegeya (asilimia 56) na Daraja la Msingi (asilimia 49) pamoja na usanifu wa kina wa Daraja la Sukuma, Daraja la Godegode, Daraja la Mkenda, Daraja la Mtera na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa daraja la Malagarasi Chini katika barabara ya Simbo – Ilagala - Kalya. Aidha, mapitio ya Usanifu wa kina na Ujenzi wa Daraja la Mirumba yanaendelea. Mradi wa ukarabati wa Daraja la Kirumi unasubiri upatikanaji wa fedha na ununuzi wa Madaraja ya Chuma (Steel Bridges Emergency Parts) uko katika hatua za mwisho.

***60. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya New Bagamoyo (Kawawa Jct – Tegeta km 18.30),** hadi kufikia Aprili 2021, kazi za upanuzi wa barabara ya ***Morocco – Mwenge (km 4.3)*** zinaendelea na utekelezaji umefikia asilimia 80. Aidha, ujenzi wa ***Mifereji ya Maji ya Mvua Kwenye Sehemu ya Mwenge – Tegeta (km 14)*** umekamilika na mradi umepokelewa.

***61. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (km 222.10),** ujenzi wa sehemu ya ***Kyaka – Bugene (km 59.1)*** umekamilika. Aidha, hadi kufikia Aprili 2021, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya ***Kumunazi – Bugene – Kasulo & Kyaka – Mutukula (km 163)*** umekamilika chini ya uratibu wa Sekretariati ya Jumuyia ya Afrika Mashariki. Vilevile, taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya ***Bugene – Burigi Chato National Park (km 60)*** kwa kiwango cha lami zinaendelea.

***62. Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **Barabara ya Isaka – Lusahunga (km 392),** kazi za ukarabati wa sehemu ya ***Isaka – Ushirombo (km 132)*** na ***Ushirombo – Lusahunga (km 110)*** zimekamilika. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya ***Lusahunga – Rusumo & Nyakasanza – Kobero (km 150)*** umekamilika. Aidha, uchambuzi wa zabuni za kumpata Mkandarasi wa kufanya ukarabati wa barabara ya ***Lusahunga – Rusumo (km 92)*** unaendelea. Utekelezaji wa

mradi wa ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi cha Nyakanazi umesimama kutokana na changamoto za kimkataba.

***63. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 259.7)** ujenzi wa barabara umekamilika kwa sehemu ya ***Tabora – Nyahua (km 85), Nyahua – Chaya (km 85.4)*** na ***Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35).***

***64. Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa ajili ya miradi ya **Barabara za Mikoa (km 630.62)** katika mwaka wa fedha 2020/21 ni ukarabati wa jumla ya kilometa **589.31** kwa kiwango cha changarawe, ujenzi wa kilometa **41.31** kwa kiwango cha lami na ujenzi wa madaraja **24**.
Hadi kufikia Aprili 2021, kilometa **54.4** za barabara za mikoa zilikuwa zimekarabatiwa kwa kiwango cha changarawe na kilometa **11.73** zimejengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, ujenzi wa madaraja ulikuwa umekamilika kwa asilimia **5.78.**

***65. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Mwanza/ Shinyanga Border – Mwanza (km 102),** hadi kufikia Aprili 2021, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea kwa ajili ya ukarabati wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

***66. Mheshimiwa Spika,*** katika **mradi wa barabara za kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam**, hadi Aprili, 2021 miradi iliyokamilika ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Mbezi – Malambamawili – Kinyerezi – Banana (km14), Tegeta - Kibaoni - Wazo Hill - Goba - Mbezi (Moro rd, km 20) sehemu ya Mbezi Mwisho – Goba, Tangi Bovu – Goba (km 9), Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.6), Banana – Kitunda – Kivule – Msongola, (km 14.7) sehemu ya Kitunda– Kivule (km 3.2), Ardhi – Makongo – Goba (sehemu ya Goba – Makongo km 4) na Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi/Morogoro Road (sehemu ya Mbezi Mwisho – Goba km 7), Wazo Hill (Madale) – Goba (km 5). Miradi iliyoendelea kutekelezwa hadi Aprili, 2021 ni ujenzi wa barabara ya Ardhi – Makongo – Goba (sehemu ya Ardhi -Makongo km 5) ambao umefikia asilimia 20 na Wazo Hill – Madale Section (km 6) uliofikia asilimia 80. Aidha, katika barabara ya Kibamba – Kisopwa – Kwembe –

Makondeko, ujenzi wa sehemu ya Kibamba – Mloganzila (km 4) umekamilika na usanifu wa kina wa sehemu ya Mloganzila – Makondeko (km1) unaendelea.

Taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa kilometa moja ya barabara ya Goba - Matosa – Temboni (km 6) pamoja na Mjimwema – Kimbiji – Pembamnazi (km 27) zinaendelea. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki (km 9) na Kongowe – Mjimwema – Kivukoni Ferry (km 25.1).

***67. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Nyamuswa – Bunda – Kisorya (km 106),** ujenzi wa barabara ya ***Kisorya – Bulamba (km 51)*** umekamilika. Hadi kufikia Aprili 2021, ujenzi wa barabara ya ***Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 56.4)*** unaendelea na umefikia asilimia 6. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa **Barabara ya Kolandoto – Lalago – Ng'oboko - Mwanhuzi (km 84)** umekamilika na barabara hii itajengwa kwa awamu. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu za ***Kolandoto – Mwanhuzi (km 10)*** na ***Lalago – Ng'oboko – Mwanhuzi (km 74).***

***68. Mheshimiwa Spika,*** ujenzi kwa kiwango cha lami wa **Barabara ya Ndundu – Somanga (km 60)** umekamilika. Aidha, hadi Aprili 2021, utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa **Barabara ya Kasulu – Manyovu** pamoja na barabara za kuingia Kasulu Mjini **(km 68**) ulikuwa unaendelea na umefikia asilimia 3.

***69. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa **Barabara ya Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road Lot1 & 2 (km 112.3),** Makandarasi wa ujenzi wa barabara ya ***Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port (km 52.3)*** na ***Ihumwa Dry Port – Matumbulu – Nala (km 60.0)*** wamepatikana na maandalizi ya ujenzi wa barabara hizi yanaendelea. Aidha, fedha za fidia kwa ajili ya wananchi walioathiriwa na mradi zimepatikana na taratibu za kuanza malipo zinaendelea.
Kwa upande wa barabara ya ***Makulu Jct. – Ntyuka R/About – Image R/About – Bahi R/About (km 6.3)***, hadi kufikia Aprili

2021, mradi huu ulikuwa katika hatua ya usanifu kwa kutumia fedha za msaada kutoka Serikali ya Japan kupitia Shirika la Maendeleo la Japan (JICA). Aidha, taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi wa barabara ya ***Ntyuka Jct. – Mvumi Hospital – Kikombo Jct. (km 76.07)*** zinaendelea na kazi ya usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya ***Kikombo Jct. – Chololo – Mapinduzi (JWTZ HQ) (km 18)*** inaendelea. Vilevile, taratibu za kuanza kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ***Upanuzi wa Barabara Kuu Zinazoingia Katikati ya Jiji la Dodoma (km 220)*** kupitia TECU zilikuwa zinaendelea.

***70. Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2021, kazi za ujenzi kwa mradi wa **Kidatu – Ifakara (km 68)** zilikuwa zinaendelea na zimefikia asilimia 22.3.

***71. Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa **Barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 383)** unaendelea. Hadi Aprili 2021, kazi za ujenzi kwa sehemu ya ***Usesula – Komanga (km 115)*** zilikuwa zimefikia asilimia 76.36 ambapo kilometa 89.8 zimekamilika kwa kiwango cha lami. Kwa sehemu ya ***Komanga – Kasinde (km 120)*** kazi za ujenzi kwa mradi huu zilifikia asilimia 81.08 ambapo kilometa 84.36 zimekamilika kwa kiwango cha lami na kwa barabara ya ***Kasinde – Mpanda (km 118)*** kazi za ujenzi kwa mradi huu zilikuwa zimefikia asilimia 65 ambapo kilometa 52.9 zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami.

***72. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 235**), hadi Aprili 2021, kazi za ujenzi wa barabara ya ***Makutano – Natta (Sanzate) (km 50)*** zilikuwa zimefikia asilimia 87.96 ambapo jumla ya kilometa 28.1 zimekamilika. Kazi za ujenzi kwa barabara ya ***Loliondo – Mto wa Mbu (km 213); Sehemu ya Waso – Sale (km 50)*** zilikuwa zimefikia asilimia 75. Kwa sehemu ya ***Sanzate – Natta (km 40)*** Mkandarasi amepatikana na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya ***Natta – Mugumu (km 45)*** yalikuwa yanaendelea. Aidha, taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya ***Tarime – Mugumu (km 86)*** zinaendelea.

***73. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Ibanda – Itungi Port/Kajunjumele – Kiwira Port (km 66.6),** upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya ***Ibanda – Itungi Port (km 26)*** umekamilika. Maandalizi ya ukarabati wa barabara hii kwa kiwango cha lami yanaendelea. Aidha, kazi za ujenzi wa sehemu ya ***Kikusya – Ipinda – Matema (km 39.1)*** zimekamilika. Vilevile, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya ***Kajunjumele (Iponjola) – Kiwira Port (km 6)*** umekamilika na maandalizi ya ujenzi wa barabara hii yanaendelea. Kuhusu ***Kasumulu/ Songwe – Tanzania/Malawi Border OSBP,*** hadi Aprili 2021, ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja cha Songwe/ Kasumulu unaendelea na umefikia asilimia 58.02.

***74. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Nzega – Tabora (km 289.7),** ujenzi wa sehemu ya ***Nzega – Puge (km 58.6)*** na ***Puge – Tabora (km 56.1)*** umekamilika. Kwa sehemu ya ***Shelui – Nzega (km 110),*** hadi Aprili, 2021 uchambuzi wa zabuni kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na Usanifu wa Kina wa mradi huu uko kwenye hatua za mwisho. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya ***Nzega – Kagongwa (km 65)*** umekamilika na maandalizi ya ujenzi wa barabara hii yanaendelea.

***75. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi (km 432.56),** ujenzi wa sehemu za ***Sumbawanga – Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 151.6), Sitalike – Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 73.65)*** umekamilika. Aidha, Usanifu wa kina wa barabara ya ***Vikonge – Uvinza (km 159)*** umekamilika. Hadi kufikia Aprili 2021, taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi wa sehemu ya barabara hii zilikuwa zinaendelea. Vilevile, usanifu wa kina wa sehemu za ***Kizi – Lyambalyamfipa – Sitalike (km 86.31)*** na ***Kibaoni – Sitalike (km 71.0)*** umekamilika. Hadi kufikia Aprili 2021, taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi wa barabara ya Kibaoni – Sitalike zilikuwa zinaendelea. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya ***Kizi – Lyambalyamfipa – Sitalike (km 86.31)***.

***76. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Nyanguge – Musoma, Mchepuo wa Usagara – Kisesa na Bulamba – Kisorya (km 202.25)** ujenzi wa sehemu ya ***Usagara – Kisesa (Mwanza Bypass, km 16.35)*** na ukarabati wa sehemu ya ***Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85.5)*** umekamilika. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ukarabati wa Barabara ya ***Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 100.4)***. Kuhusu **Barabara ya Magole – Mziha – Handeni (km 149.2),** mradi umekamilika kwa sehemu ya ***Magole – Turiani (km 48.8)*** na usanifu wa kina wa barabara ya ***Turiani – Mziha – Handeni (km 104)*** umekamilika. Hadi kufikia Aprili, 2021, maandalizi ya ujenzi wa barabara hii yalikuwa yanaendelea.

***77. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa **Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyovers) Jijini DSM na Barabara Unganishi** umeendelea kutekelezwa ambapo kazi za ujenzi wa ***Mfugale Flyover*** zimekamilika. Kwa upande wa ***"Interchange" ya Ubungo (Kijazi Interchange),*** hadi kufikia Aprili, 2021, ujenzi wa barabara za juu kwenye makutano ya Ubungo umekamilika. Aidha, ujenzi wa kituo cha maegesho ya Mabasi ya Mwendo Kasi kinachojengwa eneo lililokuwa kituo cha mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani cha Ubungo unaendelea. Vilevile, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi wa ***Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyovers) kwenye Makutano Nane (8) ya Barabara za Jijini Dar es Salaam (Mwenge, Morocco, Magomeni, Selander, Fire, Osterbay, Buguruni, Tabata)*** zimekamilika. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za utekelezaji wa mradi wa ***Ujenzi wa Mabey Flyovers Jijini Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza.***

***78. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (km 181.8),** mradi umekamilika kwa sehemu za ***Bariadi – Lamadi (km 71.8), Mwigumbi – Maswa (km 50.3)*** na ***Maswa – Bariadi (km 49.7***). Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya ***Isabdula (Magu) – Bukwimba Station – Ngudu – Ng'hungumalwa (km 10)*** umekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hii.

***79. Mheshimiwa Spika,*** upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa **Barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa (*Sehemu ya Ipole – Rungwa, km 172)*** umekamilika. Hadi kufikia Aprili 2021, maandalizi ya ujenzi wa barabara hii yalikuwa yanaendelea.

***80. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 341.25),** ujenzi wa barabara ya ***Kidahwe – Kasulu (km 63.0)*** umekamilika. Kwa upande wa barabara ya ***Nyakanazi – Kakonko (Kabingo) (km 50),*** kazi za ujenzi wa barabara hii zimekamilika kwa kiwango cha lami na ujenzi wa daraja unaendelea. Aidha, utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa sehemu ya ***Kanyani Junction – Mvugwe (km 70.5), Mvugwe – Nduta Junction (km 59.35), Kibondo Junction – Kabingo (km 62.5)*** na ***Nduta Junction – Kibondo (km 25.9)*** unaendelea. Vilevile, taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi wa barabara ya ***Kibondo – Mabamba (km 35)*** kwa kiwango cha lami kwa kuanzia na sehemu yenye urefu wa kilometa 10 zinaendelea.

***81. Mheshimiwa Spika,*** kazi za ujenzi wa **Barabara ya Kwenda Kiwanja cha Ndege cha Mafia (Mafia Airport Access Road, km 16)** zimekamilika.

***82. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa **Dodoma University Road (km 16.5),** kazi za ujenzi wa barabara ***Ihumwa – Chuo Kikuu cha Dodoma (km 12.0)*** na ***Barabara za Ikulu ya Chamwino (km 4.5)*** zimekamilika.

***83. Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa ujenzi wa **Daraja la Nyerere (Kigamboni) na Barabara Unganishi,** ujenzi wa ***Daraja la Nyerere*** na barabara ya ***Kigamboni (Daraja la Nyerere) – Vijibweni (km 1.5)*** umekamilika. Kwa sehemu ya ***Tungi – Kibada (km 3.8)*** Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya ***Kibada – Mwasonga – Tundwisongani Jct/Tundwisongani – Kimbiji (km 41.0)*** umekamilika. Hadi Aprili 2021, maandalizi ya ujenzi wa barabara hizi yalikuwa yanaendelea.

***84. Mheshimiwa Spika,*** katika barabara ya **Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 112),** taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina zinaendelea kwa sehemu ya ***Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 112), Bukoba Mjini – Busimbe – Maruku – Kanyangereko – Ngongo (km 19.10)*** na ***Kanazi (Kyetema) – Ibwera – Katoro – Kyaka II (km 60.7).***

***85. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ***Ujenzi wa Njia za Magari Mazito na Maegesho ya Dharura Katika Barabara Kuu za Ukanda wa Kati (Providing Lane Enhancement Including Climbing Lanes, Passing Bays, Rest And Emergency Lay Bays On Central Corridor)*** umepangwa kujumuishwa kwenye usanifu wa kina kabla ya kufanya ukarabati wa barabara za ukanda wa kati zilizopangwa kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambazo ni Morogoro – Dodoma (km 260), Singida – Shelui (km 110) na Shelui – Nzega (km 110) ambazo ziko katika hatua za manunuzi za kupata Wahandisi Washauri.

***86. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa upanuzi wa **Barabara ya Kimara – Kibaha (km 19.2) Ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**, ujenzi wa barabara hii unaendelea kwa kuanzia Kimara Mwisho hadi Kibaha mkoani Pwani. Hadi Aprili, 2021 mradi umefikia asilimia 87.38. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa **Barabara ya Kisarawe – Mlandizi (km 119)** kwa kiwango cha lami.

***87. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ujenzi wa **Barabara ya Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34.0)**, hadi kufikia Aprili, 2021 kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za ***Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 21.3)*** na ***Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho (km 12.7)*** hazijaanza. Serikali inaendelea kutafuta fedha za kufanya kazi hizi.

***88. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Kagoma – Lusahunga (km 172.5)**, hadi kufikia Aprili 2021, ujenzi wa barabara ***Kagoma – Lusahunga (km 154)*** na ***Muleba –***

***Kanyambogo – Rubya (Leopord Mujungi km 18.5)*** umekamilika.

***89. Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa ujenzi wa **Barabara ya Singida – Shelui (km 110),** hadi Aprili, 2021, taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***90. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road) – Gerezani (Sehemu ya Kamata – Bendera Tatu Km 1.3)** hadi Aprili, 2021 kazi za ***Upanuzi wa Daraja la Gerezani (km 1.3)*** zilikuwa zimefikia asilimia 78.8. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya ***Mbagala Rangi Tatu – Kongowe (km 3.8)*** umekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha za upanuzi na ukarabati wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

***91. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Msimba – Ruaha Mbuyuni/Ikokoto Mafinga (km 535.25)** ujenzi wa barabara ya ***Igawa – Mbarali – Ubaruku; sehemu ya Mbarali – Ubaruku (km 8.9)*** umekamilika. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2021, taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi wa sehemu ya ***Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152.0)*** zinaendelea. Vilevile, kazi za ukarabati kwa sehemu ya ***Mafinga – Igawa (km 137.9)*** na usanifu wa kina wa sehemu ya ***Mafinga – Mgololo (km 78.0)*** umekamilika. Kuhusu barabara ya ***Morogoro – Iringa (Tumbaku Jct. Mangae/Melela –Mikumi – Iyovi) (km 158.45),*** hadi kufikia Aprili, 2021, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati zinaendelea.

***92. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Same – Mkumbara – Korogwe (km 147.5),** upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu za ***Same – Himo (km 76.0), Mombo – Lushoto (km 32.0) na Lushoto – Magamba – Mlola (km 34.5)*** umekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara hizi.

Kwa upande wa barabara ya ***Same – Kisiwani – Mkomazi (km 97);*** upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa ***sehemu***

***ya Same – Kisiwani (km 5.0)*** umekamilika. Hadi kufikia Aprili 2021, maandalizi ya ujenzi wa barabara hii yalikuwa yanaendelea.

***93. Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **Barabara ya Mbeya – Makongolosi (km 267.90),** kazi za ujenzi zimekamilika kwa sehemu za ***Mbeya – Lwanjilo – Chunya (km 72).*** Kwa upande wa sehemu ya ***Chunya – Makongolosi (km 39)*** ujenzi unaendelea na umefikia asilimia 85 ambapo kilometa 38 zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami.

Vilevile, taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi wa barabara ya ***Noranga – Itigi – Mkiwa (km 56.9)*** zinaendelea. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa barabara ya ***Makongolosi – Rungwa – Noranga (km 356)*** na ***Mbalizi – Makongolosi (km 50)*** kwa kiwango cha lami.

***94. Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (km 211),** kazi za ujenzi kwa sehemu ya ***Lusitu – Mawengi (km 50)*** zinaendelea na zimefikia asilimia 68.54 ambapo kilometa 26.9 zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha zege. Aidha, hadi kufikia Aprili 2021, taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi wa sehemu ya barabara ya ***Itoni – Lusitu (km 50)*** zilikuwa zinaendelea.

***95. Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2021, kazi za ujenzi wa **Daraja Jipya la Selander (Tanzanite)** zilikuwa zimefikia asilimia 72.8 na ujenzi unaendelea. Aidha, katika mradi wa **Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (km 460)**, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Handeni - Kibirashi – Kibaya - Singida (km 460) imekamilika. Taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi wa sehemu ya barabara hii zinaendelea.

***96. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Makambako – Songea na Barabara ya Mzunguko ya Songea (km 295)**, hadi kufikia Aprili 2021, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea kwenye barabara ya mchepuo ya Songea. Aidha, Benki ya Dunia imeonesha nia ya kugharamia

ukarabati wa barabara ya Makambako – Songea, kupitia mradi ujulikanao kama "Development Corridor Transport Programme".

***97. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ujenzi wa **Barabara ya Dodoma – Iringa (km 273.3),** hadi kufikia Aprili 2021, ujenzi kwa kiwango cha lami wa meta 450 za ***Barabara ya Mchepuo wa Iringa (km 7.3)*** ulikuwa umekamilika. Aidha, kazi za uimarishaji wa matabaka katika barabara ya ***Iringa – Dodoma (km 266)*** zilikuwa zimefikia asilimia 45.

***98. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa **Barabara ya Dodoma – Babati (km 266.3)** umekamilika kwa sehemu ya ***Dodoma – Mayamaya – Mela – Bonga – Babati (km 250.8).*** Aidha, hadi kufikia Aprili 2021, upembuzi yakinifu wa barabara ya ***Mchepuo wa Babati (Babati Bypass)*** yenye urefu wa kilometa 15.5 umekamilika na usanifu wa kina unaendelea.

***99. Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 258.2)** umekamilika. Kwa upande wa sehemu ya ***Kitai – Lituhi (km 90),*** hadi kufikia Aprili 2021, taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya barabara hii na daraja la Mnywamaji zinaendelea.

***100. Mheshimiwa Spika,*** usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa **Barabara za Chuo cha Uongozi (Uongozi Institute, km 8.8)** umekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

***101. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara za Igawa – Songwe – Tunduma na Mchepuo wa Mbeya (km 273.40),** hadi kufikia Aprili 2021, upembuzi yakinifu wa barabara ya ***Igawa – Songwe – Tunduma (km 218.0)*** na ***Uyole – Songwe (Mbeya Bypass, km 48.9)*** umekamilika na usanifu wa kina unaendelea. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya ***Iwambi – Mbalizi Bypass (km 6.5)*** kwa kiwango cha lami.

***102. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa **Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili Hadi Tano (BRT Phase II – V: km 69.8),** kazi za ujenzi wa barabara ya ***Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili (CBD – Mbagala, km 20.3),*** chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) zinaendelea. Hadi Aprili, 2021 kazi za ujenzi zilikuwa zimefikia asilimia 11.82. Aidha, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya ***Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tatu (CBD – Gongolamboto & Mwenge – Tegeta (km 23.6)*** chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Aidha, maandalizi ya ujenzi wa BRT Awamu ya IV zinaendelea. Kuhusu ***Maboresho ya Barabara za BRT Awamu ya Kwanza (Jangwani)***, hadi kufikia Aprili 2021, kazi ya usanifu wa kina kwa ajili ya kujenga daraja la juu pamoja na tuta katika eneo la Jangwani zinaendelea chini ya Mradi wa Maboresho ya Usafiri Dar es Salaam (DUTP) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Aidha, mradi wa ***Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tano*** unahusisha ujenzi wa barabara ya Bandari ya Dar es Salaam - Mandela – Kawawa – Kigogo – Tabata – Segerea (km 26.5). Hadi kufikia Aprili 2021, kazi ya usanifu wa kina imekamilika. Aidha, Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) kupitia Benki ya Dunia wameonesha nia ya kugharamia mradi huu.

***103. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa **Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT),** hadi Aprili, 2021, maandalizi ya Mpango Kabambe (*Master Plan*) pamoja na usanifu wa awali wa Jengo la Makao Makuu ya ICoT Morogoro yanaendelea.

***104. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara,** kazi zinaendelea na mradi umefikia asilimia 38.

***105. Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya barabara kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2020/21 katika Barabara Kuu kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina

wa kilometa **7,032.9** za barabara. Hadi Aprili, 2021 utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

***i. Barabara ya Musoma – Makojo – Busekela (km 92)***
Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika.

***ii. Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Mto Sibiti – Lalago – Maswa (km 389)***
Upembuzi yakinifu wa barabara hii umekamilika.

***iii. Kuimarisha Uwezo wa Maabara (Central Material Labolatory – Cml) Katika Kupima Vifaa vya Ujenzi na Kuanzisha Teknolojia ya Kisasa ya (Asphalt Mix Design)***
Kazi ya kuimarisha uwezo wa maabara ya vifaa vya ujenzi na mafunzo mbalimbali kwa ajili ya utumiaji wa Mwongozo wa uchanganyaji ya lami zilikuwa zinaendelea.

***iv. Mifumo ya Kompyuta (Software) kwa Ajili ya Usanifu wa Barabara na Kuandaa Mipango ya Usafiri (Highway /Transport Planning)***
Taratibu za ununuzi wa mifumo ya kompyuta kufanya tathmini za kiuchumi (HDM 4) na leseni za kutumia mfumo wa usanifu wa kina (MIDAS) zinaendelea.

***v. Barabara ya Mpanda – Ugalla – Kaliua – Ulyankulu – Kahama (km 457)***
Mkataba umesainiwa na kazi za upembuzi yakinifu zinaendelea.

***vi. Barabara ya Ipole – Rungwa (km 172)***
Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika.

***vii. Barabara ya Mtwara Pachani – Lusewa – Lingusenguse – Nalasi (km 211)***
Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika.

***viii. Barabara ya Arusha – Kibaya – Kongwa (km 430)***
Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika.

***ix. Barabara ya Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 342)***
Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kilometa 100 za barabara hii umekamilika.

***x. Kuboresha Eneo la Mlima Kitonga (km 10)***
Hadi kufikia Aprili, 2021, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xi. Barabara ya Babati (Dareda) – Dongobeshi (km 60)***
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xii. Barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe (km 70)***
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xiii. Barabara ya Kibaoni – Majimoto – Inyonga (km 152)***
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xiv. Barabara ya Kiranjeranje – Namichiga - Ruangwa (km 120)***
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika.

***xv. Barabara ya Masaninga – Matandu – Nangurukuru – Kilwa Masoko (km 55)***
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika.

***xvi. Barabara ya Sabasaba – Sepuka – Ndago – Kizaga (km 77)***
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xvii. Barabara ya Singida Mjini – Ilongero – Haydom (km 93)***
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xviii. Barabara za Mkiu - Liganga - Madaba (km 1112); Liganga - Nkomang'ombe (km 70) na Nkomang'ombe - Coal Power Plant (km 4.14)***

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika.

***xix. Barabara ya Mkuyuni – Nyakato (km 10)***

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xx. Barabara ya Tarime – Mugumu (km 86)***

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika.

***xxi. Barabara ya Morogoro (Tumbaku Roundabout) – Mangae/Melela – Mikumi – Iyovi (km 156.45) na Daraja la Doma***

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxii. Barabara ya Mbulu – Magugu (Mbuyu wa Mjerumani) (km 63)***

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxiii. Barabara ya Morogoro (Msamvu Roundabout) – Morogoro Centre – Bigwa Junction (km 10)***

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxiv. Barabara ya Buhongwa – Igoma (km 12)***

Mradi huu unatekelezwa na TARURA chini ya Benki ya Dunia.

***xxv. Barabara ya Omurushaka – Murongo (km 125)***

TECU wanaendelea na usanifu wa awali kwa ajili ya kujenga sehemu ya Kyerwa – Omurushaka (km 50) kwa kiwango cha lami kwa utaratibu wa Sanifu na Jenga.

***xxvi. Barabara ya Simanjiro (Orkesumet) – Kia – Mererani (Part of Kongwa Ranch – Kiteto – Simanjiro – Kia (km 60)***

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxvii. Barabara ya Babati – Orkesumet – Kibaya (km 255)***

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxviii. Barabara ya Singida Bypass (km 46)***

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxix. Barabara ya Songea Bypass (km 11)***

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxx. Barabara ya Nyakato – Veta – Buswelu (km 3)***

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxxi. Daraja la Godegode (meta 70) na Barabara za Maingilio (km 6) Kati ya Barabara ya Mpwapwa – Makutano na Pwaga – Lumuma***

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxxii. Barabara ya Mlandizi – Chalinze (km 44)***

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxxiii. Barabara ya Salawe – Old Shinyanga (km 64.70)***

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxxiv. Barabara ya Mbezi Mwisho Interchange na Kuunganisha Barabara za Kuingia na Kutoka Katika Mradi wa Kituo Kikuu cha Mabasi ya Nje na Mikoani***

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika.

***xxxv. Barabara ya Mpwapwa - Gulwe - Rudi - Chipogoro; Sehemu ya Kibakwe - Chipogoro (km 75.84)***

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxxvi. Barabara ya Kihansi – Mlimba – Madeke (km 220.22)***
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea kwa kutumia fedha za mkopo nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

***xxxvii. Barabara ya Ntendo – Muze – Kilyamatundu (km 200)***
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxxviii. Barabara ya Mbamba Bay – Lituhi (km 121)***
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxxix. Barabara ya Nangurukuru - Liwale (km 210)***
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xl. Barabara ya Ushirombo – Nyikonga – Geita (Katoro) (km 59)***
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xli. Barabara ya Makete – Ndulamo – Nkenja – Kitulo (km 42)***
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xlii. Barabara ya Ngopito - Kimotorok - Singe (Babati) (km 145)***
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xliii. Barabara ya Goba - Matosa - Temboni/Morogori Road Jct And Makabe/Mbezi Mwisho - Goba Jct - Msakuzi (km 15)***
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xliv. Barabara ya Magu – Bukwimba - Ngudu - Hungumalwa (km 64)***
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xlv. Barabara ya Mbalizi - Mkwajuni (Galula – Mkwajuni - Makongolosi (km 61)***
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xlvi. Barabara ya Utete - Nyamwage (km 34)***
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika.

***xlvii. Barabara ya Mwanza Urban Along Mwanza - Nyanguge (km 25)***
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xlviii. Upanuzi wa Barabara ya Arusha - Kisongo (km 8.8)***
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xlix. Barabara ya Airport – Igombe - Nyanguge (km 46)***
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***l. Barabara ya Namanyere - Katongoro - New Kipili Port (km 64.8)***
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***li. Barabara ya Kagwira - Ikola – Karema (km 112)***
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***lii. Barabara ya Bariadi – Kisesa – Mwandoya – Ngoboko – Mwanhuzi – Sibiti –Mkalama – Iguguno (Sehemu ya Mkalama – Iguguno) (km 89)***

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***liii. Barabara ya Bariadi – Salama - Ng'haya - Magu (km 76)***

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

**Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko**

***106. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) iliendelea kutekeleza miradi ya ***ujenzi na ukarabati wa maegesho ya vivuko.*** Hadi Aprili, 2021 upanuzi wa jengo la abiria katika maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni Jijini Dar es Salaam ulikuwa katika hatua za mwisho. Vilevile, ujenzi wa miundombinu (jengo la abiria, ofisi na uzio) katika vituo kumi (10) vya vivuko uko katika hatua za manunuzi. Aidha, ujenzi wa maegesho ya Bukondo na Zumacheli katika kivuko cha Chato – Nkome upande wa Bukondo umekamilika na upande wa Zumacheli upo katika hatua za manunuzi. Ujenzi wa maegesho ya Nyamisati – Mafia umekamilika upande wa Nyamisati na upande wa Mafia ujenzi unaendelea kwa kutekelezwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).
Ukarabati wa maegesho ya vituo vinne (4) vya vivuko (Bugolora - Ukara, Rugezi - Kisorya, Nyakarilo - Kome na Kigongo – Busisi) umekamilika na maegesho ya Iramba – Majita yapo katika hatua za manunuzi. Aidha, maegesho ya Kayenzi - Kanyinga na Muleba – Ikuza yapo katika hatua ya upembuzi yakinifu.

***107. Mheshimiwa Spika***, katika miradi ya ***ununuzi wa vivuko,*** hatua iliyofikiwa hadi Aprili, 2021, ujenzi wa vivuko vipya vya Nyamisati – Mafia, Chato - Nkome na Bugolora - Ukara

umekamilika na vinafanya kazi. Aidha, ujenzi wa kivuko kipya cha Kisorya – Rugezi na ununuzi wa *fiber* boti mpya moja (1) kwa ajili ya kivuko cha Utete – Mkongo upo katika hatua za manunuzi. Ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA kwa ajili ya kuboresha huduma ya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo ya Serikali utafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

***108. Mheshimiwa Spika*****,** kuhusu miradi ya ***Ukarabati wa Vivuko,*** iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/21, hadi Aprili, 2021 ukarabati mkubwa wa vivuko vya MV Kigamboni na MV Sengerema umekamilika na vivuko vinafanya kazi. Ukarabati wa MV Tegemeo, MV KIU na MV Misungwi unaendelea. Aidha, miradi ya ukarabati wa vivuko vya MV Musoma, MV Mara, MV Ujenzi, MV Kome II, MV Nyerere na MV Kilombero II ipo katika hatua mbalimbali za manunuzi.

**Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali**

***109. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) iliendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali.

***110. Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili, 2021, kazi za ujenzi wa nyumba 5 za Majaji katika mikoa ya Kilimanjaro, Shinyanga, Mtwara, Dar es Salaam na Tabora zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, kazi za ukamilishaji (finishing) wa nyumba za makazi Magomeni Kota zilikuwa zinaendelea. Kwa ujumla, utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa nyumba za Magomeni Kota umefikia asilimia 94. Vilevile, ukarabati wa nyumba za Viongozi 272 Dodoma, 82 Dar es Salaam na 130 za watumishi wa umma mikoani zilizohamishiwa TBA toka TAMISEMI katika Mikoa 20 unaendelea ukiwa katika hatua za ukamilishaji.

Mradi mwingine uliotekelezwa ni ujenzi na ukarabati wa karakana za TEMESA na TBA ambapo, hadi Aprili, 2021 ujenzi

wa karakana ya Wilaya ya Same Mkoa wa Kilimanjaro na ukarabati wa karakana za samani TBA Dodoma umekamilika. Aidha, ujenzi wa karakana ya TEMESA Mkoa wa Simiyu na ukarabati wa karakana za TEMESA mikoa ya Dodoma, Mwanza, Mbeya, Singida na Dar es Salaam ulikuwa unaendelea.

**Usalama Barabarani na Mazingira**

***111. Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu ina jukumu la kuratibu shughuli za usalama barabarani na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara zetu. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara ilipanga kutekeleza mradi wa ufungaji (installation) wa vifaa vya kisasa vya upimaji (load cells) katika mizani 42 iliyopo katika shoroba zote za Barabara Kuu hapa nchini. Mizani hiyo ni Vigwaza, Mikese, Mikumi, Wenda, Makambako, Uyole, Mpemba, Dakawa, Nala, Njuki, Kazegunga, Mwendakulima na Mutukula. Mizani zingine ni Makuyuni, Himo, Pongwe, Sirari, Horohoro, Usagara, Tinde, Kyamyorwa, Makofia, Mkuranga, Mingoyo, Nangurukuru, Kurasini, Luhimba na Lupokela. Mizani nyingine ni Sisi kwa Sisi, Itigi, Puge, Mbanga, Nyakahura, Kyaka, Rubana, Matai, Kanondo, Msata, Kwachaga, Misima, Nkangamo na Nyakabindi. Hadi Aprili, 2021 utekelezaji wa mradi huu kwa ujumla umefikia asilimia 20.

***112. Mheshimiwa Spika,*** mradi mwingine uliopangwa kutekelezwa ni uwekaji wa mfumo wa uangalizi wa utendaji kazi (CCTV Weighbridge Management System) katika mizani arobaini na mbili (42). Hadi Aprili, 2021, Wizara ilikuwa katika hatua za mwisho za manunuzi ya kumpata Mtaalam Ushauri atakayefanya usimikaji wa mfumo huo. Vilevile, Wizara ilipanga kutekeleza ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi (One Stop Inspection Station - OSIS) kwa vituo vya Idofi Mkoani Njombe na Iboya Mkoani Songwe ambapo usanifu wa kina umekamilika na uthamini wa kubaini fidia umefanyika. Taratibu za malipo ya fidia zinafanyika.

***113. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu miradi ya mazingira, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 katika Sekta ya Ujenzi. Kazi

zilizopangwa katika mwaka 2020/21 ni kuandaa mfumo wa kusimamia mazingira na kutoa elimu ya weledi wa usimamizi wa mazingira hususan utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 kwa menejimenti ya Wizara na kuandaa programu za udhibiti wa uchafuzi wa mazingira katika sekta (Sectoral Pollution Control Programme).

Hadi Aprili, 2021 utekelezaji wa mradi huu upo katika hatua mbalimbali. Kazi zilizofanyika ni uandaaji wa hadidu za rejea kwa ajili ya kuwapata wataalam Washauri, kujumuisha maoni ya wadau kwa ajili ya kuanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Mazingira na kukamilisha mahitaji ya mafunzo ya usimamizi wa mazingira.

**MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA VIWANJA VYA NDEGE**

***114. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara kupitia TANROADS imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya ndege kama ifuatavyo:

***115. Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa ujenzi wa **Kiwanja cha *Ndege* cha Kigoma,** kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2020/21 ni ujenzi wa Jengo la Abiria pamoja na miundombinu (maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani), usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege, kujenga uzio, ujenzi wa jengo la kuongozea ndege na ujenzi wa jengo la uchunguzi wa hali ya hewa. Hadi Aprili, 2021 taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi zilikuwa zinaendelea.

***116. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa **Kiwanja cha Ndege cha Mpanda** umekamilika**.** Lengo la mwaka 2020/21 lilikuwa ni ujenzi wa uzio. Kazi hiyo imekamilika.

***117. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Songwe,** lengo la mwaka 2020/21 lilikuwa ni kumalizia ujenzi wa Jengo la Abiria na mifumo yake, usimikaji wa taa za kuongozea ndege na ukarabati wa tabaka la juu la barabara ya kutua na kuruka ndege na barabara ya

kiungio, ujenzi wa uzio wa usalama pamoja na ukarabati wa eneo la usalama kwenye barabara ya kutua na kuruka ndege (Runway End Safety Area-RESA).

Hadi Aprili, 2021, ukarabati wa tabaka la juu la barabara ya kutua na kuruka ndege na barabara ya kiungio, ujenzi wa uzio wa usalama pamoja na ukarabati wa eneo la usalama (Runway End Safety Area - RESA) umefikia asilimia 10. Utekelezaji wa mradi wa kusimika taa za kuongozea ndege unaendelea. Mkandarasi kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa jengo la abiria amepatikana na mkataba umesainiwa.

***118. Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Tabora,** lengo la mradi lilikuwa ni ujenzi wa Jengo la Abiria na miundombinu yake, jengo la kuongozea ndege, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari, uzio wa usalama pamoja na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa. Hadi Aprili, 2021 taratibu za kibenki zilikuwa zinaendelea kwa ajili ya kupata fedha za mradi kutoka kwa Mfadhili ambaye ni Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (European Investment Bank – EIB) ili utekelezaji uweze kuanza.

***119. Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga,** lengo la mradi lilikuwa ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege pamoja na ujenzi wa uzio wa usalama. Hadi Aprili, 2021 taratibu za kibenki zilikuwa zinaendelea kwa ajili ya upatikanaji wa fedha za mradi kutoka kwa Mfadhili ambaye ni Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (European Investment Bank – EIB) ili utekelezaji uweze kuanza.

***120. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga,** kazi zilizopangwa ni ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, uzio wa usalama, barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari. Kazi nyingine ni

usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege. Hadi Aprili, 2021 taratibu za kibenki zilikuwa zinaendelea kwa ajili ya upatikanaji wa fedha za mradi kutoka kwa mfadhili ambaye ni Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (European Investment Bank – EIB) ili utekelezaji uweze kuanza.

***121. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **Kiwanja cha Ndege cha Mwanza,** kazi zilizopangwa ni ujenzi wa Jengo jipya la Abiria na mifumo yake na ujenzi wa uzio wa usalama.

Hadi Aprili, 2021, kazi ya ujenzi wa uzio wa usalama umekamilika kwa asilimia 98 na asilimia 2 ni maeneo korofi yaliojaa maji ambayo yatakamilishwa mvua zikipungua. Usanifu wa Kina wa jengo jipya la abiria umekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

***122. Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Arusha,** kazi zilizopangwa ni kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege kwa meta 200 na ujenzi wa maeneo ya kugeuzia ndege (Turning Pad). Ujenzi wa uzio wa usalama, kujenga barabara mpya ya kuingilia kiwanjani pamoja na kukarabati maegesho ya magari. Mradi huu umekamilika.

***123. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Mtwara,** kazi zilizopangwa ni kufanya ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio vyake pamoja na maegesho ya ndege. Kazi zingine ni kusimika taa na mitambo ya kuongozea ndege, ujenzi wa barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari na ujenzi wa uzio wa usalama.
Hadi Aprili, 2021 ujenzi unaendelea na umekamilika kwa asilimia 55.

***124. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, katika mradi wa **Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa** kazi zilizopangwa zilikuwa ni pamoja na ujenzi wa viwanja vya ndege katika mikoa ya Geita, Iringa, Ruvuma (Songea), Lindi, Kiwanja kipya cha Simiyu, kiwanja cha Lake Manyara, Tanga, Moshi, Lindi na Mara (Musoma). Aidha, kazi

nyingine ni ujenzi wa uzio wa usalama pamoja na barabara ya kufanyia ukaguzi kwenye kiwanja cha ndege cha Dodoma.

***125. Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2021, ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio, maegesho ya ndege kwenye kiwanja cha ndege cha Geita umefikia asilimia 95; Mkataba kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Iringa awamu ya kwanza umesainiwa na Mkandarasi ameanza utekelezaji wa mradi huo. Aidha, kazi za ujenzi katika kiwanja cha ndege cha Songea kwa ujumla zimefikia asilimia 95. Utekelezaji wa miradi ya viwanja vya ndege vya Lindi na Simiyu unasubiri upatikanaji wa fedha.

Kwa kiwanja cha ndege cha Musoma mkoani Mara, Mkandarasi amepatikana na mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 28 Machi 2021. Aidha, ulipaji wa fidia unaendelea. Taratibu za manunuzi ya Makandarasi kwa ajili ya ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Moshi zipo kwenye hatua za awali; upanuzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege awamu ya pili kwenye kiwanja cha ndege cha Dodoma umekamilika na taratibu za kuanza manunuzi ya Makandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja cha Tanga, Iringa (Awamu ya Pili) na Lake Manyara zinasubiria kukamilika kwa taratibu za mkopo kutoka kwa mfadhili (Benki ya Dunia).

***126. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa ujenzi wa **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato**, kazi zilizopangwa ni ujenzi wa kiwanja kipya cha Msalato mkoani Dodoma. Aidha, kazi nyingine ni kulipa fidia kwa wakazi watakaoathiriwa na utekelezaji wa mradi huu.

Hadi Aprili, 2021, taratibu za manunuzi ya kuwapata Makandarasi wa ujenzi na Washauri Elekezi ziko katika hatua za mwisho na zoezi la ulipaji fidia lilikuwa linaendelea.

***127. Mheshimiwa Spika,*** katika **Kiwanja cha Ndege cha Bukoba,** kazi zilizopangwa ni ujenzi wa jengo la Watu Mashuhuri (VIP Lounge), ukarabati wa meta 200 za barabara

ya kuruka na kutua ndege pamoja na usimikaji wa taa za kuongozea ndege. Hadi Aprili, 2021 utekelezaji wa mradi huu unasubiri upatikanaji wa fedha.

***128. Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa ujenzi wa **Jengo la Tatu la Abiria (Terminal III)** katika **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA),** lengo lilikuwa ni kulipa fedha za madeni kwa ajili ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi wa jengo jipya la abiria (Terminal III) pamoja na miundombinu yake wakati wa kipindi cha uangalizi wa mradi. Kazi nyingine ni kulipa fidia kwa wakazi wa Kipunguni na wale wa Kigilagila kwa ajili ya wananchi waliohamishwa kupisha utekelezaji wa mradi huu. Aidha kazi nyingine ni kufanya Usanifu wa Kina wa Jengo la Pili (Terminal II) la abiria.

Mradi wa ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria (Terminal III) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) umekamilika. Kazi za Usanifu wa Kina wa Jengo la Pili (Terminal II) la abiria zinasubiri upatikanaji wa fedha.

## UTENDAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA UJENZI

### Bodi ya Mfuko wa Barabara

***129. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Mfuko wa Barabara ulitarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 916,780,529,000** kwa ajili ya kugharamia kazi za matengenezo na maendeleo ya barabara. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 641,746,370,000** zilikuwa ni kwa ajili ya kugharamia kazi za matengenezo na maendeleo ya barabara za Kitaifa (Barabara Kuu na Barabara za Mikoa) kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Aidha, kiasi cha **Shilingi 275,034,159,000** zilitengwa kwa ajili ya kugharamia kazi za matengenezo na maendeleo ya barabara za Wilaya kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Kati ya fedha hizo, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) ilitengewa **Shilingi 63,622,735,121.80,** Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilitengewa **Shilingi 27,266,886,523.26,** TANROADS ilitengewa **Shilingi 572,604,616,096.20,** TARURA ilitengewa Shilingi **245,401,978,709.34** na **Shilingi 7,884,312,549.40** zilitengwa kwa ajili ya kugharamia uendeshaji wa Bodi ya Mfuko wa Barabara.

***130. Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2021 Bodi imekusanya na kugawanya jumla ya **Shilingi 716,813,813,708** sawa na asilimia **78.19** ya bajeti ya mwaka. Kati ya hizo, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) ilipokea **Shilingi 49,745,445,017,** Ofisi ya Rais – TAMISEMI **Shilingi 21,289,561,708,** TANROADS **Shilingi 447,709,005,153,** TARURA **Shilingi 191,888,410,676** na Bodi ya Mfuko wa Barabara **Shilingi 6,189,381,154.**

***131. Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2021, Bodi imekamilisha andiko kwa ajili ya mapendekezo ya kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato vya Mfuko wa Barabara. Mapendekezo hayo yanaendelea kufanyiwa kazi na Serikali. Aidha, Bodi kupitia Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC) inaandaa makisio ya gharama za kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara (*unit cost estimations*). Kukamilika kwa kazi hiyo kutaiwezesha Bodi pamoja na Wakala wa Barabara kupanga mipango yake kikamilifu na pia itakuwa msingi wa majadiliano kati ya Wakala na Makandarasi juu ya gharama ya kazi za barabara.

Vilevile, Bodi iliendelea na ufuatiliaji wa ukusanyaji wa fedha za Mfuko kutoka vyanzo mbalimbali ili kuhakikisha ukusanyaji unafanyika kikamilifu. Aidha, Bodi iliendelea kufanya ukaguzi wa ubora wa kazi za matengenezo ya barabara kwa kutumia wataalam wa ndani na nje ili kupata thamani halisi ya fedha.

**Wakala wa Majengo Tanzania**

***132. Mheshimiwa Spika*****,** majukumu makuu ya Wakala wa Majengo Tanzania ni usimamizi na uendeshaji wa miliki za Serikali ikiwa ni pamoja na kupata viwanja kwa matumizi ya Serikali, kujenga nyumba za Serikali, kutunza nyumba na majengo ya Serikali, kujenga na kuwauzia Watumishi wa Serikali nyumba za kuishi, kuwapangishia Watumishi wa umma nyumba za Serikali na kupangisha baadhi ya nyumba hizo kibiashara. Aidha, Wakala unasimamia miradi ya ujenzi na kutoa huduma ya ushauri kwa majengo ya Serikali.

***133. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu ya Wakala yaliyopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2020/21, hadi kufikia Aprili, 2021, ujenzi wa nyumba za makazi

yenye uwezo wa kubeba kaya 656 - Magomeni Kota - Dar es Salaam ulikuwa unaendelea na ulifika asilimia 94 ya utekelezaji. Ukarabati wa karakana ya Wakala Dodoma umekamilika na ukarabati wa nyumba za viongozi 272 Dodoma, 82 Dar es Salaam na 130 za watumishi wa umma mikoani zilizohamishiwa TBA toka TAMISEMI katika mikoa 20 unaendelea. Kazi nyingine ni kuendelea na ukarabati wa nyumba 28 ambapo ukarabati umekamilika kwa nyumba 13 na nyumba 15 zinaendelea na ukarabati. Aidha, ujenzi wa nyumba 4 kati ya nyumba 100 za watumishi wa umma Dodoma unaendelea.

***134. Mheshimiwa Spika,*** Wakala vilevile umeendelea kutekeleza miradi ya ukarabati iliyohusisha ukarabati wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Tabora na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora ambayo utekelezaji wake umekamilika na ukarabati wa nyumba tano za viongozi wa Serikali Wilaya za Mwanga na Same umekamilika. Vilevile, ukarabati wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Iringa umefikia asilimia 80.

***135. Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa na Wakala ni Miradi ya Ubunifu na Ujenzi ambapo jumla ya miradi 53 imetekelezwa. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa Jengo la ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Butiama ambao umefikia asilimia 47, ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara ambao umefikia asilimia 40, ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mkalama ambao umefikia asilimia 51, ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ubungo ambao umefikia asilimia 98, Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Busega ambao umefikia asilimia 95, ujenzi wa majengo ya hospitali ya rufaa Geita na Chato ambao umefikia asilimia 91 awamu ya kwanza na asilimia 38 awamu ya pili ya utekelezaji, ujenzi wa mradi wa jengo la ofisi la makao makuu ya TANROADS –Dodoma ambao umefikia asilimia 38. Aidha, ujenzi wa nyumba ya Rais Mstaafu Jakaya Kikwete umekamilika.

***136. Mheshimiwa Spika,*** vilevile Wakala umetekeleza jumla ya miradi 45 ya ujenzi. Baadhi ya miradi hiyo ni ujenzi wa Jengo la Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Tunduma awamu ya

pili na ujenzi wa Jengo la Mionzi na Upasuaji, Jengo la Maabara pamoja na jengo la kuchomea taka katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu ambayo imekamilika. Miradi mingine ni ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe awamu wa pili uliofikia asilimia 95 ya hatua ya utekelezaji, ujenzi wa jengo la maktaba Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) umefikia asilimia 95 na ujenzi wa Chuo cha VETA Karagwe umefikia asilimia 75.

***137. Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2021, Wakala umetekeleza jumla ya miradi 165 ya Ushauri Elekezi (Consultancy). Miradi hiyo ni pamoja na ushauri elekezi katika ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali awamu ya pili katika mji wa Serikali Mtumba, Dodoma na ushauri elekezi katika ujenzi wa jengo la hospitali ya Wilaya ya Kilolo ambayo imekamilika. Aidha, ushauri elekezi katika ujenzi wa Jengo la Utawala la Halmashauri ya Mji wa Bunda umefikia asilimia 87, ushauri elekezi katika ujenzi wa makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Butiama umefikia asilimia 95 na ushauri elekezi katika ujenzi wa Ofisi za Maji Kimani na Mkoji (Iringa) umefikia asilimia 65.

Vilevile, miradi ya ushauri elekezi iliyokamilika ni ushauri elekezi katika ujenzi wa Nyumba ya Rais Mstaafu Ali Hassan Mwinyi, ushauri elekezi katika ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Mtowisa na Msanzi pamoja na ushauri elekezi katika ukarabati, upanuzi na ujenzi wa miundombinu ya Mahakama Kuu katika mikoa sita ambayo ni Tanga, Ruvuma, Shinyanga, Tabora, Kilimanjaro na Mtwara. Aidha, ushauri elekezi katika ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (NAO) mkoani Simiyu umefikia asilimia 95, ushauri elekezi katika ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Laela Sumbawanga umefikia asilimia 85 na ushauri elekezi katika ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu umefikia asilimia 35.

***138. Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2021, Wakala umetekeleza jumla ya miradi mitatu (3) ya Usimamizi. Miradi hiyo ni ujenzi wa Vihenge (Silos) vya kuhifadhia nafaka pamoja na maghala kwa ajili ya kuhifadhi chakula katika mikoa nane (8) ya Dodoma, Katavi, Manyara, Njombe, Rukwa, Ruvuma,

Shinyanga na Songwe ambao umefikia asilimia 50; ujenzi wa majengo ya RADA katika mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Mwanza ambao umekamilika na kukabidhiwa kwa mshitiri na katika mkoa wa Songwe ambao umefikia asilimia 98 pamoja na ujenzi wa Kituo cha pamoja cha Forodha Mpakani cha Kasumulu (One Stop Border Post) awamu ya kwanza na ya pili ambao umefikia asilimia 42.

**Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania**

***139. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) ilipanga kuendelea na upanuzi wa maegesho ya Kigamboni kwa ajili ya kivuko cha Magogoni – Kigamboni mkoani Dar es Salaam; ujenzi wa maegesho ya Bukondo na Zumacheli katika kivuko cha Chato - Nkome mkoani Geita; ujenzi wa maegesho ya Nyamisati – Mafia mkoani Pwani; Ujenzi wa maegesho nane (8) ya vivuko (Bugolora – Ukara, Rugezi – Kisorya, Kilambo – Namoto, Utete – Mkongo, Iramba – Majita, Nyakarilo – Kome, Kasharu – Buganguzi na Kigongo – Busisi); ujenzi wa maegesho ya Kayenzi - Kanyinya, Muleba – Ikuza na Ujenzi wa miundombinu (jengo la abiria, ofisi na uzio) katika vituo kumi (10) vya vivuko. Aidha, Wakala ulipanga kuendelea na ujenzi wa miundombinu (jengo la kukatia tiketi, jengo la abiria na ofisi) kwa ajili ya kivuko kipya cha Kayenze – Bezi mkoani Mwanza na Kivuko cha Itungi Port (Mwaya – Kajunjumele) mkoani Mbeya. Kazi nyingine ni kufanya manunuzi ya kivuko kipya cha Nyamisati – Mafia; kivuko kipya cha Bugolora – Ukara na Chato – Nkome; Ujenzi wa "fiber boat" moja (1) itakayotoa huduma ya usafiri kati ya Utete – Mkongo; ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya karakana pamoja na vivuko; ununuzi wa kivuko kipya kitakachotoa huduma ya usafiri kati ya Kisorya – Rugezi pamoja na kufanya usanifu na kusimika Mfumo wa Usimamizi na uendeshaji wa Vivuko vya Serikali.

***140. Mheshimiwa Spika,*** Wakala vilevile ulipanga kukamilisha ukarabati wa vivuko MV Tegemeo, MV Musoma, MV Mara, MV Sengerema, MV Ujenzi, MV Kigamboni, MV Misungwi na boti ya uokozi MV KIU. Aidha, Wakala ulipanga kufanya ukarabati wa vivuko MV Nyerere, MV Kilombero I, MV

Kilombero II, MV Ruhuhu na MV Tanga na ukarabati wa mitambo ya karakana ya TEMESA Morogoro na mitambo ya barabara iliyopo Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi. Aidha, Wakala ulipanga kujenga karakana tano (5) katika mikoa ya Songwe, Simiyu, Geita, Njombe na Katavi; kujenga karakana ya kisasa Jijini Dodoma na ununuzi wa karakana sita zinazohamishika (mobile workshops) pamoja na vitendea kazi vyake. Kazi nyingine ni kukarabati karakana 11 ambazo ni karakana ya MT Depot Dar es salaam, Mtwara, Mbeya, Tabora, Mwanza, Arusha, Kigoma, Mara, Ruvuma, Pwani na Vingunguti (Dar es Salaam); kuanzisha karakana 6 za ngazi ya Wilaya (Simanjiro, Same, Chato, Masasi, Kyela na Ukerewe) pamoja na kusanifu na kusimika Mfumo wa Usimamizi wa Matengenezo ya Magari.

***141. Mheshimiwa Spika,*** Wakala vilevile ulipanga kufanya matengenezo ya magari **45,681,** matengenezo na usimikaji wa mifumo **394** ya umeme, mifumo **1,395** ya majokofu na viyoyozi pamoja na mifumo **166** ya elektroniki. Aidha, Wakala ulipanga kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu inayofikia **118** na kusimamia mifumo hiyo ipatayo **62**. Aidha, Wakala utaendelea kutoa huduma ya ukodishaji wa Mitambo ya Ujenzi wa Barabara.

***142. Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2021 upanuzi wa Jengo la abiria katika kivuko cha Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni ulikuwa umekamilika, kazi inayoendelea ni usimikaji wa miundombinu ya umeme na mashine za kukatia tiketi. Kuhusu ujenzi wa miundombinu (Jengo la abiria, chumba cha kukatia tiketi, ofisi na uzio) katika kivuko cha Kayenze - Bezi na Itungi Port, ujenzi wa Jengo la abiria upande wa Kayenze umekamilika, ujenzi unaendelea upande wa Bezi na Itungi Port.

***143. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu miradi ya ***ujenzi wa vivuko***, hadi Aprili, 2021, ujenzi wa kivuko kipya kitakachotoa huduma kati ya Nyamisati na Kisiwa cha Mafia umekamilika na kivuko kimeanza kutoa huduma tarehe 05 Januari, 2021; ujenzi wa kivuko kipya kitakachotoa huduma kati ya Bugolora na Ukara

umekamilika na kivuko kimeanza kutoa huduma mwezi Oktoba, 2020; ujenzi wa kivuko kipya kitakachotoa huduma kati ya Chato na Nkome umekamilika na kivuko kinatoa huduma. Vilevile, ujenzi wa kivuko kipya kitakachotoa huduma kati ya Kisorya na Rugezi upo katika hatua ya manunuzi na ujenzi wa Boti ndogo ya abiria itakayotoa huduma kati ya Utete na Mkongo unasubiri upatikanaji wa fedha. Aidha, mradi wa kusanifu na kusimika mfumo wa kusimamia uendeshaji wa huduma za vivuko (Electronic Ferry Management Information System – EFMIS) upo kwenye hatua ya manunuzi.

***144. Mheshimiwa Spika,*** Wakala umeendelea kutekeleza miradi ya ***ukarabati wa vivuko*** ambapo ukarabati wa MV Tegemeo umeanza, mradi wa ukarabati wa vivuko MV Musoma na MV Mara unasubiri upatikanaji wa fedha; kukamilisha ukarabati wa Boti ya uokozi MV KIU; ukarabati wa MV Sengerema umekamilika, na ukarabati wa MV Ujenzi upo kwenye hatua ya kusaini mkataba. Aidha, Ukarabati wa MV Kigamboni umekamilika na kinafanya kazi, ukarabati wa kivuko MV Misungwi unaendelea na mradi wa ukarabati MV Kome II upo kwenye hatua ya manunuzi.
Vilevile, ukarabati wa vivuko MV Nyerere, MV Kilombero I, MV Kilombero II, MV Ruhuhu na MV Tanga uko hatua ya manunuzi. Aidha, ukarabati wa Mitambo ya karakana ya TEMESA Morogoro na Chuo Cha Teknolojia ya Ujenzi (ICoT) kampasi ya Morogoro upo katika hatua ya manunuzi.

***145. Mheshimiwa Spika****,* kwa upande wa miradi ya ***Ujenzi wa Karakana za TEMESA***, hadi kufikia Aprili, 2021, Wakala umeendelea na ujenzi wa Karakana ya Simiyu; ununuzi wa karakana sita (6) zinazohamishika (mobile workshop) umekamilika na mradi wa kusanifu na kusimika mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji wa matengenezo ya magari kwenye karakana za TEMESA umekamilika katika vituo vya Dodoma, Iringa na MT Depot - Dar es Salaam. Aidha, karakana tatu (3) za matengenezo ya magari ngazi ya Wilaya zimekamilika katika Wilaya za Ifakara, Kahama na Same na maandalizi ya uanzishaji wa karakana za Wilaya za Simanjiro, Kyela na Masasi yanaendelea.
Vilevile, Wizara kupitia TEMESA imeboresha vitendea kazi vya karakana kwa kununua vitendea kazi stahiki kama vile

*Diagnostic machine, Car lifter, 3D wheel alignment* na *Tyre changer* katika mikoa yote pamoja na karakana tatu za ngazi za wilaya. Pia kufanya ukarabati wa majengo ya karakana MT Depot, Singida, Dodoma, Dar es Salaam (Vingunguti), Mwanza na Mbeya na kuanza ujenzi wa awamu ya kwanza wa karakana mpya katika mkoa wa Simiyu. Kazi nyingine ni kufunga CCTV Camera katika maeneo ya karakana ili kudhibiti ubadhirifu.

***146. Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa na TEMESA ni pamoja na matengenezo ya magari ambapo hadi Aprili, 2021 jumla ya magari **13,724** yalifanyiwa matengenezo. Aidha, miradi **321** ya umeme, miradi **361** ya viyoyozi na miradi **486** ya kieletroniki imetekelezwa. Vilevile, Wakala ulitekeleza jumla ya miradi **34** ya ushauri wa kihandisi ambapo miradi **16** ni ya umeme na **18** ni ya majokofu na viyoyozi. Aidha, Wakala umeendelea kusimamia na kuendesha vivuko vya Serikali **33** katika vituo **21** nchini pamoja na kutoa huduma za ukodishaji wa magari na mitambo katika mikoa **19** na kituo kimoja cha *Government Transport Agency* (GTA).

**Bodi ya Usajili wa Wahandisi**

***147. Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Bodi hii ni kuratibu na kusimamia mienendo na shughuli za kihandisi zinazofanywa na Wahandisi pamoja na makampuni ya ushauri wa kihandisi. Bodi pia ina jukumu la kulinda maslahi ya taifa na watumiaji wa huduma za kihandisi kwa kuhakikisha kuwa shughuli zote za kihandisi zinafanywa na Wahandisi wenye sifa za utaalam, uwezo na uzoefu uliothibitishwa kwa kusajiliwa na Bodi; au makampuni ya ushauri wa kihandisi yenye utalaam, uwezo na uzoefu vilivyothibitishwa kwa kusajiliwa na Bodi. Wahandisi na makampuni ya ushauri wa kihandisi yaliyosajiliwa na Bodi wanawajibika kuzingatia viwango na maadili ya kihandisi ili kuhakikisha usalama wa maisha, mali na mazingira na thamani ya fedha.

Hadi Aprili, 2021, Bodi imesajili Wahandisi **1,321** na kampuni za ushauri wa kihandisi **14** na kufikisha jumla ya Wahandisi waliosajiliwa katika ngazi mbalimbali kuwa **29,759** na kampuni za ushauri wa kihandisi kuwa **376**. Kati ya Wahandisi

waliosajiliwa, Wahandisi **27,235** ni wa ndani na **2,524** ni wa kigeni. Kampuni za ushauri wa kihandisi za ndani ni **259** na za kigeni ni **117.** Katika kipindi hicho, Bodi ilifuta usajili kwa Wahandisi watalaam **526**, Wahandisi Washauri **14** na kampuni za ushauri wa Kihandisi **24** kwa kukiuka Sheria ya Usajili wa Wahandisi. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya miradi 203 ilikaguliwa. Vilevile, Bodi imesajili miradi **348** kati ya miradi **600** iliyopangwa katika mwaka huu na pia imekagua viwanda na Majengo **39** kati ya **60** iliyopangwa.

***148. Mheshimiwa Spika,*** Bodi pia iliandaa warsha **3** katika kanda **5** kwa Wahandisi Wataalam wanaosimamia mafunzo kwa vitendo kwa Wahandisi wahitimu. Vilevile, Bodi iliendelea kuwaapisha Wahandisi Wataalam Kiapo cha Utii kwa Taaluma (Professional Oath) ambapo hadi sasa jumla ya Wahandisi **4,361** wameapishwa.
Aidha, Bodi iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahandisi wahitimu ambapo, Wahandisi wahitimu **549** kati **1,200** wameingizwa katika mpango huo katika mwaka huu. Jumla ya Wahandisi wahitimu **8,640** wameshapitia Mpango huu tangu uanzishwe mwaka 2003. Pia, Wahandisi wahitimu **4,067** wameshahitimu mafunzo hayo na kusajiliwa na Bodi kama Wahandisi Watalaam (Professional Engineers).Bodi iliandaa na kuadhimisha Siku ya Wahandisi ya mwaka 2020 (Annual Engineers' Day 2020) ambayo ilihudhuriwa na Wahandisi zaidi ya **3,750**.

**Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi**
***149. Mheshimiwa Spika,*** majukumu makuu ya Bodi hii ni kusajili, kusimamia na kuratibu mwenendo wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi pamoja na Kampuni zao za ushauri. Aidha, Bodi ina jukumu la kukagua sehemu zinakofanyika shughuli za ujenzi ili kuhakikisha ubunifu na usimamizi wa ujenzi unafanywa na wataalam waliosajiliwa.

Hadi Aprili, 2021 wataalam **32** wamesajiliwa na Bodi, ikiwa ni asilimia **27** ya lengo na kampuni **12** zimesajiliwa ikiwa ni asilimia **67** ya lengo. Aidha, hadi Aprili, 2021 wahitimu **107** wamepatiwa mafunzo ikiwa ni asilimia **89** ya lengo. Aidha,

miradi ya ujenzi **1,437** ilikaguliwa ikiwa ni asilimia **72** ya lengo. Miradi ambayo ilikutwa na kasoro, wataalam au waendelezaji wake walichukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria ikiwemo, kutozwa faini au kufunguliwa mashtaka mahakamani na miradi ya ujenzi **705** imesajili ambayo ni asilimia **71** ya lengo.

**Bodi ya Usajili wa Makandarasi**

***150. Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Usajili wa Makandarasi ina majukumu ya kusajili na kuratibu shughuli za ukandarasi nchini na kuendeleza Makandarasi ili kufanya kazi zilizo bora kwa maslahi ya watumiaji wa huduma hizo na kwa maslahi ya Taifa kwa ujumla.

***151. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu hayo, hadi Aprili, 2021 Bodi ilisajili Makandarasi wapya **634** hivyo kufanya jumla ya Makandarasi waliosajiliwa kufikia **11,749**. Aidha, jumla ya miradi **3,562** ilikaguliwa. Miradi **948** sawa na asilimia **27** ilipatikana na mapungufu mbalimbali yakiwemo kutozingatia usalama kazini, kutosajili miradi na kufanya kazi za thamani inayozidi kiwango kinachoruhusiwa kwa daraja husika. Makandarasi waliokutwa na mapungufu hayo walichukuliwa hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria ikiwemo kutozwa faini, kupewa onyo, kusimamishwa kufanya biashara ya ukandarasi na kufutiwa usajili. Pale ambapo hapakuwa na mapungufu ya Makandarasi, wawekezaji walifikishwa mahakamani.

Vilevile, Bodi iliendesha kozi tatu **(3)** za mafunzo kupitia Mpango Maalum wa Mafunzo Endelevu kwa Makandarasi (Sustainable Structured Training Programme – SSTP) katika mikoa ya Mwanza, Dodoma, Arusha na Njombe. Jumla ya Makandarasi **659** walishiriki katika mafunzo hayo. Bodi pia iliendelea kuendesha Mfuko wa Kusaidia Makandarasi (Contractors Assistance Fund - CAF) unaotoa dhamana za zabuni na malipo ya awali kwa Makandarasi wa ndani ili kuwezesha ushiriki wa Makandarasi wa ndani katika zabuni na utekelezaji wa miradi mbalimbali. Mtaji wa mfuko huu umekua na kufikia **Shilingi bilioni 3.9** kwa mwaka 2020/21. Aidha, idadi ya wanachama wa Mfuko iliongezeka kutoka

**1,126** mwaka wa fedha 2019/20 hadi kufikia **1,179** mwaka 2020/21.

**Baraza la Taifa la Ujenzi**

***152. Mheshimiwa Spika,*** Baraza la Taifa la Ujenzi lina majukumu ya kushughulikia maendeleo ya Sekta ya Ujenzi katika nyanja zinazojumuisha kutoa ushauri wa kiufundi kwa Serikali na wadau wengine wa Sekta ya Ujenzi, uratibu wa shughuli za utafiti na mafunzo ya kisekta kwa ujumla. Jukumu lingine ni ukusanyaji na uwekaji wa taarifa za ujenzi, tathmini ya utendaji kazi wa Sekta ya Ujenzi, uanzishwaji wa mfuko wa mafunzo, uhamasishaji wa ubora wa kazi, ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa kiufundi (technical audit) na utatuzi wa migogoro ya ujenzi.
Hadi kufikia Aprili, 2021 ni pamoja na kuandaa andiko lenye mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria iliyoanzisha Baraza (Cap 162, Revised Edition (R.E.) 2008) pamoja na kuanza maandalizi ya Kanuni za Utekelezaji wa Sheria iliyoanzisha Baraza. Aidha, Baraza lilifanikiwa kutoa mafunzo ya Usimamizi wa Mikataba (Contract Administration) katika miradi ya ujenzi kwa wadau **67** yaliyohusisha Watumishi kutoka Taasisi za Umma na binafsi zinazojishughulisha na shughuli za ujenzi.

***153. Mheshimiwa Spika,*** Baraza vilevile lilitoa ushauri wa kiufundi kwa wadau mbalimbali wa Sekta ya Ujenzi katika maeneo makuu mawili ambayo ni tathmini ya gharama za ujenzi na bei ya miradi ya ujenzi pamoja na na Miongozo ya manunuzi ya miradi ya ujenzi (tools for procurement of works). Sambamba na hilo, Baraza limeendelea kuratibu utatuzi wa migogoro katika miradi ya ujenzi kwa njia ya *Arbitration* na *Adjudication*. Hadi Aprili, 2021 Baraza limeratibu usuluhishi wa mashauri **32** ya *Arbitration* na mashauri **23** kwa njia ya *Adjudication*. Kati ya mashauri hayo, mashauri 4 ya *Arbitration* yalifikia mwisho na kuamuliwa wakati mashauri 10 ya *Adjudication* yalifikia mwisho na kuamuliwa. Katika kipindi hicho migogoro mipya iliyosajiliwa ilikuwa 18 kwa *Arbitration* na 4 ya *Adjudication.*

***154. Mheshimiwa Spika,*** Baraza linaendelea kufanya tafiti kuhusu tathimini ya ushiriki wa Washauri wataalam wazalendo

(local consultants) katika kutekeleza miradi ya ujenzi ukilinganisha na Washauri wataalam wa kigeni. Aidha, Baraza linaendelea na tathmini ya gharama za ujenzi wa majengo yaliyokamilika ili kupata viwango vya gharama (unit cost) ya ujenzi wa majengo ya aina mbalimbali na tathmini ya mafanikio na changamoto za utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa njia ya "Design and Build". Vilevile, Baraza lilifanya ukaguzi wa kiufundi wa miradi ya ujenzi 63 iliyohusisha miradi ya barabara 48 na madaraja 15 ambayo inasimamiwa na TANROADS na TARURA katika mkoa wa Kigoma.

Baraza pia limeendelea na jukumu la kukusanya takwimu na taarifa za Sekta ya Ujenzi kwa mwaka 2020/21 ili kuwezesha wadau wa Sekta ya Ujenzi kufuatilia ukuaji wa Sekta. Aidha, Baraza liliendelea kukusanya na kuandaa bei za vifaa vya ujenzi na viwango vya mabadiliko ya bei hizo "indices" kwa ajili ya usimamizi wa mabadiliko ya bei za miradi ("Price Fluctuation Formula"). Katika mwaka wa fedha 2020/21, Baraza limetoa *Price Indices* za kila mwezi. Aidha, Baraza limeendelea kuratibu Mpango wa kukuza uwazi na uwajibikaji "Construction Sector Transparency Initiative (CoST)" kupitia ufadhili wa *CoST International Secretariat.*

**Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)**

***155. Mheshimiwa Spika,*** lengo la kuanzishwa kwa Kituo hiki ni kuimarisha/kuboresha Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji kwa ujumla kwa kutumia mbinu ya ukusanyaji na usambazaji wa teknolojia kwa wadau. Katika kutekeleza majukumu hayo, hadi Aprili, 2021, Kituo kiliandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa wataalam 28 wa Wizara kuhusu teknolojia mpya ya usanifu wa lami na matumizi ya mwongozo mpya wa usanifu wa Lami ulioandaliwa na Maabara ya Taifa Upimaji Kazi na Vifaa vya Ujenzi ya TANROADS (CML) ili kupunguza changamoto zitokanazo na mabadiliko ya tabia nchi yanayoathiri barabara za lami. Vilevile, Kituo kimeshiriki katika mikutano miwili (2) ya ndani ya nchi iliyokuwa inajadili kuhusu teknolojia, ubunifu na mikakati mbalimbali ili

kuboresha miundombinu yetu katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji.
Aidha, Kituo kimeendelea kuratibu na kutekeleza kazi za uanzishwaji wa Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi(Institute of Construction Technology – ICoT) na kufanikisha kuanza kwa udahili wa wanafunzi kwa mwaka wa masomo 2020/21 katika fani za *Civil, Electrical* na *Mechanical Engineering* kwa ngazi ya Cheti (NTA Level 4). Hadi kufikia Aprili, 2021 maandalizi ya nyaraka kwa ngazi zinazofuata za *NTA Level 5* na 6 yanaendelea na yapo katika harua za mwisho. Aidha, Kituo kimeendelea kuimarisha huduma za Maktaba Mtandao kupitia ICoT ili kuendelea kutoa huduma kuhusu Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji kwa lengo la kuboresha mifumo na upashanaji habari za teknolojia.

Kazi nyingine ni kuandaa na kuchapisha nakala 300 za jarida la kituo lenye mada mbalimbali zinazohusu teknolojia, usalama barabarani na taarifa za miradi mbalimbali ya kimkakati katika kuimarisha miundombinu ya usafirishaji.

### C.1.2 SEKTA YA UCHUKUZI

***156. Mheshimiwa Spika**,* katika mwaka wa fedha 2020/2021, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 3,152,858,739,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,062,148,630,000** ni fedha za Maendeleo na **Shilingi 90,710,109,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

### Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

***157. Mheshimiwa Spika**,* katika bajeti ya mwaka 2020/2021, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa **Shilingi 90,710,109,000** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 63,639,165,000** ni fedha za Mishahara na **Shilingi 27,070,944,000** ni fedha za Matumizi Mengineyo kwa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Uchukuzi. Hadi kufikia Aprili, 2021, fedha za Matumizi ya Kawaida zilizotolewa kwa Sekta ya Uchukuzi na Taasisi zake ni **Shilingi 74,184,903,187.70** sawa na **asilimia 81.78** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 9,030,322,916.60** ni fedha kwa Matumizi ya Kawaida

ya Wizara na **Shilingi 65,154,580,271.10** ni fedha za Matumizi ya Kawaida ya Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Uchukuzi.

**Bajeti ya Maendeleo**

***158. Mheshimiwa* Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021, Sekta ya Uchukuzi ilitengewa jumla ya **Shilingi 3,062,148,630,000** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,937,678,920,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 124,469,710,000** ni fedha za nje. Hadi kufikia Aprili, 2021, jumla ya fedha zilizotolewa ni **Shilingi 1,706,818,762,216.91** sawa na **asilimia 55.7** ya bajeti iliyoidhinishiwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,609,663,552,216.91** ni fedha za ndani sawa na **asilimia 54.8** ya bajeti iliyoidhinishwa na **Shilingi 97,155,210,000** ni fedha za nje sawa na **asilimia 78.1** ya bajeti ya fedha za nje iliyoidhinishwa.

**HUDUMA ZA USAFIRI MIJINI NA VIJIJINI**

**Udhibiti wa Usafiri kwa Njia ya Barabara**

***159. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeendelea kusimamia na kudhibiti usafiri katika sekta ndogo za reli, barabara na usafiri wa waya. Aidha, Mamlaka imeendelea kufuatilia mwenendo wa mabasi ya masafa marefu na treni (Vehicle Tracking System - VTS) ili kuimarisha shughuli za udhibiti wakati wote na mahali popote vyombo hivi vilipo. Hadi Aprili, 2021, jumla ya mabasi 5,386 na vichwa vya treni vitano (5) vilikuwa vimeunganishwa kwenye mfumo huo. Kazi ya kuboresha mfumo na kuufunga kwenye mabasi yanayotoa huduma kwenye njia fupi inaendelea. Mfumo huu pia umeunganishwa na ofisi za Jeshi la Usalama Barabarani ili kuweza kufuatilia mwenendo wa mabasi hayo.

***160. Mheshimiwa Spika,*** LATRA kwa kushirikiana na Kituo cha Taifa cha Kuhifadhia Data Kimtandao (National Internet Data Centre - NIDC) na Mamlaka ya Mapato Tanzania, imeendelea kuratibu uunganishaji wa mfumo wa tiketi za kielektroniki (Electronic Ticketing System) kwa mabasi ya abiria na mifumo ya wamiliki wa mabasi nchini ili kuwa na mfumo mmoja jumuishi (Universal Electronic Ticketing System). Hadi sasa jumla ya mabasi 2,194 kati ya mabasi 5,386 sawa na

asilimia 40 ya mabasi yote yanayotoa huduma za usafiri wa mabasi ya mikoani yameunganishwa katika mfumo wa tiketi mtandao. Aidha, LATRA inaendelea kufanya maandalizi ya miundombinu ya mawasiliano ili kuunganisha vituo vikuu vya mabasi vya Dodoma na Magufuli, Dar es Salaam na mifumo ya LATRA ili kusaidia wasafiri na wadau mbalimbali kupata taarifa sahihi za safari za mabasi katika vituo hivyo.

***161. Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kuwasihi na kuwataka Wamiliki wa mabasi na Chama chao kuendelea kutumia mifumo ya TEHAMA kwenye uendeshaji wa shughuli zao ikiwemo matumizi ya tiketi mtandao. Wizara kupitia LATRA kwa kushirikiana na Taasisi nyingine itaendelea kutoa ushirikiano katika kutatua changamoto mbalimbali katika matumizi ya mfumo huo na kuhakikisha kuwa kila mtoa huduma anajiunga katika matumizi ya TEHAMA. Matumizi ya mfumo huu yatasaidia kupata takwimu sahihi za watumiaji wa huduma, kuondoa changamoto ya wapiga debe kwenye vituo vya mabasi, kupunguza gharama za uendeshaji kwa watoa huduma na kusimamia mapato ya Serikali. Aidha, abiria wataweza kupata huduma popote walipo hivyo kupunguziwa gharama na muda wa kufuata tiketi kwa mawakala wa mabasi hayo.

***162. Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuongeza ufanisi wa usafiri ardhini, kupunguza gharama za uendeshaji kwa watoa huduma pamoja na kuongeza usalama na ubora wa huduma za usafiri ardhini, Serikali kupitia LATRA inatarajia kuandaa viwango vya vifaa na utaratibu wa kaguzi za lazima kwa magari ya biashara (mandatory inspection for commercial vehicles). Ukaguzi huu pia utahusisha kusajili na kuthibitisha madereva wa magari (Commercial Drivers Certification). Lengo la usajili huu ni kuwatambua madereva wenye sifa za kuendesha vyombo vinavyodhibitiwa ili kuimarisha usalama na kuboresha huduma za usafiri kwa njia ya barabara.

***163. Mheshimiwa Spika,*** kumeibuka wimbi la Watanzania wenye Malori ya Mizigo kusajili malori yao katika nchi jirani na kuendelea kubeba mizigo kutoka hapa nchini kwenda

nchi hizo. Magari haya yanatumika kubeba mizigo kutoka Bandari za Tanzania, Makaa ya Mawe kutoka Migodi ya hapa nchini, Saruji na mizigo mingine inayozalishwa humu nchini kwenda nchi jirani. Miongoni mwa magari hayo, yamo yanayobeba mizigo kutoka hapa nchini kwenda nchi ya tatu. Kwa mfano, magari yenye usajili wa Rwanda yanayobeba makaa ya Mawe kutoka mgodi wa makaa ya mawe uliopo Ngaka, Ruvuma kwenda Kajiado na Thika nchini Kenya.

***164. Mheshimiwa Spika,*** takwimu zinaonesha kuna ongezeko la magari yaliyosajiliwa nchini Rwanda na Burundi yanayoingia nchini Tanzania kwa ajili kuleta au kuchukua shehena. Kati ya mwaka 2014/15 na 2019/20, idadi ya magari kutoka nchini Rwanda imeongezeka kutoka magari 2,598 hadi 36,715 wakati magari ya Tanzania yaliyoingia nchini Rwanda yaliongezeka kutoka magari 4,705 hadi 29,570. Aidha, kuna takriban magari 200 ya Rwanda kwenda nchi za jirani yanayobeba saruji kila siku kutoka kiwanda cha Twiga kilichoko Dar es Salaam. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara kupitia LATRA inafanya tathmini ya sababu na athari zitokanazo na mwenendo huu wa usajili wa magari kwa lengo la kubaini hatua stahiki zitakazochukuliwa na Serikali.

**Udhibiti wa Usafiri kwa Njia ya Reli**

***165. Mheshimiwa Spika***, LATRA imeendelea kudhibiti usafiri kwa njia ya Reli. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, ukaguzi uliofanyika ulihusu njia na mitambo ya reli kwenye Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) kutoka Dar es Salaam hadi Tunduma; ukaguzi kwenye miundombinu na vitendea kazi vinavyotumika katika njia ya reli ya Moshi hadi Arusha; pamoja na kufanya uchunguzi wa vyanzo vya ajali za treni zilizotokea. Kaguzi hizo zimewezesha kutoa taarifa zilizotumiwa na TRC na TAZARA kuboresha miundombinu na matengenezo ya mitambo inayotumika kwenye usafiri wa reli. Aidha, LATRA imefanya kaguzi mbalimbali katika ujenzi unaoendelea wa Reli ya Kisasa (Standard Gauge Railway - SGR) ili kujiridhisha na ubora wake pamoja na viwango vya usalama. Changamoto za kiusalama zilizobainika wakati wa ukaguzi huo zilitolewa taarifa na kuwataka TRC kuzifanyia kazi wakati ujenzi wa reli unaendelea.

**Huduma za Usafiri wa Treni Mijini**

***166. Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) imeendelea kutoa huduma za usafiri wa abiria Jijini Dar es Salaam kati ya Stesheni za Dar es Salaam na Mwakanga. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, treni hii ilisafirisha jumla ya abiria 1,019,557 ikilinganishwa na abiria 1,006,678 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2019/2020. Hili ni ongezeko la asilimia 1.2. Kwa upande wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), huduma ya usafiri wa treni ya jijini Dar es Salaam imeendelea kutolewa kuanzia Stesheni kuelekea maeneo ya Ubungo na Pugu. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, jumla ya abiria 2,093,324 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 2,842,342 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2019/2020. Upungufu huu wa abiria kwa asilimia 26.4 umetokana na kuhamishwa kwa kituo cha abiria cha Stesheni Dar es Salaam kwenda Stesheni ya Kamata ili kupisha shughuli zinazoendelea za ujenzi wa SGR.

**Shirika la Reli Tanzania (TRC)**

***167. Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Reli Tanzania (TRC) limeendelea kusimamia, kuboresha na kuendeleza miundombinu na huduma za usafiri wa reli yenye jumla ya urefu wa Kilometa 2,706 kwa ajili ya kuhudumia nchi jirani za Burundi, Rwanda, Uganda na Kenya. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi April, 2021, TRC ilisafirisha tani za mizigo 257,602 ikilinganishwa na tani 249,960 zilizosafirishwa kipindi kama hicho mwaka 2019/2020. Ongezeko hili la asilimia 3.1 limetokana na ukarabati wa mabehewa uliofanyika pamoja na uimarishaji wa njia kipande cha Dar es Salaam hadi Isaka (km 970). Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya abiria wa masafa marefu 333,638 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 369,638 waliosafirishwa kipindi kama hicho katika mwaka 2019/20. Huu ni upungufu wa asilimia 9.7. Sababu za upungufu huu ni pamoja na athari za mlipuko wa ugonjwa wa COVID 19 na kufungwa kwa njia kutokana na ajali.

Kwa ujumla TRC iliweza kukusanya mapato ya shilingi bilioni 37.92 katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 27.49 zilizokusanywa katika

kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 37.9.

***168. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, Serikali imeendelea kusimamia ujenzi wa reli ya Dar es Salaam hadi Mwanza kwa kiwango cha *Standard Gauge* (SGR). Ujenzi wa reli ya Kati kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro (km 300) umekamilika kwa asilimia 91. Shughuli zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa makalvati uliokamilika kwa asilimia 99.7, ujenzi wa daraja lenye urefu wa jumla ya km 2.54 katikati ya Jiji la Dar es Salaam uliokamilika kwa asilimia 94.2, kutandika reli kwenye urefu wa jumla ya km 257, ujenzi wa Vivuko uliokamilika kwa asilimia 99 na ujenzi wa Stesheni umekamilika kwa asilimia 99.8.

***169. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu kipande cha reli kutoka Morogoro hadi Makutupora (km 422), ujenzi unaendelea na umekamilika kwa asilimia 60.2. Kazi zinazoendelea kufanyika ni pamoja na usanifu uliokamilika kwa asilimia 89.08, uzalishaji wa Mataruma ya Zege uliokamilika kwa asilimia 92.58, kutandika reli kwenye urefu wa jumla ya km 99, ukataji wa miinuko na ujazaji mabonde uliokamilika kwa asilimia 90.62, uchorongaji wa mahandaki manne (4) umekamilika kwa asilimia 100, ujenzi wa makalvati uliokamilika kwa asilimia 75.13, ujenzi wa Vivuko vya Mifugo uliokamilika kwa asilimia 83.31 na ujenzi wa Stesheni uliokamilika kwa asilimia 50.14.

***170. Mheshimiwa Spika,*** kazi za ujenzi wa mfumo wa umeme katika Mradi wa SGR imekamilika kwa asilimia 100 kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro na asilimia 35.62 kwa kipande cha Morogoro hadi Makutupora. Aidha, tarehe 8 Januari 2021, Serikali kupitia TRC ilisaini Mkataba na ubia wa Kampuni ya *China Civil Engineering Construction Corporation* (CCECC) na *China Railways Construction Cooperation* (CRCC) za nchini China kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya Mwanza-Isaka (Km 341). Malipo ya awali (advance payments) ya ujenzi wa kipande hiki ya Shilingi bilioni 376.44 yamefanyika Aprili, 2021. Kazi ya ujenzi inatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Mei, 2021 na sasa Mkandarasi

anaendelea na maandalizi ya ujenzi ikiwemo uletaji wa mitambo.

***171. Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na majadiliano na Taasisi za fedha na Washirika Mbalimnali wa Maendeleo walioonesha nia ya kugharamia ujenzi wa reli ya SGR vipande vya Makutupora – Tabora (km 294) na Tabora – Isaka (km 133). Maeneo mengine yanayoendelea kutafutiwa fedha za ujenzi ni pamoja na Tabora – Kigoma (km 411), Keza - Ruvubu (km 36), Uvinza-Musongati (km 200), Kaliua – Mpanda - Karema (km 321) na Isaka - Rusumo (km 371).

***172. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ununuzi wa vifaa vya majaribio ya Reli ya SGR, Mkataba wa ununuzi wa Vichwa viwili (2) vya Treni za umeme pamoja na Mabehewa 30 ulisainiwa Oktoba, 2020. Vifaa hivyo vitawasili nchini kwa awamu mbili (2) kama ifuatavyo: Vichwa viwili (2) vya umeme na Mabehewa 12 ya abiria yatawasili Agosti, 2021 na miezi minne baadaye (Disemba, 2021), Mabehewa 18 yaliyobaki yatawasili. Majaribio ya kwanza ya Reli ya SGR yamepangwa kufanyika Agosti, 2021 na majaribio ya pili yatafanyika Disemba, 2021.

***173. Mheshimiwa Spika,*** baada ya ujenzi wa reli na majaribio ya matumizi yake kukamilika, TRC itaanza kutoa huduma rasmi. Ili kuwezesha kutoa huduma, masuala yafuatayo yametekelezwa:

i. Majadiliano ya zabuni ya ununuzi wa vichwa vya treni vitano (5) vinavyotumia dizeli na umeme yanaendelea na yatakamilika Juni, 2021;

ii. Zabuni kwa ajili ya ununuzi wa Vichwa vya umeme 17 vinavyotumia dizeli na umeme, Treni za umeme za abiria (EMU) imekamilika;

iii. Malipo ya awali (Advance payment) ya ununuzi wa mabehewa ya abiria 59 yalifanyika Februari, 2021. Kazi ya uzalishaji wa mabehewa imeanza; na

iv. Majadiliano ya zabuni ya ununuzi wa mabehewa ya mizigo 1,430 yamekamilika Aprili, 2021.

***174. Mheshimiwa Spika,*** itakumbukwa kuwa, tumekuwa tukitoa taarifa kwenye Bunge lako Tukufu kuhusu ukarabati wa miundombinu ya reli iliyopo (MGR) kutoka Dar es Salaam – Isaka (Km 970) kupitia Mradi wa Tanzania *Intermodal and Rail Development Project – TIRP*, chini ya Mkandarasi Kampuni ya *China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC)*. Napenda kutoa taarifa kuwa, Mradi huu ulioanza Juni, 2018 kwa kutumia mkopo wa Benki ya Dunia umekamilika. Kipande cha kwanza kutoka Dar es Salaam - Kilosa (Km 283) kilikamilika Novemba, 2020; na kipande cha Kilosa - Isaka (Km 687) kilikamilika Oktoba, 2020. Kazi nyingine zilizokamilika kupitia Mradi huu ni pamoja na usanifu wa ujenzi wa eneo la treni la kupakia na kupakua mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam; ukarabati wa vituo vya kuhudumia mizigo vya Ilala na Isaka; ununuzi wa vifaa vya kutolea huduma na Vichwa vitatu (3) vya treni vinavyotarajiwa kuwasili Agosti, 2021; na ununuzi wa mabehewa 44 ya mizigo yanayotarajiwa kuwasili nchini Juni, 2021.

***175. Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili 2021 ni pamoja na kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli katika jiji la Dodoma. Kazi hii inatarajiwa kukamilika Juni, 2021. Aidha, uundaji wa vichwa vya treni saba (7) vya sogeza umekamilika.

***176. Mheshimiwa Spika,*** katika Hotuba ya mwaka 2020/21 ilitolewa taarifa kuhusu njia ya reli iliyoathiriwa kutokana na mvua kubwa zilizonyesha kuanzia mwezi Oktoba, 2019 hadi Mei, 2020. Napenda kutoa taarifa kuwa Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa huduma ya usafiri wa treni zinapatikana muda wote. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, kazi iliyofanyika katika miundombinu ya reli iliyoharibiwa na mvua ni pamoja na ukarabati wa njia ya reli ya Kaliua – Mpanda, uimarishaji wa daraja la Mto Ugala na ukarabati wa njia ya reli katika maeneo ya Kigwe - Bahi na Godegode - Gulwe.

***177. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuongeza Mtandao wa reli ya Kati kwa kujenga reli mpya ya *standard gauge*, kukarabati reli iliyopo na kugharamia tafiti mbalimbali za njia mpya za reli kwa kutumia fedha za Mfuko wa Reli (Railway Infrastructure Fund). Kazi nyingine zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 kupitia Mfuko huo ni pamoja na:

i. Kufanya ukarabati wa njia ya reli ya Tanga – Arusha. Ukarabati wa kipande cha Tanga – Moshi ulikamilika na huduma zake zilizinduliwa rasmi tarehe 20 Julai 2019 na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kipande cha Moshi – Arusha, kazi ya ukarabati wa njia hiyo ilikamilika na huduma zake kuzinduliwa rasmi tarehe 24 Oktoba, 2020 na Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli;

ii. Kukamilishwa kwa ukarabati wa Mabehewa 197;

iii. Kuendelea na ukarabati wa mabehewa 38 yanayotarajiwa kukamilika Juni, 2021;

iv. Kutafuta Mtaalam wa Uwekezaji (Transaction Advisor) kwa ajili ya kuandaa Andiko la kutafuta mwekezaji kwenye mradi wa usafiri wa Treni ya Abiria jijini Dar es Salaam kwa utaratibu wa ubia (PPP). Kazi ya manunuzi ya Mtaalam huyo inaendelea; na

v. Kuendelea na taratibu za kumuajiri Mtaalam wa Uwekezaji (Transaction Advisor) atakayekuwa na jukumu la kuandaa taarifa na kuunadi kwa wawekezaji Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Tanga – Arusha – Musoma (km 1223) kwa *Standard Gauge* kwa mfumo wa ubia (PPP).

**Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)**

***178. Mheshimiwa* Spika,** huduma za kusafirisha abiria na mizigo kwa njia ya reli kati ya Dar es Salaam, Tanzania na New Kapiri Mposhi, Zambia na kulinda na kuimarisha

miundombinu ya reli yenye urefu wa Km 1860 pamoja na maeneo yote yaliyo ndani ya ukanda wa reli (Mita 50 pande zote kutoka katikati ya reli) zimeendelea kutekelezwa na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (Tanzania Zambßia Railway Authority - TAZARA). Mamlaka hii inamilikiwa na Serikali mbili za Tanzania (yenye reli ya urefu wa Km 975) na Zambia (yenye reli ya urefu wa Km 885) kwa hisa za hamsini (50) kwa hamsini (50).

***179. Mheshimiwa* Spika,** katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, TAZARA ilisafirisha jumla ya tani 167,242 za mizigo ikilinganishwa na tani 148,681 zilizosafirishwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2019/2020 ikiwa ni ongezeko la asilimia 12.5. Ongezeko hili limechangiwa na kuanza kufanya kazi kwa Injini saba (7) zilizofungwa vipuri vipya vilivyonunuliwa pamoja na matengenezo ya njia ya reli hasa kwenye maeneo korofi ya reli. Aidha, katika kipindi hicho, Mamlaka ilisafirisha abiria 350,008 wa njia ndefu ikilinganishwa na abiria 401,706 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2019/ 2020. Huu ni upungufu wa asilimia 12.9 uliotokana na kuwepo kwa janga la ugonjwa wa Corona (COVID 19) uliosababisha kusitisha treni za abiria kuvuka mpaka kwenda Zambia na kutoka Zambia kuja Tanzania. Treni hizi kwa sasa zinafanya safari kati ya Dar es Salaam na Mbeya kwa upande wa Tanzania na Kati ya Nakonde na New Kapiri Mposhi kwa upande wa Zambia.

***180. Mheshimiwa* Spika,** kufuatia kuimarika kwa miundombinu ya reli, TAZARA imeingia Mkataba wa kutumia njia ya reli (Access Fee) na Kampuni ya Callabash kutoka Zambia. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, Kampuni hii ilisafirisha jumla ya tani za mizigo 199,410 ikilinganishwa na tani za mizigo 150,974 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2019/2020 kupitia bandari ya Dar es Salaam kuelekea katika nchi za Zambia na DR Congo. Ukodishaji huu umeiingizia Mamlaka mapato ya Shilingi bilioni 19.7. Kwa ujumla, TAZARA na Callabash wamesafirishaji jumla ya tani za mzigo 366,652 katika kipindi hicho.

***181. Mheshimiwa* Spika,** kazi nyingine zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 ni pamoja na kukamilika kwa ukarabati wa Injini saba (7); kufanya matengenezo ya kiwango cha juu, kati na chini kwa Mabehewa ya mizigo 431 na Mabehewa ya abiria 92; kubadilisha Mataruma ya Zege 5,312 na Mataruma ya Mbao 1,946; kusambaza na kushindilia kokoto zenye ujazo wa tani 13,550; kufanya matengenezo ya kawaida ya Injini, Mabehewa ya mizigo na abiria; kukarabati mtambo wa kusambaza na kushindilia kokoto na kunyoosha reli (Tamping Machine) na kufanya matengenezo ya njia ya reli. Aidha, mitambo mitatu (3) kati ya minane (8) inayohitajika kwa ajili ya kusaidia uzalishaji wa kokoto na mataruma ya zege katika mgodi wa kokoto Kongolo, Mbeya imenunuliwa. Mitambo hiyo ni pamoja na mtambo wa kuchoronga miamba (Drill Rig), gari la kubeba mawe mazito ndani ya mgodi (Dump Truck) na mtambo wa kukatua miamba (Excavator).

***182. Mheshimiwa Spika***, Serikali za Tanzania na Zambia kwa upande mmoja na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa upande mwingine zipo katika hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za Makubaliano ya Itifaki ya 16 ya ushirikiano wa kiufundi. Kupitia Itifaki hizi, Serikali ya China imekuwa ikitoa mikopo yenye masharti nafuu kwa TAZARA. Miradi itakayotekelezwa kupitia Itifaki ya 16 ni pamoja na ununuzi wa vipuri vya kuimarisha njia ya reli, vichwa vya treni na mabehewa.

**USAFIRI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA MAJI**

**Udhibiti wa Huduma za Usafiri kwa njia ya Maji**

***183. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (Tanzania Shipping Agencies Corporation - TASAC) imeendelea kudhibiti ulinzi na usalama wa vyombo vya usafiri kwa njia ya maji na kudhibiti uchafuzi wa mazingira majini utokanao na shughuli za usafiri kwa njia ya maji. Pia, Shirika limeendeleza na kupanua huduma za sekta ya usafiri kwa njia ya maji; kudhibiti huduma za bandari na usafiri kwa njia ya maji; na kuhimiza ufanisi, uchumi na ushindani katika biashara ya uwakala wa Meli. Aidha, TASAC imeendelea kufanya kazi za uwakala wa Meli kwa nia ya kulinda maslahi

mapana ya nchi katika usafirishaji wa makinikia, madini, nyara za Serikali, wanyama hai, mafuta ya kupikia, petroli, vilainishi, silaha, vilipuzi, sukari ya nyumbani na viwandani, kemikali, gesi, mbolea, ngano na mazao ya mafuta (oil products).

***184. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, TASAC imeendelea kuimarisha usalama, ulinzi na kudhibiti uchafuzi wa mazingira utokanao na Meli ili kuhakikisha mazingira endelevu ya Bahari na Maziwa. Katika kipindi hicho, Shirika lilifanya kaguzi 5,334 za vyombo vidogo (chini ya tani 50) ambapo jumla ya vyombo 4,955 sawa na asilimia 92.89 vilikidhi matakwa ya kiusalama na kupewa vyeti vya ubora katika maeneo ya Mtwara, Lindi, Dar es Salaam, Tanga, Kagera, Katavi, Kigoma, Mara, Mbeya, Mwanza, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Njombe, Geita na Ukerewe. Aidha, jumla ya kaguzi 225 zilifanyika kwa Meli zenye ukubwa wa tani 50 au zaidi, zilizosajiliwa Tanzania na zinazotoka nje ya nchi.

Kati ya kaguzi hizo, kaguzi 204 sawa na asilimia 90.67 zilikidhi viwango vya ubora. Kaguzi hizo zilifanyika katika maeneo ya maji mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Kigoma, Tanga, Kagera, Mtwara, Lindi, Mara, Geita, Rukwa/Katavi, Mwanza, Ukerewe na Mbeya. Meli zilizobainika kutokidhi matakwa ya kiusalama zilipewa maelekezo ya kusimamisha utoaji wa huduma hadi marekebisho yatakapofanyika.

***185. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TASAC imeendelea kuratibu shughuli za utafutaji na uokoaji wakati wa matukio na ajali za usafiri kwa njia ya maji, kupitia kituo cha kuratibu shughuli za utafutaji na uokoaji Majini (Maritime Rescue Coordination Centre - MRCC) kilichopo Dar es Salaam. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, Kituo kilipokea taarifa za ajali nne (4) za vyombo vya usafiri kwa njia ya maji ambazo zilitokea katika maeneo ya maji yaliyomo Tanzania Bara. Ajali hizo zilihusisha jumla ya watu 136; ambapo kati yao watu 20 walipoteza maisha na watu 116 waliokolewa. Aidha, Kituo kilipokea jumla ya taarifa za matukio (maritime distress) 11 yaliyohusisha jumla ya watu 50, ambao wote waliokolewa.

***186. Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kutumia mifumo ya kielektroniki ili kuimarisha utendaji, kuboresha utoaji huduma, kuweka uwazi na kuvutia uwekezaji. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, Shirika limeimarisha mfumo wa kielektroniki wa uingizaji shehena (Manifest Billing), uhifadhi na ufuatiliaji wa taarifa zinazohusiana na watoa huduma za bandari, uingizaji na utoaji wa mizigo inayoingia na kutoka nje ya nchi (exports and imports manifest billing) pamoja na taarifa za mizigo inayopita kwenye mipaka (*Border post seaborne cargo manifest billing*). Mifumo mingine iliyoanzishwa ni pamoja na Mfumo wa Ugomboaji wa shehena katika maeneo ya Forodha, Mfumo wa uwakala wa Meli, Mfumo wa uhakiki Shehena (*Shipping Business Management System*) na Mfumo wa mabaharia (*Seafarers online application*).

***187. Mheshimiwa Spika,*** TASAC imeendelea kutekeleza na kuboresha biashara ya usafiri kwa njia ya maji ili kuiwezesha Tanzania kunufainika na fursa ya kijiografia iliyonayo. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, TASAC ilihudumia jumla ya Meli 337 zilizoingia nchini na kufanya ugomboaji wa shehena kupitia kadhia 13,015 za bidhaa zote zenye maslahi mapana kwa Taifa ambazo ziliondoshwa nchini. Aidha, Shirika lilifanya uhakiki wa shehena iliyopakuliwa na kupakiwa kwenye meli 556. Aina na kiwango cha shehena kilichofanyiwa uhakiki katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 ni pamoja na:

i. Shehena ya kichele (dry bulk cargo) yenye uzito wa tani 2,091,121.11 kutoka kwenye idadi ya meli 83;

ii. Shehena ya mchanganyiko (break bulk) yenye uzito wa tani 568,693.77 kutoka kwenye idadi ya meli 85;

iii. Makasha (containers) 404,366 ya mizigo aina mbalimbali kutoka kwenye meli 272;

iv. Idadi ya magari yapatayo 106,809 kutoka kwenye meli 116; na

vi. Mizigo aina mbalimbali kutoka kwenye makasha (destuffing and stuffing tally) 2,537.

***188. Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kukagua utendaji wa bandari nchini na usafiri wa meli kwa lengo la kujiridhisha na uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, viwango vya huduma, utoshelevu wake kwa wateja na kutoa miongozo kadiri ilivyoonekana inafaa. Bandari zilizokaguliwa ni pamoja na Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Kigoma, Kyela na Mwanza. Aidha, Shirika lilifanya kaguzi za utendaji wa makampuni ya uwakala wa meli, Uwakala wa ugomboaji shehena, wakusanyaji na watawanyaji shehena ndogondogo (cargo consolidators and de-consolidators), bandari kavu, wapima uzito wa makasha (Gross mass verifiers) na watoa huduma mchanganyiko bandarini.

**Huduma za Uchukuzi Baharini**

***189. Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Meli ya Tanzania na China (SINOTASHIP) imeendelea kutoa huduma za uchukuzi wa masafa marefu baharini. Kampuni hii ilianzishwa kwa Sheria ya Makampuni Sura ya 212 na kupewa majukumu ya kutoa huduma za uchukuzi wa masafa marefu baharini. Kampuni inamilikiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

***190. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, kampuni ilisafirisha jumla ya tani 609,000 za shehena ya mizigo ikilinganishwa na tani 605,000 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2019/ 2020. Hili ni ongezeko la asilimia 0.7 ya mizigo iliyosafirishwa. Aidha, katika kipindi hicho, Kampuni ilifanya biashara ya uwakala na kuhudumia meli ambapo jumla ya makasha 50,000 yalihudumiwa katika bandari ya Dar es Salaam ikilinganishwa na makasha 47,000 ya mwaka 2019/2020. Hili ni ongezeko la asilimia 6.4. Ongezeko hili linatokana na kutanuka kwa biashara ya uwakala wa meli ambapo kwa sasa kampuni ni wakala wa meli za COSCO na *Oriental Overseas Container Line (OOCL)* zinazoleta na kuondosha mizigo katika bandari ya Dar es Salaam.

**Huduma za Uchukuzi Katika Maziwa**

***191. Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Huduma za Meli (Marine Services Company Limited - MSCL) imeendelea kutoa huduma ya usafiri wa abiria na mizigo katika maziwa makuu ya Tanganyika, Victoria na Nyasa. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, Kampuni hii inayomilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 ilisafirisha jumla ya abiria 220,122 ikilinganishwa na abiria 55,053 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2019/2020. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 400. Kuongezeka kwa abiria kumetokana na kuanza kutoa huduma kwa Meli mbili (2) za New Victoria *Hapa Kazi Tu* na New Butiama *Hapa Kazi Tu* baada ya kufanyiwa ukarabati mkubwa na kuanza kutoa huduma mwezi Agosti, 2020. Aidha, katika kipindi hicho, Kampuni ilisafirisha tani za mizigo 13,941.44 ikilinganishwa na tani za mizigo 26,830.16 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020. Upungufu wa mizigo iliyosafirishwa katika kipindi hicho unatokana na kusimama kwa Meli ya MV Clarias; na Meli za mizigo ambazo ni MV Umoja inayosafirisha shehena ya mizigo kutoka Mwanza kwenda Portbell, Uganda na MT Sangara inayosafirisha shehena ya mafuta kutoka Kigoma kwenda DR Congo kwa ajili ya ukarabati mkubwa.

***192. Mheshimiwa Spika,*** Kuhusu mapato, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, MSCL ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 3.58 ikilinganishwa na Shilingi milioni 897.86 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020. Mapato haya ni sawa na ongezeko la asilimia 399. Aidha, matumizi ya mifumo ya TEHAMA pia yamechangia katika kuongeza mapato kutokana na kudhibiti upotevu wa mapato.

***193. Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya MSCL imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Meli moja (1) mpya ya kubeba abiria na mizigo pamoja na Chelezo katika Ziwa Victoria. Aidha, MSCL iliendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa meli katika Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria pamoja na Ujenzi wa Meli mpya ya Mizigo Bahari ya Hindi. Hadi kufikia Aprili, 2021 utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

i. Ujenzi wa Meli mpya ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo umekamilika kwa asilimia 69.5 na utakamilika Disemba, 2021;

ii. Ujenzi wa chelezo katika Ziwa Victoria umekamilika ambapo mradi upo kwenye kipindi cha uangalizi;

iii. Ukarabati wa Meli za MV Victoria na MV Butiama umekamilika na Meli hizo zinaendelea kutoa huduma tangu Agosti, 2020. Mradi huu sasa upo kwenye kipindi cha uangalizi;

iv. Mzabuni wa ujenzi wa Meli Mpya *Wagon Ferry* yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 za mabehewa ya mizigo katika Ziwa Victoria amepatikana na taratibu za upekuzi (Due Dilligence) zinaendelea kabla ya kusainiwa kwa Mkataba;

v. Mzabuni wa ujenzi wa Meli mpya ya kubeba shehena ya mizigo (Barge/Cargo Ship) katika Ziwa Tanganyika amepatikana na taratibu za upekuzi zinaendelea kabla ya kusainiwa kwa mkataba;

vi. Mzabuni wa ujenzi wa Meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo katika ziwa Tanganyika amepatikana na taratibu za upekuzi zinaendelea kabla ya kusainiwa kwa mkataba;

vii. Mzabuni wa ukarabati mkubwa wa Meli ya MV Umoja (Ziwa Victoria) amepatikana na taratibu za upekuzi zinaendelea kabla ya kusainiwa kwa mkataba;

viii. Mzabuni pekee aliyepatikana kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa meli ya MV. Liemba katika Ziwa Tanganyika alikosa vigezo. Hivyo, Zabuni hiyo imetangazwa upya na itafunguliwa Juni, 2021;

ix. Zabuni kwa ajili ya ujenzi wa Meli mpya ya mizigo katika Bahari ya Hindi ilifunguliwa tarehe 8 Machi, 2021. Uchambuzi wa zabuni hizo unaendelea;

x. Nyaraka za zabuni zinaendelea kuandaliwa kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa Meli ya uokozi na kuvuta tishari ya MT.Ukerewe katika Ziwa Victoria; na

xi. Nyaraka za zabuni zinaendelea kuandaliwa kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa Meli ya kubeba shehena ya mafuta ya MT.Nyangumi katika Ziwa Victoria.

**Huduma za Bandari**

***194. Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (Tanzania Ports Authority - TPA) imeendelea kumiliki Bandari za Mwambao na za Maziwa kwa kusimamia na kuendeleza Bandari hizo, kuendeleza huduma za kibandari, kuweka viwango na masharti kwa watoa huduma za Bandari nchini, kusimamia na kudhibiti huduma za bandari, kulinda mazingira na usalama wa Bandari kwa viwango vinavyokubalika pamoja na kuweka mazingira mazuri yatakayowavutia wawekezaji kuwekeza katika sekta ya bandari. Aidha, Mamlaka imeendelea kutangaza bandari kimasoko, kushirikisha na kusimamia sekta binafsi katika uendeshaji wa shughuli za kibandari.

***195. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, TPA ilihudumia shehena ya tani za mapato milioni 9.97 na kukusanya mapato ya **shilingi bilioni 670.66** ikilinganishwa na shehena ya tani za mapato milioni 10.42 iliyohudumiwa na kukusanya **shilingi bilioni 744.17** katika kipindi kama hicho katika mwaka 2019/2020. Aidha, jumla ya magari 107,869 yalipakuliwa katika Bandari ya Dar es Salaam ikilinganishwa na magari 125,758 yaliyopakuliwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2019/2020. Sababu za kushuka kwa utendaji huu ni pamoja na athari za mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 uliosababisha mdodoro wa shughuli za usafirishaji kwa njia ya maji duniani pamoja na uchache wa vifaa na mitambo ya kuhudumia shehena.

***196. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu uhudumiaji wa makasha, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, Kitengo cha Shehena Mchanganyiko (TPA General Cargo) kilihudumia makasha (TEUs) 70,716 ikilinganishwa na makasha (TEUs)

101,649 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020. Aidha, Kitengo cha TICTS kilihudumia makasha (TEUs) 469,229 ikilinganishwa na makasha (TEUs) 458,526 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020. Pamoja na athari za mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19, ufinyu wa nafasi katika gati za TPA kulikosababishwa na kazi zinazoendelea za maboresho ya Bandari ya Dar es Salaam kulisababisha Kitengo cha Shehena Mchanganyiko kuhudumia makasha machache.

***197. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPA inaendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya uboreshaji wa bandari ya Tanga. Mkataba wa mradi wa uboreshaji wa Bandari hii ulisainiwa Julai, 2020 kati ya TPA na M/s *China Harbour Engineering Co Ltd*. Utekelezaji wa Mradi huu ambao utagharimu Shilingi bilioni 256.8 ulianza Septemba, 2020 na utakamilika Juni, 2022. Kazi zitakazotekelezwa kwenye Mradi huu zinajumuisha kuongeza kina cha lango la kuingia na kugeuzia meli na kuimarisha na kuboresha gati na 1 na 2. Kuhusu ujenzi wa Gati la kupokelea mafuta kutoka Uganda lililoko eneo la Chongoleani, TPA inaendelea na maandalizi ya ujenzi wa Gati hilo wakati majadiliano ya utekelezaji wa mradi huu baina Tanzania na Uganda yakiwa yanaendelea.

***198. Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali ya Mitaa (TAMISEMI) zinatambua changamoto na athari za uwepo wa bandari zisizo rasmi (bandari bubu) katika pwani ya Bahari ya Hindi na kwenye Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Hadi sasa kuna jumla ya Bandari zisizo rasmi 694 zilizotambuliwa. Kati ya hizo, bandari 240 ziko katika mwambao wa bahari ya Hindi; Bandari 329 katika Ziwa Victoria, Bandari 108 katika ziwa Tanganyika na Bandari 17 katika Ziwa Nyasa. Athari za uwepo za bandari hizi ni pamoja na hatari za kiulinzi, kiusalama na upotevu wa mapato ya Serikali. Aidha, kuna ushindani usio sawia (unfair Competition) baina ya bandari rasmi na zisizo rasmi pamoja na biashara inayofanywa baina ya hizo bandari mbili tofauti. Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI imeshazielekeza Taasisi zinazohusika na suala hili kuendelea na zoezi la kutathmini bandari zisizo

rasmi ili kuishauri Serikali kuzirasmisha kwa lengo la kuimarisha usalama, kuongeza fursa za ajira na mapato ya Serikali. Hadi Aprili, 2021, jumla ya Bandari zisizo rasmi 119 zimeainishwa katika awamu ya kwanza kwa ajili ya kuzifanyia tathmini ya kina ya kuzirasimisha. Kati ya hizo, katika mwambao wa Bahari ya Hindi zipo 31, Ziwa Victoria (79), Ziwa Tanganyika sita (6) na Ziwa Nyasa tatu (3).

***199. Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 katika miradi ya kuboresha Bandari za Mwambao wa Bahari ya Hindi za Dar es Salaam na Mtwara ni pamoja na:

i. Kukamilisha ujenzi wa gati Na. 5 katika Bandari ya Dar es Salaam. Ujenzi wa gati Na. 6-7 unaendelea na unatarajiwa kukamilika Juni, 2021;

ii. Kusaini Mkataba kwa ajili ya kazi ya kupanua, kuchimba na kuongeza kina cha lango la kuingilia na kutokea meli katika Bandari ya Dar es Salaam. Mkataba huu uliosainiwa Februari, 2021 utatekelezwa na Kampuni ya M/S CHEC (China) kuanzia Mei, 2021; na

iii. Kukamilika kwa ujenzi wa gati moja (multipurpose terminal) lenye urefu wa mita 300 katika Bandari ya Mtwara. Mradi huu ulioanza Machi, 2017 ulikamilika Oktoba, 2020.

***200. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa bandari zilizopo kwenye Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:

**i. Bandari za Ziwa Victoria:**

a. Mradi wa ujenzi wa Bandari ya Magarini, Muleba uliohusisha ujenzi wa gati, majengo ya mizigo na abiria, vyoo, mnara wa tanki la maji, nyumba ya mlinzi ulianza Aprili, 2018 na kukamilika Juni, 2019;

b. Ujenzi wa Bandari ya Nyamirembe uliohusisha ujenzi wa gati na majengo ya utawala, abiria na kuhifadhia mizigo ulikamilika Novemba, 2019; na

c. Ujenzi wa mradi wa Bandari ya Lushamba uliohusisha ujenzi wa Gati, Jengo la Abiria, Ghala la Mizigo, Mnara wa Tanki la Maji, Uzio na Nyumba ya Mlinzi ulikamilika Julai, 2019.

**ii. Bandari za Ziwa Tanganyika:**
a. Ujenzi wa gati la Kalya/Sibwesa uliohusisha ujenzi wa gati na miundombinu mingine (ofisi ya walinzi, ghala la kuhifadhia mizigo, jengo la abiria, choo pamoja na banda la jenereta) ulikamilika Februari, 2020. Mradi huu uko katika kipindi cha uangalizi;

b. Ujenzi wa mradi wa bandari ya Lagosa unaohusisha ujenzi wa gati na majengo ya utawala, abiria na ghala la kuhifadhia mizigo ulikamilika Disemba, 2020. Mradi huu pia uko katika kipindi cha uangalizi;

c. Ujenzi wa bandari ya Karema unaohusisha ujenzi wa gati, majengo ya abiria, maghala ya mizigo na ofisi mbalimbali; uongezaji wa kina, *breakwaters* na usawazishaji wa eneo umekamilika kwa asilimia 35. Mradi huu ulioanza kutekelezwa Oktoba, 2019 kupitia Kampuni ya *Xiamen Ongoing Construction Group Co. Limited* utakamilika Oktoba, 2021; na

d. Ujenzi wa mradi wa Magati ya Kibirizi na Ujiji unaohusisha ujenzi wa Gati, majengo ya abiria, maghala ya mizigo, minara ya matanki ya maji, ofisi ya meneja wa Bandari, uzio na nyumba ya mlinzi umekamilika kwa asilimia 20. Mradi huu unaotekelezwa kupitia Kampuni ya *China Railway 15 Bureau Group Corporation* ulianza Machi, 2019 na utakamilika Julai, 2021.

**iii. Bandari za Ziwa Nyasa:**
a. Ujenzi wa Gati za Mbamba Bay, Manda na Matema upo katika hatua ya upembuzi yakinifu kwa kutumia Mhandisi Mshauri kampuni ya Royal Haskoning DHV ya Uholanzi ikishirikiana na CPCS ya Canada na Inter Consult ya Tanzania. Upembuzi yakinifu ulianza Oktoba, 2019 na utakamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2021. Mhandisi Mshauri

ameshawasilisha Taarifa ya Kati (Interim Report) ikijumuisha upimaji wa ardhi, maji na udongo;

b. Mradi wa ujenzi wa gati la Ndumbi unaohusu sehemu ya kushushia abiria na mizigo (ramp) na sakafu ngumu umekamilika kwa asilimia 65. Mradi huu ulianza kutekelezwa Disemba, 2019 kwa kutumia Mkandarasi M/s CHICO na utakamilika Oktoba, 2021; na

c . Mradi wa ujenzi wa meli mpya ya abiria na mizigo yenye uwezo wa kusafirisha abiria 400 na tani 200 za mizigo uliotekelezwa na Kampuni ya Songoro Marine Transport Ltd ya Tanzania umekamilika na kuzinduliwa rasmi na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Februari, 2021.

***201. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ununuzi wa vifaa na mitambo kwa ajili ya kutoa huduma za kibandari katika bandari zinazoendeshwa na TPA, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, vifaa na mitambo iliyonunuliwa ni pamoja na:

i. Mizani inayohamishika (Movable Weighbridges) miwili (2) yenye uwezo wa kupima tani 100 kila moja;

ii. Malori (highway tractors) tisa (9) yenye uwezo wa tani 30 kila moja;

*iii. Reach Stacker* saba (7) zenye uwezo wa kubeba tani 45 kila moja;

iv. Krini (Mobile Crane) mbili (2), moja (1) ina uwezo wa kubeba tani 30 na nyingine ina uwezo wa kubeba tani 15;

v. Krini (All Terrain Crane) moja (1) yenye uwezo wa kubeba tani 50 na Krini (Portal Crane) moja (1) yenye uwezo wa kubeba tani 30;

vi. Krini (Mobile Crane) moja (1) yenye uwezo wa kubeba tani 45;

vii. Krini (Harbour Mobile Crane) mbili (2) zenye uwezo wa kubeba tani 100 kila moja;

viii. Krini (Mobile Crane) moja (1) yenye uwezo wa kubeba tani 120;

ix. Vijiko (Wheel loader) sita (6) vyenye uwezo wa kubeba tani 7 kila moja;

x. Grabs tano (5) zenye uwezo wa kubeba tani 15 kila moja;

xi. Mashine za kunyanyulia mizigo (Forklifts) 12 zenye uwezo wa kubeba tani 3 kila moja;

xii. Mashine za kunyanyulia mizigo (Forklifts) 12 zenye uwezo wa kubeba tani 25 kila moja; na

xiii. Mashine za kunyanyulia mizigo (Forklifts) mbili (2) zenye uwezo wa kubeba tani 16 kila moja.

## USAFIRI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA ANGA

### Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Anga

***202. Mheshimiwa Spika,*** udhibiti wa huduma za usafiri wa anga, viwanja vya ndege, masuala ya kiusalama na kiuchumi katika usafiri wa anga na utoaji wa huduma za uongozaji ndege zimeendelea kutolewa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga (Tanzania Civil Aviation Authority - TCAA). Huduma za uongozaji ndege zimeendelea kutolewa kupitia vituo 14 vya Dar es Salaam, Zanzibar, Mwanza, Arusha, Pemba, Tabora, Kigoma, Dodoma, Iringa, Songwe, Mtwara, Tanga, Songea na Kilimanjaro. Mamlaka hii pia imeendelea kudhibiti Viwanja vya Ndege vinavyomilikiwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA), Wizara ya Maliasili na Utalii, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na Sekta Binafsi. Lengo ni kuimarisha utoaji huduma, kukuza utalii nchini na kuendelea kuhakikisha utekelezaji wa Sheria na Kanuni za uendeshaji wa Viwanja vya Ndege zinafuatwa.

***203. Mheshimiwa Spika,*** itakumbukwa kuwa katika Hotuba ya mwaka 2020/2021, tulitoa taarifa ya kukamilika kwa Mradi wa kufunga Mfumo wa kuongoza Ndege kutua salama (Instrument Landing System - ILS) uliogharimu Shilingi bilioni 4.6 katika Kiwanja cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume - Zanzibar. Hatua iliyokuwa inafuata ilikuwa ni kufanya majaribio ya mitambo hiyo lakini haikufanyika kutoka janga la virusi vya Corona, hivyo kufanya huduma hiyo kutokutolewa. Napenda kutoa taarifa kuwa Mitambo hiyo imefanyiwa majaribio na kuonesha kuwa inafaa kwa ajili ya kuongozea ndege. Hatua inayofuata ni kutoa mafunzo kwa waongoza ndege kuhusu matumizi ya mitambo hiyo. Mafunzo hayo yatafanyika kwa kushirikisha wataalam kutoka Tanzania bara na Tanzania Zanzibar.

***204. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, idadi ya Abiria wanaotumia usafiri wa anga imepungua hadi kufikia abiria 2,495,379 ikilinganishwa na abiria 4,423,732 waliotumia usafiri huo katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2019/2020. Upungufu huu ni sawa na asilimia 43. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, idadi ya Abiria wanaosafiri ndani ya nchi imepungua hadi abiria 1,676,107 ikilinganishwa na Abiria 2,342,059 waliosafiri katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020. Upungufu huu ni sawa na asilimia 28.4. Idadi ya Abiria wanaosafiri kwenda na kutoka nje ya nchi imepungua kutoka abiria 2,081,673 hadi kufikia abiria 819,272. Upungufu huu ni sawa na asilimia 60. Sababu za kupungua kwa abiria wanaosafiri ndani na nje ya nchi umetokana na mlipuko wa ugonjwa wa COVID 19 ambapo nchi nyingi zilifunga na kuzuia safari za anga.

***205. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, mizigo iliyosafirishwa ni tani 19,779 ikilinganishwa na tani 20,417 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020. Upungufu huu ni sawa na asilimia 3.1. Aidha, katika kipindi hicho, miruko ya safari za Ndege imeshuka hadi miruko 103,110 kutoka miruko 175,567 ya mwaka 2019/2020. Huu ni upungufu wa miruko kwa asilimia 41.3. Kushuka kwa usafirishaji wa abiria, mizigo na miruko ya Ndege kwa kiasi kikubwa

kunatokana na mlipuko wa virusi vya Corona unaoendelea duniani kote.

***206. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kusaini au kupitia upya Mikataba ya usafiri wa Anga (Bilateral Air Services Agreements - BASA) kati yake na nchi nyingine ili kufungua soko la usafiri wa anga nchini kwa lengo kuboresha huduma za usafiri wa anga, kuvutia mashirika mengine kutoa huduma nchini na kuimarisha ushindani katika utoaji wa huduma za usafiri wa anga nchini. Hadi Aprili, 2021, Tanzania ilikuwa imeingia Mikataba ya BASA na nchi 74.

Kati ya Mikataba hiyo, Kampuni na Mashirika ya Ndege 17 kutoka nchi 15 yanafanya safari za Ndege mara 86 kwa juma kati ya Tanzania na nchi hizo. Mashirika hayo ya Ndege ni pamoja na: Emirates, LAM Mozambique, Kenya Airways, Royal Dutch (KLM), Ethiopian Airlines, Qatar Airways, Egypt Air, Rwandair, Oman Air, Turkish Airlines, Malawi Airlines, Fly Dubai, Uganda Airlines, Air Zimbabwe, AB Aviation, EWA Air na Airlink (PTY) Ltd.

***207. Mheshimiwa Spika,*** Kazi nyingine zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 ni pamoja na:

i. Kukamilisha ujenzi na ufungaji wa Rada za kuongozea ndege za kiraia katika kituo cha Songwe;

ii. Kubadilisha mfumo wa usambazaji taarifa za ndege kimtandao (AXIM - Aeronautical Information Exchange Modal) kwa ajili ya kuboresha taarifa na takwimu za ndege;

iii. Kufanya uhakiki wa vifaa vya kuongozea mienendo ya ndege katika vituo vya KIA, JNIA, AAKIA na Mwanza;

iv. Kuandaa Kanzi Data kwa ajili ya sehemu za uwanda wa Nchi unaoonesha miinuko, milima, mabonde na vizuizi (e-TOD – Electronic terrain and obstacle data) katika viwanja vya kimataifa vya Julius Nyerere, Kilimanjaro na Abeid Amani Karume;

v. Kukamilika kwa ufungaji wa mitambo ya umeme wa nishati ya jua (solar) katika vituo vya ndege vya Dodoma, Mtwara, Tanga, Iringa, Kigoma, Pemba, Arusha na Songwe kwa gharama ya shilingi milioni 240. Nishati hii ni mbadala ya umeme na inapunguza gharama za uendeshaji na utoaji huduma za usafiri wa anga;

vi. Kukamilisha Makubaliano (negotiation) kati ya TCAA na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO) kuhusu kufanya utafiti wa awamu ya pili ya ufungaji wa mtambo wa kusoma mwendendo wa ndege na hivyo kutoa taarifa sahihi za mahali ndege ilipo uitwao *Automatic Dependent Surveillance-Broadcast* (ADS-B) kwa upande wa Magharibi wa nchi;

vii. Kuendelea na manunuzi ya vifaa vya mawasiliano ya sauti kati ya Marubani na waongoza ndege katika Kiwanja cha JNIA;

viii. Kufunga kanzidata ya kutunza takwimu za sekta ndogo ya usafiri wa anga. Mradi huu umekamilika kwa asilimia 20;
ix. Kukagua viwanja vya ndege vya kimataifa vya Julius Nyerere, Amani Abedi Karume na Kilimanjaro ili kusimamia, kudhibiti na kuboresha usalama wa usafiri wa anga;

x. Kuendelea na uhakiki wa maeneo mapya ya ujenzi wa Viwanja vya ndege ikiwa ni pamoja na Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato;

xi. Kusimamia udhibiti wa usalama wa viwanja vya ndege, mashirika ya ndege pamoja na watoa huduma zinazoendana na usafiri wa anga ili kuhakikisha kwamba viwanja vya ndege nchini havitumiki kwa matendo ya kihalifu dhidi ya usalama wa usafiri wa anga; na

xii. Kutoa mafunzo ya usalama na leseni za ukaguzi (Screeners Certification Licences) katika viwanja vya ndege kwa maafisa usalama 315 kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

**Huduma za Viwanja vya Ndege**

***208. Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) imeendelea kutoa huduma kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya Usafiri wa Anga. Mamlaka hii ina jukumu la kusimamia, kuendesha na kuendeleza viwanja vya ndege 59 vinavyomilikiwa na Serikali isipokuwa vilivyo chini ya Mamlaka za Hifadhi, Halmashauri, Jeshi na Taasisi binafsi. Katika utekelezaji wa majukumu yake, TAA imeendelea kusimamia shughuli za uendeshaji wa Jengo jipya la Tatu la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere na kuhakikisha huduma zinaendelea kutolewa katika Jengo hilo; kuboresha huduma za ulinzi na usalama katika Viwanja vya Ndege pamoja na kutoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi wake.

***209. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TAA imeendelea kuboresha ulinzi na usalama viwanjani ili kukidhi matakwa ya kimataifa na kuvutia uwekezaji. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, kazi ya kufunga mifumo ya ufuatiliaji mienendo ya shughuli za kiusalama na uendeshaji (CCTV) katika Viwanja vya Ndege vya JNIA, Mtwara na Lake Manyara imekamilika. Aidha, kazi ya ujenzi wa uzio wa usalama katika Kiwanja cha ndege cha Mwanza inaendelea.

***210. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TAA imekamilisha kazi ya upanuzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege kutoka mita 1,688 hadi mita 1,888 katika Kiwanja cha Ndege cha Arusha. Uboreshaji huu umewezesha Kiwanja hiki kuwa na uwezo wa kupokea ndege yenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 50. Kazi nyingine zilizotekelezwa kwenye kiwanja hiki ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa maegesho mapya ya ndege (*remote Apron*), barabara ya kiungio (taxiway), maegesho ya magari (*Car Parking*), ufungaji wa mfumo wa kielektroniki wa maegesho ya magari na ujenzi wa barabara ya kuingia kiwanjani (Access Road) kwa kiwango cha lami. Aidha, maandalizi ya ukarabati wa Jengo la abiria yanaendelea. Uboreshaji wa Kiwanja hiki utasaidia kuvutia mashirika ya ndege hususan yanayobeba Watalii kutumia kiwanja hiki kwani abiria wa mashirika hayo ikiwemo ATCL watapata huduma bora wawapo Kiwanjani.

***211. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha ufanisi wa utoaji huduma katika viwanja vya ndege, Mamlaka imeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi mara kwa mara kwa wafanyakazi wake. Hadi Aprili, 2021, TAA ilitoa mafunzo kwa jumla ya wafanyakazi 251 katika nyanja za Zimamoto na Uokoaji, ulinzi na usalama, uendeshaji na TEHAMA. Aidha, TAA imeandaa na kukamilisha programu za ulinzi na usalama kwa Viwanja vya Ndege vya JNIA, Mwanza, Songwe, Mtwara, Lindi, Nachingwea, Arusha, Lake Manyara, Kilwa Masoko, Mafia, Iringa, Dodoma, Songea, Geita na Tanga. Mamlaka Pia imefanya zoezi la uokoaji wakati wa dharura ya ajali katika Kiwanja cha ndege cha Lake Manyara na zoezi la utayari wa matukio hatarishi ya kiusalama (*Security Contingency Exercises*) kwa Kiwanja cha ndege cha Mtwara.

***212. Mheshimiwa Spika*****,** ili kuhakikisha Mamlaka inaendana na kasi ya ukuaji wa shughuli za usafiri wa anga nchini unaopelekea mahitaji ya upanuzi na ujenzi wa viwanja vipya, TAA imeendelea na juhudi za utwaaji, upimaji na upatikanaji wa Hati Miliki katika Viwanja vya Ndege mbalimbali ikiwemo Dodoma, Iringa na Chunya.

***213. Mheshimiwa Spika,*** uendelezaji na uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (Kilimanjaro International Airport - KIA) umeendelea kusimamiwa na Kampuni ya Kuendeleza Viwanja vya Ndege ya Kilimanjaro (Kilimanajaro Airports Development Company - KADCO). Kampuni hii inamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100. Kampuni za Ndege zinazotoa huduma za ratiba maalum za safari katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro ni pamoja na Air Tanzania, Kenya Airways, Ethiopian Airline, Precision Air, Qatar Airways, Turkish Airlines, KLM Airlines, Air Kenya, Uganda Airlines na Rwandair. Makampuni yanayofanya safari zisizokuwa na ratiba maalum (kukodi) ni pamoja na Coastal Aviation, Regional Air, Northern Air, Zurik Air, El-Al Israel airlines na Auric Air.

***214. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, KADCO ilihudumia abiria 260,584 ikilinganishwa na abiria 661,502 waliohudumiwa katika kipindi kama hicho

katika mwaka 2019/2020. Hii ni pungufu kwa asilimia 61. Utendaji huu uliwezesha Kampuni kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 5.8 katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 ambayo ni upungufu kwa asilimia 378 ikilinganishwa na mapato ya jumla ya shilingi bilioni 22.27 yaliyokusanywa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2019/2020. Sababu za upungufu huo ni pamoja na kushuka kwa idadi ya watalii wanaowasili nchini kulikosababishwa na nchi nyingi kukumbwa na janga la COVID-19.

***215. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia KADCO imeendelea kukarabati jengo la mizigo inayohitaji ubaridi (Cold Storage Facility) ili kuvutia biashara ya usafirishaji wa mizigo mbalimbali kama vile mbogamboga, matunda na maua kupitia Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, kazi ya kufufua mashine mbili (2) za upoozaji (Compressor), ukarabati wa sakafu na kuziba nafasi zinazopitisha hewa (evaporator fans) 11 kwenye jengo ili kutunza ubaridi kwa muda mrefu imekamilika. Ukarabati huu umelenga kuwezesha bidhaa zinazosafirishwa kuwasili katika nchi husika zikiwa katika viwango vya ubora wa kimataifa. Hivyo, napenda kutumia fursa hii kuwasihi na kuwakaribisha wafanyabiashara ya mbogamboga, minofu ya nyama na samaki, matunda na maua kutumia kiwanja cha KIA kwani huduma za kuhifadhi mizigo kwenye ubaridi zinapatikana.

***216. Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa kuboresha huduma, ulinzi na usalama katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 ni pamoja na:

i. Kufunga kamera 183 za mfumo wa CCTV katika jengo la abiria (Terminal building), jengo la VIP na maeneo muhimu ya kuingia na kutoka kiwanjani;

ii. Kufunga mashine mpya za kisasa sita (6) za X-ray kwa ajili ya ukaguzi wa abiria na mizigo. Kati ya hizo, mashine nne (4) ni za ukaguzi wa mizigo ya wastani (ambazo zimefungwa kwenye jengo la abiria) na mashine mbili (2) ni za uwezo wa kukagua mizigo mikubwa (Cargo Screening Machines); na

iii. Kuboresha huduma za zimamoto na kuweka mazingira bora ya utendaji ya watumishi wa kitengo cha zimamoto kwa kununua vifaa mbalimbali kama *Foam compound* lita 5000, *Dry Chemical powder* (DCP) kilogramu 1500, *firesuit, fire blanket, na* kujenga bweni jipya la wanawake wa zimamoto.

**Huduma za Usafiri wa Anga**

***217. Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Ndege ya Tanzania (Air Tanzania Company Limited - ATCL) imeendelea kutoa huduma za kusafirisha abiria na mizigo ndani na nje ya Tanzania. Lengo la Kampuni hii inayomilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 ni kuinua uchumi wa nchi na ustawi wa wananchi, kutoa huduma nyingine zinazohusiana na usafiri wa anga ikiwa ni pamoja na matengenezo ya ndege, utoaji wa huduma Kiwanjani (ground handling services), uendeshaji wa kumbi za kupumzikia abiria na huduma ndani ya ndege. Kampuni binafsi zilizotoa huduma kwa ufanisi ndani ya nchi ni pamoja na Precision Air, AsSalaam, Auric, Coastal Air, Zanair, Air Excel, Tanzaniar, Sky aviation na Tropical air.

***218. Mheshimiwa Spika,*** ili ATCL iweze kutekeleza Mpango Mkakati wake wa miaka mitano ulioanzia mwaka 2017/18 – 2021/22 katika utanuzi wa mtandao wa safari za ndani ya nchi, kikanda na kimataifa kwa ufanisi, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, Serikali imeinunulia ATCL ndege mbili (2) aina ya A220-300 na ndege moja aina ya Dash 8 Q400. Utengenezaji wa Ndege hizo haukukamilika kwa muda uliopangwa kutokana na athari za mlipuko wa COVID-19 uliosababisha viwanda kusimamisha uzalishaji. Kati ya ndege hizo, ndege moja aina ya Dash 8 Q400 inatarajiwa kuwasili nchini Juni, 2021 na ndege nyingine mbili aina ya Airbus (A220-300) zinatarajiwa kuwasili nchini mwezi Agosti na Oktoba, 2021.

***219. Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizokamilika ni pamoja na:

i. Ununuzi wa jozi moja (1) ya Injini kwa ajili ya ndege aina ya Dash 8 Q400. Ununuzi wa Injini hizo utapunguza gharama za uendeshaji zilizokuwa zinatokana na ukodishaji wa injini wakati

injini zilizopo kwenye ndege zikipata hitilafu au zikiwa kwenye mzunguko wa kawaida wa matengenezo. Wastani wa gharama za kukodi injini hizo ni takriban Dola za Marekani 115,407.16 kwa mwezi; na

ii. Ukarabati wa miundombinu ya jengo, mfumo wa umeme na ufungaji wa jenereta katika karakana iliyopo Kiwanja cha Kimataifa cha Kilimanjaro ijulikanayo kama *Kilimanjaro Maintenance Facilities* (KIMAFA).

***220. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, ATCL imetoa huduma za usafiri wa anga katika vituo vya ndani 15 kutoka vituo 13 ilivyokuwa inatoa huduma katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020. Vituo hivyo ni Dar es Salaam, Zanzibar, Dodoma, Kilimanjaro, Mwanza, Arusha, Bukoba, Kigoma, Mbeya, Tabora, Songea, Iringa, Geita, Mtwara na Mpanda. Hivi sasa imesimama kutoa huduma katika vituo vya Iringa na Mtwara ili kupisha maboresho ya Viwanja hivyo. Kwa safari za kikanda na kimataifa zilizositishwa Machi, 2020 na kurejeshwa Novemba, 2020 kutokana na ugonjwa wa COVID – 19, ATCL kwa sasa inatoa huduma katika vituo vya kikanda vya Hahaya (Comoro), Entebbe (Uganda), Mumbai (India), Lusaka (Zambia) na Harare (Zimbabwe). Aidha, safari za kwenda Guangzhou, China, zitaanza Mei, 2021 baada ya kusimamishwa kuanza Machi, 2021 kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa COVID – 19 katika nchi hiyo.

***221. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, ATCL imesafirisha jumla ya abiria 389,419. Kati ya hao, abiria 347,006 walikuwa wa soko la ndani ya nchi na abiria 36,413 walitokana na soko la nje ya nchi. Utendaji huu ni pungufu kwa asilimia 32 ikilinganishwa na abiria 563,516 wa ndani na nje ya nchi waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020. Upungufu wa abiria umetokana na kuendelea kuwapo kwa masharti ya kuzuia kuenea kwa ugojwa wa COVID -19.

***222. Mheshimiwa Spika*****,** ATCL imeendelea kuboresha uwezo wake wa matengenezo ya ndege inazomiliki. Hadi Aprili, 2021,

ATCL ina uwezo wa kufanya matengenezo yote madogo ya ndege zake ndani ya nchi kwa kutumia wataalam wazawa. Pia, inafanya matengenezo makubwa hapa nchini kwa asilimia 70. Lengo ni kufanya matengenezo makubwa na madogo hapahapa nchini kwa asilimia 100 na kutoa huduma hiyo kwa makampuni mengine.

***223. Mheshimiwa Spika*,** ndege ya ATCL aina ya Dash 8 Q300 ambayo ilikuwa mbovu tangu mwaka 2016 imepelekwa nchini Malta kufanyiwa matengenezo makubwa (6C Check). Matengenezo hayo yanatarajiwa kukamilika Juni, 2021 na hivyo kuifanya ATCL kuwa na jumla ya ndege 12. Kukamilika kwa matengenezo ya Ndege hii kutaongeza wigo wa utoaji huduma zenye tija hata katika viwanja vyenye abiria kati ya 30 hadi 50.

***224. Mheshimiwa Spika*,** Serikali inatambua juu ya uwepo wa gharama kubwa za uendeshaji za ATCL na hivyo kusababisha hasara isiyo ya lazima. Hivyo, Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kupunguza gharama za uendeshaji. Hatua hizo ni pamoja na kulitafutia ufumbuzi deni lililorithiwa na ATCL iliyofufuliwa ili litoke katika Vitabu vya Mahesabu. Uwepo wa deni hili umechangia katika kuongeza gharama za uendeshaji.
Hatua nyingine ni kufanya mapitio ya Mkataba wa Ukodishaji Ndege kati ya ATCL na Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) ili kuiongezea ATCL nguvu ya ushindani. Maboresho hayo hayatagusa maeneo yanayohusu uwezo wa kufanyia matengenezo ndege zilizonunuliwa. Aidha, Serikali imeendelea kuisadia ATCL kuongeza mapato nje ya ubebaji wa abiria na mizigo kwa kuipa uendeshaji wa kumbi za kupumzikia wageni (lounges) katika viwanja vya Ndege vya Kimataifa vya Julius Nyerere (JNIA) na Kilimanjaro (KIA); na kuijenga uwezo wa kutoa huduma kwa ndege na abiria (ground handling services) katika Viwanja vya Ndege.

**HUDUMA ZA HALI YA HEWA**

***225. Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Hali ya Hewa (Tanzania Meteorological Authority - TMA) imeendelea kusimamia, kudhibiti na kuratibu utoaji wa huduma za hali ya hewa hapa

nchini. Majukumu mengine ni pamoja na kutoa utabiri wa hali ya hewa na tahadhari kuhusiana na hali mbaya ya hewa kwa walengwa, kupima na kufuatilia mifumo ya hali ya hewa na kutafiti kisayansi mabadiliko ya hali ya hewa nchini, kubadilishana taarifa za hali ya hewa katika mtandao wa dunia (Global Telecommunication System - GTS) kulingana na makubaliano ya Kimataifa na kuiwakilisha Tanzania katika masuala ya hali ya hewa Kikanda na Kimataifa. Aidha, Mamlaka iliendelea kutoa huduma za hali ya hewa kwa sekta za uzalishaji zikiwemo kilimo, viwanda, madini, utafiti na uvunaji wa gesi na uvuvi. Taarifa hizo zimechangia kuongeza ufanisi katika sekta hizo na hivyo kuongeza mchango wa huduma za hali ya hewa katika kufikia azma ya kukuza uchumi wa nchi yetu ili kufikia kiwango cha uchumi shindani.

***226. Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka iliendelea kutoa taarifa za mrejeo wa mwenendo wa hali ya hewa kadiri mabadiliko ya mifumo ya hali ya hewa yanapojitokeza ambapo usahihi wa utabiri umefikia asilimia 87.9. Kiwango hiki cha usahihi wa utabiri ni juu ya kiwango kinachokubalika na Shirika la Hali ya Hewa Duniani ambacho ni asilimia 70. Ubora huo wa utabiri umechangiwa kwa kiasi kikubwa na uboreshaji wa miundombinu na huduma za hali ya hewa ikiwemo ununuzi wa vifaa vya kisasa. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, kazi ya ukarabati wa vituo viwili (2) vya hali ya hewa vilivyopo KIA na JNIA imekamilika; ufungaji wa rada ya hali ya hewa huko Mtwara ulikamilika na kukabidhiwa Disemba, 2020; na malipo ya ununuzi wa Rada mbili (2) za hali ya hewa zitakazofungwa Mbeya na Kigoma yamekamilika kwa asilimia 90 na utengenezaji uko katika hatua za mwisho.

***227. Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 ni pamoja na:

i. Kuendelea na utekelezaji wa mfumo wa kudhibiti ubora wa huduma bora za hali ya hewa kwa sekta ya usafiri wa anga kulingana na viwango vya kimataifa. Hatua hii inatokana na kukidhi vigezo baada ya kufanyiwa ukaguzi wa Kimataifa kati ya tarehe 11 - 15 Januari, 2021na hivyo kuendelea kumiliki cheti cha ubora cha ISO 9001:2015;

ii. Kufanya tafiti mbalimbali za hali ya hewa na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo tafiti juu ya tathmini ya mvua za msimu wa Oktoba-Disemba, 2019 na athari zake katika jamii kwa upande wa Zanzibar. Tafiti hii ilichapishwa katika Jarida la Kimataifa linalojulikana kama (Journal of Atmospheric and Climate Sciences); na

iii. Kuendelea kufikisha huduma za hali ya hewa kwa wananchi kwa kuongeza idadi ya redio na luninga zinazotoa matangazo ya hali ya hewa. Hadi sasa taarifa za hali ya hewa zinatolewa katika vituo vya luninga 11 na vituo vya redio 65.

## C. 2 TAASISI ZA MAFUNZO

***228. Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa majukumu ya Taasisi za Mafunzo zinazosimamiwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 ni kama ifuatavyo:

### Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi

***229. Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT) ni kutoa mafunzo katika fani za Ujenzi, Umeme na Mitambo katika ngazi za chini na kati ili kuzalisha wataalam watakaohudumia Sekta ya Ujenzi. Kazi nyingine ni kuendesha mafunzo maalum (Short Courses Programmes) kwa wahitimu wa fani za kihandisi na zinazoendana ili kuwaandaa na kuwajengea uwezo wahitimu hao. Aidha, kazi nyingine ni kufanya tathimini ya mahitaji ya mafunzo ili kubainisha maeneo ambayo wataalam katika Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi wanahitaji maarifa mapya na kuandaa mafunzo ili kupunguza pengo lililopo kwa wataalam wa sekta katika suala la maarifa, ujuzi na teknolojia na kuendelea kutoa mafunzo ya matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvukazi katika kazi za ujenzi, matengenezo na ukarabati wa barabara. Vilevile, Taasisi ina jukumu la kuandaa na kuendesha semina na warsha kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali za Kikanda na Kimataifa kama Shirikisho la Barabara duniani (PIARC) na nyinginezo kuhusu namna bora ya uwekezaji katika miundombinu ya barabara na usafirishaji pamoja na kuandaa na kuendesha warsha, Makongamano na Mikutano mbalimbali kwa

ushirikiano na Taasisi mbalimbali za ndani, kikanda na Kimataifa kama ERB, CRB, IET, ILO, PIARC, IRF, ASANRA kwenye masuala yanayohusu teknolojia katika Sekta ya Ujenzi na usafirishaji.

***230. Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2021, Taasisi ilitoa mafunzo kwa wanafunzi **408** wa kozi ya ufundi Stadi (Artisans) ngazi ya VET daraja la I na II. Aidha, kupitia mafunzo ya kozi fupi wanafunzi waliohitimu ni **218** na wanaoendelea na masomo katika ngazi ya NTA 4 katika mwaka wa masomo 2020/21 ni Wanafunzi **26**.

Aidha, Taasisi imefanya matengenezo na ukarabati wa miundombinu msingi ya Taasisi ambayo ni matengenezo ya magari, ukarabati wa miundombinu ya maji safi, majitaka na umeme, ukarabati mabweni, ukarabati wa nyumba za watumishi na madarasa. Vilevile, ununuzi wa vitendea kazi, vifaa vya kufundishia na samani ulifanyika. Vilevile, Taasisi iliendelea na utoaji wa mafunzo ya matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika kazi za ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe na lami kwa barabara zinazopitisha magari machache yaani 'low traffic volume sealed roads' kupitia ICoT Tawi la Mbeya.

Taasisi ilitoa mafunzo kwa washiriki **104** katika kozi mbalimbali. Pia, Taasisi ilifanya uhamasishaji wa matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvukazi kwa kushiriki kwenye maonesho na kutembelea katika Halmashauri za mikoa. Mikoa iliyohusika na zoezi hili ni Dar es Salaam na Pwani ambapo jumla ya wadau **24** walifikiwa. Vilevile,Taasisi ilishiriki maonesho ya Nanenane na mkutano wa kitaalam wa Bodi ya Wahandisi (ERB) ambapo wadau wapatao **214** walifikiwa. Aidha, Taasisi iliendesha kozi maalum ya lami baridi kwa kushirikiana na ILO ambapo washiriki **20** walihudhuria mafunzo.

### Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)

***231. Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Bahari Dar es Salaam (Dar es Salaam Maritime Institute - DMI) kimeendelea kutoa mafunzo ya Ujuzi na Utaalamu (Certificates of Competency) katika masuala ya usafiri kwa njia ya maji kwa kuzingatia

viwango vilivyowekwa na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) na Shirika la Bahari Duniani (IMO). Aidha, Chuo hiki kinachoendesha mafunzo yake kwa kuzingatia Ubora wa Viwango vya Kimataifa yaani *ISO 9001:2015* kinatambuliwa na Baraza la Usimamizi wa Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE).

***232. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Chuo kilidahili jumla ya wanafunzi 4,527 ikilinganishwa na wanafunzi 2,410 waliodahiliwa katika mwaka 2019/20. Hii ni sawa na ongezeko la wanafunzi kwa asilimia 87.8. Kati ya hao, wanafunzi 2,937 wamejiunga na mafunzo ya muda mfupi na wanafunzi 1,590 wamejiunga katika mafunzo ya muda mrefu. Aidha, Chuo kimeanzisha kozi ya muda mrefu *Oil and Gas Engineering, Mechatronics Engineering, na Mechanical and Marine Engineering* kwa kiwango cha shahada ambapo jumla ya wanafunzi 63 walidahiliwa na wanaendelea na masomo. Pia Chuo kimeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake ambapo jumla ya watumishi 22 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu na Wafanyakazi 15 wamehudhuria kozi za muda mfupi.

**Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)**

***233. Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kimeendelea kutoa mafunzo, kufanya tafiti, kutoa ushauri wa kitaalam na machapisho katika Sekta ya Uchukuzi ili kuandaa wataalam katika njia zote za usafirishaji na uchukuzi ambazo ni barabara, anga, reli, maji na usafirishaji kwa njia ya bomba. Katika mwaka 2020/21, Chuo kilitoa mafunzo katika kozi 28 za muda mrefu ikilinganishwa na kozi 24 zilizotolewa katika mwaka wa masomo wa 2019/20. Ongezeko hili la kozi limefanya Chuo kuwa na wanafunzi 10,988 ikilinganishwa na wanafunzi 7,662 waliokuwepo katika mwaka wa masomo 2019/20. Hili ni ongezeko la wanafunzi 3,326 sawa na asilimia 43.

Aidha, mafunzo ya kozi 14 za muda mfupi yalitolewa katika mwaka 2020/21 ikilinganishwa na kozi 13 zilizotolewa katika mwaka wa masomo 2019/20. Kozi hizo zilidahili wanafunzi 1,821 ikilinganishwa na wanafunzi 2,070 waliopata mafunzo haya katika mwaka wa masomo 2019/20. Udahili huu ni sawa

na upungufu wa asilimia 14. Ili kukabiliana na upungufu wa washiriki wa kozi za muda mfupi, Chuo kimejipanga kuongeza idadi ya kozi mpya zinazoendana na mahitaji ya sekta ya usafirishaji na uchukuzi kwa kuzingatia miradi ya kimkakati inayotekelezwa nchini.

***234. Mheshimiwa Spika***, Serikali inatambua kuwa usafiri wa anga ni mhimili na kichocheo muhimu katika ukuaji wa uchumi na biashara. Ufanisi, uhakika na ubora wa huduma za usafiri wa anga unachangia kwa kiwango kikubwa ukuaji wa sekta nyingine kama vile utalii, biashara, viwanda na madini. Kutokana na kuwepo kwa changamoto ya uhaba wa marubani na wahandisi wa matengenezo ya ndege pamoja na gharama kubwa za kutoa mafunzo hayo nje ya nchi, mwezi Juni, 2015, Serikali kupitia NIT ilianzisha Shule Kuu ya Teknolojia ya Anga (School of Aviation Technology - SAT). Kupitia Shule hiyo, Chuo kinatoa mafunzo ya uhandisi wa matengenezo ya ndege, uhudumu wa ndani ya ndege na urubani. Kozi za uhudumu ndani ya ndege na uhandisi wa matengenezo ya ndege zilianza kutolewa mwaka wa masomo 2015/2016. Utoaji wa mafunzo ya urubani uko katika hatua za mwisho za kupata ithibati kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) baada ya kupata ndege za mafunzo. Hata hivyo, Chuo kinaendelea na majadiliano ya Mkataba wa ununuzi wa ndege mbili (2) za mafunzo. Aidha, ujenzi wa *Aviation Complex* yenye ghorofa mbili (2) imekamilika. Jengo hili lina madarasa, maabara, ukumbi wa mikutano, ofisi za watumishi na sehemu ya kuegesha ndege.

***235. Mheshimiwa Spika***, ili kufanikisha utoaji wa mafunzo ya urubani kwa kujenga miundombinu ya mafunzo, Chuo kimepata eneo lenye ukubwa wa ekari 60 katika Kiwanja cha KIA na eneo la mita za mraba 2,340 katika Kiwanja cha JNIA. Aidha, Chuo kimepata ithibati ya kuwa Kituo cha Mafunzo ya kozi za umahiri (Authorized Training Center - ATC) zinazosimamiwa na ICAO kupitia Chama cha Kimataifa cha Usafiri wa Anga (*International Air Transport Association* - IATA). Katika mwaka wa masomo wa 2020/21, Kituo kimetoa mafunzo ya taaluma za anga katika kozi nne (4) za kimataifa.

***236. Mheshimiwa Spika***, Chuo kimeendelea kuhakikisha kuwa kinazalisha wataalam wa usafiri wa anga wenye umahiri, weledi na uzoefu wa kufanya kazi katika mazingira halisi. Katika kufikia azma hii, Chuo kinaendelea kufanya tathimini ya mazingira na masuala ya kijamii pamoja na usanifu wa michoro (scheme design) ya ujenzi wa majengo matano (5) katika kampasi ya Mabibo, Dar es Salaam. Majengo haya yatajumuisha Karakana ya Mafunzo Maalum ya Uhandisi, jengo la kufunga vifaa maalum vya Mafunzo ya Uhudumu Ndani ya Ndege, Kituo cha Umahiri cha Mafunzo ya Usafiri wa Anga na Operesheni katika Usafirishaji pamoja na mabweni mawili (2) ya wanafunzi. Kuhusu mradi wa uanzishwaji wa Kituo cha Umahiri katika Taaluma ya Mafunzo ya Anga na Operesheni za Usafirishaji kinachofadhiliwa na Benki ya Dunia, katika mwaka 2020/21, kimedahili jumla ya wanafunzi 2,711.

***237. Mheshimiwa Spika***, Chuo kimepata ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ili kuanzisha Kituo cha Kikanda cha Umahiri cha Mafunzo ya Usalama Barabarani. Kituo hiki kitatoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri elekezi katika nyanja zote za usalama barabarani katika nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kutatua changamoto za usalama barabarani. Hadi Aprili, 2021 Chuo kilikuwa kimeandaa mtaala mmoja wa *Weighbridge Operations and Management* pamoja na *Teaching manual* kwa ajili utoaji mafunzo kwenye kituo hiki. Aidha, Chuo kimeandaa Hadidu za Rejea (ToR) za kupata mtaalamu wa kuwajengea uwezo wanataaluma ili waweze kutoa mafunzo yanayokidhi ubora wa kimataifa.

***238. Mheshimiwa Spika***, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kinaendelea na taratibu za kukipandisha hadhi yake ili kuwa Chuo Kikuu cha Usafirishaji chini ya ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Katika taratibu za kupandisha Chuo hadhi, mwaka 2020/21, Chuo kilipeleka watumishi 65 katika mafunzo ya muda mrefu. Kati yao, watumishi 46 wanasoma nchini na 19 nje ya nchi ambapo watumishi 30 wanasoma shahada ya uzamivu, 30 shahada ya uzamili, wawili (2) shahada ya kwanza na watatu (3) mafunzo maalum ya urubani na ukufunzi.

**Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam (CATC)**

***239. Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC) kimeendelea kutoa mafunzo katika taaluma za Uongozaji Ndege (Air Traffic Controllers), Mafundi wa Mitambo ya Kuongozea Ndege na Mawasiliano (Communication, Navigation and Surveillance), Wataalam wa Mawasiliano ya Taarifa za Anga (Aeronautical Information Officers), usalama wa anga na upekuzi (aviation security), Wasimamizi na Waandaaji wa Safari za Ndege (Flight Operations Officers), usafirishaji wa bidhaa hatarishi (Dangerous goods), makosa ya kibinadamu (Human factor), usimamizi wa Viwanja vya Ndege (Airport Management) na mafunzo ya uendeshaji wa Ndege zisizo na rubani (Drones). Katika mwaka 2020/21, jumla ya wanafunzi 684 walihitimu mafunzo yao ambapo kati yao wanafunzi 662 ni Watanzania na wanafunzi 22 ni wageni kutoka nchi ya Somalia.

**Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma**

***240. Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma kimeendelea kutoa mafunzo ya hali ya hewa katika ngazi ya awali na ya kati. Katika mwaka 2020/21, jumla ya wanafunzi 27 walihitimu mafunzo ambapo kati yao wanafunzi 20 walihitimu mafunzo ya hali ya hewa katika ngazi ya Cheti na wanafunzi saba (7) walihitimu mafunzo ya hali ya hewa katika ngazi ya Diploma. Aidha, kazi ya ukarabati wa Mabweni na Majengo ya Utawala inaendelea.

## C.3 MASUALA MTAMBUKA

**Rasilimali watu na Maendeleo ya Watumishi**

***241. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, jumla ya Watumishi 19 walistaafu. Kwa kuzingatia taratibu za utumishi wa Umma na kuwajali wastaafu hao, Wizara iliwagharamia mafunzo ya muda mfupi ya kujiandaa na maisha baada ya kustaafu kazi wakati mafao yao yanaendelea kuandaliwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF). Aidha, Wizara imeendelea kuwaendeleza Watumishi wake kitaaluma kwa kuwapeleka katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Hadi Aprili, 2021, jumla ya watumishi 202 walihudhuria mafunzo katika taaluma mbalimbali. Kati ya

hao, watumishi 17 walishiriki mafunzo ya muda mrefu na Watumishi 185 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi.

**Ushirikishwaji wa Wanawake Katika Kazi za Barabara**

***242. Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuongeza ushiriki wa wanawake kwenye kazi za barabara, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara imetekeleza kazi mbalimbali. Kazi hizo ni pamoja na kutoa elimu kwa wadau kuhusu kazi za ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara ikiwa ni pamoja na elimu juu ya Mwongozo wa Ushirikishwaji Wanawake katika kazi za barabara. Aidha, Wizara iliendelea kutoa semina kwa Waratibu wa Mikoa kuhusu Sheria ya Manunuzi na Matumizi ya Mfumo wa TANePS, taratibu za kusajili Kampuni na usimamizi wa vikundi vya wanawake waliopo katika vikundi au waliosajili kampuni ili waweze kusimamia na kuelekeza kikamilifu Wanawake waliotayari kushiriki kazi za barabara.

**Maboresho ya Sheria za Kisekta**

***243. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushiriki katika ukamilishaji wa rasimu ya Kanuni za Usajili wa Makandarasi (The Contractors Registration Criteria) chini ya Sheria ya Usajili wa Makandarasi ya mwaka 1997 pamoja na kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ili kuboresha utendaji wa Bodi na kutambua taaluma zingine zinazosimamiwa na Sheria hiyo.

**Masuala Mengine Yaliyotekelezwa na Wizara**

***244. Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Ujenzi imeendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu Sera na Mipango inayosimamiwa na Wizara pamoja na kuzitunza na kuhifadhi barabara zetu, kuzingatia Sheria na Kanuni za Matumizi ya Barabara. Vilevile, Wizara imeendelea kuboresha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuongeza ufanisi na kutoa huduma kwa wakati. Mfumo wa utoaji wa vibali vya kusafirisha mizigo maalum (Special Loads Permit System) kwa njia ya kielektroniki unaendelea kutoa huduma kwa wasafirishaji nchini na nje ya nchi. Aidha, Wizara imeanzisha ‘command centre’ ili kufuatilia uendeshaji wa shughuli za

mizani kwa kununua mfumo wa usimamizi wa vituo vya mizani wa kamera za CCTV (Weighbridge CCTV Camera Management System) kwa ajili ya kazi ya ufuatiliaji wa shughuli za mizani kwa masaa 24 kwa kuanzia na vituo 13 vya mizani nchi nzima. Matokeo chanya ya ufuatiliaji huo yameonekana, ambapo tozo za uharibifu wa barabara kutokana na uzidishaji wa uzito zimeongezeka kutokana na kupungua kwa vitendo vya rushwa katika mizani kutoka kwa wasafirishaji waliozidisha uzito.

***245. Mheshimiwa Spika***, Wizara vilevile imenunua Mtambo wa Kupima Ubora wa Barabara zinazojengwa ambao utatumika wakati wa zoezi la ufuatiliaji wa miradi ya barabara inayoendelea kujengwa. Mtambo huo utawezesha kutambua mapungufu yaliyopo katika barabara mpya zilizojengwa na pia una uwezo wa kupima barabara zote nchi nzima kwa muda mfupi. Sambamba na hilo, Wizara imenunua magari manne (4) mapya kwa ajili ya kazi za ufuatiliaji wa miradi nchi nzima.

***246. Mheshimiwa Spika***, vilevile Wizara imewezesha kuanzisha Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology - ICoT) kwa kuunganisha Chuo cha Ujenzi Morogoro (Morogoro Works Training Institute – MWTI) na Chuo cha Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi (Appropriate Technology Training Institute – ATTI) ambacho kimeanzisha kozi katika ngazi za Cheti katika fani za Ujenzi, Umeme na Mekanika. Awali Chuo cha Ujenzi Morogoro na Chuo cha Teknolojia Stahiki- ATTI vilikuwa vikitoa kozi zisizotambulika na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi Stadi (National Council for Technical Education – NACTE) na idadi ya wanafunzi walikuwa wachache. Kwa kuanzishwa ICoT, kozi zinazotolewa na Taasisi hiyo zinatambuliwa na NACTE na inadahili wanafunzi wengi kwa mwaka hivyo kuongeza idadi ya watalaam kwenye fani ya Ujenzi, Umeme na Makenika.

***247. Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za kuwaongezea ujuzi Wahandisi wa Wizara, katika mwaka 2020/21, jumla ya watumishi kumi (10) wa Wizara (Ujenzi) na Taasisi zake wameshikizwa katika miradi mbalimbali ya ujenzi wa

barabara, madaraja na viwanja vya ndege. Lengo la kushikizwa kwa wataalam hao katika miradi hiyo ni kupata ujuzi katika masuala ya ujenzi kutoka kwa Makandarasi na Washauri Elekezi wa Kigeni na wa Ndani ili watumie utaalam huo katika kutekeleza miradi mbalimbali hapa nchini.

***248. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21, Wizara imetoa mafunzo kwa watumishi 152 kuhusu kujikinga dhidi ya magonjwa yasiyoambukizwa. Mafunzo hayo yalihusisha mada kuhusu watumishi kubadili tabia za ulaji chakula, lishe na kufanya mazoezi ya viungo. Aidha, Wizara inaendelea kutoa mafunzo na kuwaelimisha watumishi namna ya kujikinga dhidi ya magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza. Wizara pia inaandaa programu za kuwawezesha wanawake kushiriki katika uendeshaji wa Mradi wa Reli ya kisasa pindi itakapokamilika. Programu hizo ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wahitimu wa kila fani kutoka katika Vyuo vikuu na vya kati, kuunda dawati la wanawake la usafirishaji wa Reli pamoja na kuwajengea uwezo katika mafunzo ya Uongozi na uendeshaji wa usafiri wa Reli.

Majukumu mengine yaliyotekelezwa na Wizara ni pamoja na yafuatayo:

i. Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na majukumu mengine yanayosimamiwa na Sekta ya Ujenzi kupitia Mpango Kazi wa mwaka wa fedha 2020/21;

ii. Kuandaa na kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Wizara ya Fedha na Mipango Taarifa ya Hesabu ya Mwaka wa Fedha 2019/2020;

iii. Kuandaa Taarifa za Takwimu za Sekta ya Ujenzi kwa mwaka 2019;

iv. Kuimarisha Mifumo ya Udhibiti wa Ndani wa Wizara; na

v. Kupitia Mkataba wa Huduma kwa Mteja (Client Service Charter).

## C.4 CHANGAMOTO ZILIZOIKABILI WIZARA NA MIKAKATI YA KUZITATUA

***249. Mheshimiwa Spika***, katika utekelezaji wa majukumu yake, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imekabiliwa na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo na mikakati ya kuzitatua ni: -

i. Upungufu wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo. Hali hii inasababisha Wizara (Ujenzi) kuwa na malimbikizo makubwa ya madai na madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wanaotekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ambapo hadi Aprili, 2021 madai na madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri yaliyohakikiwa yamefikia Shilingi **869,026,582,530.09.**

***Mkakati***

Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango inahakikisha fedha za miradi zinalipwa kwa wakati ili kupunguza gharama za riba inayoendelea kuongezeka. Aidha, Serikali inaendelea kujadiliana na Wawekezaji mbalimbali ikiwa ni pamoja na Taasisi za fedha ili kupata mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya kutekeleza Miradi Mikubwa ya Maendeleo. Vilevile, Serikali inaendelea kushawishi Sekta Binafsi kuwekeza katika uendelezaji na uboreshaji wa miradi ya uchukuzi.

ii. Kuchelewa kutolewa kwa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na hivyo kusababisha utekelezaji wa miradi ya barabara, madaraja, viwanja vya ndege na vivuko kuchelewa kuanza.

***Mkakati***

Menejimenti ya Wizara imeunda Kitengo (Result Management Office) cha Wataalam wenye weledi na ujuzi wa kupitia nyaraka kwa kina na kuwasilisha Wizara ya Fedha kwa hatua zao za haraka.

iii. Msongamano wa magari barabarani hususan katika Jiji la Dar es Salaam na miji mingine inayokua kwa kasi kama vile Mbeya, Mwanza, Arusha na Dodoma.

***Mkakati***

Katika Jiji la Dar es Salaam mikakati iliyopo ni pamoja na kujenga barabara za juu (flyovers) ambapo ujenzi umekamilika katika maeneo ya TAZARA (Mfugale Flyover) na Ubungo (Kijazi Interchange) na ujenzi unaendelea katika maeneo ya Uhasibu na Chang'ombe. Serikali pia inaendelea na ujenzi wa Daraja Jipya la Selander. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika kwa ajili ya kuboresha makutano ya barabara katika maeneo ya KAMATA, Magomeni, Mwenge, Tabata/Mandela, Morocco, Buguruni, Mbezi Mwisho, Fire pamoja na makutano ya barabara za Kinondoni/Ali Hassan Mwinyi na Selander (Ali Hassan Mwinyi/ UN Road Jct). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa barabara za Mabasi Yaendayo Haraka kwa Awamu ya II, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi huo kwa awamu ya III zinaendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara hizo kwa Awamu IV na V yanaendelea.

Kwa upande wa jiji la Dodoma, mikakati iliyopo ni kujenga barabara za *Dodoma City Outer Ring Road Lot I & II* kuanzia Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port (km 52.3) na barabara ya Ihumwa Dry Port – Matumbulu – Nala(km 60) kwa njia nne ambapo Mkandarasi wa kazi hii anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Mkakati mwingine ni ujenzi wa barabara ya Makulu Jct. – Ntyuka R/About – Image R/About – Bahi R/About (km 6.3), Ntyuka Jct. – Mvumi Hospital – Kikombo Jct. (km 76.07) ambazo zipo katika hatua mbalimbali za maandalizi ya ujenzi. Mradi mwingine ni Upanuzi wa Barabara Kuu Zinazoingia Katikati ya Jiji la Dodoma (km 220).

iv. Uvamizi wa maeneo ya hifadhi ya barabara (Road Reserve).

***Mkakati***

Kuendelea kuelimisha Umma ili wananchi waweze kufahamu vyema Sheria ya Barabara Na. 13 ya Mwaka 2007.

v. Uwezo mdogo wa mtaji walionao Makandarasi wa ndani hivyo hushindwa kushiriki kikamilifu katika fursa za kazi

kutokana na masharti ya upatikanaji wa dhamana za zabuni, dhamana za ushiriki wa kazi na mitaji ya kuwezesha kufanya kazi kutoka mabenki kuwa magumu na kutozingatia mahitaji halisi ya shughuli za kihandisi. Aidha, kushindwa kupata mitaji kunawafanya Makandarasi kushindwa kukua na kupata fursa ambazo zitawezesha kuwakwamua kutokana na uwezo wao mdogo.

***Mkakati***
Bodi ya Usajili wa Makandarasi inaendelea kuimarisha Mfuko Maalum wa Kutoa Dhamana ya kusaidia Makandarasi wadogo na wa Kati. Mfuko kwa sasa umefikisha mtaji wa Shilingi Bilioni 3.9 na idadi ya wanachama imefikia 1,167. Wizara kupitia Bodi ya Usajili wa Makandarasi itaendeleza jitihada za kuhamasisha Makandarasi wa ndani kujiunga ili kuomba zabuni kwa utaratibu wa ubia. Aidha, Wizara kupitia Bodi ya Usajili wa Makandarasi, Baraza la Taifa la Ujenzi na Bodi ya Usajili wa Wahandisi imeendelea kutoa mafunzo kwa Wahandisi Washauri na Makandarasi wa Ndani ili wasimamie na kutekeleza miradi kikamilifu hususan mikataba ya ujenzi na matengenezo ya barabara.

Vilevile, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo Makandarasi na Washauri wa ndani kwa kutenga miradi maalum ya ujenzi na usimamizi. Aidha, mafunzo ya matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvukazi (Labour Based Technology – LBT) yataendelea kutolewa na Wizara kwa Makandarasi wazawa ikiwemo wanawake kwenye vikundi na makampuni ili kuwajengea uwezo kwa lengo la kushiriki katika miradi mbalimbali ya ujenzi.

vi. Uzidishaji wa uzito wa mizigo katika magari unaofanywa na wasafirishaji na hivyo husababisha uharibifu mkubwa wa barabara.

***Mkakati***
Wizara kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi ilianzisha doria maalum katika Barabara Kuu zote ili kufanya ufuatiliaji wa matukio yanayoripotiwa kutoka *Command Centre* na kwa

raia wema. Matokeo ya ufuatiliaji ni pamoja na kubaini na kuwachukulia hatua za kisheria na za kinidhamu Watumishi wanaohusika na uendeshaji na usimamizi wa vituo vya mizani wasio waaminifu wanaoshirikiana na wasafirishaji kukiuka Sheria na Kanuni za udhibiti uzito wa magari. Hadi sasa kuna jumla ya kesi nne (4) ambazo zimefunguliwa katika mahakama ya mkoa Jijini Dodoma. Vile vile Wizara inafunga mfumo wa kisasa wa kieletroniki wa *Load Cell* (Electronic Load Cell) ambapo *Load Cell* hizo zinasaidia kuweza kujua hali ya upimaji wa uzito katika mizani kwa saa 24 kwa ufuatiliaji kutokea ofisini mbali na vituo vya mizani. Pia zina uwezo wa kujifanyia *calibration* na zinahimili mabadiliko ya hali ya hewa hivyo kupunguza gharama za uendeshaji unaotokana na matengenezo ya mara kwa mara kama ilivyo kwa mizani iliyopo sasa ambayo si ya kielektroniki.

vii. Tishio la homa inayosababishwa na virusi vya Corona (COVID 19). Hali hii imeleta hofu kubwa katika Sekta ya Uchukuzi hususan kwenye Bandari na Viwanja vya Ndege hivyo kuathiri Utendaji wa Taasisi zinazotoa huduma katika maeneo hayo.

***Mkakati***

Wizara inaendelea kuchukua tahadhari katika Vituo vya Mipakani, Viwanja vya Ndege na maeneo ya Bandari ili kudhibiti maambukizi ya virusi vya Corona. Aidha, vifaa vya kinga vimeendelea kutolewa kwa Wafanyakazi katika maeneo hayo pamoja na utoaji wa elimu ya kinga kwenye vyombo vya usafiri.

viii. Sekta ndogo za usafiri wa anga, reli, hali ya hewa na usafiri kwa njia ya maji zinakabiliwa na changamoto ya uhaba wa Wataalam wenye ujuzi na uzoefu.

***Mkakati***

Wizara (Sekta ya Uchukuzi) kupitia Vyuo vyake vya Kisekta imeendelea kutoa mafunzo kwa Wataalam waliopo, kuajiri wapya na kuvijengea uwezo Vyuo hivyo.

ix. Uvamizi, uharibifu na hujuma kwa miundombinu ya reli, hususan reli zenyewe, mataruma, vifungio na madaraja.

***Mkakati***

Wizara itaendelea kushirikiana na vyombo vya dola pamoja na jamii inayozunguka maeneo ya Reli ili kusimamia Sheria zilizopo kuhusu uharibifu huo pamoja na kutoa elimu na hamasa kwa jamii inayopakana na maeneo ya Reli ili kuelewa umuhimu wa Reli na kuwa walinzi wa miundombinu hiyo.

x. Mabadiliko ya hali ya hewa (Climate Change) yanayosababisha Mifumo ya hali ya hewa kubadilika mara kwa mara na kusababisha uharibifu wa miundombinu kutokana na mafuriko.

***Mkakati***

Wizara imeendelea kupanua Mtandao wa Rada za Hali ya Hewa kwa kununua rada mbili zaidi ili kufanya nchi kuwa na jumla ya rada saba (7) ambazo zinatosha kuangaza nchi nzima; na kuongeza vifaa na kupanua mtandao wa vituo vya hali ya hewa nchini. Lengo ni kuboresha utoaji wa utabiri na tahadhari juu ya matukio ya hali mbaya ya hewa. Aidha, Wizara imeendelea kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kutumia huduma za hali ya hewa.

xi. Baadhi ya Viwanja vya Ndege kutokuwa na taa na miundombinu kwa ajili ya kuwezesha usafiri wa anga wakati wa usiku hivyo kulazimika kupanga safari za ndege wakati wa mchana ni moja ya changamoto inayokabili usafiri wa anga nchini.

***Mkakati***

Serikali imeendelea kuvifanyia maboresho Viwanja vya Ndege vya ndani ya nchi ili kuwezesha ndege kuruka nyakati za usiku na pia kuboresha barabara za kurukia Ndege kuweza kuhimili aina ya Ndege zilizopo.

## D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA SEKTA ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22

***250. Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2021/22 ni wa kwanza katika kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III) na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wenye dhima ya *Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu* umelenga kuendelea kutekeleza miradi ya Kimkakati ambayo itakuwa na matokeo makubwa katika Sekta nyingine za kiuchumi. Miradi hiyo ni pamoja na Ujenzi wa Reli Mpya ya Standard Gauge (SGR), Ufufuaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania na Ujenzi na Ukarabati wa Meli katika Maziwa Makuu. Aidha, maeneo mengine yaliyopewa kipaumbele katika mwaka wa fedha 2021/2022 ni pamoja na ukarabati wa miundombinu ya Reli iliyopo; Upanuzi wa bandari; huduma za usafiri wa anga, maji na nchi kavu; ujenzi wa barabara, madaraja na vivuko; ujenzi wa viwanja vya ndege ikiwemo kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Msalato pamoja na miradi ya Makao Makuu ya Nchi ikiwemo barabara za pete za ndani na nje (Dodoma inner and outer ring roads). Vipaumbele vingine vilivyozingatiwa ni miradi iliyopo kwenye Ahadi mbalimbali za Viongozi Wakuu wa Serikali tangu Awamu ya Kwanza; na Miradi ambayo Washirika wa Maendeleo wameonesha nia ya kutoa fedha za utekelezaji ambapo Serikali inatakiwa kutoa mchango wake (Counterpart Fund).

***251. Mheshimiwa Spika,*** Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Sekta ya Ujenzi na Sekta ya Uchukuzi ni kama ifuatavyo:

### D.1.1 SEKTA YA UJENZI

### Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

***252. Mheshimiwa Spika,*** Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekta ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2021/22 ni **Shilingi 38,540,787,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 35,186,389,000.00**

ni Bajeti ya Mishahara na **Shilingi 3,354,398,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Sekta ya Ujenzi imetengewa jumla ya **Shilingi 1,588,703,487,200.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **1,288,703,487,200.00** ni fedha za ndani na Shilingi **300,000,000,000.00** ni za fedha za nje. Aidha, kati ya fedha za ndani **Shilingi 635,849,127,200.00** ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara na fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali ni **Shilingi 652,854,360,000.00.**

Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyooneshwa katika ***Kiambatisho Na.1.*** Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo ni kama ifuatavyo:

**MRADI WA KUJENGA UWEZO (INSTITUTIONAL CAPACITY BUILDING)**

***253. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 318.68** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu kwa lengo la kujenga uwezo wa watumishi wa Sekta ya Ujenzi kwa kuwapatia mafunzo na vitendea kazi vya ofisi kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi.

**MIRADI YA VIVUKO, UJENZI WA NYUMBA NA MAJENGO YA SERIKALI**

**Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko**

***254. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 15,312.13** kwa ajili ya kazi zifuatazo:

***255. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,046.83** zimetengwa kwa ajili ya mradi wa **Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko**. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na upanuzi wa Jengo la Abiria na Maegesho ya Kigamboni kwa ajili ya kivuko cha Magogoni – Kigamboni; ujenzi wa maegesho ya Zumacheli ya kivuko cha Chato – Nkome; maegesho ya Nyamisati na Mafia kwa ajili ya Kivuko kipya cha Nyamisati – Mafia; maegesho ya vivuko vya Kayenze – Kanyinya, Muleba – Ikuza

na maegesho mapya ya Ijinga - Kahangala (Magu) na Bwiro – Bukondo (Ukerewe) mkoani Mwanza.

Kazi nyingine ni ujenzi na ukarabati wa maegesho matano (5) ya Kilambo – Namoto, Utete – Mkongo, Iramba – Majita, Nyakarilo – Kome na Kasharu – Buganguzi pamoja na ujenzi wa ofisi, majengo ya abiria na uzio kwenye vituo kumi (10) vya vivuko ambavyo ni Bugolora, Ukara, Kome, Nyakarilo, Maisome, Kaunda, Nkome, Kisorya, Musoma na Kinesi. Fedha hizi pia zitatumika kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya ujenzi wa maegesho ya vivuko.

***256. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi wa **Ujenzi wa Vivuko Vipya** umetengewa **Shilingi milioni 7,449.93** kwa ajili ya ujenzi wa vivuko vipya vya Kisorya – Rugezi, Ijinga – Kahangala, Bwiro – Bukondo, Nyakarilo – Kome, Nyamisati – Mafia pamoja na ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA. Kazi nyingine ni ufuatiliaji na tathmini ya miradi hiyo.

***257. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi wa **Ukarabati wa Vivuko** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,816.17** kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa kivuko MV Ujenzi; kufanya ukarabati wa Kivuko MV Musoma, MV Mara, MV Kome II, MV Misungwi, MV Nyerere, MV Mafanikio, MV Kyanyabasa, MV Ruvuvu ya zamani, MV Tanga pamoja na ukarabati wa kivuko cha MV Kilombero II na kukihamishia Mlimba – Malinyi. Kazi nyingine ni kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya ukarabati wa vivuko.

**Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali**

***258. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 69,601.08** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2021/22 kwa ajili ya mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali. Kazi zitakazotekelezwa ni kama ifuatavyo:

***259. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi wa **Ujenzi wa Nyumba za Viongozi wa Serikali** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 11,190.83** kwa ajili ya

ujenzi wa nyumba **20** za Viongozi Dodoma pamoja na kuendelea na ujenzi wa nyumba **5** za Majaji katika Mikoa ya Kilimanjaro, Mtwara, Shinyanga, Dar es Salaam na Tabora.

***260. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi wa **Ujenzi wa nyumba 150 za Watumishi wa Umma** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 14,373.27** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba **150** za Watumishi wa Umma Jijini Dodoma.
***261. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi wa **Ujenzi wa jengo la Makazi katika eneo la Ilala Kota Wilaya ya Ilala** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,943.79** kwa ajili ya kuanza ujenzi.

***262. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi wa **Ukarabati wa Nyumba na Ununuzi wa Samani kwa Ajili ya Ikulu Ndogo** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 21,719.22** kwa ajili ya ukarabati wa nyumba 40 za viongozi Dodoma na nyumba 30 katika mikoa mingine pamoja na kufanyia matengenezo kinga ya nyumba za makazi za Magomeni Kota. Kazi nyingine ni ununuzi wa samani za Ikulu Ndogo, ukarabati wa nyumba 66 zilizokuwa zinamilikiwa na iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA) zilizohamishiwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) pamoja na ukarabati wa nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na TAMISEMI/NHC zilizohamishiwa TBA katika mikoa 20.

***263. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi wa **Kujenga Uwezo wa Wabunifu Majengo, Wakadiriaji Majenzi na Huduma za Ushauri** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,513.61** kwa ajili ya kuwajengea uwezo Wabunifu Majengo (Architects) na Wakadiriaji Majenzi (Quantity Surveyors) kupitia Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), Huduma za Ushauri pamoja na maandalizi ya viwango vya msawazo (*standards and specifications*) kwa ajili ya kazi na miradi ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali pamoja na samani.

***264. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi **Ujenzi na Ukarabati wa Karakana za TEMESA na TBA**

umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10,012.84** kwa ajili ya ukarabati wa karakana kumi na moja za TEMESA zilizopo Tabora, Mwanza, Arusha, Mtwara, Mbeya, M.T Depot Dar es Salaam, Kigoma, Mara, Ruvuma, Pwani na Vingunguti pamoja na ukarabati wa karakana za TBA katika mikoa ya Tabora, Arusha, Mwanza, Morogoro, Mbeya na Dar es Salaam. Aidha, fedha hizo zitatumika kuendelea na ujenzi wa karakana za TEMESA katika Mikoa ya Songwe, Simiyu, Geita, Njombe na Katavi pamoja na ujenzi wa karakana mpya ya kisasa ya magari jijini Dodoma na kiwanda kipya cha kutengeneza samani Dodoma.

***265. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Mradi wa **Ununuzi wa Mitambo, Vitendea Kazi na Uendeshaji wa Karakana Zinazohamishika (Mobile Workshops)** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** kwa ajili ya ununuzi wa mitambo ya matengenezo ya magari na vitendea kazi. Kazi nyingine ni uendeshaji wa karakana zinazohamishika kwa ajili ya matengenezo ya magari ya Serikali katika Wilaya ambazo ziko mbali na makao makuu ya mikoa.

***266. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi wa **Kuanzisha Karakana za Wilaya** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 800.06** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi na ukarabati wa karakana za Wilaya sita (Simanjiro, Masasi, Ukerewe, Chato, Mafia na Kyela).

***267. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa **Kusanifu na Kusimika Mfumo wa Usimamizi na Ufuatiliaji wa Matengenezo ya Magari,** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 3,000.00** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

***268. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 1,047.46** zimetengwa kwa ajili ya **Ufuatiliaji na Tathmini Kwenye Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali pamoja na wahitimu wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi**.

**MIRADI YA BARABARA NA MADARAJA**

***269. Mheshimiwa Spika,*** miradi ya barabara na madaraja itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2021/22 ni kama ifuatavyo:

**Barabara ya Soni - Bumbuli - Dindira – Korogwe (km 74)**

***270. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 924.00** kwa ajili ya kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Mtwara – Newala - Masasi (km 210)**

***271. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 6,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi wa barabara ya Mtwara – Newala – Masasi; sehemu ya Mtwara – Mnivata (km 50) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Mnivata – Tandahimba - Masasi (km 160).

**Barabara ya Likuyufusi – Mkenda (km 122.50)**

***272. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 3,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nachingwea – Liwale (km 130)**

***273. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 800.00** zimetengwa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Ubena Zomozi - Ngerengere (km 11.6)**

***274. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 500.00** zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya TAMCO – Vikawe – Mapinga (km 24)**

***275. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,900.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Makofia – Mlandizi (km 36.7)**

***276. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, barabara ya Makofia – Mlandizi imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Musoma - Makojo - Busekela (km 92)**

***277. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,000.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Suguti – Kusenyi (km 5) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kongwa Jct – Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 98)**

***278. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,000.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Mpwapwa – Idilo (km 5) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Muhutwe – Kamachumu – Muleba (km 54)**

***279. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,500.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Iringa – Ruaha National Park (km 104)**

***280. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,500.00** kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Muheza – Amani (km 36)**

***281. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 5,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200)**

***282. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ukarabati wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kibaoni - Majimoto - Muze - Kilyamatundu (km 352)**

***283. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 6,500.00** zimetengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Kibaoni – Majimoto – Inyonga (km 152) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ntendo – Muze – Kilyamatundu (km 200) sehemu ya Ntendo – Muze (km 37).

**Daraja la Kigongo - Busisi (J.P. Magufuli) na Barabara Unganishi**

***284. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 19,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa daraja hili lililopo mkoani Mwanza na barabara unganishi.

**Daraja la Mzinga**

***285. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 500.00** zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa daraja hili lililopo katika Barabara ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe.

**Daraja la Ugalla**

***286. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja hili lililopo katika mkoa wa Katavi.

**Daraja la Kitengule na Barabara Unganishi**

***287. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 3,950.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa daraja hili lililopo mkoa wa Kagera pamoja na barabara unganishi zenye urefu wa kilometa 18.

**Barabara ya Morogoro - Dodoma (km 260.0) pamoja na Daraja la Mkundi**

***288. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Morogoro – Dodoma (km 260.0) pamoja na Daraja la Mkundi ili kuikarabati barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Daraja Jipya la Wami**

***289. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 4,050.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa daraja hili lililopo katika barabara ya Chalinze - Segera.

**Barabara ya Njombe - Makete - Isyonje (km 157.4)**

***290. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 13,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa barabara ya Njombe – Makete – Isyonje sehemu ya Njombe – Moronga (km 53.9) na kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Moronga – Makete (km 53.5). Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa sehemu ya barabara ya Isyonje – Makete (km 50) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Omugakorongo - Kigarama - Murongo (km 105)**

***291. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 4,500.00** zimetengwa kwa ajili ya fidia na kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nanganga - Ruangwa - Nachingwea (km 145)**

***292. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 8,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara za Masasi – Nachingwea (km 45) na kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 100) sehemu ya Nanganga – Ruangwa (km 53.20).

**Barabara ya Mpemba – Isongole (km 51.2)**

***293. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,510.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa daraja la Songwe katika barabara ya Mpemba – Isongole (km 51.2). Kazi nyingine ni kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Ruanda – Iyula – Nyimbili (km 21.0) na Katumbasongwe – Kasumulu – Ngana – Ileje (km 90.10).

**Barabara ya Tanga - Pangani – Makurunge (km 174.5)**

***294. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, **Shilingi milioni 7,200.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 13,810.00** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Tanga – Pangani (km 50). Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Pangani – Mkange (km 124.5) na Daraja la Pangani.

**Barabara ya Kisarawe – Maneromango (km 54)**

***295. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Geita – Bulyanhulu – Kahama (km 120)**

***296. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 6,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara za Geita – Bulyanhulu Jct (km 58.3), Bulyanhulu Jct – Kahama (km 61.7) na Uyogo – Nyamilangano – Nyandekwa – Kahama (km 54) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50)**

***297. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 12,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Nyamirembe Port – Katoke (km 50), Chato Ginery - Bwina (km 8.1) na SIDO -Chato Zonal Hospital (km 5.3).

**Barabara ya Geita – Nzera (km 54)**

***298. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 4,000.00** zimetengwa kwa ajili ya

kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Geita – Nzera (km 54) na Sengerema – Nyehunge (km 54).

**Barabara ya Arusha - Moshi - Himo - Holili (km 199.51)**

***299. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,010.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kijenge – Usa River (km 20), kuanza ujenzi wa barabara ya Mianzini – Ngaramtoni (km 18) na kuendelea na maandalizi ya upanuzi wa sehemu ya Tengeru – Moshi – Himo (km 105) pamoja na Mizani ya Himo.

**Barabara za Kuelekea Kwenye Mradi wa Kufua Umeme Katika Maporomoko ya Mto Rufiji (Access Roads To Rufiji Hydropower Project)**

***300. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,030.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Bigwa – Matombo – Mvuha (km 78) sehemu ya Bigwa – Matombo (km 40) pamoja na ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara za Maneromango – Vikumburu – Mloka (km 100) na Kibiti – Mloka – Mtemele – Striggler's Gorge. Aidha, mradi huu utahusisha kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Ubena Zomozi – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 178) sehemu ya Ngerengere – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 166.4) ikiwa ni maandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro (km 152.3)**

***301. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10,510.00** kwa ajili ya kuendelea na ukarabati (overlay) wa barabara ya Mlandizi – Chalinze (km 44.24) na ujenzi wa barabara ya Kwa Mathiasi (Morogoro Road) – Msangani (km 8.3). Kazi nyingine ni kuendelea na maboresho ya maeneo hatarishi (Assorted Accident Blackspot) ya barabara ya Dar es Salaam – Morogoro na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Vigwaza. Aidha, mradi huu unahusisha pia maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mlandizi – Chalinze – Morogoro kwa kiwango cha Expressway kwa kutumia utaratibu wa ubia

kati ya Serikali na Sekta Binafsi (Public Private Partnership - PPP).

**Barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (km 54.1)**

***302. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,000.00** kwa ajili ya kuanza ukarabati na upanuzi wa barabara hii sehemu ya Tegeta – Bagamoyo (km 46.9) na kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mbegani – Bagamoyo (km 7.2).

**Barabara ya Usagara – Geita – Buzirayombo – Kyamyorwa (km 110)**

***303. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi kwa sehemu za Uyovu – Bwanga (km 43) na Bwanga – Biharamulo (km 67).

**Barabara ya Nyakahura - Kumubuga - Rulenge - Kabanga Nickel Road (km 141)**

***304. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 6,000.00** kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba (km 34), Kumubuga – Rulenge – Murugarama (km 75) na Rulenge – Kabanga Nickel (km 32).

**Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 265.1)**

***305. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2021/22**,** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 19,102.63**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 3,180.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 15,922.625** ni fedha za nje kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi waliojenga barabara za Tabora – Ndono (km 42), Ndono – Urambo (km 52), Kaliua – Kazilambwa (km 56) na Urambo – Kaliua (km 28). Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kazilambwa – Chagu (km 36) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Uvinza – Malagarasi (km 51.1).

**Barabara ya Ifakara - Kihansi - Mlimba - Madeke - Kibena (Njombe) (km 220)**

***306. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 8,500.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi Milioni 7,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 1,500** ni fedha za nje kwa ajili ya kuanza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya Kihansi – Mlimba - Taweta – Madeke – Kibena (km 220) kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Aidha, mradi huu utahusisha kuanza ujenzi wa barabara ya Ifakara – Kihansi (km 50). Kazi nyingine ni kufanya maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kibena – Lupembe - Madeke (km 130).

**Barabara ya Karatu - Mbulu - Haydom - Sibiti River - Lalago - Maswa (km 389)**

***307. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,500.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Karatu – Mbulu – Hydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389) kwa kuanzia na sehemu ya Mbulu – Hydom.

**Barabara ya Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga / Bomang'ombe – Sanya Juu (km 84.80)**

***308. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 6,620.00** kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Sanya Juu – Kamwanga sehemu ya Sanya Juu – Alerai (km 32.2) na KIA – Mererani (km 26). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa barabara za Kwa Sadala – Masama – Machame Jct (km 16) na Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8). Kazi nyingine ni kuanza ukarabati wa barabara ya Bomang'ombe – Sanya Juu (km 25) na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Tarakea – Holili (km 53).

**Barabara ya Tukuyu – Mbambo – Katumba (km 80.3)**

***309. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya ***Shilingi* milioni 4,830.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu za Bujesi – Mbambo (km 26)

na Tukuyu - Mbambo (km 34.60). Kazi nyingine ni kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mbambo – Ipinda (km 19.7).

**Barabara ya Dodoma – Manyoni (km 127) na Barabara Kuingia Manyoni Mjini (km 4.8)**

***310. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 120.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Muhalala (Manyoni).

**Barabara ya Tabora - Mambali - Bukene - Itobo (km 114)**

***311. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Namanyere - Katongoro - New Kipili Port (km 64.80)**

***312. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 350.00** kwa ajili ya kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii.

**Barabara ya Dumila – Kilosa – Mikumi (km 141)**

***313. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 7,035.00** kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi na Mhandisi Mshauri wa sehemu ya Dumila – Rudewa (km 45) na kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Rudewa – Kilosa (km 24.0). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Kilosa – Ulaya – Mikumi (km 72) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 157)**

***314. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 4,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 107) na kuanza ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50) kwa kiwango cha lami.

**Ujenzi wa Madaraja Makubwa**

***315. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 22,550.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa Madaraja ya Magufuli (Morogoro), Magara (Manyara), Momba (Rukwa), Lukuledi (Lindi) na Mara (Mara). Kazi nyingine ni kuanza ukarabati wa daraja la Kirumi (Mara), kuendelea na ujenzi wa Daraja la Sibiti (Singida) na barabara unganishi, Daraja la Msingi (Singida) na Daraja la Ruhuhu (Ruvuma), Daraja la Sukuma (Mwanza) na Daraja la Kiyegeya (Morogoro). Aidha, kazi nyingine ni kuanza usanifu na ujenzi wa Daraja la Mirumba (Katavi), ujenzi wa Daraja la Simiyu (Mwanza), Daraja la Sanza (Singida), Daraja la Mkenda (Ruvuma) na Daraja la Mpiji Chini (Dar es Salaam). Vilevile, mradi huu utahusisha kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Daraja la Mtera, Daraja la Godegode (Dodoma) na Daraja Mitomoni (Ruvuma), kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Daraja la Malagarasi Chini (Kigoma) na kununua madaraja ya chuma ya dharura (Steel Bridges Emergency Parts).

**Barabara ya New Bagamoyo (Kawawa Jct – Tegeta (km 17.2)**

***316. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 4,538.40** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na upanuzi wa sehemu ya Morocco – Mwenge (km 4.3)

**Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (km 183.1)**

***317. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 6,010.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2021/22 kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa sehemu ya Kyaka – Bugene (km 59.1) pamoja na kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Kumunazi – Kasulo – Bugene (km 124) sehemu ya Bugene – Burigi Chato National Park (km 60) na Murushaka – Nkwenda – Murongo (km 125) sehemu ya Kyerwa – Chonyonyo (km 50).

**Barabara ya Isaka – Lusahunga (km 242.20)**

***318. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 11,510.00** zinazojumuisha **Shilingi milioni 1,510.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 10,000.00** fedha za nje zimetengwa kwa ajili

ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga (km 110), kuendelea na ujenzi wa kituo cha Pamoja cha Ukaguzi – OSIS cha Nyakanazi na kuanza ukarabati wa sehemu ya Lusahunga – Rusumo (km 92).

**Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 259.75)**

***319. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 7,920.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2021/22, ambapo **Shilingi milioni 520.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 7,400.00** ni fedha za nje kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35), Tabora – Nyahua (km 85) na Nyahua – Chaya (km 85.4).

**Barabara za Mikoa (km 770.5)**

***320. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 53,350.00** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya barabara za mikoa na madaraja katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ukarabati wa jumla ya **kilometa 698.3** kwa kiwango cha changarawe, ujenzi wa kilometa **72.2** kwa kiwango cha lami pamoja na ujenzi na ukarabati wa madaraja/makalavati **34**. ***Kiambatisho Na. 2*** kinaonesha orodha ya miradi ya Barabara za Mikoa itakayotekelezwa kwa kutumia fedha za Bajeti ya Maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali*.*

**Barabara ya Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza (km 102)**

***321. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 350.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2021/22, kwa ajili ya kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kuifanyia ukarabati barabara hii.

**Mradi wa Kuondoa Msongamano Barabara za Dar es Salaam (km 138.50)**

***322. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 11,360.00** kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi wa barabara ya Mbezi – Malambamawili – Kinyerezi – Banana (km 14), Mbezi Mwisho

– Goba (km 7), Tangi Bovu – Goba (km 9), Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.6), Ardhi – Makongo – Goba; Sehemu ya Goba – Makongo (km 4) na Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi/Morogoro Road (Mbezi Mwisho); sehemu ya Madale – Goba (km 5).

***323. Mheshimiwa Spika,*** Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya Ardhi – Makongo (km 5) na Wazo Hill – Madale (km 6); kuanza ujenzi wa barabara za Kibamba – Kisopwa – Kwembe – Makondeko (km 14.66), sehemu ya Mloganzila – Mloganzila Citizen (km 4), Kongowe – Mjimwema – Kivukoni (One Lane Widening: km 25.1), Mji Mwema – Kimbiji – Pembamnazi (km 27) na Goba – Matosa – Temboni (km 6) pamoja na upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki (km 9.1).

**Barabara ya Nyamuswa – Bunda – Kisorya (km 107.4)**

***324. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 4,510.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa sehemu ya Kisorya – Bulamba (km 51.0) na kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 56.4).

**Barabara ya Kolandoto - Lalago - Ng'oboko - Mwanhuzi (km 136.4)**

***325. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Kolandoto – Mwanhuzi (km 62.4) na Lalago – Ng'oboko – Mwanhuzi (km 74.0).

**Barabara ya Ndundu – Somanga (km 60)**

***326. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 7,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Ndundu – Somanga (km 60) na kuanza ukarabati wa barabara za Kongowe – Ndundu (km 160.65) na Nangurukuru – Mbwemkuru (km 95).

**Barabara ya Kasulu – Manyovu (km 68)**

***327. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 15,000.00** zimetengwa ambapo **Shilingi milioni 1,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 14,000.00** ni fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kasulu – Manyovu pamoja na barabara za kuingia Kasulu mjini (km 68.0) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Dodoma *City Outer Dual Carriageway Ring Road Lot1 & 2* (km 112.3)**

***328. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 40,600.00.** Kati ya hizo, **Shilingi milioni 11,600.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 29,000.00** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya mzunguko ya Dodoma (Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road) sehemu ya Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port (km 52.3), sehemu ya Ihumwa Dry Port – Matumbulu – Nala (km 60) na fidia kwa ajili ya upanuzi wa barabara ya Bahi R/About - Image R/About – Ntyuka R/About – Makulu R/About (km 6.3). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya barabara ya Ntyuka Jct – Mvumi Hospital – Kikombo Junction (km 76.07) na barabara ya Kikombo Jct – Chololo – Mapinduzi (JWTZ HQ) (km 18). Aidha, fedha hizi zitatumika kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya upanuzi wa barabara kuu zinazoingia katikati ya Jiji la Dodoma (km 220) zinazohusisha barabara ya Dodoma – Morogoro (km 70), Dodoma – Iringa (km 50), Dodoma – Singida (km 50) na Dodoma – Arusha (km 50).

**Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/ Songea (km 499)**

***329. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,550.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kidatu – Ifakara (km 66.9) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha (km 396) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 365.36)**

***330. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 28,327.14** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2021/22 kwa ajili ya mradi huu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 1,810.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 26,517.14** ni fedha za nje kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa sehemu ya Tabora – Sikonge (km 30) na kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu za Usesula – Komanga (km 115.5), Komanga – Kasinde (km 112.18) na Kasinde – Mpanda (km 107.68).

**Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 235)**

***331. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 14,000.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu za Makutano – Sanzate (km 50), Sanzate – Natta (km 40) na Waso – Sale Jct (km 50). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara za Natta – Mugumu (km 45) na sehemu ya Tarime – Mugumu (km 86).

**Barabara ya Ibanda – Itungi Port (km 26)**

***332. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 15,760.00** kwa ajili ya kufanya ukarabati wa barabara za Ibanda – Itungi (km 26) na Iponjola – Kiwira Port (km 6). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi mpakani Songwe/Kasumulu (Songwe/Kasumulu – Tanzania/ Malawi Border – OSBP), ukarabati wa Uyole – Kasumulu (sehemu ya Ilima *Escarpment* km 3) na kulipa madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara ya Kikusya – Ipinda – Matema Beach (sehemu ya Tenende – Matema km 34.6).

**Barabara ya Nzega – Tabora (km 289.7)**

***333. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,620.00** kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Nzega – Puge (km 58.6) na Puge – Tabora (km 56.1). Aidha, kazi nyingine ni kuanza upembuzi

yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya Shelui – Nzega (km 110) na kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nzega – Kagongwa (km 65) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi (km 541.56)**

***334. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 8,540.00** kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa sehemu za Sumbawanga – Kanazi (km 75), Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.60), Sitalike – Mpanda (km 36) na Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 37.65). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Mpanda – Mishamo – Uvinza (km 194) kwa kuanzia na sehemu ya Vikonge na Uvinza na barabara ya Kibaoni – Sitalike (km 71). Aidha, kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kizi – Lyambalyamfipa – Sitalike (km 86.3).

**Barabara ya Nyanguge – Musoma/ Usagara – Kisesa Bypass (km 214.25)**

***335. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,020.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi wa barabara za Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85.5) na Usagara – Kisesa (Mwanza Bypass km 16.35). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ukarabati wa sehemu ya Nyanguge – Simiyu/ Mara Border (km 100.4) na kuweka taa za barabarani kwenye barabara ya kutoka Mwanza Mjini kuelekea Uwanja wa Ndege wa Mwanza.

**Barabara ya Magole – Mziha – Handeni (km 149.2)**

***336. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,010.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi wa barabara ya Magole – Turiani (km 45.2) na kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Turiani – Mziha – Handeni (km 104) kwa kiwango cha lami.

**Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyovers) Jijini DSM na Barabara Unganishi**

***337. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,650.00** katika mwaka wa fedha 2021/22. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 650.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 5,000.00** ni fedha za nje kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Ubungo (Kijazi Interchange) pamoja na kuanza maandalizi ya kuboresha makutano ya barabara katika maeneo ya KAMATA, Magomeni, Mwenge, Tabata/Mandela, Morocco, Buguruni, Mbezi Mwisho, Fire pamoja na makutano ya barabara za Kinondoni/Ali Hassan Mwinyi na Selander (Ali Hassan Mwinyi/ UN Road Jct). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa *Mabey Flyovers* katika majiji ya Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza.

**Barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (km 121)**

***338. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,520.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi wa barabara za Mwigumbi – Maswa (km 50.3) na Maswa – Bariadi (km 49.7). Aidha, Wizara imepanga kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa Mchepuo wa Maswa (Maswa Bypass; km 11) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Isabdula – Magu – Kwimba Station – Ngudu – Ng'hungumalwa (km 10.0).

**Barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa (Sehemu ya Ipole – Rungwa (km 172)**

***339. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,000.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 341.25)**

***340. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 72,840.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 16,180.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 56,660.00** ni fedha za nje kwa ajili ya kulipa

madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Kidahwe – Kasulu (km 63) na Nyakanazi – Kabingo (km 50). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa barabara za Kanyani Junction – Mvugwe (km 70.5), Mvugwe – Nduta Junction (km 59.35), Nduta Junction – Kabingo (62.5) na Nduta Junction – Kibondo (km 25.9). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kibondo – Mabamba (km 35).

**Barabara ya Kwenda Kiwanja cha Ndege cha Mafia (Mafia Airport Access Road (km 16)**

***341. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara hii.

**Daraja la Kigamboni (Nyerere) na Barabara Unganishi**

***342. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,160.00** kwa ajili ya kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Tungi – Kibada (km 3.8) na kuanza ujenzi wa barabara ya Kibada – Mwasonga – Tundwisongani Jct/ Tundwisongani – Kimbiji (km 41).

**Barabara ya Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 215.8)**

***343. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,050.00** kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 136) ili kuifanyia ukarabati. Kazi nyingine ni kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Bukoba Mjini – Busimbe – Maruku – Kanyangereko – Ngongo (km 19.1) na Kanazi (Kyetema) – Ibwera – Katoro – Kyaka II (km 60.7) kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

**Fedha za Matengenezo na Ukarabati wa Barabara**

***344. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 635,849.13** kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa barabara,

upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, udhibiti wa uzito wa magari, usalama barabarani na mazingira, matengenezo na ukarabati wa vivuko pamoja na kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi zinazosimamia masuala ya barabara na vivuko. Fedha hizi zinasimamiwa na Bodi ya Mfuko wa Barabara.

**Ujenzi wa Njia za Magari Mazito na Maegesho ya Dharura Katika Barabara Kuu ya Ukanda wa Kati (Providing Lane Enhancement Including Climbing Lanes, Passing Bays, Rest and Emergency Lay Bays on Central Corridor)**

***345. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 165.00** katika mwaka wa fedha 2021/22 kwa ajili ya maandalizi ya kuanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa maeneo ya kujenga njia za magari mazito kwenye miinuko na kujenga maegesho ya dharura katika barabara kuu ya Ukanda wa Kati. Aidha, mradi huu utajumuishwa kwenye usanifu wa kina kabla ya kufanya ukarabati wa barabara za ukanda wa kati zilizopangwa kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambazo ni Morogoro – Dodoma (km 260), Singida – Shelui (km 110) na Shelui – Nzega (km 110) ambazo ziko katika hatua za manunuzi za kupata Wahandisi Washauri.

**Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) Ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**

***346. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 9,753.00** katika mwaka wa fedha 2021/22 kwa ajili ya kuendelea na upanuzi wa barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) sehemu ya Kimara – Kibaha Mizani (km 19.2) na madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji.

**Barabara ya Kisarawe – Mlandizi (km 119)**

***347. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 700.00** kwa ajili ya maandalizi ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34)**

***348. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 600.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2021/22 kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu za Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho (km 12.7) na Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 21.3).

**Barabara ya Kagoma – Lusahunga (km 172.50)**

***349. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 800.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2021/22 kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa barabara ya Muleba – Kanyambogo – Rubya (km 18.5).

**Barabara ya Singida – Shelui (km 110)**

***350. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,100.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2021/22 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya kufanya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara hii.

**Barabara ya Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road) – Gerezani (*sehemu* ya Kamata – Bendera Tatu: km 1.3)**

***351. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 2,694.51** zinazojumuisha **Shilingi Milioni 1,190.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 1,504.511** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa daraja la Gerezani na kuanza maandalizi ya upanuzi wa sehemu ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe (km 3.8).

**Barabara ya Msimba – Ruaha Mbuyuni/Ikokoto Mafinga (km 365.90)**

***352. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 5,610.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ukarabati wa sehemu za Mafinga – Nyigo (km 74.1) na Nyigo – Igawa (km 63.8). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara za Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152). Aidha, mradi huu utahusisha kuendelea na usanifu wa kina wa barabara ya Mafinga – Mgololo (km 78) na maandalizi ya ukarabati wa

barabara ya Morogoro – Iringa sehemu ya Tumbaku Jct – Mangae/Melela – Mikumi – Iyovi.

**Barabara ya Same – Mkumbara – Korogwe (km 239.5)**

***353. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 8,100.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2021/22 kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ukarabati wa sehemu za Same – Himo (km 76) na Mombo – Lushoto (km 32). Kazi nyingine ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara za Lushoto – Magamba – Mlola (km 34.5) na kuendelea na ujenzi wa barabara ya Same – Kisiwani – Mkomazi (km 97) sehemu ya Same – Kisiwani kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Mbeya – Makongolosi – Mkiwa (km 579.9)**

***354. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 13,175.45** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa sehemu za Mbeya – Lwanjilo (km 36) na Lwanjilo – Chunya (km 36). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Chunya – Makongolosi (km 39) na kuanza ujenzi wa sehemu za Mkiwa – Itigi - Noranga (km 56.9) 5, kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mbalizi – Makongolosi (Galula) km 56 na Makongolosi – Rungwa – Noranga; sehemu ya Makongolosi – Rungwa (km 50).

**Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (km 211)**

***355. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 13,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha zege wa sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Itoni – Lusitu (km 50).

**Ujenzi wa Daraja Jipya la Selander (Tanzanite)**

***356. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 19,050.00** zinazojumuisha **Shilingi milioni 50** fedha za ndani na **Shilingi milioni 19,000.00** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Daraja Jipya la Selander (km 1.030) na barabara unganishi zenye jumla ya urefu wa kilometa 5.2.

**Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida**

***357. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 4,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Handeni – Kibirashi (km 50). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kongwa – Kibaya – Arusha (km 430) na barabara ya Singida – Sepuka – Ndago – Kizaga (km 75).

**Barabara ya Makambako – Songea na Barabara ya Mchepuo ya Songea (Songea Bypass) (km 295)**

***358. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ukarabati wa barabara ya Makambako – Songea pamoja na kuendelea na kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mchepuo wa Songea (Songea Bypass).

**Barabara ya Dodoma – Iringa (km 267.1)**

***359. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 7,250.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya mchepuo ya Iringa (Iringa Bypass km 7.3) na kuendelea kuimarisha matabaka ya barabara ya Iringa – Dodoma.

**Barabara ya Dodoma – Babati (km 263.4)**

***360. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 180.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Dodoma – Mayamaya (km 43.65), Mayamaya – Mela (km 99.35), Mela – Bonga (km 88.8) na kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya mchepuo wa Babati (Babati Bypass km 15.5).

**Barabara ya Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 343.20)**

***361. Mheshimiwa Spika,*** katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 11,540.00.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **milioni 2,540.00** fedha

za ndani na **Shilingi milioni 9,000.00** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Tunduru – Matemanga (km 59), Matemanga – Kilimasera (km 68.2), Kilimasera – Namtumbo (km 60) na Mbinga – Mbamba Bay (km 66). Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa sehemu ya barabara ya Kitai – Lituhi (km 90) pamoja na Daraja la Mnywamaji.

**Ujenzi wa Barabara za Chuo cha Uongozi (Uongozi Institute)**
***362. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara za ndani ya eneo la Chuo cha Uongozi Bagamoyo.

**Barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma na Mbeya *Bypass* (km 273.40)**
***363. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 4,237.07** zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha usanifu wa kina na kuanza maandalizi ya ukarabati wa barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma (km 218) na barabara ya mchepuo ya Mbeya (Uyole – Songwe (km 49). Kazi nyingine ni kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Iwambi – Mbalizi (km 6.5) kwa kiwango cha lami.

**Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT Phase I – V: km 69.8)**
***364. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 62,950.00** zimetengwa kwa ajili ya mradi huu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 7,950.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 55,000.00** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili. Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tatu na Nne na kuendelea na maandalizi ya maboresho ya miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka iliyojengwa katika Awamu ya Kwanza katika eneo la Jangwani. Aidha, mradi huu utahusisha pia kufanya maandalizi ya ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tano.

**Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology - ICoT)**

***365. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi milioni 6,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi mkoani Morogoro na maandalizi ya ujenzi wa majengo ya ICoT tawi la Mbeya.

**Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Tanzania**

***366. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 10,000.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2021/22, kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) pamoja na Ofisi za Mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe, Lindi na Songwe.

**MIRADI YA USALAMA BARABARANI NA MAZINGIRA**

***367. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina majukumu yanayohusu kuratibu na kuimarisha shughuli za usalama barabarani, mazingira na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara zetu. Katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi wa **Usalama Barabarani** umetengewa jumla ya Shilingi **milioni 1,665.63,** fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Ukaguzi vya Pamoja (One Stop Inspection Station) katika maeneo ya Idofi (Iringa), Mpemba (Songwe), Himo (Kilimanjaro) na Segera (Tanga); uwekaji wa vifaa vya kisasa (Electronic Load Cells) vya upimaji uzito wa magari katika mizani 42; maboresho ya Mfumo wa Utoaji Vibali (Special Load Permit System); maboresho katika Mfumo wa Kukusanya Taarifa za Ajali Barabarani na kufunga Mfumo wa Ufuatiliaji wa Utendaji Kazi katika Mizani (CCTV Weighbridge Management System). Kazi nyingine ni kutoa mafunzo ya kudhibiti uzito wa magari kwa Wahandisi na mafundi sanifu, kufanya utafiti wa uharibifu wa barabara unaotokana na kuzidisha uzito wa magari pamoja na Mapitio ya Sera ya Usalama Barabarani.

***368. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa **Kujenga Uwezo wa Taasisi Katika Masuala ya Usalama Barabarani, Mazingira na Maboresho** umetengewa Shilingi **milioni 168.10**, kwa ajili ya kufanya tathmini ya usalama barabarani ili kubaini athari za

kijamii na kiuchumi pamoja na kufanya mapitio ya miongozo ya usalama barabarani.

***369. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa **Menejimenti ya Usimamizi wa Mazingira** umetengewa **Shilingi milioni 243.40** katika mwaka wa fedha 2021/22 kwa ajili ya kuandaa mkakati wa kukabili majanga kwa sekta ya ujenzi (Works Sector Disaster Management Strategy), kuanzisha mfumo wa kusimamia na kukusanya taarifa za mazingira (Environmental Information Management System), kufanya mapitio ya miongozo ya tathmini na usimamizi wa mazingira ya sekta ya Ujenzi na kuandaa mpango tekelezi wa mazingira wa Sekta (Sector Environment Action Plan).

**MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA VIWANJA VYA NDEGE**

***370. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22 miradi ya ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 95,123.11.** Kiasi hicho kinajumuisha **Shilingi milioni 63,975.79** fedha za ndani na **Shilingi milioni 31,147.32** fedha za nje. Miradi ifuatayo imepangwa kutekelezwa katika kipindi hicho:

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma**

***371. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 8,532.90** zinazojumuisha **Shilingi milioni 5,500.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 3,032.90** fedha za nje kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB). Fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Abiria pamoja na ukarabati na upanuzi wa maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani), usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege, kujenga uzio wa usalama, ujenzi wa jengo la kuongozea ndege na ujenzi wa jengo la uchunguzi wa hali ya hewa.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mpanda**

***372. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/2022, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 11.00** fedha za ndani kwa ajili ya maandalizi ya kufanya usanifu wa Jengo la abiria kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora**

***373. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/2022, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,635.10.** Kati ya hizo, **Shilingi milioni 602.20** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 3,032.90** ni fedha za nje kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Abiria na miundombinu yake, jengo la kuongozea ndege, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari, uzio wa usalama pamoja na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe**

***374. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 9,795.50** katika mwaka wa fedha 2021/2022 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa Jengo la Abiria na mifumo yake, usimikaji wa taa za kuongozea ndege na ukarabati wa tabaka la juu la barabara ya kutua na kuruka ndege na barabara ya kiungio, ujenzi wa uzio wa usalama pamoja na ukarabati wa eneo la usalama kwenye barabara ya kutua na kuruka ndege.

**Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**

***375. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, kiasi cha **Shilingi milioni 6,325.75** kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Jengo jipya la Abiria na mifumo yake, upanuzi wa maegesho ya ndege na Ujenzi wa uzio wa usalama.

**Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha**

***376. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 220.02** kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa usalama pamoja na maandalizi ya ujenzi wa jengo la abiria.

**Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara**

***377. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, mradi huu umetengewa kiasi cha **Shilingi milioni 5,899.30** kwa ajili ya kufanya ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio vyake pamoja na maegesho ya ndege. Kazi zingine ni kusimika taa na mitambo ya kuongozea ndege, ujenzi wa barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari na ujenzi wa uzio wa usalama.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga**

***378. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/2022, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,632.90.** Kati ya hizo, **Shilingi milioni 600.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 3,032.90** ni fedha za nje kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na barabara za viungio, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, uzio wa usalama, barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari. Kazi nyingine ni usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga**

***379. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,632.90.** Kati ya hizo, **Shilingi milioni 600.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 3,032.90** ni fedha za nje kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB). Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na kiungio chake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, uzio wa usalama, barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari. Kazi nyingine ni pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege.

**Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa**

***380. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 21,206.53.** Kati ya hizo, Shilingi milioni **20,711.53** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 495.00** fedha za nje kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya ndege katika mikoa ya Geita, Iringa, Ruvuma (Songea), Lindi, Kiwanja kipya cha Simiyu, kiwanja cha Lake Manyara, Tanga, Moshi na Mara (Musoma). Aidha, kazi nyingine ni ujenzi wa uzio wa usalama pamoja na barabara ya kufanyia ukaguzi kwenye kiwanja cha ndege cha Dodoma, ujenzi wa barabara wa kuruka na kutua ndege kwa kiwango cha lami kwenye kiwanja cha ndege cha Nachingwea, ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Inyonga pamoja na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Mkoa wa Manyara.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Msalato**

***381. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 32,170.72.** Kati ya hizo**, Shilingi milioni 13,650.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 18,520.72** fedha za nje kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja kipya cha Msalato mkoani Dodoma pamoja na kulipa fidia kwa wakazi watakaoathiriwa na utekelezaji wa mradi huu.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba**

***382. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, mradi huu umetengewa kiasi cha **Shilingi milioni 11.00** fedha za ndani kwa ajili ya kazi za maandalizi ya ujenzi wa jengo la Watu Mashuhuri (VIP Lounge), ukarabati wa mita 200 za barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na usimikaji wa taa za kuongozea ndege.

**Ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria Katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA)**

***383. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha fedha 2021/22, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 49.483** kwa ajili ya kuunganisha umeme wa 33 KV kutoka Gongolamboto pamoja na kuanza maandalizi ya kufanya Usanifu wa Kina wa Jengo la Pili la abiria.

**FEDHA ZA MFUKO WA BARABARA**

***384. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya **Shilingi 635,849,127,200.00** kutoka Mfuko wa Barabara zimetengwa kwa ajili ya kufanya kazi za matengenezo na ukarabati wa barabara kuu na za mikoa. Kati ya fedha hizo, TANROADS imetengewa **Shilingi 567,342,742,235.00** kwa ajili ya matengenezo ya barabara na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) imetengewa **Shilingi 63,038,082,471.00** kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara za mikoa, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara, ukarabati na ununuzi wa vivuko, usalama barabarani pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hiyo. Aidha, **Shilingi 5,468,302,494.00** zitatumika kugharamia uendeshaji wa Bodi ya Mfuko wa Barabara.

***385. Mheshimiwa Spika,*** mgawanyo wa **Shilingi 63,038,082,471.00** zilizotengwa kwa ajili ya Wizara (Ujenzi) ni kama ifuatavyo: **Shilingi 16,784,830,349.00** ni kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara zenye urefu wa kilometa **5,310; Shilingi 4,740,226,000.00** ni kwa ajili ya manunuzi na ukarabati wa vivuko pamoja na ujenzi wa maegesho ya vivuko; **Shilingi 4,161,577,576.00** ni kwa ajili ya miradi ya Usalama Barabarani na Mazingira na **Shilingi 4,738,982,546.00** ni kwa ajili ya kazi za usimamizi na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na Wizara (Ujenzi) pamoja na kujenga uwezo wa watumishi. Aidha, **Shilingi 32,612,466,000.00** zimetengwa kwa ajili ya miradi ya barabara za mikoa itakayohusisha ukarabati wa jumla ya kilometa **426** kwa kiwango cha changarawe, ujenzi wa kilometa **30.8** kwa kiwango cha lami pamoja na ujenzi na ukarabati wa madaraja/makalavati **32** katika mikoa mbalimbali nchini. Mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi) umeonyeshwa katika **Viambatisho Na. 3** na **4.**

***386. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi 567,342,742,235.00** fedha za Mfuko wa Barabara ambazo zimetengwa kwa ajili ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) zitatumika kufanya matengenezo ya barabara kuu, barabara za mikoa, madaraja na uendeshaji wa mizani**.**
Mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo umeoneshwa katika **Viambatisho Na. 5, 5A - 5D.**

**USHIRIKISHWAJI WA WANAWAKE KATIKA KAZI ZA BARABARA**

***387. Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara, kwa mwaka wa fedha 2021/22 Wizara (Ujenzi) imepanga kutoa mafunzo kwa Makandarasi wanawake ya namna ya kuomba zabuni na kujaza zabuni kwa ufanisi; kutoa mafunzo kwa wanawake na vikundi vya wanawake juu ya kufanya matengenezo na ukarabati wa barabara kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi na kuwasaidia kusajili kampuni zao za ujenzi pamoja na kufuatilia kwa karibu kazi za barabara zinazofanywa na wanawake Makandarasi.

Wizara vilevile imepanga kutembelea vyuo vya elimu ya juu ili kutoa ushauri (Mentorship and Coaching) kwa wasichana wanaosoma fani za Sayansi zinazohusiana na Sekta ya Ujenzi. Aidha, Wizara itaendelea kutembelea Shule za Sekondari ili kuhamasisha wasichana kusoma masomo ya Sayansi na Hisabati. Vilevile, Wizara itaendelea kuelimisha Umma juu ya Ushirikishwaji wa Wanawake katika kazi za barabara.

## MPANGO WA KAZI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA UJENZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22

### Wakala wa Barabara Tanzania

***388. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Wakala wa Barabara Tanzania umepanga kujenga barabara kuu zenye urefu wa **kilometa 467.11** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja **14** pamoja na ukarabati wa **kilometa 32.47** kwa kiwango cha lami katika barabara kuu. Kazi nyingine ni kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa ambayo yatahusisha matengenezo ya kawaida (routine and recurrent maintenance) kwa **kilometa 33,171.89,** matengenezo ya muda maalum **kilometa 4,783.72** na sehemu korofi **kilometa 549.38** pamoja na matengenezo ya madaraja **3,291**. Mpango huu pia unajumuisha shughuli za udhibiti wa uzito wa magari na hifadhi za barabara, kazi za dharura pamoja na mradi wa matengenezo ya barabara kwa mikataba ya muda mrefu.

***389. Mheshimiwa Spika,*** miradi ya barabara za mikoa iliyopangwa kutekelezwa na Wakala ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa **kilometa 103.0** ambapo **kilometa 72.2** zitajengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 30.8** zitajengwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara. Kazi nyingine ni ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara zenye urefu wa **kilometa 1,124.3**. Kati ya hizo, **kilometa 698.3** na madaraja/ makalavati **34** yatakarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 426** pamoja na madaraja/ makalavati **32** yatajengwa/yatakarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

***390. Mheshimiwa Spika,*** vilevile Wakala utaendelea kutekeleza jukumu la kusimamia miradi ya ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege. Miradi iliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na kuanza ujenzi wa Kiwanja kipya cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, kuanza ujenzi wa Jengo la Abiria katika kiwanja cha ndege cha Mwanza pamoja na ukarabati na upanuzi wa Viwanja vya Ndege vya Kigoma, Shinyanga, Tabora, Sumbawanga, Iringa na Musoma.
Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa viwanja vya Ndege vya Songea, Mtwara na Songwe. Aidha, Wakala utaendelea na maandalizi ya ukarabati wa Jengo la Pili la Abiria (Terminal Building II) katika kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) pamoja na ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Tanga, Lake Manyara, Lindi, Arusha, Bukoba, Moshi, Nachingwea na Dodoma.

**Wakala wa Majengo Tanzania**

***391. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22 Wakala wa Majengo Tanzania utaendelea kutekeleza majukumu yake yanayohusisha kujenga na kutunza nyumba na majengo ya Serikali, kujenga na kuwauzia Watumishi wa Umma nyumba za kuishi, kuwapangishia Watumishi wa umma nyumba za Serikali na kupangisha nyumba kibiashara pamoja na kujenga na kusimamia miradi ya ujenzi. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba 20 za Viongozi Dodoma, ujenzi wa nyumba 150 za watumishi jijini Dodoma, ujenzi wa jengo la makazi katika eneo la Ilala Kota wilaya ya Ilala, ununuzi wa samani kwenye Ikulu Ndogo pamoja na ujenzi wa nyumba 5 za majaji Tanzania Bara (Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mtwara, Shinyanga na Tabora). Kazi nyingine ni ukarabati wa nyumba 66 zilizokuwa zinamilikiwa na iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA), ukarabati wa nyumba za watumishi wa Umma katika mikoa 20 zilizokuwa zinamilikiwa na TAMISEMI/NHC, ukarabati wa nyumba 40 za viongozi Jijini Dodoma na nyumba 30 za viongozi za mikoani pamoja na matengenezo kinga ya nyumba za makazi za Magomeni Kota.Aidha, Wakala utafanya ukarabati wa Karakana za samani za Wakala kwa mikoa ya Dar es salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Morogoro, ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza Samani

katika Jiji la Dodoma, pamoja na huduma ya ushauri katika ujenzi na ukarabati wa majengo ya Serikali.

***392. Mheshimiwa Spika,*** Wakala umepanga kutekeleza jumla ya miradi 313 ya Washitiri kwa mchanganuo ufuatao; miradi 71 ya ubunifu na ujenzi ambapo miradi 53 inaendelea kutekelezwa ikiwemo ujenzi wa Jengo la ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Butiama, ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara, ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Mkalama, ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Busega, ujenzi wa majengo ya hospitali ya rufaa Geita na Chato awamu ya kwanza na awamu ya pili pamoja na ujenzi wa mradi wa jengo la ofisi la makao makuu ya TANROADS –Dodoma. Aidha, Wakala umepanga kutekeleza miradi mingine mipya 18 ya Ubunifu na Ujenzi.

***393. Mheshimiwa Spika,*** Wakala pia umepanga kutekeleza miradi 182 ya ushauri elekezi, ambapo miradi 165 inaendelea kutekelezwa ikiwemo ushauri katika ujenzi wa Ofisi za Maji Kimani na Mkoji (Iringa), ujenzi wa Jengo la Utawala la Halmashauri ya Mji wa Bunda, ujenzi wa makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Butiama, ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Laela Sumbawanga, ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu na Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (NAO) mkoani Simiyu. Aidha, Wakala umepanga kutekeleza miradi mingine mipya 17 ya ushauri.

***394. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wakala utatekeleza miradi 54 ya ujenzi ambapo miradi 45 inaendelea kutekelezwa ikiwemo ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe awamu wa pili, ujenzi wa jengo la maktaba Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) na ujenzi wa Chuo cha VETA Karagwe. Pia Wakala umepanga kutekeleza miradi mingine mipya tisa (9) ya ujenzi. Aidha, miradi 6 ya usimamizi imepangwa kutekelezwa ambapo miradi mitatu (3) inaendelea kutekelezwa ikiwemo ujenzi wa Vihenge (Silos) vya kuhifadhia nafaka pamoja na maghala kwa ajili ya hifadhi ya chakula (NFRA) katika mikoa minane (8) ya Dodoma, Katavi, Manyara, Njombe, Rukwa, Ruvuma,

Shinyanga na Songwe, ujenzi wa majengo ya RADA katika mkoa wa Songwe pamoja na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Forodha Mpakani cha Kasumulu (One Stop Border Post) awamu ya kwanza na ya pili. Aidha, Wakala umepanga kutekeleza miradi mingine mipya mitatu (3) ya usimamizi.

**Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania**

***395. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Wakala umepanga kuendelea na usimamizi na uendeshaji wa vivuko vya Serikali vipatavyo **34** ambavyo vinatarajiwa kutoa huduma kwa abiria **40,778,628**, magari **1,579,788** na tani za mizigo **463,668** kwa mwaka. Vilevile, Wakala utaendelea kutoa huduma ya ukodishaji wa magari na mitambo ya ujenzi wa barabara.

***396. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu miradi ya ***maegesho ya vivuko,*** Wakala umepanga kuendelea na upanuzi wa eneo upande wa Kigamboni kwa ajili ya kivuko cha Magogoni – Kigamboni; ujenzi wa maegesho ya Zumacheli kwa ajili ya kivuko cha Chato- Nkome; ujenzi wa maegesho ya Mafia na Nyamisati kwa ajili ya kivuko cha Mafia - Nyamisati; ujenzi na ukarabati wa maegesho matano (5) katika kivuko cha Kilambo – Namoto, Utete – Mkongo, Iramba – Majita, Nyakarilo – Kome na Kasharu – Buganguzi; ujenzi wa miundombinu mipya (jengo la kupumzikia abiria, ofisi na uzio) katika vituo kumi (10) vya vivuko; ujenzi wa maegesho mapya ya Kayenzi - Kanyinya na Muleba- Ikuza na ujenzi wa maegesho mapya manne ya Ijinga – Kahangara (Magu) na Bwiro – Bukondo (Ukerewe).

***397. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza miradi ya ***ujenzi na ukarabati wa vivuko,*** Wakala umepanga kujenga vivuko vipya vitano (5) kwa ajili ya kutoa huduma katika maeneo ya Kisorya – Rugezi, Ijinga – Kahangara, Bwiro – Bukondo, Nyakarilo – Kome na Nyamisati – Mafia. Sambamba na hilo, Wakala pia umepanga kuendelea na ununuzi wa mfumo wa uratibu na uendeshaji vivuko vya Serikali nchini. Aidha, Wakala umepanga kukamilisha ukarabati wa vivuko vya MV Musoma, MV Mara, MV Ujenzi, MV Kome II, MV Nyerere, MV Kilombero II, MV Mafanikio, MV Kyanyabasa, MV Tanga, MV

Ruvuvu ya zamani na kumalizia ukarabati wa kivuko MV Misungwi.

***398. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa ***Ujenzi na Ukarabati wa Karakana,*** Wakala umepanga kuendelea na ujenzi wa karakana tano (5) katika mikoa ya Songwe, Simiyu, Katavi, Geita na Njombe; ununuzi wa vitendea kazi katika karakana za TEMESA; ununuzi wa karakana zinazohamishika (Mobile Workshops); uanzishwaji wa karakana sita (6) ngazi ya Wilaya katika Wilaya za Simanjiro, Masasi, Chato, Mafia, Kyela na Ukerewe pamoja na ukarabati wa karakana kumi na moja (11) katika mikoa ya Tabora, Mwanza, Arusha, Mtwara, Mbeya, MT Depot - Dar es salaam, Kigoma, Mara, Ruvuma, Pwani na Vingunguti. Aidha, Wakala unatarajia kukarabati mitambo ya karakana za TEMESA Morogoro na mitambo ya karakana ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi Morogoro (ICoT) pamoja na kusanifu na kusimika mfumo wa usimamizi wa matengenezo ya magari, umeme na elektroniki.

***399. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika mwaka 2021/22, Wakala umelenga kufanya matengenezo ya magari **51,824,** matengenezo na usimikaji wa mifumo **323** ya umeme, **1,607** ya majokofu na viyoyozi na mifumo **28** ya elektroniki. Aidha, Wakala umepanga kutoa ushauri wa Kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo **118** ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu na kusimamia mifumo hiyo inayofikia **64**.

**Bodi ya Mfuko wa Barabara**

***400. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Mfuko wa Barabara unatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 908,355,896,000.00** kutoka katika vyanzo vyake vilivyoweka kisheria. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 635,849,127,200.00** zitagawanywa kwa ajili ya matengenezo ya barabara kuu na za mikoa, ukarabati wa barabara za mikoa, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, udhibiti wa uzito wa magari, usalama barabarani na mazingira, matengenezo na ukarabati wa vivuko pamoja na kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi zinazosimamia masuala ya Barabara na Vivuko chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Fungu 98 -Ujenzi). Aidha,

**Shilingi 272,506,768,800.00** zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Wilaya zilizo chini ya Ofisi ya Rais –TAMISEMI (Fungu 56).

***401. Mheshimiwa Spika,*** mchanganuo wa bajeti ya Mfuko wa Barabara kwa mwaka wa fedha 2021/22 ni kama ifuatavyo: Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) **Shilingi 63,038,082,471.00,** Ofisi ya Rais, TAMISEMI **Shilingi 27,016,321,059.00,** TANROADS **Shilingi 567,342,742,235.00,** TARURA **Shilingi 243,146,889,529.00** na Bodi ya Mfuko wa Barabara **Shilingi 7,811,860,706.00.**

***402. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Bodi itaendelea kufanya tafiti mbalimbali ili kupata vyanzo vipya vya mapato na teknolojia ya gharama nafuu ya matengenezo ya barabara. Moja ya kazi iliyopangwa ni kuandaa utaratibu wa kuweka tozo na kukusanya mapato kwenye magari yanayotumia gesi. Vilevile, Bodi itaendelea kufanya ukaguzi wa ubora wa kazi za matengenezo ya barabara katika mikoa yote nchini ili kuhakikisha kuwa miradi inayotekezwa inakidhi thamani ya fedha zilizotumika. Sambamba na hilo, Bodi itaendelea kuwaelimisha watumiaji wa barabara kuhusu umuhimu wa kutunza na kulinda miundombinu ya barabara katika maeneo yao ili kupunguza uharibifu wa barabara.

**Bodi ya Usajili wa Wahandisi**

***403. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22 Bodi itaendelea kufanya kaguzi za shughuli za kihandisi nchini ili shughuli zote za kihandisi zifanywe na Wahandisi waliosajiliwa na kwa kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi. Bodi imepanga kusajili Wahandisi **3,056,** mafundi sanifu **400** na kampuni za ushauri wa kihandisi **15.** Bodi pia itaendelea kusimamia mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa Wahandisi Watalaam na Washauri. Bodi imepanga kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa Wahandisi wahitimu **3,461** ambapo, **1,961** ni wanaoendelea na mafunzo na **1,500** ni wapya.

Vilevile, Bodi itaendelea kuhamasisha wadau mbalimbali katika mpango wake wa kujenga kituo cha Umahiri cha

Uhandisi (Engineering Excellence Centre) ambacho kitasaidia kutoa ushauri wa uanzishwaji wa viwanda na uendelezaji wa viwanda kwa ujumla.

**Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi**
***404. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Bodi imepanga kusajili Wataalam **150** katika fani za Wabunifu Majengo, Wakadiriaji Majenzi, Wabunifu wa Ndani ya Majengo, Wabunifu wa Mandhari ya Nje ya Majengo, Wasanifu Teknolojia ya Majengo, Watathmini majengo, Wasimamizi ujenzi na Wasimamizi miradi. Aidha, Bodi imepanga kusajili kampuni **20** za Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, Wabunifu wa Ndani ya Majengo, Wabunifu wa Mandhari ya Nje ya majengo, wasanifu Teknolojia ya majengo, Watathmini majengo, Wasimamizi ujenzi na Wasimamizi miradi. Vilevile, Bodi imepanga kuendelea na Mafunzo kwa Vitendo kwa wahitimu **180** katika fani za Wabunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi, Wabunifu wa Ndani ya Majengo, Wabunifu wa Mandhari ya Nje ya Majengo, Wasanifu Teknolojia ya Majengo, Watathmini Majengo, Wasimamizi Ujenzi na Wasimamizi Miradi.

Bodi pia imepanga kufanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi **2,600** katika mikoa yote 26 Tanzania Bara na kusajili miradi ya majengo **1,000.** Aidha, Bodi imepanga kuendesha mitihani ya kitaalam kwa wahitimu **175** katika fani za Wabunifu Majengo, Wakadiriaji Majenzi, Wabunifu wa Ndani ya Majengo, Wabunifu wa Mandhari ya Nje ya Majengo, Wasanifu Teknolojia ya Majengo, Watathmini Majengo, Wasimamizi Ujenzi na Wasimamizi miradi. Aidha, Bodi itafanya mikutano nane (8) na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kwa lengo la kuhamasisha kusoma masomo ya sayansi na hatimaye kusomea taaluma za Wabunifu Majengo, itaendesha mashindano ya insha kwa wanafunzi wa sekondari, kama njia ya kuhamasisha kusoma masomo ya sayansi na hatimaye kusomea taaluma za Wabunifu Majengo, Wakadiriaji Majenzi, Wabunifu wa Ndani ya Majengo, Wabunifu wa Mandhari ya Nje ya Majengo, Wasanifu Teknolojia ya Majengo, Watathmini Majengo, Wasimamizi Ujenzi na Wasimamizi Miradi.

**Bodi ya Usajili wa Makandarasi**

***405. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22 Bodi imepanga kusajili jumla ya Makandarasi wapya **940** na kukagua jumla ya miradi ya ujenzi **3,100**. Bodi pia inatarajia kuendesha kozi **sita (6)** za mafunzo katika Mikoa ya Morogoro, Mwanza, Mbeya, Dar es Salaam, Singida na Kilimanjaro. Pia Bodi imepanga kuendesha warsha moja **(1)** ya mafunzo ya ushirikiano wa ubia (Joint Venture) katika Mkoa wa Mtwara. Aidha, Bodi itaendeleza Mfuko maalum wa kutoa dhamana ya kusaidia Makandarasi wote wa ndani. Vilevile, Bodi itaendelea kuhamasisha Makandarasi Wazalendo kujiunga ili kuomba zabuni kwa mfumo wa ubia ili waweze kupata kandarasi mbalimbali.

**Baraza la Taifa la Ujenzi**

***406. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22 Baraza limepanga kukamilisha mapitio ya Sheria iliyoanzisha Baraza na kuandaa kanuni zake, kutoa ushauri wa kiufundi na kitalaam kwa wadau wa Sekta ya Ujenzi pamoja na kuratibu utatuzi wa migogoro inayojitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi. Baraza pia litaendelea kufanya tafiti mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha sekta ya ujenzi; kutoa huduma za ukaguzi wa miradi ya ujenzi kwa wadau wa Sekta ya Ujenzi; kukusanya na kutoa takwimu na taarifa za sekta ya ujenzi pamoja na kuendelea na taratibu za kuanzisha Kituo Maalum cha Taarifa za Sekta ya Ujenzi. Kazi nyingine ni kuratibu Mpango wa Kukuza Uwazi na Uwajibikaji (Construction Sector Transparency Iniative - CoST) katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa umma na kuhamasisha ushiriki wa sekta isiyo rasmi katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa ubora zaidi.

**Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji Tanzania (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)**

***407. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Kituo kimepanga kuendelea na kusambaza teknolojia katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji hapa nchini. Aidha, Kituo kimepanga kusambaza majarida kutoka kwa wadau

mbalimbali pamoja na kuandaa, kuchapisha na kusambaza majarida yake yatakayoandaliwa mara nne (4) kwa mwaka kuhusu teknolojia, maarifa, na taarifa mbalimbali muhimu katika Sekta ya ujenzi na usafirishaji.

***408. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Kituo kitaendelea kutoa huduma ya maktaba mtandao (e-library) chini ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi. Aidha, Kituo kimepanga kuandaa na kuendesha mafunzo kwa wadau yanayolenga kutatua changamoto zinazoikabili sekta ya ujenzi na usafirishaji pamoja na kuendesha makongamano ya Watalaam wa Taasisi mbalimbali zinazohusika na miundombinu na usafirishaji ili kukaa pamoja kujadili na kutafuta majibu ya changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya ujenzi na usafirishaji. Kituo pia kimepanga kununua *software* ya HDM4 na kuendesha mafunzo ya namna ya kuitumia kwa Wataalam wa Wizara kwa ajili ya kupanga, kusimamia na kuendeleza miradi ya miundombinu ya barabara na madaraja. Kazi nyingine ni kushiriki kikamilifu katika kuandaa na kufanyika kwa Mkutano wa tisa wa Vituo vya usambazaji wa Teknolojia Afrika (yaani 9th T2 *Centre Conference*) utakaofanyika Msumbiji, Oktoba, 2021 baada ya kuahirishwa kufanyika Mei, 2020 kutokana na janga la ugonjwa wa COVID 19.

### D.1.2 SEKTA YA UCHUKUZI

### Mwelekeo wa Sekta ya Uchukuzi katika kipindi cha Miaka Mitano ya kuanzia mwaka 2020 - 2025.

***409. Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Uchukuzi imeendelea kuhakikisha kuwa huduma za usafiri na usafirishaji zinaimarishwa na kuendelezwa kwa kuzingatia malengo ya kitaifa ambayo ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 (Vision 2025); Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano (FYDP III 2021/2022 - 2025/2026); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020; Maagizo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Serikali; na Sera, Mikakati na Miongozo mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa. Katika utekelezaji wa miongozo hiyo muhimu, katika kipindi kijacho cha miaka mitano ijayo inayoanzia mwaka 2021/2022 hadi mwaka 2025/2026, Sekta ya Uchukuzi itatekeleza masuala yafuatayo:

i. Kuendelea na ujenzi wa reli ya SGR na utoaji huduma zake nchini;

ii. Kuendelea na ukarabati wa reli ya Kati iliyopo na uboreshaji wa huduma zake;

iii. Kuendelea na uboreshaji wa bandari za Mwambao na kwenye maziwa;

iv. Kuendelea na ukarabati wa meli za kwenye maziwa na ujenzi wa meli mpya;

v. Kuendelea na ufufuaji wa Shirika la Ndege nchini (ATCL) kwa kununua vitendea kazi na mifumo pamoja na kuimarisha utoaji wa huduma za usafiri wa anga zinazotolewa na Kampuni binafsi;

vi. Kuendelea na uboreshaji wa huduma za hali ya hewa nchini na udhibiti wa huduma za usafiri kwa njia ya barabara, reli, maji na anga nchini.

vii. Kuchangia katika kuibua uchumi wa rasilimali za Maji (Blue Economy) kwa kuimarisha miundombinu na huduma za bandari na shughuli nyingine za lojistiki na uchukuzi;

viii. Kutumia Fursa za Kijiografia zilizopo kuimarisha huduma na miundombinu ya usafiri na usafirishaji na shughuli nyingine za lojistiki na uchukuzi;

ix. Kuanza ujenzi wa reli katika Majiji ya Dar es Salaam na Dodoma;

x. Upanuzi na ukarabati wa viwanja vya ndege nchini pamoja na huduma zinazotolewa katika viwanja hivyo;

xi. Kuimarisha ulinzi na usalama wa usafiri wa anga, ardhini na njia ya maji; na

xii. Kuimarisha Vyuo vya mafunzo ya Kisekta ili kutoa taaluma za usafiri wa anga, reli, maji na barabara.

**Makadirio ya Ukusanyaji wa Mapato, Matumizi ya Kawaida na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

***410. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/2022, Sekta ya Uchukuzi (Fungu 62) imetengewa jumla ya **Shilingi 2,120,049,821,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 91,743,411,000** zimetengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,028,306,410,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na.6.** Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Shilingi 64,672,467,000** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 27,070,944,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Katika Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotengwa, **Shilingi 1,828,306,410,000** ni fedha za Ndani na **Shilingi 200,000,000,000** ni fedha za Nje.

***411. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Kampuni ya Huduma za Usafiri wa Meli katika Maziwa (MSCL) imetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 135** fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi milioni 199.25** fedha kutoka katika vyanzo vya ndani ya Kampuni ili kuboresha na kuimarisha utoaji wa huduma ya usafiri wa abiria na mizigo katika maziwa makuu ya Tanganyika, Victoria na Nyasa. Fedha hizo zimetengwa ili kugharamia mipango ifuatayo:

i. Kuendelea na ujenzi wa Meli mpya ya abiria na mizigo katika Ziwa Victoria;

ii. Ujenzi wa Meli mpya (Wagon Ferry) yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 za Mabehewa ya mizigo katika Ziwa Victoria;

iii. Ujenzi wa Meli Mpya Wagon Ferry yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 za mabehewa ya mizigo katika Ziwa Victoria. Mzabuni wa ujenzi wa meli hii amepatikana na taratibu za upekuzi (due dilligence) zinaendelea kabla ya kusainiwa kwa mkataba;

iv. Kuanza ujenzi wa Meli mpya (Barge/Cargo Ship) ya kubeba shehena ya mizigo katika Ziwa Tanganyika;

v. Ujenzi wa Meli mpya ya abiria 600 na tani 400 za mizigo katika ziwa Tanganyika;

vi. Ukarabati mkubwa wa Meli ya MV Umoja (Ziwa Victoria);

vii. Ukarabati mkubwa wa MV. Liemba (Ziwa Tanganyika);

viii. Ukarabati mkubwa wa MT Sangara (Ziwa Tanganyika);

ix. Ujenzi wa Meli mpya ya mizigo katika Bahari ya Hindi;

x. Ukarabati mkubwa wa Meli ya uokozi na kuvuta tishari ya MT.Ukerewe;

xi. Ukarabati mkubwa wa Meli ya kubeba shehena ya mizigo (mafuta) ya MT. Nyangumi katika Ziwa Victoria;

xii. Kuendelea na ufungaji wa mifumo ya TEHAMA; na

xiii. Kuendelea kutoa huduma za usafirisha katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa.

***412. Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) imetengewa **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali zimetengwa ili kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Uendeshaji na uwekaji wa miundombinu wa Jengo la Tatu la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa – JNIA;

ii. Ujenzi wa Uzio wa Usalama katika Viwanja vya Ndege vya Mwanza na Dodoma;

iii. Ukarabati wa Jengo la Abiria katika Kiwanja cha Ndege Arusha; na

iv. Ufungaji wa Mifumo ya kuhudumia Abiria katika Viwanja vya Ndege vya Mwanza, Arusha, Songwe, Bukoba na Dodoma.

Aidha, jumla ya **Shilingi bilioni 26.7** fedha zinazotokana na mapato ya ndani ya TAA zimetengwa ili kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo;

i. Kufunga mfumo wa maegesho ya magari katika Viwanja vya Ndege vya Dodoma na Mwanza;

ii. Ununuzi wa mashine za ukaguzi wa abiria na mizigo katika Viwanja vya Ndege vya Arusha, Musoma na Moshi;

iii. Kuandaa Mpango Kabambe wa matumizi bora ya ardhi kwa Viwanja vya Ndege vya Dodoma, Iringa, Geita, Tanga na Lake Manyara;

iv. Upimaji na upatikanaji wa Hati Miliki katika Viwanja vya Ndege mbalimbali ikiwemo Dodoma, Msalato, Simiyu, Iringa, Songea, Lake Manyara na Nachingwea; na

v. Kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi ili kuwaongezea ujuzi na kukidhi viwango vya Kimataifa vya uendeshaji Viwanja vya Ndege.

***413. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ujenzi wa reli mpya ya *standard gauge* pamoja na kuendeleza mtandao mzima wa reli ili kuboresha huduma ya usafirishaji wa mizigo na abiria, jumla ya **Shilingi bilioni 897.005** fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali zimetengwa ili kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Kukamilisha malipo ya mwisho ya mkandarasi na mshauri kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Kati ya *Standard Gauge* kwa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (Km 300);

ii. Kuendelea na ujenzi wa reli ya Kati ya *Standard Gauge* kwa kipande cha Morogoro - Makutupora (Km 422);

iii. Kuendelea na ujenzi wa reli ya Kati kwa kiwango cha *Standard Gauge* kutoka Isaka-Mwanza (Km 341);

iv. Ununuzi wa vitendea kazi (injini na mabehewa) kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya *Standard Gauge*;

v. Ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaostahili kulipwa ili kupisha ujenzi wa reli ya SGR;

vi. Kuendelea na taratibu za upatikanaji wa fedha za ujenzi wa reli kwa sehemu za Makutupora - Tabora (Km 294) na Tabora - Isaka (Km 133);

vii. Kuendelea na taratibu za upatikanaji wa fedha kwa maeneo ya ujenzi wa reli kwa sehemu za Tabora - Kigoma (Km 411), Kaliua - Mpanda - Karema (Km 320) na Uvinza - Musongati (Km 240);

viii. Kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa reli ya Isaka - Rusumo (Km 371);

ix. Kuendelea kugharamia mafunzo ya wataalam watakaotumika katika uendeshaji na usimamizi wa treni ya *Standard Gauge*; na

x. Kuwagharamia Wataalam Washauri (Transaction Advisors) kwa ajili ya kuandaa Miradi na kutafuta Wawekezaji kwa mfumo wa ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) kwa miradi ya Tanga – Arusha - Musoma na Mtwara - Mbamba Bay na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma.

***414. Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Reli (Railway Fund) umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 294.80** fedha za ndani ili kugharamia uboreshaji na uendelezaji wa miundombinu ya reli iliyopo ya *Meter Gauge* (MGR), kujenga reli mpya ya *Standard Gauge* (SGR), ukarabati na ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo injini na mabehewa, na kufanya tafiti mbalimbali kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa reli. Fedha hizo zimetengwa ili kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Ukarabati wa njia ya reli iliyopo kati ya Tabora - Kigoma (Km 411);

ii. Ukarabati wa njia ya reli iliyopo kati ya Tabora - Isaka - Mwanza (Km 385);

iii. Matengenezo ya njia ya reli ya Tanga - Arusha (Km 470);

iv. Ukarabati wa karakana, stesheni na majengo ya reli;

v. Ukarabati wa mfumo wa ishara na mawasiliano wa reli iliyopo;

vi. Kuunda upya vichwa vya treni 5 vya njia kuu na vichwa 4 vya sogeza;

vii. Uwekaji alama za mipaka katika maeneo ya reli;

viii. Ufufuaji wa Mgodi wa kuzalisha kokoto wa Pangani, Tanga;

ix. Ununuzi wa mabehewa 100 ya mizigo na injini 8 kwa ajili ya reli iliyopo;

x. Ukarabati wa Mabehewa 600 ya mizigo na 37 ya abiria; na

xi. Kufanya tafiti malimbali kwa ajili ya ujenzi wa reli.

***415. Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2021/2022, Mamlaka ya Hali ya Hewa (Tanzania Meteorological Authority - TMA) imetengewa **Shilingi bilioni 39.7** kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi bilioni 25.5** fedha za mapato ya ndani ya Mamlaka ili kutoa huduma za hali ya hewa pamoja na kuanzisha, kuendesha na kutunza vituo vya hali ya hewa; kudhibiti na kuratibu shughuli za hali ya hewa nchini Tanzania. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

i. Kukamilisha ufungaji wa Rada mbili (2) za Hali ya Hewa na miundombinu yake katika Mikoa ya Dodoma na Kilimanjaro;

ii. Kuimarisha uwezo wa karakana ya kuhakiki vifaa vya hali ya hewa;

iii. Kununua mitambo ya mawasiliano ya Hali ya Hewa;

iv. Ukarabati wa miundombinu na ujenzi wa mabweni katika Chuo cha Hali ya Hewa;

v. Ujenzi wa Kituo Kikuu cha Utabiri;

vi. Kuboresha Rada mbili (2) za hali ya hewa zilizopo Dar es Salaam na Mwanza;

vii. Kununua vifaa vya kisasa vya hali ya hewa ikiwemo mitambo ya kisasa ya kupima hali ya hewa inayojiendesha yenyewe na vifaa vya uangazi katika Bahari na Maziwa;

viii. Kuanza ujenzi wa Kituo Kikuu cha Utabiri wa hali ya hewa;

ix. Kudhibiti na kuratibu huduma za hali ya hewa zinazotolewa nchini kwa kuhakikisha taratibu na matakwa ya kisheria yanafuatwa katika utoaji wa huduma za hali ya hewa;

x. Kuendesha na kuimarisha Mtandao wa Vituo vya Hali ya Hewa hapa nchini; na

xi. Ukarabati wa Vituo sita (6) vya Hali ya Hewa vya Mpanda, Singida, Mahenge, Tabora, Shinyanga and Songea.

***416. Mheshimiwa Spika*****,** Mradi wa kuboresha huduma za Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) umetengewa **Shilingi bilioni 450** fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi bilioni 56.61** fedha kutoka katika vyanzo vya ndani ya Kampuni ili kuiwezesha ATCL kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa kusafirisha abiria, mizigo, vifurushi ndani na nje ya nchi. Ili kufikia malengo hayo, kazi zifuatazo zitatekelezwa:

i. Kuendelea na malipo ya Ndege mbili (2) mpya zenye uwezo wa kubeba abiria kati ya 160 hadi 180, Ndege moja (1) aina ya Boeing 787-8 Dreamliner na Ndege moja (1) ya mizigo aina ya Boeing 767-300;

ii. Kuanza ununuzi wa Ndege mpya aina ya Dash 8 Q400 na kumalizia malipo ya ndege mbili aina ya Airbus A220-300;

iii. Ununuzi wa vifaa vya kuhudumia Ndege (Ground Handling Service Equipment);

iv. Gharama za kuanzia kutoa huduma kwa Ndege mpya mbili (2) za aina ya A220-300;

v. Ukarabati wa karakana za matengenezo ya Ndege (Hangar) zilizopo JNIA na KIA (KIMAFA);

vi. Ukarabati wa nyumba 38 za Watumishi wa ATCL zilizopo KIA;

vii. Ukarabati wa jengo la ATCL Makao Makuu;

viii. Ukarabati wa stoo ya kuhifadhi vifaa na vipuri vya Ndege iliyoko JNIA;

ix. Kurejesha safari za Mtwara na Iringa baada kukamilika kwa ukarabati wa viwanja;

x. Kutanua mtandao wa safari za Kikanda kwenda Lubumbashi, Kinshasa, Nairobi na kurejesha safari katika kituo cha Johannesburg;

xi. Kuongeza vituo vya ndani ambavyo ATCL itajihudumia yenyewe kwa mizigo, abiria na ndege (Ground handling service) kwenye vituo vyenye miruko mingi vikiwemo vya Mwanza, Kilimanjaro na Mbeya;

xii. Kujenga jengo la ofisi Dodoma;

xiii. Kujenga miundombinu ya kuhudumia na kuhifadhi mizigo (cargo facilities); na

xiv. Kuendelea na maboresho ya stoo za kutunzia vifaa na vipuri vya ndege.

***417. Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2021/2022, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 762.64** kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 571.65** ni fedha kutoka katika vyanzo vya ndani ya Mamlaka na **Shilingi bilioni 190.98** ni fedha za nje za mkopo kutoka Benki ya Dunia (International Development Agency - IDA). Fedha hizo zimetengwa ili kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Kuhudumia Shehena ya tani za mapato 15.073 milioni, ikijumuisha tani za shehena ya makasha (TEUs) 148,200 zitakazo hudumiwa na vitengo vya TPA. Aidha, Kitengo cha TICTS kinatarajia kuhudumia makasha (TEUs) 650,500;

ii. Kukamilisha mradi wa uboreshaji wa gati Na. 7 na yadi ya makasha (158,000 m2) iliyopo nyuma ya gati Na. 5 hadi 7 katika Bandari ya Dar es Salaam;
iii. Kuanza kazi za uchimbaji na upanuaji wa lango la kuingilia na kugeuzia meli katika Bandari ya Dar es Salaam;

iv. Kuanza utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Matanki ya kuhifadhia Mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam;

v. Kuendelea na ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala, Ruvu;

vi. Kuanza kazi za ujenzi wa barabara inayounganisha gati jipya katika Bandari ya Mtwara;

vii. Kukamilisha ujenzi wa sakafu ngumu (heavy duty paving- 5,600 m2) kwa ajili kuhudumia Shehena ya korosho na ukarabati wa Ghala Na. 3 katika Bandari ya Mtwara;

viii. Kukamilisha mradi wa kupanua na kuchimba lango la kuingilia na eneo la kugeuzia meli (entrance channel and turning basin) katika Bandari ya Tanga;

ix. Kuendelea na maboresho ya Bandari ya Tanga awamu ya pili ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa gati Na. 1 na Na. 2;

x. Kuendelea na ununuzi wa mitambo na vifaa mbalimbali kwa bandari zote;

xi. Kuendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA na mfumo wa usalama bandarini (Port Integrated Security System - ISS); na

xii. Kuendelea na ukamilishaji wa miradi ya uboreshaji wa Bandari katika Maziwa.

***418. Mheshimiwa Spika*****,** Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) imetenga **Shilingi bilioni 67** kutoka katika vyanzo vyake vya ndani ili kusimamia ubora wa huduma za usafiri wa anga kulingana na viwango vya kimataifa vilivyowekwa na Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (The International Civil Aviation Organization – ICAO). Aidha, TCAA inatoa leseni na kudhibiti utoaji wa huduma za usafiri wa anga; kuweka Viwango katika utoaji wa huduma za usafiri wa anga na kusimamia, kukuza na kuendeleza shughuli za biashara ya usafiri wa anga ndani na nje ya nchi ili wananchi wapate huduma bora na nafuu

zaidi. Katika kufikia malengo hayo, kazi zitakazofanyika ni pamoja na:

i. Kununua mitambo ya kuongozea ndege kwa njia ya mawasiliano ya sauti (VHF AREA COVER Relay Systems) kati ya waongoza ndege na marubani kwa vituo vya Mwanza, JNIA na Mtwara;

ii. Kutoa mafunzo ya Usafiri wa Anga yanayokidhi viwango vya Kimataifa katika sekta ya usafiri wa anga kwa Watanzania na nje ya nchi;

iii. Kuendelea kuboresha Daftari la Usajili wa Ndege (Aircraft Register);

iv. Kusimamia udhibiti wa usalama wa usafiri wa anga (Aviation Security) katika Viwanja vya Ndege, Mashirika ya Ndege pamoja na Watoa Huduma zinazoendana na usafiri wa anga;

v. Kushiriki katika mazungumzo na nchi nyingine duniani kwa ajili ya kuingia na kupitia upya Mikataba ya Usafiri wa Anga;
vi. Kusimamia na kudhibiti ubora wa Viwanja vya Ndege nchini;

vii. Kuhakikisha matukio na ajali zinazotokana na usafiri wa anga zinapungua;

viii. Kuimarisha uwezo wa Tanzania katika kusimamia Sekta na kudhibiti usalama wa anga; na

ix. Kuboresha miundombinu na vifaa vya kuongozea Ndege.

***419. Mheshimiwa Spika*****,** Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetenga **Shilingi bilioni 33.6** kutoka katika vyanzo vyake vya ndani ili kudhibiti huduma za usafiri ardhini katika Sekta ndogo za reli, barabara na waya. Fedha hizo zitatumika kutekeleza miradi ifuatayo:

i. Kuimarisha ushindani na kuhakikisha huduma za usafiri wa ardhini zinaendelea kuwa endelevu;

ii. Kuimarisha ubora wa utoaji huduma za usafiri wa ardhini;

iii. Kuchochea maendeleo ya sekta ya usafiri kwa kushawishi wawekezaji wakubwa katika sekta ya usafiri ardhini;

iv. Kuimarisha usalama wa huduma za usafiri wa reli na barabara;

v. Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa tiketi mtandao

vi. Kuanza utekelezaji wa ujenzi wa Vituo vya Ukaguzi wa lazima wa magari ya biashara.

vii. Kuongeza uwezo wa Mamlaka kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi; na209

vii. Kushirikiana na Wizara katika kuboresha Sheria, Kanuni, Sera na mahusiano ya kitaasisi katika Sekta za Usafiri Ardhini.

***420. Mheshimiwa Spika*****,** Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) limetenga jumla ya **Shilingi bilioni 4.24** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi bilioni 92.58** fedha zinazotokana na makusanyo yake ya ndani ili kusimamia ulinzi na usalama wa vyombo vya majini, usimamizi wa kuzuia uchafuzi wa mazingira majini utokanao na meli, kuendeleza manufaa ya sekta ndogo ya usafiri majini, kudhibiti huduma za Bandari na usafiri majini na kulinda maslahi mapana ya nchi katika usafirishaji wa bidhaa muhimu. Kazi zitakazotekelezwa ili kufikia malengo hayo ni pamoja na:

i. Kusajili, kukagua na kutoa Vyeti vya Ubora kwa Meli/vyombo vya usafiri kwa njia ya maji;

ii. Kusimamia mafunzo, utoaji wa Vyeti na huduma kwa Mabaharia kwa mujibu wa itifaki ya Shirika la Bahari Duniani (IMO), STCW, 78;

iii. Ujenzi wa Vituo vya kuratibu shughuli za Utafutaji na Uokoaji katika Ziwa Victoria;

iv. Ununuzi wa Boti Moja (1) kwa ajili ya *survillance and monitoring*';

v. Kuweka mfumo wa Mawasiliano kwa ajili ya Usalama wa Usafiri katika Ziwa Victoria;

vi. Kutoa leseni kwa watoa huduma zinazodhibitiwa na kusimamia masharti ya leseni hizo;

vii. Kudhibiti gharama, nauli na tozo mbalimbali za usafiri majini kwa kuzingatia Sheria na Kanuni;

viii. Kufanya ukaguzi wa meli za nje zinazokuja katika bandari za Tanzania Bara na meli zilizosajiliwa nchini;

ix. Kuratibu shughuli za utafutaji na uokoaji sambamba na mazoezi ya utafutaji na uokozi;

x. Kuweka mifumo thabiti ya kukabiliana na uchafuzi wa mazingira majini utokanao na meli;

xi. Kuimarisha uratibu wa shughuli za kukabiliana na matukio ya meli kuvujisha / kumwaga mafuta baharini;

xii. Kuhakiki shehena zinazoshushwa au kuingizwa melini kupitia katika bandari nchini.

xiii. Kuimarisha mifumo na kukuza matumizi ya TEHAMA katika kudhibiti huduma za usafiri kwa njia ya maji na ufanyaji biashara ya meli.

xiv. Kushughulikia malalamiko ya watumiaji na watoa huduma katika sekta ndogo ya usafiri wa maji ili kuendeleza maelewano na kukuza tija;

xv. Kusimamia viwango vya huduma na tozo ili kuleta haki kwa pande zote za wadau; na

xvi. Kufuatilia mienendo ya makampuni ya meli kwa nia ya kuzuia mienendo inayoweza kuleta athari hasi kwenye uchumi.

***421. Mheshimiwa Spika*****,** Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 17.9** fedha kutoka katika vyanzo vyake vya ndani kwa ajili ya kuboresha na kuimarisha miundombinu ya reli pamoja na maeneo yote yaliyo ndani ya ukanda wa reli mita 50 pande zote kutoka katikati ya reli. Ili kufikia malengo hayo, fedha hizo zitatumika kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka kutoka lengo la Shilingi bilioni 112.3 mwaka 2020/2021 hadi Shilingi bilioni 115.2 mwaka 2021/2022;

ii. Kusafirisha shehena ya mzigo tani 450,000 na jumla ya abiria 800,000;

iii. Kufanya matengenezo ya miundombinu ya njia kuu ya reli iliyopo;

iv. Kufanya matengenezo ya injini na mabehewa kwa kiwango cha juu, kati na chini.

v. Kufanya matengenezo kwenye mitambo ya Ishara na mawasiliano.

vi. Kufanya matengenezo kwenye Majengo ya Ofisi na Stesheni zilizopo kwenye Reli.

***422. Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2021/2022, Kampuni ya Ubia kati ya Tanzania na China (SINOTASHIP) imetenga **Shilingi bilioni 3** kutoka katika vyanzo vyake ili kuendelea kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo katika masafa marefu kwa njia ya bahari pamoja na kusimamia usalama wa

mabaharia, mizigo na meli. Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya kazi zifuatazo:

i. Kuboresha ukusanyaji wa mapato kutoka Shilingi bilioni 17.5 mwaka 2020/2021 hadi Shilingi bilioni 18.00 mwaka 2021/2022;
ii. Kuendelea kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo kutoka tani 609,000 mwaka 2020/2021 hadi tani 610,000 ifikapo Juni, 2022;

iii. Kuendelea na jitihada za kuongeza mapato nje ya biashara ya msingi (core business) kwa njia ya kushawishi kuongeza idadi ya meli na mizigo itakayoingia katika Bandari nchini kutoka makasha 50,000 mwaka 2020/2021 na kufikia makasha 51,000 mwaka 2021/2022;

iv. Kupunguza gharama za uendeshaji wa kampuni kutoka Shilingi bilioni 12.5 mwaka 2020/21 na kufikia Shilingi bilioni 12.0 mwaka 2021/2022; na

v. Kushirikiana na taasisi za fedha ndani na nje ili kufanikisha kupata mikopo itakayowezesha kununua Meli moja ya mizigo kutegemeana na hali ya soko.

vi. Kuboresha ukusanyaji wa mapato kutoka Shilingi bilioni 17.5 mwaka 2020/21 na kufikia Shilingi bilioni 18.00 mwaka 2021/2022;

vii. Kuendelea kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo kutoka tani 609,000 mwaka 2020/21 na kufikia tani 610,000 ifikapo Juni, 2022;

viii. Kuendelea na jitihada za kuongeza mapato nje ya biashara ya msingi (core business) kwa njia ya kushawishi kuongeza idadi ya meli na mizigo itakayoingia katika bandari nchini kutoka makasha 50,000 mwaka 2020/21 na kufikia makasha 51,000 mwaka 2021/2022;
ix. Kupunguza gharama za uendeshaji wa kampuni kutoka Shilingi bilioni 12.5 mwaka 2020/21 na kufikia Shilingi bilioni 12.0 mwaka 2021/2022; na

x. Kushirikiana na taasisi za fedha ndani na nje ili kufanikisha kupata mikopo itakayowezesha kununua meli moja ya mizigo kutegemeana na hali ya soko.

***423. Mheshimiwa Spika*,** Kampuni ya Kuendeleza Viwanja vya Ndege ya Kilimanjaro (KADCO) imetenga **Shilingi bilioni 1.95** kutoka katika vyanzo vyake ili kuendesha na kuendeleza miundombinu ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA). Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na:

i. Kuboresha huduma za zimamoto kwa kununua vifaa mbalimbali pamoja na kujenga bweni jipya la wanawake wa zimamoto;

ii. Kuboresha miundombinu ya huduma za TEHAMA; na

iii. Kununua na kusimika mfumo mpya na wa kisasa wa kukusanya tozo za maegesho ya magari kiwanjani.

**TAASISI ZA MAFUNZO**

**Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT)**

***424. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi) imeanzisha Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi iliyosajiliwa na NACTE kwa namba ya usajili REG/SAT/035. Taasisi hii imeanzishwa kwa kuunganisha kilichokuwa Chuo cha Ujenzi Morogoro (Morogoro Works Training Institute - MWTI) na Chuo cha Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi (Appropriate Technology Training Institute - ATTI) cha Mbeya vilivyokuwa chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi). Makao Makuu ya Taasisi hii (Main Campus) yapo Morogoro kilipokuwa Chuo cha Ujenzi Morogoro na Tawi la Taasisi hiyo lipo Mbeya kilipokuwa Chuo cha ATTI – Mbeya.

Katika mwaka wa fedha 2021/22, Taasisi imepanga kutekeleza kazi mbalimbali zikiwemo kudahili na kutoa mafunzo kwa wanafunzi **280** wa Stashahada ya Ufundi kwa Mtaala wa NACTE na kuendelea kutoa mafunzo ya *NTA Level*

*5* kwa wanafunzi wa Stashahada waliopo, kutoa mafunzo kwa wanafunzi **900** katika fani za ufundi stadi (Basic Artisans) na mafunzo ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi (Labor Based Technology) pamoja na kufanya tathmini ya mafunzo kwa Wilaya za Tanzania Bara na Visiwani. Aidha, Taasisi imepanga kuendesha kozi tano **(5**) kwa washiriki **100**; kutoa mafunzo katika matumizi ya kompyuta na *software* za kihandisi; kufanya matengenezo ya miundombinu ya maji, majengo na umeme, kufanya ukarabati kwenye majengo ya Taasisi; ujenzi wa majengo mawili ya ofisi za ;kwa ajili ya ICoT Morogoro na Mbeya; ujenzi wa karakana mpya kwa ajili mafunzo kwa vitendo na ujenzi wa maabara kwa ajili ya kufundishia fani za uhandisi ujenzi na TEHAMA.

**Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)**

***425. Mheshimiwa Spika*,** Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimetengewa jumla ya **Shilingi milioni 500** fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali; **Shilingi bilioni 4,776.68** fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia na **Shilingi bilioni 8,854 fedha** kutoka vyanza vya ndani ya Chuo ili kuboresha miundombinu ya Chuo, utoaji wa mafunzo na mazingira ya kufundishia. Fedha hizo zitatumika kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia mafunzo ya taaluma za usafiri wa anga ambapo ununuzi wa Ndege mbili (2) za kufundishia kozi ya urubani utafanyika;

ii. Kujengea uwezo watumishi kupitia ziara za kitaaluma, mafunzo ya muda mrefu na mfupi, mafunzo ya vitendo na kubadilishana wakufunzi na vyuo vya nje ya nchi;

iii. Kutengeneza na kuhuisha mitaala ya mafunzo inayokidhi mahitaji ya soko la Kimataifa kwenye taaluma za uchukuzi na usafirishaji;

iv. Kutoa udhamini kwa wanafunzi wasichana wa Kitanzania kusoma kozi za mafunzo ya taaluma za usafiri wa anga na operesheni za usafirishaji;

v. Kuendelea na Ujenzi wa Kituo cha Rasilimali Mafunzo (Mabibo) - Dar-es-Salaam;

vi. Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya Kituo cha Umahiri katika Taaluma ya Mafunzo ya Anga na Operesheni za Usafirishaji kinachofadhiliwa na Benki ya Dunia;

vii. Kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Kikanda cha Umahiri ya Mafunzo ya Usalama Barabarani chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika;

viii. Kuendelea kuandaa nyaraka mbalimbali za uanzishwaji wa Chuo Kikuu cha Usafirishaji kwa ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China;

ix. Uandaaji wa Matumizi Bora ya Ardhi na ujenzi wa miundombinu katika eneo la Chuo mkoani Lindi kwa ajili ya uanzishwaji wa Mafunzo na Kituo Atamizi cha kuandaa mafundi mahiri wenye ujuzi kwenye sekta ya usafiri wa majini, mafuta na gesi;

x. Ununuzi wa vifaa vya kufundishia mafunzo ya usafiri wa anga na uhandisi;

xi. Kuanza ujenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Usafiri wa Anga kitakachokuwa Katika Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro (KIA);

xii. Kuanza ujenzi wa Majengo mapya matano (5) katika Kampasi ya Mabibo Dar-es- Salaam;

xiii. Kukamilisha upatikanaji wa Ithibati ya kufundisha kozi za Marubani kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA).

### Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)

***426. Mheshimiwa Spika*****,** Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) kimetenga jumla ya **Shilingi billioni 1.0** kutoka Mfuko Mkuu

wa Serikali na **Shilingi bilioni 3.14** fedha zinazotokana na vyanzo vyake vya mapato ili kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuanza ununuzi wa kifaa cha kufundishia (Simulator);

ii. Kujenga majengo mapya ya Chuo yatakayoboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

iii. Kuongeza miundombinu ya kufundishia na kujifunzia;

iv. Kufanya ukarabati wa miundombinu;

v. Kufanya tafiti; na

vi. kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi.

**E. SHUKRANI**

***427. Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwashukuru wananchi na wadau mbalimbali hasa sekta binafsi kwa ushirikiano wao katika kutekeleza malengo ya Sekta zetu. Shukurani za pekee ziwaendee Waheshimiwa wabunge wenzangu kwa michango yao ambayo imechangia katika kuimarisha huduma zitolewazo na Wizara. Naomba waendelee na moyo huo ili tuweze kuendeleza Sekta hii ambayo ni muhimu katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

***428. Mheshimiwa Spika,*** shukurani zangu hazitakuwa kamili bila kuwashukuru Viongozi wenzangu katika Wizara nikianzia na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Mhandisi **Godfrey Msongwe Kasekenya (Mb.)** na Mheshimiwa **Mwita Mwikwabe Waitara (Mb.);** Makatibu Wakuu nikianzia na Mbunifu ß **Elius Asangalwisye Mwakalinga** aliyekuwa Katibu Mkuu (Ujenzi); Bwana **Gabriel Joseph Migire** (Uchukuzi) na Mhandisi **Joseph Kizito Malongo** (Ujenzi). Aidha, nawashukuru Wakuu wa Idara, Viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, Watumishi na Wataalamu wote wa Wizara kwa kujituma katika kusimamia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara. Nawasihi waendelee na juhudi hizo katika kipindi kijacho ili tuweze kutekeleza malengo tuliyojiwekea kwenye sekta zetu.

***429. Mheshimiwa Spika,*** Washirika mbalimbali wa Maendeleo wamechangia katika utekelezaji wa Programu na Mipango mbalimbali ya Wizara. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwatambua Washirika hao wa Maendeleo ambao ni pamoja na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini (IMO), Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO), Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (BADEA), OPEC Fund, Umoja wa Nchi za Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Japan (JICA), Korea Kusini (KOICA), Abu Dhabi Fund, Ujerumani (KfW), Uingereza (DFID), Uholanzi (ORIO), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Kuwait (KFAED), Uturuki, HSBC, TMEA, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za SADC, Nchi za Urusi, Afrika Kusini, Uingereza, Marekani, Uholanzi, Japan, India, China, Denmark, Norway, Ubelgiji, Ujerumani, Taasisi za fedha za CRDB, NSSF, PSSSF na TIB, Asasi zisizokuwa za Kiserikali; Sekta Binafsi pamoja na wengine wengi.

***430. Mheshimiwa Spika,*** mwisho, nakushukuru tena wewe binafsi na Mhe. Naibu Spika. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara (**www.mwt.go.tz**).

## F. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2021/22

***431. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 3,747,294,095,200.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,627,244,274,200.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Ujenzi na **Shilingi 2,120,049,821,000.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Uchukuzi. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:

### SEKTA YA UJENZI (FUNGU 98)

***432. Mheshimiwa Spika,*** **Shilingi 1,627,244,274,200.00** za Fungu 98 (Ujenzi) zinajumuisha **Shilingi 38,540,787,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara (Ujenzi) na Taasisi ambapo **Shilingi 35,186,389,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 3,354,398,000.00** ni za Matumizi Mengineyo. Bajeti ya

Maendeleo ni Shilingi **1,588,703,487,200.00** ambazo zinajumuisha **Shilingi 1,288,703,487,200.00** fedha za ndani na **Shilingi 300,000,000,000.00** fedha za nje. Fedha za ndani zinajumuisha **Shilingi 635,849,127,200.00** za Mfuko wa Barabara na **Shilingi 652,854,360,000.00** za Mfuko Mkuu wa Serikali.

**SEKTA YA UCHUKUZI (FUNGU 62)**

***433. Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Uchukuzi imetengewa jumla ya **Shilingi 2,120,049,821,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, **Shilingi 91,743,411,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 64,672,467,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 27,070,944,000.00** ni za Matumizi Mengineyo. Aidha, Miradi ya Maendeleo imetengewa **Shilingi 2,028,306,410,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,828,306,410,000.00** ni fedha za Ndani na **Shilingi 200,000,000,000.00** ni fedha za Nje.

***434. Mheshimiwa Spika***, pamoja na Hotuba hii, nimeambatanisha Miradi ya Wizara itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2021/22 **(Kiambatisho Na. 1-7)** ikiwa ni pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza Miradi hiyo. Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

**WAZIRI WA ULINZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono tutaendelea na utaratibu wetu nimuite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayoshughulika na hii Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ifuatayo ni taarifa ya kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2021

pamoja na maoni na ushauri kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 142(a) – (c) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Juni 2020, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu zifuatazo; Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi, sehemu hii inabainisha mpangilio wa taarifa iliyowasilishwa; Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi unaojikita katika masuala makubwa mawili yafuatayo: Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2020/2021; Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022; Sehemu ya Tatu inahusu Maoni na Ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2021/2022. Kwa kuzingatia Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua baadhi ya miradi iliyotekelezwa na Sekta hii katika mwaka wa fedha 2020/2021. Kamati ilifanya ziara hii kuanzia tarehe 12 hadi 16 Machi, 2021 katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam. Miradi iliyotembelewa kwa Sekta ya Ujenzi ni; - Ujenzi wa nyumba za Magomeni, Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi yaendayo haraka Awamu ya II (BRT II), Ujenzi wa Daraja la jipya la Selander (Tanzanite) na Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi ambayo ipo Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Miradi ya Sekta ya Uchukuzi iliyotembelewa ni pamoja na Ujenzi wa Reli ya Kisasa kipande cha Dar es Salaam- Morogoro (Km 300) na kipande cha Morogoro- Makutopora (Km422), Ujenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Chuo cha Bahari ya Dar es Salaam (*DMI*) na karakana ya vichwa vya treni iliyopo Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yaliyobainika katika ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo yafuatayo ni mambo saba yaliyobainika katika ziara; Utekelezaji wa miradi ya maendeleo umekuwa na faida nyingi kwa kutoa fursa mbalimbali za ajira kwa wataalamu wa ujenzi, mafundi, wazalishaji, wauzaji na wasambazaji wa vifaa vya ujenzi na hata watoa huduma kama vile mama lishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa nyumba za magomeni kota umerejesha hadhi na kuboresha muonekano wa mazingira hivyo ni muhimu sana Serikali kuhakikisha inaingia mkataba wa utunzaji wa nyumba na madhari ya eneo la mradi pamoja na kuhakikisha ukaguzi unafanyika mara kwa mara ili kuzuia uharibifu unaoweza kujitokeza pindi nyumba za Magomeni Kota zitakapokabidhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji mdogo wa Serikali katika vyuo vya kati jambo linalosababisha vyuo hivyo kuwa katika mazingira magumu na kupoteza mvuto kwa wanafunzi. Kuwepo kwa malalamiko kwa wafanyakazi waliopo katika miradi mbalimbali ya Serikali kuhusiana na stahili mbalimbali. Ni muhimu stahili zote za wafanyakazi zizingatiwe kwa kuhakikisha vyombo mbalimbali vya Serikali kama vile OSHA na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii vinapata na kushughulikia madai hayo ili kuepusha migogoro pindi miradi husika itakapokuwa inakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti na Uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2020/2021.Fungu 98- Sekta ya Ujenzi; Makusanyo ya Mapato kwa mwaka 2020/2021 Fungu 98- Sekta ya Ujenzi

makusanyo yaliyofikiwa hadi mwezi Februari 2021 ni asilimia 46.35.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo fedha za Matumizi ya Kawaida zimetolewa asilimia 54 hadi kufika mwezi Februari, 2021 kama uchambuzi wa Kamati kwenye jedwali unavyoonesha. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo sekta ya ujenzi 2020/2021 ni shilingi Trilioni 1,577,586,784,000.00. Hadi mwezi Februari 2021 zimetolewa asilimia 49 ambazo ni shilingi Bilioni 772,331,190,151.92.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini hali ya utolewaji wa fedha za ndani za miradi ya maendeleo kwa sekta ya ujenzi si ya kuridhisha hasa fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambao hadi Februari, 2021 zimetolewa shilingi bilioni 138,655,097,992.32 sawa na asilimia 32% tu ya fedha zilizokuwa zimeidhinishwa, wakati huo fedha za Mfuko wa Barabara zimetolewa Shilingi Bilioni 403,184,932,487.02 sawa na asilimia 62.83.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi hadi Februari 2021 utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara, ujenzi wa barabara kuu unatekelezwa kwa asilimia 84, ukarabati barabara kuu asilimia 6 na Barabara za Mikoa asilimia 17 kama ilivyooneshwa katika jedwali Na.03.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini changamoto katika utekelezaji wa shughuli za ujenzi na ukarabati wa barabara ni ucheleweshaji wa kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani *-VAT. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa ujenzi wa Viwanja vya Ndege, Katika mwaka wa fedha 2020/21, Kamati imebaini miradi hii inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti na kutokutolewa fedha kwa wakati kwani kati ya fedha zilizoidhinishwa mwaka 2020/21 zimetolewa asilimia 19 tu ambapo fedha za ndani zimetolewa asilimia 21 na fedha za nje asilimia 25.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 62 - Sekta ya Uchukuzi; katika upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo; fedha za matumizi ya kawaida zimetolewa asilimia 65 hadi kufika mwezi Februari, 2021 kama uchambuzi wa Kamati unavyoonyesha katika jedwali Na. 4.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 fedha za miradi ya maendeleo ziliidhinishwa shilingi 3,062,148,630,000/= ambapo hadi kufika mwezi Februari, 2021, zimetolewa shilingi 993,685,730,000/= sawa na asilimia 32 ya fedha zote zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Sekta ya Uchukuzi siyo wa kuridhisha na umeathiri utekelezaji wa miradi. Mfano, miradi ambayo imepata fedha kwa kiasi kidogo na mingine bila kupatikana ni Chuo cha *NIT* hakikupata fedha ya haina yoyote. Ununuzi wa rada, vifaa vya miundombinu ya hali ya hewa ni asilimia tatu na ununuzi wa meli mpya na ukarabati katika Maziwa Makuu ni asilimia nne tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingine iliyosalia yote imepata fedha chini ya asilimia 45. Miradi hii ya ununuzi na ukarabati wa meli za maziwa, *MSCL* asilimia 10; ununuzi wa ndege mpya, *ATCL* asilimia 10; ujenzi wa reli ya SGR asilimia 33; na uendeshaji wa jengo la tatu la abiria *(JNIA)* asilimia 43.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati. Wakati wa kuchambua na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali. Maoni na ushauri huo uligusa masuala muhimu kama vile bandari, reli, viwanja vya ndege na barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kati ya mambo yaliyoshauriwa, yapo

ambayo Serikali imeyazingatia na mengine yanaendelea kuzingatiwa kama yalivyofafanuliwa katika kipengele hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Sekta ya Ujenzi - Fungu 98 inatarajia kukusanya mapato ya jumla ya shilingi milioni 70 kutoka Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, Huduma za Ufundi na Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Sekta ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa shilingi 1,617,244,274,200. Kati ya fedha hizo shilingi 38,540,787,000 bajeti ya Matumizi ya Kawaida ambayo shilingi 35,186,389,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake na shilingi 3,354,398,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Fedha za miradi ya maendeleo ni shilingi 1,578,703,487,200.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha za ndani zilizotengwa, shilingi 635,849,127,200 ni fedha za Mfuko wa Barabara ambazo ni sawa na asilimia 50 ya fedha zote za ndani zilizotengwa. Uchambuzi wa Kamati umebaini, makadirio ya fedha za miradi ya maendeleo kwa sekta ya ujenzi mwaka wa fedha 2021/2022, kumekuwa na ongezeko la shilingi 1,116,703,000/= sawa na ongezeko la asilimia 0.07. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo za ndani zimeongezeka kiasi cha shilingi 26,480,897,200/=. Kwa upande wa fedha za nje zilizokadiriwa kutolewa mwaka 2021/2022 zimepungua kiasi cha shilingi 25,364,194,000/= ukilinganisha na fedha za nje zilizoidhinishwa mwaka wa fedha unaoishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uchukuzi - Fungu 62 katika mwaka wa fedha 2021/2022 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 2,393,816,049,584/=. Kati ya fedha hizo, shilingi 89,268,639,584/= zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Fedha za miradi ya maendeleo zilizotengwa kwa ajili ya Sekta ya Uchukuzi ni shilingi 2,304,547,410,000/= ambapo kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 2.1 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 200 ni fedha za nje kutoka Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika *ADB.*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini fedha za ndani zinazoombwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ni pungufu ya fedha zilizoidhinishwa mwaka wa fedha unaoisha 2020/2021. Upungufu huu ni shilingi 633,131,510,000/= sawa na upungufu wa asilimia 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa Serikali ilitoa maelezo kuwa upungufu huu hautaathiri utekelezaji wa miradi, bado Kamati ina hofu kuhusu kuathirika kwa miradi inayoendelea katika sekta hii kwa mwaka huu wa fedha kutokana na upungufu wa fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa fedha za nje zinazoombwa kuidhinishwa mwaka fedha 2021/2022 zimeongezeka kiasi cha shilingi 75,530,290,000/= sawa na ongezeko la asilimia 61.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifuatayo ni sehemu ya maoni na ushauri wa Kamati. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi. Sekta hizi ni sekta nyeti na muhimu kwa maendeleo ya nchi kwani zinachochea kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi wa nchi na kuleta maendeleo kwa Taifa. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 fedha zinazoombwa kuidhinishwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ni jumla ya shilingi 4,011,060,323,784/= kiasi ambacho ni 4% ya fedha za Bajeti Kuu zilizotengwa kwa mwaka 2021/2022 ambazo ni shilingi 36,258,806,000,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inazidi kusisitiza ushauri wake kuwa fedha zinazoidhinishwa na Bunge lako Tukufu zitolewe kwa wakati ili kuhakikisha miradi inatekelezwa katika muda uliopangwa na hatimaye wananchi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sekta ya uchukuzi; moja, kuhusu ujenzi wa reli nchini, Kamati inaendelea kusisitiza ushauri wake kuwa ujenzi wa reli ya kisasa ya kati, uende sambamba na ununuzi wa vichwa na mabehewa ya treni ili

mradi utakapokamilika mnamo mwezi Agosti, 2021 kwa sehemu ya Dar es Salaam hadi Morogoro huduma za usafirishaji zianze kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kutoa kipaumbele cha ajira kwa vijana wa Kitanzania wanaofanya kazi ya kufufua mabehewa ya treni na vichwa vya treni, lakini wakiwa na elimu ya Darasa la Saba katika Karakana ya Morogoro, kwani wamepata uzoefu ambao utaendelea kusaidia nchi yetu hasa wakati huu ambapo miundombinu ya reli na usafiri wa treni unapewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuzingatia kuwaajiri wahandisi wa ndani wa kutosha wenye fani mbalimbali muhimu na zinazohitajika kwa uendeshaji wa reli pamoja na kutoa mafunzo mbalimbali ya uendeshaji wa treni na uratibu wa matumizi ya reli mpya ili mradi utakapokamilika pawepo na wataalam wa ndani ambao watakuwa tayari kuupokea na kuusimamia vizuri; vifaa vinavyotumika katika mradi wa *SGR* vibaki nchini pindi mradi utakapomalizika ili viendelee kufanya kazi katika miradi mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine Serikali kuendelea kutafuta wawekezaji ambao watakodisha njia ya reli na kupitisha treni zao kusafirisha mizigo na abiria ili kuongeza mapato yatakayotokana na reli hii; ili kuepusha uvamizi wa maeneo ya reli na kuondoa usumbufu kwa wananchi, Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* liweke alama zinazoonyesha mwisho wa eneo la reli ili kuondoa usumbufu kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Reli lianze kujiendesha kisasa kwa kufunga vyombo vya kielektroniki ili kuweza kutunza kumbukumbu zote za kiutendaji, ufuatiliaji wa mizigo kwa wateja, udhibiti wa mafuta, udhibiti wa mwendo na usalama. Hii italifanya shirika hili kuweza kujiendesha kisasa na kupunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bandari, Kamati inashauri yafuatayo: Serikali kwa kupitia Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Viwanda na Biashara, iitishe kikao cha pamoja na wadau mbalimbali wa bandari nchini ili kubadilishana mawazo na kuona namna nzuri ya uendeshaji wa bandari ili kuifanya bandari iweze kujiendesha kibiashara na kuvutia wafanyabiashara wengi kuitumia, jambo ambalo litaongeza mapato ya Serikali. Sambamba na hilo, ufanyike utafiti wa kina wa masoko ili kubaini sababu zinazopelekea idadi ya wateja kuhamia bandari nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa *TANCIS* wa Malipo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania uangaliwe ili uweze kwenda sambamba na uhalisia kwani mfumo huu umekuwa moja kati ya mambo yanayochangia kuchelewesha huduma bandarini na hivyo kuwa kikwazo kwa bandari na hata kwa wateja. Pia Serikali iangalie upya utendaji kazi wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania *(TASAC)* kwani kumekuwa na malalamiko ya wateja wa bandari kuhusu kuwa na mlolongo mrefu wa kuidhinisha tozo na kusababisha ucheleweshaji, viwango vya tozo na mipaka ya utekelezaji wa majukumu ya *TASAC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iharakishe kukamilisha bandari za nchi kavu katika maeneo ya Kwala - Pwani, Ihumwa - Dodoma, Fela - Mwanza, Katosho - Kigoma, King'ori - Arusha, Isaka – Kahama; na Inyala - Mbeya ili kupunguza gharama kwa wateja kusafiri mpaka Dar es Salaam kwa ajili ya kutoa mizigo. Sulala la wadau wote wa bandari kuhamia kwenye jengo moja liwe jambo la lazima na la haraka ili kurahisisha na kuongeza ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilifanikiwa kufunga *flow meter* katika Bandari ya Dar es Salaam kwa ajili ya upimaji wa mafuta yanayoingia nchini; na kwa kuwa *flow meter* hii kwa sasa ipo katika kipindi cha uangalizi, ni muhimu sana kutafuta mtaalam aliyebobea katika mitambo ya aina hii ili apime ufanisi wa utendaji kazi wa *flow meter* hii. Aidha, baada ya kipindi cha majaribio kwisha, kuhakikisha mfumo

wake unabadilishwa na kuwa wetu kwa ajili ya kujihakikishia usalama. Ni muhimu kujiridhisha ikiwa mfumo huo ambao kwa sasa upo katika majaribio kama unafanya vipimo sahihi. Aidha, Serikali iendelee na jitihada za kutengeneza *flow meter* nyingine mbili za Bandari ya Tanga na Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TAZARA*, Kamati inashauri yafuatayo: Serikali iharakishe mazungumzo baina ya nchi wabia wa reli ya *TAZARA* kuhusu kuimarisha reli hii kutokana na umuhimu wake katika kukuza uchumi; Serikali ikamilishe manunuzi ya injini na vipuri pamoja na mitambo ya kusaidia kuzalisha kokoto na mataruma ya zege kwenye mgodi wa kokoto uliopo Kongolo - Mbeya na kusaidia viweze kuingia nchini kwa haraka ili vianze kutumika kwa ajili ya kuongeza mapato ya *TAZARA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iharakishe mchakato wa ajira za watumishi wa *TAZARA* ili kupata wafanyakazi wenye ujuzi na weledi wa kutosha kuliongezea Shirika hili uwezo kwani wafanyakazi wengi wamemaliza muda wao na wengi wamestaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA):* Serikali kuongeza wigo katika Bajeti ili kuiwezesha *TAA* kutekeleza majukumu yake ya kusimamia, kuendesha na kuendeleza viwanja vya ndege na hatimaye kutoa huduma bora. Huu ndiyo msingi wa Kamati kuwa inasisitiza mamlaka hii iachiwe angalau asilimia 40 ya maduhuli yatokanayo na viwanja vya ndege ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kulichukuwa deni la malipo ya awali *advance payment* ya ujenzi wa jengo la III la abiria katika Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere ambapo *TAA* imekuwa ikilipa kiasi cha Dola za Kimarekani 592,717 kila mwezi. Deni lililosalia hadi mwezi Januari, 2021 lilikuwa Dola za Kimarekani 22,943,910. *TAA* itaendelea kulipa deni hilo kila mwezi na linakadiriwa litaisha mwezi Novemba. Hivyo tunaiomba Serikali ilichukuwe deni hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL): ATCL* iangaliwe kama Kampuni ya kibiashara na siyo kutoa huduma; Kuwepo na mikakati ya Kitaifa ya kuhakikisha kuwa *ATCL* inakuwa na uwezo wa kushindana na kutengeneza faida; Serikali iyachukuwe madeni yote ya nyuma *ATCL* ambayo kwa kiasi kikubwa yanachangia kuharibu mizania ya hesabu za *ATCL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, shirika liendelee kufanya utaratibu wa kuongeza safari za ndani na za kikanda ili kuimarisha mtandao wa safari zake. Kamati inatambua changamoto ya mlipuko wa ugonjwa wa Corona ambao umesababisha mdororo hasa soko la usafiri wa anga duniani. Hata hivyo, ni muhimu kuendelea na mikakati hii ili hali itakapotulia Shirika liweze kufanya kazi vizuri. Wafanyakazi wa Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL)* kupewa mafunzo ya kudumu ili kuweza kutoa huduma nzuri wakati wote. Hii itasaidia Kampuni kushindana na makampuni mengine yanayofanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Ujenzi; kuhusu Wakala wa Barabara- *TANROADS*, Kamati inaendelea kusisitiza ushauri ufuafuatao: Serikali itekeleze Sera yake ya kuunganisha mikoa yote kwa barabara za lami. Baadhi ya Mikoa hiyo ni Lindi – Morogoro, Morogoro - Mlimba - Madeke – Njombe – Mbeya -Makongorosi – Chunya – Tabora – Katavi, Tabora – Mbeya, Makete - Njombe, Kigoma - Kagera, Lindi – Ruvuma, Arusha – Mara. Aidha, miradi ya barabara inayoendelea ipewe kipaumbele na ile ambayo haijaanza ifanyiwe upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ijenge kwa kiwango cha lami barabara muhimu zifuatazo: Barabara zinazounganisha nchi yetu na nchi nyigine hususan Mikoa ya Kigoma - Kagera, Rukwa - Katavi, Ruvuma - Mtwara; Barabara zinazounganisha Makao Makuu ya Mikoa kama vile Kigoma – Kasulu, Kagera - Katavi – Kigoma – Tabora; Barabara za kiuchumi kama vile za Mtwara – Newala – Masasi, ambayo ni barabara inayopita katika maeneo ambayo yanazalisha korosho kwa wingi ukizingatia kwamba zao la korosho

linachangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa mikoa ya kusini na nchi kwa ujumla; Barabara ya Handeni – Kibrashi – Kibaya – Singida ambayo ni barabara yenye tija kiuchumi kutokana na kuwepo kwa bomba la mafuta linalounganishwa na nchi ya Uganda; na barabara nyingine ni ya Bukoba – Karagwe - Kyerwa ambayo inapita katika maeneo yanayozalisha kahawa kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zinazounganisha Wilaya na Makao Makuu ya Mikoa, hizi pia zipewe kipaumbele ili kuwezesha wakulima kuweza kuyafikia masoko ya mazao yao. Barabara zilizohaidiwa na viongozi wakubwa wa nchi waliopo madarakani na waliostaafu nazo zipewe kipaumbele. Madai ya Wakandarasi yazingatiwe kwa kulipwa kwa wakati ili kuepusha hasara zinazoweza kutokea endapo fedha hizo zitachelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanyika katika sekta ya ujenzi nchini, ni muhimu sana Serikali kuhakikisha inaajiri Wahandisi wa kutosha ili waweze kusimamia miradi kwa ufanisi, tofauti na ilivyo sasa, idadi ya Wahandisi Wizarani haindani na miradi iliyopo, hivyo ufanisi kuwa mdogo. Serikali kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi na Bodi ya Usajili wa Wakandarasi kuendelea kutoa mafunzo kwa Wahandisi Washauri na Wakandarasi wa ndani ili waweze kusimamia na kutekeleza ujenzi wa barabara kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya ujenzi isimamie ipasavyo Sheria ya Barabara kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa kutumia vyombo vya habari, kama runinga, magazeti, na kadhalika; Serikali iendelee na juhudi kufunga mizani ya kisasa zinazopima magari huku yakiwa kwenye mwendo kasi katika vituo ambavyo vina msongamano mkubwa wa magari kwenye mizani ili kuokoa muda, fedha na usumbufu kwa wasafiri na wasafirishaji; Serikali iongeze kasi ya ujenzi wa vituo vya pamoja vya ukaguzi ambavyo vinajengwa katika Ukanda wa Kati na Ukanda wa Dar es Salaam. Wakati wa ujenzi wa barabara ni vyema Wakala wa Barabara wahakikishe wanaweka sehemu maalum kwa ajili ya kuvukia mifugo kwa

ajili ya kuepusha ajali na vifo vya wanyama na pia kuzuia uharibifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa viwanja vya ndege, Kamati inashauri yafuatayo: Serikali ikamilishe kwa haraka ujenzi unaoendelea wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza hasa ujenzi wa jengo la abiria; Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya ndege ili miradi hii iweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wakala wa Ufundi *(TEMESA)*, Wakala uendelee kukamilisha mchakato wa kuchagua karakana za kutengeneza magari ya Serikali kwenye Wilaya ili kuondoa usumbufu wa magari ya Serikali kusafiri umbali mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wakala wa Nyumba *(TBA),* Kamati inaishauri Serikali, Wakala uchukue hatua za makusudi na kuweka mkakati wa kudumu ili kukusanya madeni ya kiasi cha shilingi bilioni 17 ambazo kwa kiasi kikubwa Wakala unazidai Wizara, Idara pamoja na Taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TBA* imekuwa ikinyanyaswa na Taasisi za Serikali. Mara nyingi Wizara nyingine hazilipi fedha kwa *TBA.* Tunaomba Serikali iliangalie haraka; kuhakikisha kuwa inaingia mkataba wa utunzaji wa nyumba na mandhari ya eneo la mradi pamoja na kuhakikisha ukaguzi unafanyika mara kwa mara ili kuzuia uharibifu unaoweza kujitokeza pindi nyumba hizo zitakapohamiwa eneo lile la Magomeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa jumla; fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo zitolewe kwa wakati ili kuharakisha utekelezaji wa miradi na kuleta maendeleo. Serikali ichukue hatua za makusudi kuweka mikakati ya kudumu ili kulipa madeni ambayo kwa kiasi kikubwa Mashirika, Taasisi na Wakala inazidai Taasisi, Mashirika na Wakala nyingine za Serikali. Serikali iangalie umuhimu kuacha fedha angalau asilimia 40

ya maduhuli kwa Mashirika, Taasisi zake ili yaweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuchukua hatua za haraka kuajiri Watumishi kwenye Taasisi mbalimbali hasa zinazokuwa na upungufu mkubwa; Umuhimu wa vyuo vya kati kuboreshwa; Kamati imekuwa ikihimiza siku zote Serikali kuhakikisha inakuwa na wataalam wa kutosha katika sekta ya ujenzi katika ngazi za chini na ngazi za juu. Hii itakuwa kwa Taifa letu imejikita katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali na uanzishwaji wa viwanda.

Hivyo basi, Serikali haina budi kujikita kuwekeza vya kutosha katika vyuo vya ufundi ili kuweza kupata mafundi wa kutosha ambao watasaidia mwendelezo wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iendelee kuongeza ushirikishwaji na mafundi mainjinia wa ndani katika ujenzi wa miundombinu. Utaratibu wa *GN* uangaliwe kwani umebainika kuwa ni moja ya changamoto ya ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi. Ucheleweshaji huu unaotokea sababu ya kuchelewa kupata *GN* kwa ajili ya msamaha wa kodi ni muhimu sana sheria hii iangaliwe upya kwa ajili ya msamaha wa kodi. Ni muhimu sana sheria hii iangaliwe upya hasa kwa kazi ambazo haziwezi kusubiri *GN* ikiwa ni pamoja na kazi za dharura na matengenezo ya kawaida, fidia zitolewe kwa wananchi wanapopisha ujenzi na upanuzi wa miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi ni muhimu sana katika kuchochea maendeleo ya nchi. Miradi iliyo ndani ya sekta hii, ni mikubwa na inahitaji fedha nyingi ili yote iweze kukamilika kwa wakati uliopangwa. Hivyo, kamati inaona ni muhimu Serikali kushirikisha sekta binafsi katika kutelekeza miradi hii mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati walioshiriki kuandaa ripoti hii. Napenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha

maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Kwa namna ya pekee naomba niwashukuru Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa *Engineer* Dkt. Leonard Chamuriho akisaidiwa na Naibu Mawaziri; Mheshimiwa *Engineer* Msongwe Godfrey Kasekenya na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara hii *Engineer* Joseph K. Malongo, Sekta ya Ujenzi na ndugu Gabriel Joseph Migire, Sekta ya Uchukuzi. Kamati pia inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa ushirikiano walioipa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumshukuru aliyekuwa Katibu wa Bunge ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha kamati hii wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Nimpongeze pia ndugu Nenelwa Mwihambi kwa kuteuliwa kuwa Katibu wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, shukrani maalum ziende kwa Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, Ndugu Athumani Hussein; Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Gerald Singano Magiri; pamoja na Makatibu wa Kamati Ndugu Hosiana John Mvuta na Ndugu Janet Juliani Malangu; Msaidizi wa Kamati Ndugu Grace Samweli; pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wote waliyoiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2021 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

# TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021; PAMOJA NA MAONI NA USHAURI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

---

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2020/ 2021; pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia Kanuni ya 142 (a) – (c) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Juni 2020, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi, sehemu hii inabainisha mpangilio wa taarifa inayowasilishwa;

b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi unaojikita katika masuala makubwa mawili yafuatayo: -

i) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2020/2021;

ii) Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

c) Sehemu ya Tatu inahusu Maoni na Ushauri wa Kamati.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

### 2.1 Ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua baadhi ya miradi iliyotekelezwa na Sekta hizi katika mwaka wa fedha 2020/2021. Kamati ilifanya ziara hii kuanzia tarehe 12 hadi 16 Machi, 2021 katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam. Miradi iliyotembelewa kwa Sekta ya Ujenzi ni; - Ujenzi wa nyumba za Magomeni, Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi yaendayo haraka Awamu ya II (BRT II), Ujenzi wa Daraja la jipya la Selander (Tanzanite) na Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi *(Institute of Construction Technology – ICoT)* Morogoro.

Aidha, Miradi ya Sekta ya Uchukuzi iliyotembelewa ni pamoja na Ujenzi wa Reli ya Kisasa kipande cha Dar es Salaam-Morogoro (Km 300) na kipande cha Morogoro- Makutopora (Km422)**,** Ujenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) na karakana ya vichwa vya treni Morogoro.

#### *2.2.1 Mambo yaliyobainika katika Ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo*

**Mheshimiwa Spika**, yafuatayo ni mambo saba yaliyobainika katika ziara:-

a) Utekelezaji wa miradi ya maendeleo umekuwa na faida nyingi kwa kutoa fursa mbalimbali za ajira kwa wataalamu wa ujenzi, mafundi, wazalishaji, wauzaji na wasambazaji wa vifaa vya ujenzi na hata watoa huduma kama vile mama lishe;

b) Wanafunzi wa fani ya ujenzi kutoka vyuo mbalimbali kupata mafunzo ya vitendo *(field work)* katika kipindi cha utekelezaji wa mradi;

c) Vifaa vingi vya ujenzi vimetumika kutoka viwanda vya ndani na baadhi ya vifaa vimenunuliwa toka nje ya nchi ambapo kodi mbalimbali zimelipwa Serikalini na hivyo Pato la Taifa kuongezeka; na

d) Ujenzi wa nyumba za magomeni kota umerejesha hadhi na kuboresha muonekano wa mazingira hivyo ni muhimu sana Serikali kuhakikisha inaingia mkataba wa utunzaji wa nyumba na mandhari ya eneo la mradi pamoja na kuhakikisha ukaguzi unafanyika mara kwa mara ili kuzuia uharibifu unaoweza kujitokeza pindi nyumba za Magomeni Kota zitakapohamiwa;

e) Kuchelewa kwa ujenzi (BRT II) kutokana na kusimama kwa ujenzi wa vituo vya mabasi na madaraja ya juu kutokana mabadiliko ya usanifu, na madhaifu ya ubora wa kazi vilisababisha Mkandarasi kuagizwa kubomoa sehemu zote zenye kasoro na kujenga upya hivyo mradi kuwa nyuma ukilinganisha na hatua iliyopaswa kufikiwa;

f) Uwekezaji mdogo wa Serikali katika vyuo vya kati jambo linalosababisha vyuo hivyo kuwa katika mazingira magumu na kupoteza mvuto kwa wanafunzi;

g) Kuwepo na malalamiko kwa wafanyakazi waliopo katika miradi mbalimbali ya Serikali kuhusiana na stahili mbalimbali. Ni muhimu stahili zote za wafanyakazi zizingatiwe kwa kuhakikisha vyombo mbalimbali vya Serikali kama vile OSHA na Mifiko ya Hifadhi ya Jamii vinapita na kushughulikia madai hayo ili kuepusha migogoro pindi miradi husika itakapokamilika; na

### *2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti na Uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021*

#### *2.2.1 Fungu 98 - Sekta ya Ujenzi*

#### *a) Makusanyo ya Mapato kwa Mwaka 2020/2021*

**Mheshimiwa Spika**, fungu 98- Sekta ya Ujenzi makusanyo yaliyofikiwa hadi mwezi Februari 2021 ni **asilimia 46.35**

#### *b) Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo*

**Mheshimiwa Spika**, fedha za Matumizi ya Kawaida zimetolewa **asilimia 54** hadi kufika mwezi Februari, 2021 kama uchambuzi wa Kamati kwenye jedwali unavyoonesha.

**Mheshimiwa Spika,** fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo sekta ya ujenzi 2020/21 ni **Shilingi Trilioni 1,577,586,784,000.00.** Hadi mwezi Februari 2021 zimetolewa **asilimia 49** ambazo ni **Shilingi Bilioni 772,331,190,151.92**.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini hali ya utolewaji wa fedha za ndani za miradi ya maendeleo kwa sekta ya ujenzi si yakuridhisha hasa fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambao hadi Februari, 2021 zimetolewa **Shilingi Bilioni 138,655,097,992.32** sawa na **asilimia 32%** tu ya fedha zilizokuwa zimeidhinishwa, wakati huo fedha za Mfuko wa Barabara zimetolewa **Shilingi Bilioni 403,184,932,487.02** sawa na **asilimia 62.83.**

#### *c) Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi hadi Februari 2021*

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara, ujenzi wa barabara kuu umetekelezwa kwa **asilimia 84,** ukarabati barabara kuu **asilimia 6** na Barabara za Mikoa **asilimia 17** kama inavyooneshwa katika jedwali Na.03.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini changamoto katika utekelezaji wa shughuli za ujenzi na ukarabati wa barabara ni ucheleweshaji wa kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (*Value Added Tax-VAT*).

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu utekelezaji wa ujenzi wa Viwanja vya Ndege, Katika mwaka wa fedha 2020/21, Kamati imebaini miradi hii inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti na kutokutolewa fedha kwa wakati kwani kati ya fedha zilizoidhinishwa mwaka 2020/21 zimetolewa **asilimia 19** tu ambapo fedha za ndani zimetolewa **asilimia 21** na fedha za nje **asilimia 25.**

### *2.2.2 Fungu 62 - Sekta ya Uchukuzi*

#### a) Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, fedha za Matumizi ya Kawaida zimetolewa **asilimia 65** hadi kufika mwezi Februari, 2021 kama uchambuzi wa Kamati kwenye unavyoonesha katika jedwali namba 04.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21 fedha za miradi ya maendeleo ziliidhinishwa **Shilingi Trilioni 3,062,148,630,000.00)** ambapo hadi kufika mwezi Februari 2021, zimetolewa **Shilingi Bilioni 993,685,730,000.00**) sawa na **asilimia 32** ya fedha zote zilizoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Sekta ya Uchukuzi si wakuridhisha na umeathiri utekelezaji wa miradi. Mfano; Miradi ambayo imepata fedha kwa kiasi kidogo ni Maendeleo ya Miundombinu na Vifaa vya Mafunzo-NIT haukupata fedha yeyote, Ununuzi wa Rada, Vifaa vya Miundombinu ya Hali ya Hewa (3%) na Ununuzi wa Meli Mpya na Ukarabati katika Maziwa Makuu asilimia (4%).

**Mheshimiwa Spika**, miradi mingine iliyosalia yote imepata fedha chini ya asilimia arobaini na tano. Miradi hiyo ni Ununuzi

na ukarabati wa Meli za Maziwa-MSCL (10%), Ununuzi wa Ndege Mpya ATCL (10%), Ujenzi wa Reli ya –SGR (33%), uendeshaji wa Jengo la Tatu la Abiria-JNIA (43%).

### 2.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua na kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2020/21, Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali. Maoni na ushauri huo uligusa masuala muhimu kama vile Bandari, Reli, Viwanja vya Ndege na Barabara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kati ya mambo yaliyoshauriwa, yapo ambayo Serikali imeyazingatia na mengine yanaendelea kuzingatiwa kama yalivyofafanuliwa katika kipengele hiki.

### 2.4 Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

#### 2.4.1 Sekta ya Ujenzi-Fungu 98

**a) Makisio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Sekta ya Ujenzi (fungu 98) inatarajia kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi Milioni 70,000,000.00** kutoka Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, Huduma za Ufundi na Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi.

**b) Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022, Sekta ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa **Shilingi Trilioni 1,617,244,274,200.00.** Kati ya Fedha hizo **Shilingi Bilioni 38,540,787,000.00** bajeti ya Matumizi ya Mawaida ambayo **Shilingi 35,186,389,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake na **Shilingi 3,354,398,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Fedha za miradi ya Maendeleo ni **Shilingi Trilioni 1,578,703,487,200.00.**

**Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha za ndani zilizotengwa **Shilingi Bilioni 635,849,127,200.00** ni fedha za Mfuko wa barabara ambazo ni sawa na **asilimia 50** ya fedha zote za ndani zilizotengwa.

Uchambuzi wa Kamati umebaini, makadirio ya fedha za Miradi ya Maendeleo kwa sekta ya Ujenzi mwaka wa fedha 2021/2022, kumekuwa na ongezeko la **Shilingi Bilioni 1 (1,116,703,000.00)** sawa na ongezeko la **asilimia 0.07.** Aidha, fedha za miradi ya maendeleo za ndani zimeongezeka kiasi cha **Shilingi 26,480,897,200.00**.

Kwa upande wa fedha za nje zilizo kadiriwa kutolewa mwaka 2021/2022 zimepungua kiasi cha **Shilingi 25,364,194,000.00** ukilinganisha na fedha za nje zilizoidhinishwa mwaka wa fedha unaoishia.

### 2.4.2 Sekta ya Uchukuzi-Fungu 62

#### a) Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022 sekta ya Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi Trilioni 2,393,816,049,584.00).** Kati ya fedha hizo **Shilingi Biloni 89,268,639,584** zimetengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida**.**

Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotengwa kwa ajili ya Sekta ya Uchukuzi ni **Shilingi Trilioni 2,304,547,410,000.00** ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi Trilioni 2.1 (2,104,547,410,000.00)** ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni 200 (200,000,000,000.00)** ni fedha za nje kutoka Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini fedha za ndani zinazoombwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka mpya wa fedha 2021/2022 ni

pungufu ya fedha zilizoidhinishwa mwaka wa fedha unaoisha 2020/2022. Upungufu huu ni wa **Shilingi Bilioni 633,131,510,000.00** sawa na upungufu wa **asilimia 21**.

**Mheshimiwa Spika**, japokuwa Serikali ilitoa maelezo kuwa upungufu huu hautoathiri utekelezaji wa miradi, bado Kamati inahofu kuhusu kuathirika kwa miradi inayoendelea katika Sekta hii kwa mwaka huu wa fedha kutokana na upungufu wa fedha za Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za nje zinazoombwa kuidhinishwa mwaka fedha 2021/22 zimeongezeka kiasi cha **Shilingi 75,530,290,000.00** sawa na ongezeko la **asilimia 61**.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi. Sekta hizi ni sekta nyeti na muhimu kwa maendeleo ya nchi kwani zinachochea kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi wa nchi na kuleta maendeleo kwa Taifa. Kwa mwaka wa fedha 2021/22 fedha zinazoombwa kuidhinishwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ni juml ya **Shilingi Trilioni 4,011,060,323,784.00** kiasi ambacho ni **asilimia 4** ya fedha za Bajeti kuu zilizotengwa kwa mwaka 2021/22 ambazo ni **Shilingi Trilioni 36,258,806**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inazidi kusisitiza ushauri wake kuwa fedha zinazoidhinishwa na Bunge lako Tukufu zitolewe kwa wakati ili kuhakikisha miradi inatekelezwa katika muda uliopangwa na hatimae wananchi waweze kunufaika.

### 3.2 Sekta ya Uchukuzi

1. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu ujenzi wa reli nchini Kamati inaendelea kusisitiza ushauri wake kuwa;

a) Ujenzi wa reli ya Kisasa ya kati, uende sambamba na ununuzi wa vichwa na mabehewa ya treni, ili mradi utakapokamilika mnamo mwezi Agosti, 2021 kwa sehemu ya Dar es Salaam hadi Morogoro huduma za usafirishaji zianze kufanyika;

b) Serikali ichukuwe hatua za haraka kusuluisha mgogoro wa umiliki eneo katika stesheni ya SGR Morogoro. Mgogoro huu ni kati ya Halmashauri ya mji wa Morogoro, Magereza na Wananchi jambo ambalo linakwamisha ujenzi wa vyoo vya stesheni na kituo cha mabasi madogo yatakayopokea abiria watakaosafiri na treni ya mwendokasi;

c) Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kutoa kipaumbele cha ajira kwa vijana wa Kitanzania wanofanya kazi ya kufufua Mabehewa ya treni lakini wakiwa na elimu ya darasa la saba katika Karakana ya Morogoro kwani wamepata uzoefu ambao utaendelea kusaidia nchi yetu hasa wakati huu ambapo miundombinu ya reli na usafiri wa treni unapewa kipaumbele;

d) Serikali kuzingatia kuwaajiri wahandisi wakutosha wa ndani wenye fani mbalimbali muhimu na zinazohitajika kwa uendeshaji wa reli pamoja na kutoa mafunzo mbalimbali ya uendeshaji wa treni na uratibu wa matumizi ya reli mpya ili mradi utakapokamilika pawepo na wataalam wa ndani ambao watakuwa tayari kuupokea na kuusimamia vizuri;

e) Vifaa vinavyotumika katika mradi wa SGR vibaki nchini pindi mradi utakapomalizika ili viendelee kufanya kazi katika miradi mingine;

f) Serikali kuendelea kutafuta wawekezaji ambao watakodisha njia ya reli na kupitisha treni zao kusafirisha mizigo na abiria ili kuongeza mapato yatakayotokana na reli hii;

g) Ili kuepusha uvamizi wa maeneo ya reli na kuondoa usumbufu kwa wananchi, Shirika la Reli Tanzania-TRC liweke alama zinazoonesha mwisho wa eneo la reli ili kuondoa usumbufu kwa wananchi;

h) Shirika la reli lianze kujiendesha kisasa kwa kufunga vyombo vya kielektroniki ili kuweza kutunza kumbukumbu zote za kiutendaji, ufuatiliaji wa mizigo kwa wateja, uthibiti wa mafuta, udhibiti wa mwendo na usalama. Hii italifanya Shirika hili kuweza kujiendesha kisasa na kupunguza gharama za uendeshaji; na

i) Juhudi ziendelezwe kuhakikisha ujenzi wa reli nchini unafanywa kwa ushirikiano na sekta binafsi au mikopo yenye gharama nafuu kwani itasaidia kuharakisha zoezi zima la ujenzi wa reli nchini na Serikali itaweza kuweka fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mingine ya maendeleo.

2. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Bandari Kamati inashauri yafuatayo;

a) Serikali kwa kupitia Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Viwanda na Biashara iitishe kikao cha pamoja na wadau mbalimbali wa bandari nchini ili kubadilishana mawazo na kuona namna nzuri ya uendeshaji wa bandari ili kuifanya bandari iweze kujiendesha kibiashara na kuvutia wafanyabiashara wengi kuitumia jambo ambalo litaongeza mapato ya Serikali; Sambamba na hilo kufanyike utafiti wa kina wa Masoko ili kubaini sababu zinazopelekea idadi ya wateja kuhamia bandari zingine;

b) Mfumo wa TANCIS wa Malipo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania uangaliwe ili uweze kwenda sambamba na uhalisia kwani mfumo huu umekuwa moja kati ya mambo yanayochangia kuchelewesha huduma bandarini na hivyo kuwa kikwazo kwa bandari na hata wateja;

c) Serikali iangalie upya utendaji kazi wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania-TASAC kwani kumekuwa na malalamiko ya wateja wa bandari kuhusu kuwa na mlolongo mrefu wa kuidhinisha tozo na kusababisha ucheleweshaji, viwango vya tozo na mipaka ya utekelezaji wa majukumu ya TASAC;

c) Serikali iharakishe kukamilisha bandari za nchi kavu katika maeneo ya Kwala -Pwani, Ihumwa -Dodoma, Fela-Mwanza, Katosho-Kigoma, King'ori-Arusha, Isaka-Kahama, na Inyala-Mbeya ili kupunguza gharama kwa wateja kusafiri mpaka Dar es salaam kwa ajili ya kutoa mizigo;

c) Sulala la wadau wote wa bandari kuhamia kwenye jengo moja liwe jambo la lazima na la haraka ili kurahisisha na kuongeza ufanisi wa bandari;

d) Serikali iangalie mazingira ya uwekezaji wa bandari ya Bagamoyo ili uweze kwenda sambamba na faida kwa wananchi na Taifa kwa ujumla. Vile vile, Serikali ilipe fidia kwa wananchi waliobakia ndani ya eneo linalotarajiwa kujengwa bandari hii ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima wakati mradi huu utakapoanza;

e) Kwa kuwa Serikali imefanikiwa kufunga *flow meter* katika bandari ya Dar es Salaam kwa ajili ya upimaji wa mafuta yanayoingia nchini. Na kwa kuwa *flow meter* hii kwa sasa ipo katika kipindi cha uangalizi, ni muhimu sana kutafuta mtaalam aliyebobea katika mitambo ya aina hii ili apime ufanisi wa utendaji kazi wa *flow meter* hii. Aidha, baada ya kipindi cha majaribio kuisha kuhakikisha mfumo wake unabadilishwa na kuwa wakwetu kwa ajili ya kujihakikishia usalama. Pia ni muhimu kujiridhisha ikiwa mfumo huo ambao kwa sasa upo katika majaribio kama unafanya vipimo sahihi; Aidha, Serikali iendelee na jitihada za kutengeneza *flow meter* zingine mbili za bandari ya Tanga na Mtwara;

f) Kuhusu Bandari ya Mtwara, kasi ya uanzishwaji wa bandari ya hii iende sambamba na ujenzi wa njia ya treni ya Mtwara-Mbamba Bay na matawi ya Liganga na Mchuchuma; na

g) Kwakuwa Serikali sasa imerasimisha bandari bubu na kuanza kukusanya mapato, ni vema na muhimu kuboresha mazingira ya miundombinu ya bandari hizo ili umuhimu wa urasimishaji na mapato yanayopatikana yaweze kuonekana kwa uhalisi wake kwa wamiliki na watumiaji wa bandari hizi.

3. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Kampuni ya Huduma za Meli-MSCL; Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali ijipange kutengeneza meli zote kumi na nne (14) zilizopo katika Maziwa Makuu ili kuiwezesha Kampuni ya Meli Tanzania kumudu kujiendesha kibiashara;

b) Serikali iharakishe ujenzi wa meli katika ziwa Tanganyika na kukarabati meli iliyopo ya MV Liemba kwani kijiografia bandari hii inapakana na nchi ya Kongo (Kalemii) ambako kuna mizigo mkubwa wa biashara ambao utaiwezesha Serikali kupata mapato;

c) Kuimarisha njia za ukusanyaji mapato ya Kampuni kwa kufunga mitambo ya kieletroniki kwa ajili ya kukatia tiketi abiria katika vyombo vyake vyote ili kuzuia upotevu wa mapato.

4. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu TAZARA, Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali iharakishe mazungumzo baina ya nchi wabia wa reli ya TAZARA kuhusu kuimarisha reli hii kutokana na umuhimu wake katika kukuza uchumi;

b) Serikali ikamilishe manunuzi ya injini na vipuri pamoja na mitambo ya kusaidia kuzalisha kokoto na mataluma ya zege kwenye mgodi wa kokoto uliopo Kongolo- Mbeya na kusaidia viweze kuingia nchini kwa haraka ili vianze kutumika kwa ajili ya kuongeza mapato ya TAZARA;

c) Serikali iharakishe mchakato wa ajira za watumishi wa TAZARA ili kupata wafanyakazi wenye ujuzi na weledi wa kutosha kuliongezea Shirika uwezo kwani wafanyakazi wengi wamemaliza muda wao na kustaafu;

d) Serikali ihakikishe inatoa kwa wakati fedha za ujenzi wa kipande cha reli chenye urefu wa kilometa 18 kutoka Chikola kwenda kwenye mgodi wa Magamba ili kuweza kurahisisha usafirishaji wa makaa ya mawe kwani mzigo unaotoka ni

mkubwa hivyo unaweza kuipatia TAZARA mapato ya kutosha; na

e) Serikali kuhakikisha inalipa madeni yote ya wafanyakazi wastaafu wa TAZARA.

5. **Mheshimiwa Spika,** kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA: -

a) Serikali kuongeza wigo katika Bajeti ili kuiwezesha TAA kutekeleza majukumu yake ya kusimamia, kuendesha na kuendeleza viwanja vya ndege na hatimae kutoa huduma bora. Huu ndio msingi wa Kamati kuwa inasisitiza Mamlaka hii iachiwe angalau **asilimia 40** ya maduhuli yatokanayo na viwanja vya ndege ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa ufanisi;

b) Serikali kulichukuwa deni la malipo ya awali *(advance payment)* ya ujenzi wa jengo la III la abiria katika Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere ambapo TAA imekuwa ikilipa kiasi cha **Dola za Kimarekani 592,717** kila mwezi. Deni lililosalia hadi mwezi Januari 2021 lilikuwa **Dola za Kimarekani 22,943,910**. Ikiwa TAA itaendelea kulipa deni hili kila mwezi linakadiriwa litaisha mwezi Novemba 2024.

c) Serikali kuongeza wigo wa bajeti ya TAA ili iweze kulipa gharama za utwaaji na umiliki wa viwanja vya ndege jambo linalosabisha TAA kuchukuwa muda mrefu kufanya zoezi la kupata Hati Miliki ambapo kati ya Viwanja vya Ndege 58 ni viwanja 12 tu vilivyopata Hati Miliki. Ni vema Serikali kuhakikisha Viwanja vyote vya ndege na mali zake vinakuwa Hati Miliki na uzio kwa ajili ya kuepusha hatari za binadamu na wanyama na kuepuka migogoro ya ardhi.
Aidha, Serikali kuangalia upya vigezo vya utozaji wa kodi ya pango la ardhi katika maeneo ya viwanja vya ndege.

d) Serikali ihakikishe inatenga fedha kwa ajili ya malipo ya fidia za maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya viwanja vya ndege nchini hususani eneo la Kipunguni ambapo kunadaiwa deni la **Shilingi Bilioni 29.8;** na

e) Ili kupata wataalam wenye uzoefu walioshiriki kwenye ujenzi wa mitambo na mifumo ya viwanja vya ndege, Serikali irejeshe jukumu ya ujenzi wa Viwanja vya Ndege kwa TAA hata kama ni kwa awamu ili kuwajengea uwezo wa ujenzi, utunzaji na ufahamu wataalam wahandisi waliopo TAA.

6. **Mheshimiwa Spika**, Kuhusu Kampuni ya Ndege Tanzania-ATCL

a) ATCL iangaliwe kama Kampuni ya kibiashara na sio kutoa huduma; Kuwepo na mikakati ya kitaifa ya kuhakikisha kuwa ATCL inakuwa na uwezo wa kushindana na kutengeneza faida;

b) Serikali iyachukuwe madeni yote ya nyuma ATCL, ambayo kwa kiasi kikubwa yanachangia kuharibu mizania ya hesabu za ATCL;

c) Shirika liendelee kufanya utaratibu wa kuongeza safari za ndani na za kikanda ili kuimarisha mtandao wa safari zake. Kamati inatambua changamoto ya mlipuko wa ugonjwa wa Corona ambao umesababisha mdororo hasa soko la usafiri wa anga duniani, hata hivyo ni muhimu kuendelea na mikakati hii ili hali itakapotulia Shirika liweze kufanya vizuri; na

d) Wafanyakazi wa Kampuni ya Ndege Tanzania- ATCL kupewa mafunzo ya huduma kwa wateja, mara kwa mara, ili kuweza kutoa huduma nzuri wakati wote. Hii itasaidia Kampuni kushindana na makampuni mengine yanayofanya biashara ya usafiri wa anga.

7. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia- TAZARA Kamati inashauri yafuatayo; -

a) Serikali iweke mkakati wa dhati kuinusuru TAZARA ili iweze kujiendesha. Moja ya mkakati uwe ni kufanya mazungumzo na Serikali ya Zambia na kufikia muafaka wa namna bora ya uendeshaji wa reli hii, ikiwa ni pamoja na, kufanya mapitio ya kurekebisha Sheria iliyoianzisha TAZARA, Namba 23 ya Mwaka 1975;

b) Serikali ilipe madeni ya wafanyakazi; pamoja na, kuendelea kusaidia kulipa wafanyakazi wa TAZARA mishahara mpaka hapo itakapowekeza mtaji wa kutosha; na

c) Serikali kujenga kipande cha reli chenye urefu wa kilometa 18 kwenda kwenye mgodi wa Magamba ili kuweza kurahisisha usafishaji wa makaa ya mawe kwani mzigo unaotoka ni mkubwa hivyo unaweza kupatia TAZARA mapato ya kutosha kujiendesha.

### 3.3 Sekta ya Ujenzi

1) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Wakala wa Barabara-TANROADS, Kamati inaendelea kusisitiza ushauri ufuafuatao:-

a) Serikali itekeleze Sera yake ya kuunganisha Mikoa yote kwa barabara za lami. Baadhi ya Mikoa hiyo ni Lindi – Morogoro, Morogoro -Mlimba -Madeke Njombe, Mbeya-Makongorosi-Chunya-Tabora, Katavi-Tabora, Mbeya – Makete -Njombe, Kigoma-Kagera, Lindi –Songea, Arusha–Mara. Aidha, miradi ya barabara inayoendelea ipewe kipaumbele na ile ambayo haijaanza ifanyiwe upembuzi yakinifu;

b) Serikali ijenge kwa kiwango cha lami barabara muhimu zifuatazo: -

i. Barabara zinazounganisha nchi yetu na nchi nyigine hususani Mikoa ya Kigoma-Kagera, Rukwa-Katavi, Ruvuma-Mtwara;

ii. Barabara zinazounganisha Makao Makuu ya Mikoa kama vile Kigoma-Kasulu-Kagera, Katavi – Kigoma – Tabora;

iii. Barabara za kiuchum kama vile, Mtwara – Newala – Masasi, ambayo ni barabara inayopita katika maeneo ambayo yanazalisha korosho kwa wingi ukizingatia kwamba zao la korosho linachangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa mikoa ya kusini na nchi kwa ujumla; barabara ya Handeni – Kibrashi -

Kibaya– Singida ambayo ni barabara yenye tija kiuchumi kutokana na kuwapo kwa bomba la mafuta linalounganishwa na nchi ya Uganda na barabara ya Bukoba-Karagwe-Kyerwa ambayo inapita katika maeneo yanayozalisha kahawa kwa wingi.

iv. Barabara zinazounganisha Wilaya na Makao Makuu ya Mikoa, hizi pia zipewe kipaumbele ili kuwezesha wakulima kuweza kuyafikia masoko ya mazao; na

v. Barabara zilizohaidiwa na viongozi wakubwa w anchi waliopo madarakani na waliostaafu nazo zipewe kipaumbele.

c) Madai ya Makandarasi yazingatiwe kwa kulipwa kwa wakati ili kuepusha hasara zinazoweza kutokea endapo fedha hizo zitachelewa.

d) Kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanyika katika sekta ya ujenzi nchini, ni muhimu sana Serikali ikahakikisha inaajiri Wahandisi wa kutosha ili waweze kusimamia miradi kwa ufanisi tofauti na ilivyo sasa idadi ya Wahandisi Wizarani haindani na miradi iliyopo hivyo ufanisi kuwa mdogo.

e) Serikali kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi na Bodi ya Usajili wa Makandarasi kuendelea kutoa mafunzo kwa wahandisi washauri na Makandarasi wa ndani ili waweze kusimamia na kutekeleza ujenzi wa barabara kikamilifu. Aidha, kuhamasisha wakandarasi wazalendo kujiunga na kuomba zabuni kwa utaratibu wa ubia na kupata dhamana kupitia mfuko Maalum wa kutoa dhamana ya kusaidia makandarasi wadogo na wa kati. Vilevile, kuhamasisha zaidi kwa kuendelea kutoa mafunzo kwa Wahandisi na Makandarasi wanawake.

f) Sekta ya Ujenzi isimamie ipasavyo Sheria ya barabara kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa kutumia vyombo vya habari, kama runinga, magazeti, redio na simu za mkononi. Aidha, vyombo vinavyohusika na usimamizi wa sheria ya barabara kuwa macho wakati wote na endapo kutaonekana mtu

anajenga ndani ya hifadhi ya barabara kuzuiwa na kubomolewa mapema. Aidha, Wakala wa Barabara iendelee na zoezi la kuweka alama za mipaka katika maeneo ya barabara ili kuepusha usumbufu wakati maeneo hayo yanapohitajika;

g) Serikali iendelee na juhudi kufunga mizani ya kisasa zinazopima magari huku yakiwa kwenye mwendo katika vituo ambavyo vinamsongamano mkubwa wa magari kwenye mizani ili kuokoa muda, fedha na usumbufu kwa wasafiri na wasafirishaji;

h) Serikali iongeze kasi ya ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi ambavyo vinajengwa katika Ukanda wa Kati na Ukanda wa Dar es Salaam ili kurahisisha usafirishaji wa bidhaa pamoja na kuokoa muda wa mizigo kukaa barabarani;

i) Wakati wa ujenzi wa barabara ni vema wakala wa barabara wahakikishe wanaweka sehemu maalum kwa ajili ya kuvukia mifugo kwa ajili ya kuepusha ajali na vifo vya wanyama, na pia kuzuia uharibifu wa barabara;

j) Wakati wa ujenzi wa barabara zipo taasisi nyingi za Serikali zinapeleka madai kwa wakandarasi wa barabara kwa ajili ya ulipiaji malighafi zinazotumika kwenye ujenzi, kama vile Wizara ya Madini (kokoto, mawe, kifusi), Wizara ya Maji na umwagiliaji (vima vya maji), Wizara ya Viwanda na Mazingira (uharibifu wa mazingira); pamoja na, ushuru unaotozwa na Halmashauri za miji; gharama hizi zinaongeza gharama za ujenzi wa barabara, hivyo, Kamati inaishauri Serikali isamehe kodi hizo kwani zinalipwa na Serikali na si wakandarasi;

k) Serikali iangalie namna nzuri ya kuhamisha miundombinu ambayo imejengwa katika miradi ya ujenzi wa barabara kama vile miundombinu ya maji na umeme kwani imebainika kuwa kati ya vikwazo vinavyochelewesha miradi na pia huongeza gharama kwani hulipwa na Serikali na si Mkandarasi;

l) Serikali ihakikishe inaweka mikakati ya kupunguza msongamano ya magari kwenye miji inayokua kwa kasi, kama vile, Mbeya, Mwanza, Arusha na hivi sasa Dodoma. Mikakati hiyo iwe ya kujenga barabara za mzunguko (ring roads) pamoja na barabara za kulipia *(road tolls).*

2) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu ujenzi wa viwanja vya ndege, Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali ikamilishe kwa haraka ujenzi unaoendelea wa kiwanja cha ndege cha Mwanza hasa ujenzi wa jengo la abiria;

b)Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 kwa ajili ya ujenzi wa Viwanja vya Ndege ili miradi hii iweze kukamilika kwa wakati na kuepuka riba ambazo hutokana na miradi kutokamilika kwa wakati;

c)Ni muhimu Serikali iharakishe kujenga na kuimarisha Viwanja vya Ndege vitakavyozalisha mapato na kujiendesha; kama vile, Kiwanja cha Ndege cha Moshi (kwa ajili ya utalii), Kiwanja cha Ndege cha Iringa (kwa ajili ya Utalii) na Kiwanja cha Ndege cha Mtwara (kwa ajili ya uwekezaji);

d) Serikali ilipe fidia mapema na kwa wakati kwa wananchi wanaopisha ujenzi mathalani kiwanja cha ndege, Lake Manyara, Simiyu; na

e) Serikali iweke taa za kuongozea ndege hususan katika Kiwanja cha Ndege cha Songwe-Mbeya ili ndege ziweze kutua na kuruka wakati wote. Vilevile, kuweka uzio katika maeneo ya viwanja vya ndege ili kuzuia hatari zinazoweza kutokea.

3) **Mheshimiwa Spika,** kuhusu Wakala wa Ufundi na Umeme-TEMESA, Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Wakala uendelee kukamilisha mchakato wa kuchagua karakana za kutengeneza magari ya Serikali kwenye Wilaya

ili kuondoa usumbufu wa magari ya Serikali kusafiri umbali mrefu kwenda kufanya matengenezo;

b) Wakala uchukue hatua za makusudi na kuweka mkakati wa kudumu ili kukusanya madeni ya **Shilingi bilioni 39** ambayo, zinadaiwa taasisi za Serikali ili Wakala huu uweze kijiendesha kibiashara badala ya kutegemea ruzuku kutoka Serikalini; na

c) Serikali iajiri wataalam waliobobea kwenye fani ya ufundi wa magari na kuhakikisha kunakuwa na mitambo ya kisasa ili kuendana na kukua kwa teknolojia kwani mara nyingi magari ya Serikali yamekuwa yakitengenezwa kwenye karakana binafsi za mitaani jambo ambalo si sahihi;

4) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Wakala wa Nyumba-TBA; -

a) Kamati inashauri Serikali Wakala uchukue hatua za makusudi na kuweka mkakati wa kudumu ili kukusanya madeni ya kiasi cha **shilingi bilioni 17** ambazo kwa kiasi kikubwa Wakala unazidai Wizara, Idara pamoja na Taasisi za Serikali; na

b) kuhakikisha kuwa inaingia mkataba wa utunzaji wa nyumba na mandhari ya eneo la mradi pamoja na kuhakikisha ukaguzi unafanyika mara kwa mara ili kuzuia uharibifu unaoweza kujitokeza pindi nyumba hizo zitakapohamiwa.

### 3.4 Maoni na Ushauri wa Jumla

1. Fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo zitolewe kwa wakati ili kuharakisha utekelezaji wa miradi na kuleta maendeleo kwa haraka;

2. Serikali ichukue hatua za makusudi na kuweka mikakati yaa kudumu ili kulipa madeni ambayo kwa kiasi kikubwa Mashirika/Taasisi/Wakala inazidai Taasisi/Mashirika/Wakala nyingine za Serikali. Hili limeendelea kuwa changamoto kubwa kwa Mashirika na Taasisi za Serikali;

3. Serikali iangalie umuhimu kuacha fedha angalau asilimia 40 ya maduhuli kwa Mashirika/Taasisi zake ili yaweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa ufanisi.

4. Serikali kuchukuwa hatua za haraka kuajiri Watumishi kwenye Taasisi/ Mashirika na Wakala waliopo chini ya Wizara hii kwani zinakabiliwa na changamoto ya upungufu mkubwa wa watumishi pamoja na watumishi wengi kuwa katika umri mkubwa ambao baada ya muda mfupi watastaafu. Uchambuzi wa Kamati ulibaini baadhi ya Mashirika/ Taasisi na Wakala zenye upungufu mkubwa wa watumishi ni Mamlaka ya Bandari Tanzania-TPA, Kampuni ya Huduma za Meli-MSCL, Wakala wa Majengo Tanzania-TBA, TEMESA, Wakala wa Barabara Tanzania-TANROADS, Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi-ICOT;

5. Umuhimu wa Vyuo vya kati kuboreshwa, Kamati imekuwa ikihimiza siku zote Serikali kuhakikisha inakuwa na wataalam wa kutosha katika sekta ya ujenzi katika ngazi za chini (artisans), ngazi ya kati (technicians) na wa ngazi ya juu (engineers). Hii ni kwa kuwa taifa letu sasa limejikita katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali pamoja na uanzishwaji wa viwanda, hivyo basi Serikali haina budi kujikita na kuwekeza vya kutosha katika vyuo vya ufundi ili kuweza kupata mafundi wa kutosha ambao watasaidia uendelezaji wa miundombinu ya usafirishaji, viwanda, uzalishaji mali na hatimae kuboresha maisha ya watu;

6. Serikali iendelee kuongeza ushirikishwaji wa mafundi na mainjinia wa ndani katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali ili kuwekeza ujuzi na miradi hiyo itakapokamilika iwe rahisi kuiendeleza na hata kujenga mingine kwa kutumia wataalam wa ndani;

7. Utaratibu wa GN uangaliwe kwani imebainika utaratibu huu umekuwa moja ya changamoto ya ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi ujenzi. Ucheleweshaji huu unaotokea sababu ya kuchelewa kupata GN kwa ajili ya msamaha wa kodi, ni muhimu sana Sheria ya Value Added Tax (VAT) kuangaliwa upya hasa kwa kazi zile ambazo haziwezi kusubiri

GN ikiwa ni pamoja na kazi za dharura na matengenezo ya kawaida;

8. Fidia zitolewe kwa wananchi wanaopisha ujenzi na upanuzi wa miradi mbalimbali ikuhusisha miradi ya ujenzi na upanuzi wa barabara, ujenzi wa reli, ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima pamoja na usalama wa miradi husika.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, sekta ujenzi na Uchukuzi ni muhimu sana katika kuharakisha na kuchochea maendeleo ya nchi. Miradi iliyo ndani ya Sekta hii ni mikubwa na inahitaji fedha nyingi ili yote iweze kukamilika kwa wakati uliopangwa. Hivyo, Kamati inaona ni muhimu Serikali kushirikisha Sekta binafsi katika kutekeleza miradi hii mikubwa.

### a) Shukrani

**Mheshimiwa spika,** napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango waliyoitoa wakati wa ziara na vikao vya Kamati hususan vikao vya uchambuzi wa Bajeti. Kwa namna ya pekee naomba kuwatambua wajumbe wa Kamati hii kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Moshi Seleman Kakoso, Mb -Mwenyekiti
2. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka, Mb ‘’
5. Mhe. Capt. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb ‘’
6. Mhe. Mariam Nassoro Kilangi, Mb ‘’
7. Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb ‘’
8. Mhe. Fredrick Edward Lowassa, Mb ‘’
9. Mhe. Eng. Mwanaisha Ng’anzi Ulenge, Mb ‘’
10. Mhe. Mohamed Maulid Ali, Mb ‘’
11. Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb ‘’
12. Mhe. Mbarouk Juma Khatibu, Mb ‘’
13. Mhe. Masache Njeu Kasaka, Mb ‘’

14. Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb ‘’
15. Mhe. Amina Ally Mzee, Mb ‘’
16. Mhe. Rose Vicent Busiga, Mb ‘’
17. Mhe. Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mb ‘’
18. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb ‘’
19. Mhe. Stella Simon Fiyao, Mb ‘’
20. Mhe. Aeshi Khalfan Hilaly, Mb ‘’
21. Mhe. Abdulaziz M. Abood, Mb ‘’
22. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate, Mb ‘’
23. Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb ‘’
24. Mhe. Ahmed Yahya Abdulwakil, Mb ‘’
25. Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb ‘’

**Mheshimiwa spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni na Ushauri kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Kwa namna ya pekee naomba niwashukuru Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Eng. Dkt. Leonard M. Chamuriho, (Mb) akisaidiana na Manaibu Mawaziri Mhe. Msongwe Geofrey Kasekenya, (Mb) na Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara, (Mb).

Aidha, Kamati inawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara hii Eng. Joseph K. Malongo (Sekta ya Ujenzi) na Ndg. Gabriel Joseph Migire (Sekta ya Uchukuzi). Kamati pia inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa ushirikiano walioipa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kumshukuru aliyekuwa Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Nimpongeze pia Ndugu Nenelwa Mwihambi kwa kuteuliwa kuwa Katibu wa Bunge. Aidha, shukrani maalumu ziende kwa Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu. Gerald Singano Magili pamoja na Makatibu wa Kamati Ndugu Hosiana John Mvunta na Ndugu Janeth Julian Malangu, Msaidizi wa Kamati Ndugu. Grace Samwel pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao ulioiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Seleman Kakoso, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**
**YA MIUNDOMBINU**

17 Mei, 2021

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwa utaratibu wetu wamemaliza mawasilisho tutaendelea na nimeletewa hapa majina mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge ambao wanataka kuchangia, hoja hii ya Mheshimiwa Waziri.

Kabla michango hiyo haijaanza acha niseme machache; kwanza ni tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba msisahau siku ya leo mara baada ya kusitishwa kikao cha Bunge kutakuwa na mafunzo kwa Wabunge wote kuhusu huduma ya vifurushi yaani bando *services* vinavyotolewa na makampuni ya simu.

Mafunzo hayo yatatolewa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na yatafanyika ukumbi wa Msekwa. Mafunzo haya ni muhimu sana hili Waheshimiwa Wabunge tuweze kujua namna ya kuwaelekeza wananchi tunaowawakilisha.

Sasa nimesema niseme mambo machache, nayo yanahusu Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi; tumepata changamoto kidogo na nichukue fursa hii kuwapa pole sana

wananchi wa Mbeya Mjini kwa changamoto iliyotokea katika mgomo wa madaladala na bajaji.

Mheshimiwa Waziri wa wizara hii Mbeya Mjini kwa muda mrefu miundombinu haiko sawasawa na sababu hiyo inayosababisha migomo. Wanachi kwa maana wanayojishughulisha na bajaji, wanaojishughulisha na daladala, wanaweza wakawa wanaonekana kama sio wananchi watiifu hivi, hawatii sheria, lakini kimsingi ni kwamba miundombinu ni mibovu ambayo ipo chini yenu Wizara ya Ujenzi, lakini pia iliyoko chini ya TAMISEMI.

Hapa nitazungumza kwa kifupi halafu muangalie utaratibu Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI namna mtakavyolifanyia kazi jambo hili, kwa sababu Mbeya ni Jiji kama majiji mengine. Ukienda Mbeya utagundua hili jiji linaitwa jiji lakini kimsingi ni halmashauri tu kama zingine huko tena zingine ni bora zaidi. Sasa si kazi yangu si kutaja kwamba ina tofauti gani na majiji mengine lakini miundombinu ya Mbeya ni mibaya.

Sasa nimepitia hapa bajeti Mheshimiwa Waziri ni kama tunaeleza jambo ambalo mimi nashindwa kuelewa ni wakati gani tutamaliza lakini Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ukurasa wa 66 inasema: "*Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika kwa barabara ya kutoka Igawa mpaka Tunduma.*"

Hivyo ndivyo inavyosema, kwa maana kwamba kilomita 220 upembuzi yakinifu na usanifu wa kina tayari, lakini kwenye kitabu chako Mheshimiwa Waziri unasema mnaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Sasa nawaza ilani ya mwaka jana tuliyoinadi inasema umekamilika, sasa hivi tumetayarisha bajeti inayosema tunaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Sasa ni shughuli gani hii ambayo haiishi Mheshimiwa Waziri?

Pia kwa muktadha huo huo nimalizie, kwa muktadha huo huo, nyinyi mmeshapita pale Mbeya Mjini malori yanayoelekea Malawi, malori yanayoelekea Zambia yote

yanatumia barabara hii, eneo pekee lililotengenezwa ni eneo la Igawa. Mbeya Mjini msongamano wake hauna jina, ni tofauti na Dar es Salaam ukisema kuna msongamano kwa sababu kuna mvua, yaani pale ni msongamano iwe jua au mvua, kila siku. Hii barabara ya *TANZAM* jamani na humu mmeweka kwamba kuna kilomita tano ambazo mmezitengea bilioni tano, nikawa najiuliza ni kutoka wapi kuelekea wapi hizi kilomita tano, ni kutoka Uyole mpaka Iwambi pale au na zenyewe ziko Igawa tena. *(Makofi)*

Kwa hiyo foleni itaendelea, sasa jamani naomba sana yani tunapofikiri kuhusu maendeleo ya nchi hii, tutazame kwa uwiano, lakini pia tuangalie uzito na biashara zinazofanyika katika hayo maeneo, barabara hii inaleta usumbufu mkubwa na nichukue fursa hii kumpongeza sana *RPC* wa Mbeya, Urichi Matei sasa hivi hamjasikia sana ajali, ni kwa sababu sasa hivi kumeshakuwa na foleni upande wa Mbalizi magari lazima yapaki, upande wa Iwambi magari yapaki muda mrefu ili abiria tupite halafu yakianza malori abiria tunasimama. Kwa hiyo amechukua hiyo hatua, lakini sio ya muda mrefu, kwa sababu muda ni mali na hii foleni tunayoisababisha hapo changamoto ni kubwa sana. *(Makofi)*

Niwaombe, huu upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambao kila siku tunauzungumza kwa kweli ufike mahali sasa ukamilike, tuanze kuona huo ujenzi wa hizi barabara. Nimetaja hizo nchi chache tu ambazo ndiyo zinatumia sana hii barabara kwa sababu jiji hili liko mpakani, kwa hiyo linalisha sehemu nyingi. Hata hivyo, mmefanya kazi nzuri upande wa ule mpaka wetu na Malawi. Mmejenga meli mpya za kisasa, sasa mizigo tena inafuatwa mpaka Dar es Salaam, kwa nini hii *TAZARA* waliyoisema Kamati yetu msiitazame, kwamba mnapopeleka *SGR* Tabora; nyingine itaanzia Mwanza sijui mpaka Isaka mpaka wapi; huku Nyanda za Juu Kusini mizigo yake itakuwa inaenda vipi? *(Makofi)*

Hii reli ya *TAZARA* iko vizuri, inahitaji tu matengenezo kidogo, lakini pia muiwekee umeme ili iwe ni ya kisasa, ndicho kinachotakiwa. Kwa hiyo Mheshimiwa muyatazame hayo kwa upana kwa kweli, nyanda za juu kusini *SGR* namna

mtakavyopeleka hilo jambo, sio sisi tunasoma tu kila siku humu ndani, hapana ni mikoa mingi ipo huko na yote tunategemea hiyo *TAZARA. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nitaanza kuita Waheshimiwa Wabunge ambao wanatakiwa sasa kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kwagilwa Reuben, atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Mtaturu na Mheshimiwa Flatei Massay ajiandae.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu na nyeti kwa nchi yetu. Awali ya yote, naomba niunge mkono hoja.

Nimesimama hapa ili niweze kuzungumzia mradi mkubwa wa kihistoria ambao nchi yetu inaendelea nao wa *SGR.* Nilisamama hapa mara ya mwisho nikauzungumzia, lakini leo nataka nizungumzie na niishauri Serikali namna bora ya ku-*finance* mradi huu wa *SGR.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu mkubwa na mzuri kwa nchi yetu kama hatukujipanga vizuri na namna ya kuu-*finance* vilio vitakuwa vikubwa sana huku kuhusu barabara na mambo mengine ya miundombinu mingine. Hii ni kwa sababu fedha nyingi tunayoipata itakuwa inakwenda hapa, halafu tunashindwa kupeleka maendeleo kwenye maeneo mengine ya miradi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipo kitu kinaitwa *credit rating,* nimesimama hapa niishauri Serikali kufanya mchakato wa kufanya *credit rating* ya nchi yetu. Zipo kampuni duniani zinazofanya mchakato huu wa kui-*rate* nchi na faida ya kui-*rate* nchi ni kwamba utakuwa na uwezo, ukishakuwa *rated* una uwezo wa kwenda kwenye masoko ya mikopo makubwa na ukapata fedha kwa kiwango kikubwa na cha uhakika zaidi kuliko ambavyo sasa tuna-*finance* mradi huu kwa kutumia *concessional loans*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza *concessional loans* zenyewe zilivyo zina masharti mengi na ambayo zinafanya sekta zetu binafsi zisiweze kushiriki kwenye maendeleo. Unapokuwa umechangua *finance* kwa kutumia *concessional,* yule anayekupa fedha ndiye anayechangua kampuni ya kusimamia, ndiye anayechagua kampuni ya kujenga pia. Tungekuwa tumejielekeza kwenye kufanya *credit rating* ili tuweze ku-*issue infrastructure bonds,* ingetuwezesha sisi kuamua nani tumpe kazi gani kwenye mradi upi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyozungumza nitatolea mfano *Standard Charted Bank* kwa kushirikiana na *Export Credit Agencies* walitupa sisi kama nchi mkopo wa bilioni 1.46. Mkopo huu ambao tumepewa kwa ajili ya kujenga hii *SGR* ni gharama kubwa ku-*service* mkopo huu kwa sababu gani, kwa sababu ukitumia njia hii ya kupata mkopo ni kwamba unaruhusu madalali katikati *Standart Charted* hana hela ya...

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kwagilwa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Getere.

**TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa mdogo wangu Kwagilwa kwamba tunapozungumza habari ya miradi ya kimkakati ya kimaendeleo katika nchi za kiafrika, bora uchague moja, upewe mkopo kutoka nje wenye masharti ya kwamba mradi ukiisha ukishindwa kulipa wauchukue au utafute mkopo wa bei nafuu kwenye nchi yako mradi uendelee kuwa wako. Kwa hiyo ndio mambo tunayopewa kuchagua hayo.

**NAIBU SPIKA:** Kabla sijakuuliza Mheshimiwa Kagilwa, Mheshimiwa Getere na Waheshimiwa Wabunge wote niwakumbushe humu ndani tumekuwa na mazoea si mabaya

tukiitana nje lakini humu ndani ni Waheshimiwa, kuna wakati huwa inaleta changamoto kidogo mtu akiitwa mdogo wa mtu, kaka wa mtu, shemeji wa mtu na mambo kama hayo au mke wa mtu kwa maana hiyo hiyo.

Mheshimiwa Kwagilwa unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge aliyezungumza inaelekea hajui hiki ninachokiongea, kwa hiyo taarifa hiyo siipokei. Nazungumzia *infrastructure bonds,* ni mkopo kama ulivyo mkopo mwingine na mkopo huu hauna sharti lolote la kwamba ukishindwa kulipa mradi huu unachukuliwa haiko hivyo. Uki-*issue infrastructure bonds* kunakuwa na watu wanao-*subscribe* wengi kutoka nje wenye fedha wanakupa. Hiki ndicho ninachokizungumzia.

Mheshimiwa Naibuu Spika, nilikuwa natolea mfano kwamba tulipata ile 1.6 kutoka *Standard Charted,* yupo *Standard Charted* pale, maana yake tumemlipa fedha wako *Export Credit Agencies* maana yake tumewalipa fedha na yote hii inaenda ina *amount* kwenye deni letu la Taifa, ungekuwa ume-*issue bond* ungekuwa umechukuwa tu fedha moja kwa moja kutoka kwa yule anayekukopesha bila kupita kwa mtu mwingine. Hiki ndicho ninachokizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hivyo tutaweza kujenga barabara zetu za ndani kwa makusanyo yetu sasa, haya tunayokusanya kupitia *TRA.* Kwa mfano, Barabara ya Handeni – Kiteto – Kibirashi – Kondoa - Singida itaweza kujengwa, lakini ilivyo hivi sasa tumefanya bajeti *allocation* ya bilioni nne, hapo hapo kuna miradi mingine ya barabara kwa fedha hizo, tutakamalisha lini ujenzi wa barabara hizi ambazo ni za muhimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nashauri kama tutaweza tufanye *credit rating* kwa kutumia Kampuni ya *Standard and Poor,* kama tukiweza tufanya *credit rating* kwa kutumia *moody* kama tukiweza tufanye *credit rating* kwa kutumia *fitch.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza kufanya kwa kutumia kampuni mbili au tukiona ni gharama tufanye kwa kutumia kampuni moja. Tafsiri ya *credit rating* ni kwamba mnakuwa *declared* kama nchi ambayo ina uwezo wa kuhimili deni na kulipa pale inapogoma. Hiki ndio tunachokishauri na ndicho ninachokishauri kifanyike na Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunapozungumza kwenye huu mradi huu wa *SGR* mpaka sasa loti Na.3 haina fedha na haina mkandarasi. Mpaka sasa loti Na.4 Tabora - Isaka haina fedha na haina mkandarasi, hata hii unayoongelea loti Na.5 ya Isaka - Mwanza wamekuja Wachina hapa wameahidi kutupa 1.32 bilioni, hiyo ni *concessional loans,* sharti la kwanza kampuni zao mbili ndio zijenge.

Ndugu zangu hatutaweza kulinda hata ubora wa mradi wenyewe, yaani mtu anapokupa, ajenge yeye, asimamie yeye, sasa wewe ushiriki wako ni upi kwenye hii? Tukiangalia kwenye sekta ya ujenzi ndio sekta ambayo imekuwa mfululuzo kwenye miaka hii ya karibuni lakini watanzania wanashiriki vipi kwenye sekta hii ya ujenzi, hawawezi kushiriki kama tunaendelea kuchagua *financing* za namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nimeongea kwa wakati, nikushukuru sana kwa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Flatei Massay atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Isack Mheshimiwa Selemani zedi ajiandae

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kupata nafasi ya kuongea...

**NAIBU SPIKA:** *Sorry,* Mheshimiwa Miraji Mtaturu atafuatiwa na Mheshimiwa Flatei Massay na Mheshimiwa Francis Isack ajiandae.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunirejesha tena kwenye orodha yako. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na kukutana leo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru na kuipongeza sana hotuba nzuri ya Waziri wetu wa Ujenzi ambayo ameitoa hapa asubuhi, ambayo imeonyesha dira ya kuweza kuboresha miundombinu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze yeye pamoja na Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara hii ambao wanafanya kazi nzuri sana kusimamia shughuli za ujenzi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wote tunakiri wazi kwamba miundombinu ya barabara reli na usafirishaji ni kiungo muhimu katika uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba maendeleo ya nchi yetu yanategemea sana ujenzi katika miundombinu pamoja na usafirishaji. Tukifanikiwa kuimarisha ujenzi wa miundombinu katika nchi yetu tutaharakisha sana uchumi wa nchi yetu, ndio maana leo tunapopata nafasi ya kuchangia hapa tunatoa ushauri kwa Serikali yetu ili kuboresha namna bora ya kuweza kuongeza miundombinu katika maeneo yote ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali, imekuwa ikiongeza fedha mwaka hadi mwaka katika kuhakikisha kwamba tunaimarisha sana miundombinu. Ushahidi uko wazi, katika *trend* ya utoaji wa fedha imeonekana katika bajeti hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pamoja na juhudi hizi, ninataka nieleze tu kwenye maeneo haya ya barabara kwa maana ya barabara zetu zinazojengwa. Tumekuwa na kikwazo, kumekuwa na utaratibu wa kwamba lazima *GN* itoke ndiyo ifanikishe ujenzi uanze.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya niwaombe sana Wizara, niwaombe Serikali waondoe urasimu wa ucheleweshaji wa *GN* kutoka. Hizi fedha ambazo tunasema leo zimetoka haziwezi kuanza kazi mpaka *GN* itoke. Imekuwa ni kikwazo maeneo mengi, wakandarasi wanakuwa wako tayari lakini wanazuiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini muda mwingine mradi unakuwa labda una miaka miwili au mitatu. Katika muda wa mwaka mmoja ukiisha ule muda wa *lot* ya kwanza unakuta haiwezi kuendelea mpaka *GN* itoke tena, tunatangaza upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana Serikali kwenye eneo hili, niendelee kushauri kwamba waongeze bidi katika eneo hili, inawezekana sisi wenyewe mawasiliano ndani ya Serikali tuweze kuongeza nguvu katika kutoa *GN* kwa wakati ili kuisaidia miradi hii iweze kutekelezwa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hii ya *GN* inakwenda sambamba pia na utoaji wa fedha za miradi. Tumekuwa tukipitisha hapa kwenye bajeti hizi za kila mwaka, lakini tumekuwa tunachelewa kutoa fedha. Lakini pia kuna wakandarasi ambao hawalipwi kwa wakati, wameshamaliza wamewasilisha zile *certificates* zao lakini bado hawalipwi kwa wakati. niiombe sana Wizara, niiombe Serikali wawalipe wakandarasi kwa wakati ili wawe na nguvu ya kuitekeleza miradi hii ambayo tunawapatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili nitaongelea kwenye upande wa viwanja vya ndege. Viwanja vyetu vya ndege huko nyuma walikuwa wanajenga wenyewe Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, kwa mujibu wa sheria walikuwa wao wanasimamia lakini pia wanafanya ujenzi. Lakini baadaye *TANROADS* walipewa jukumu hili la kujenga viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina tatizo kabisa na *TANROADS, TANROADS* ni wazuri sana kwenye maeneo ya *runways,* wanajenga vizuri kabisa. Lakini tuna changamoto

ya *facilities* nyingine katika viwanja vya ndege. Kwa hiyo, eneo hili limekuwa na utata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana Serikali ifikirie upya; wawarudishie Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wajenge wenyewe viwanja vyao kwa sababu sheria inawafanya wao wasimamie viwanja. Ili wasimamie vizuri lazima wajenge wenyewe ikiwemo kuangalia *facilities* zinazotakiwa katika viwanja hivyo zikiwemo zile *airport towers, lounges* zile za kuweza kusimamia kwa ajili ya kuchukulia abiria. Kwa hiyo, nilitaka niseme hili Serikali iangalie upya maelekezo haya waliyokuwa wameyatoa huko awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa fedha nimeeleza vizuri. Nieleze kukumbusha barabara muhimu sana za uchumi; barabara ya Singida – Kwa Mtoro – Kiberashi – Tanga ni barabara yenye kilometa 461. Barabara hii pamoja na kuwa sasa tutaitumia na ni barabara ya kihistoria, na ni barabara inayogusa mikoa minne, tunachoangalia kwenye randama hapa, tumetengewa sasa kilometa 20 badala ya 50 hata zilizotajwa mwanzoni. Barabara hii itachukua muda mrefu kuimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu, ninaomba iongezewe fedha ili iweze kumalizika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii imeongoza thamani sasa, inapita sambamba na bomba la mafuta linalotoka Tanga kwenda Hoima. Kwa hiyo kiulinzi na kiusalama barabara hii ni muhimu sana. Niombe barabara hii ijengwe kwa sababu imesubiri kwa muda mrefu kuunganisha mikoa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama haitoshi, barabara ile ya Mkiwa – Itigi mpaka kwenda kule Rungwa kwenda mpaka Makongorosi. Barabara hii nayo imeshatajwa muda mrefu. Niiombe sana Serikali tutenge fedha barabara hii ikamilike ifungue fursa za uchumi katika mikoa yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo lile la Wilaya yangu pale Ikungi kuna barabara inaitwa Ikungi – Mang'onyi mpaka kule Kilimatinde. Barabara hii ni ya kiuchumi, kuna kampuni kubwa za madini zitalipa kodi. Niombe barabara hii iangaliwe namna ya kuwekewa lami ili iongeze fursa za uchumi katika eneo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilidhani nikieleza suala la barabara kwa nguvu sana pia nikumbushe barabara ile ya wenzetu kule Kahama, barabara ya Bulyankulu – Kahama, kilometa 51. Nayo ni barabara muhimu sana ya uchumi ili nayo ikiwekwa lami kwa sababu kodi tunapata nyingi kupitia madini itasaidia kuongeza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niendelee kusema tena barabara ni muhimu, miundombinu ni muhimu, naomba Serikali iweze kujenga barabara za lami ili kukuza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo, ninaunga mkono hoja iliyoko mbele yetu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Flatei Massay, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Isack, Mheshimiwa Selemani Zedi ajiandae.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipatia nafasi hii pia kwa kuzisemea barabara ambazo kimsingi zimeshakuwa kwenye ahadi za ilani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyofahamu ilani ni mkataba wetu sisi na wananchi na hasa kwa Chama Cha Mapinduzi ambapo 2015 kuja mwaka 2020 tuna barabara ambayo imewekwa kwenye Ilani ya Uchaguzi, barabara ya

Karatu – Haydom – Dongobesh kuja Singida kwenda Sibiti, Lalago.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeiona katika kitabu chetu hapa, na barabara hii imeahidiwa na Rais wetu mpendwa, Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kutoka 2015 kuja 2020. Lakini pia juzi Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Sita amekuja Dongobesh ameahidi barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni barabara moja tu iliyobaki ambayo inaunganisha mikoa minne ambayo haikujengwa kwa kiwango cha lami. Barabara hii inatoka Jimbo la Karatu kuja Jimbo la Mbulu Mji, maana yake inaunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini inatoka Mbulu Mjini kuja Haydom kwenda Singida, maana yake inaunganisha Mkoa wa Singida na Mkoa wa Manyara. Na kutoka pale inaelekea Maswa, maana yake unakutana na Mkoa tena ule wa Simiyu, na kwenda pia Shinyanga kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nieleze kwamba barabara hii ndiyo barabara iliyosahaulika moja kwa moja. Ni barabara chache mno ambazo hazikuunganishwa kwa lami kwa mikoa hii. Kwa hiyo, masikitiko yangu nataka nioneshe Mheshimiwa Waziri aelewe.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Yahaya Massare.

**T A A R I F A**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu kumpa taarifa mchangiaji anayechangia sasa hivi, Mheshimiwa Flatei, si barabara hiyo tu iliyosahaulika, ni

pamoja na barabara ya Mkiwa – Itigi – Rungwa – Makongorosi kutokea upande wa Mkoa wa Singida, imesahaulika toka Uhuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naona taarifa za nyongeza za barabara. Sasa sijajua na mimi nikupe taarifa nyongeza ya barabara nyingine; Mheshimiwa Flatei Massay, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii ya Mheshimiwa Massare naipokea kwa moyo mweupe, na ile ya kwako naipokea kwa sababu najua kuna barabara imesahaulika ya kutoka pale Mbeya kwenda mpaka Tunduma kule, hali ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nieleze tu Waziri aelewe kwamba wameteuliwa na Mheshimiwa Rais sasa wamekuwa Mawaziri wako watatu, yaani Waziri na Manaibu wawili. Tangu Uhuru, Mbulu imeanzishwa 1905, haina barabara. Ukiangalia Mbulu kwa maeneo yote barabara ziko nyingi; barabara ya kutoka Dongobesh kwenda Babati, kilometa 63, imeahidiwa pale iko kwenye ilani, hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, na tunapouliza maswali, mimi nimeleta barabara hii mara 20 ndani ya Bunge hili, nimeuliza maswali 20, nimechangia kwenye mchango wa namna hii ninavyoongea hii ni mara ya tano. Na barabara hii acha tu nikwambie, ina magari mengi. Na kwa uchumi wa watu wa Mbulu, Singida, Karatu, Simiyu, Meatu, hakuna namna yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe, mara ya kwanza nimekuja kusema barabara hii nikaambiwa iko kwenye upembuzi wa awali, nikatulia. Nimekuja 2017 wakasema iko kwenye upembuzi wa kati, nikatulia. Nimekuja tena wakasema iko kwenye upembuzi yakinifu, nikatulia. Juzi hapa wananiambia sasa iko kwenye *design and building;* natuliaje sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mbulu wametutuma hapa kuhakikisha kwamba barabara hii inajengwa kwa kiwango cha lami. Sasa nikuombe unisikie leo; nifanyeje ile nieleweke? Kwenye ilani ipo, kwenye ahadi za Rais wetu ipo, wametuambia bajeti iliyopita iliwekwa kwenye kitabu cha bajeti inaonekana kilometa 50 zitajengwa kwa kiwango cha lami. Leo naona huku wamepunguza tena imekuja kilometa 25. Sasa nawaza kwa nini tunafanyiwa hivi. Kama rasilimali tunagawana katika Tanzania nchi yetu tugawane kwa usawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani, naitwa Flatei, Mbunge wa Mbulu, nimekuja huku niambie tufanyeje sasa. Kama tumetumwa, tumeeleza na uwakilishi upo eneo hili halijengwi. Leo naangalia kitabu cha bajeti hapa, sitaki kusema vibaya lakini mnielewe tu ndugu zangu kwangu hakuna barabara ya lami. Lakini wengine nimeona hapa siyo sahihi**,** wamewekewa bajeti ya kufanya ukarabati wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukarabati wa barabara, sisi hatujawahi kuiona barabara ya lami kabisa, wengine humu wana ukarabati. Kwa nini sisi tutakutana lini na changamoto hii kuisha? Wengine wana ukarabati; nini maana ya ukarabati? Wameshakaa na barabara, muda umefika hali yao imeshakuwa nzuri, barabara inakarabatiwa. Sisi ambao barabara hakuna hata kilometa moja lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri na Wizara ya Ujenzi ijue; nikipata nafasi kwenye kushika shilingi nitaishika mpaka ya mwisho ili kuhakikisha barabara hii inafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hii *password* ya kwamba kila siku upembuzi yakinifu, upembuzi wa awali, upembuzi wa kati; lini unaisha ili barabara hii ikajengwe kwa kiwango cha lami? Wananchi wanataka kusikia haya, wananchi wanataka kuona greda zinaanza kazi na barabara inajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nimeshaomba mara nyingi, kuna Hospitali kubwa ya Haydom kule, maeneo haya watu hawawezi kupita, barabara imeharibika. Ni kweli wanajenga, sikatai, wanajenga kwa maana ya *rough road,* lakini kila ikijengwa, kila mwaka lazima barabara ile ijengwe ya Haydom – Mbulu – Hydom – Sibiti – Lalago, kilometa 389.

Mheshimiwa Naibu Spika, nifanyeje? Ni mtaalam wa sarakasi, au niruhusu basi sasa hivi nipande hapo nipige sarakasi tatu, nne, ili Naibu Waziri na Waziri wajue kwamba huyu Mbunge amechukia. Niruhusu basi naomba. Nipige? Nipige sarakasi kadhaa hapa? Niruhusu, mimi najua Kanuni haziruhusu, basi niruhusu nipige wajue kwamba kwamba nimetumwa na wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini kuiomba barabara. Nipige?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay…

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipige?

**WABUNGE FULANI:** Piga!

**NAIBU SPIKA:** Usipige. Tunafahamu unajua sana kupiga sarakasi lakini…

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, najua sarakasi, sasa nafanyaje?

**NAIBU SPIKA:** Mimi nakulinda, usije ukaumia kwenye viti.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ilani ipo; ahadi ya Marais ipo; ahadi nyingine zipo; nipige? Mimi naomba nipige kabisa. Nipige? Maana hali ilishakuwa mbaya, wananchi wanataka barabara, Waziri haelewi; Haydom – Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti; nifanyeje? Kwenye ilani ipo, kwenye kila kitu ipo, nifanyaje? Nipige? Sasa nafanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri aje kwende *wind up* yake pale asiposema barabara hii anajenga lini kwa kweli humu ndani hatutaelewana, kama ni kuvunja sheria tutazivunja zote na kama kupiga nitapiga zote humu ndani. Haiwezekani wengine wapate barabara, sisi tunaongea kila siku habari ya barabara humu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia, twende moja kwa moja kwenye eneo lolote la bajeti hii. Wenzetu wana *billions* kadhaa, sisi tuna bilioni tano tu; itajenga barabara lini? Kilometa 389. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana, wewe ni mgeni lakini wamekuja wengi; amekuja Prof. Mbarawa kaona barabara ile, amekuja *Engineer* Nditiye kaona barabara ile, kaja Naibu Waziri kaona barabara ile, nampongeza amekuja kuona. Sasa akija kuona wananchi wanajua naam, barabara inajengwa, mwaka unapita, miaka inapita; inakuaje sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, *principles* zetu ni kwamba iko kwenye ilani, *principles* zetu ni kwamba ahadi za wananchi, *principles* zetu ni kwamba Marais wameahidi, sasa mama Samia Suluhu Hassan niwaambie ni mama mzuri sana, kashaahidi. Na amesema kazi iendelee. Sasa kazi inaendelea kwingine, Mbulu Vijijini haiendelei? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwaka huu wa fedha barabara mtangaze ili ijengwe ili wananchi wale ambao miaka yote wamekuwa wakitutuma humu, ametumwa Maru amekaa miaka 25 hakupewa; katumwa Akunayi naye kaka hakupewa, tumetumwa mimi na Issaay, tusipewe tena?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mungu awabariki. Sasa sijui niunge mkono, sijui niache? Naunga mkono kwa shida sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako...

**NAIBU SPIKA:** Kanuni?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 76. Naomba mwongozo wako kwa sababu hii bajeti tunayojadili ni bajeti muhimu sana na haya tunayowaambia tunaiambia Serikali na Serikali ni mtambuka. Humu ndani tuna Mawaziri sita tu, na Naibu Mawaziri wako saba tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kama haya mambo ya kutokupeleka fedha kwenye bajeti yanahusu Wizara ya Fedha; kuna mambo mengine ya vibali vya ujenzi, *GN* na nini, inahusu mambo ya Mazingira na nini. Lakini humu tuna Mawaziri sita tu na Naibu Mawaziri wako saba tu; haya mambo yanakwendaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Zuberi Kuchauka akiomba Mwongozo wa Kiti kuhusu kuwepo kwa baadhi ya Mawaziri hapa na wengine yeye hawaoni, kwa hiyo, anajiuliza yaani haya tunayozungumza je na wao watayachukua kwa uzito wa namna hii?

Waheshimiwa Wabunge, kwanza, kama alivyosema yeye mwenyewe ni kwamba Serikali ni moja, kwa hiyo, anayesikiliza atafikisha huo ujumbe; moja. Lakini la pili, hata mimi wakati nazungumza nimeeleza hapa kuhusu Waziri wa Ujenzi lakini nikasema pia Waziri wa TAMISEMI, najua nini, humu ndani lazima Waziri wa TAMISEMI atapata taarifa kwamba yeye na Waziri wa Ujenzi wanahitajika kwenda Mbeya.

Maana yake ni nini; hapa tulimsoma Mheshimiwa William Lukuvi, kwamba ndiye msimamizi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Waziri Mkuu hayupo. Kwa hiyo, madam yeye amekaa pale, uwe na uhakika kwamba shughuli zote za Serikali humu ndani zinao usimamizi. Kwa hiyo ujumbe wataupata kila mtu vile unavyostahili. (*Makofi)*

Kwa hiyo, hata mpiga sarakasi ujumbe wake utafika kwenye sehemu inayotakiwa kwa sababu miundombinu anayosema hizi ni zile barabara kubwa. Lakini barabara kubwa haziwezi kufanya kazi peke yake bila barabara ndogo ambazo ni za TAMISEMI. Kwa hiyo, wakati wa TAMISEMI Waziri wa Ujenzi na Manaibu wake walikuwa wanasikiliza kwamba hizi barabara wanazozisema Wabunge zinailisha barabara gani kubwa.

Na sasa na yeye anaposikiliza kuhusu barabara kubwa anazoeleza Mbunge yeyote, barabara kubwa au kama hivi tunavyosema ujenzi wa reli na vitu kama hivyo, wao kama Serikali wanafahamu ni barabara zipi zitatakiwa kulishana namna hiyo.

Kwa hiyo msiwe na wasiwasi Waheshimiwa Wabunge michango yenu ndiyo maana huwa mnazungumza na mimi hapa mbele, na ndiyo kazi yangu. Mnazungumza na mimi, ukishazungumza na mimi usiwe na wasiwasi, hata kama Waziri wa Ujenzi hakuwepo hapa ujumbe ataupata. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Francis Isack, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Zedi, Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe ajiandae.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kupata nafasi hii muhimu sana ya kuchangia Wizara ambayo inabeba uchumi wa nchi hii. Kwa sababu miundombinu ndiyo inayobeba kila kitu; mazao, *products* za viwanda na kila kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwanza kwenye jimbo langu. Jimbo langu kwa barabara za

*TANROADS* ina mtandao wa kilometa zipatazo 234.5, lakini katika mtandao huu neno lami kwetu sisi ni msamiati kwa sababu kuna kilometa 2.5 tu tena tumezibahatisha tu kwa ile barabara inayokwenda Mwanza kwa kuibia kidogo pale Igugulu, kilometa mbili katika mtandao mzima wa barabara za *TANROADS,* kilometa 234. Sisi watu wa Mkalama lami kwetu ni msamiati.

Mheshimiwa Naibu Spika, na katika barabara za *TARURA,* takribani kilometa 647 mtandao, hatuna hata robo kilometa ya lami. Sasa tunapofika kwenye suala hili la bajeti kama mwenzangu alivyotaka kuruka sarakasi hapa kwa kweli haka kamgawanyo ka bajeti katika nchi hii inabidi sasa kawe kanaangaliwa kwa vipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu wakati wenzetu wanaomba bajeti za kuziba viraka vya lami ambazo wameshazitumia mpaka zimechakaa sasa wanataka wazibe, sisi hatuna hata kipande cha lami. Kwa hiyo, inapofika wakati huu kwa kweli sisi tunaporudi kwa wananchi wetu wanatuuliza hivi ninyi Bungeni kule mna nchi yenu tofauti, mbona wenzenu wana lami za kutosha, sisi tutatembea kwa vumbi mpaka lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unapofika wakati huu wa kugawa hizi bajeti lazima tuangalie vipaumbele. Hii habari ya kusema fedha zikipatikana zitajengwa, fedha zikipatikana, sisi mnatupa wakati mgumu, na sisi tuna wananchi ambao wanataka kula matunda ya nchi yao nzuri inayoongozwa na mama yetu Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ipo barabara ambayo ipo kwenye Ilani, inayoanzia pale Iguguno inapita kwenye Makao Makuu ya Wilaya Nduguti inakwenda mpaka Simiyu kupitia daraja la Sibiti ambalo limejengwa kwa fedha nyingi za nchi hii. Barabara hii ukiacha tu kwamba inaunganisha mikoa miwili; Mkoa wa Simiyu na Mkoa wa Singida na wote tunatambua kwamba Mkoa wa Singida ndiyo Mkoa ambao unalima Alizeti kwa wingi na ninyi mnafahamu tatizo kubwa la mafuta katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile wote mnafahamu kwamba Mkoa wa Simiyu ni miongoni mwa mikoa mikubwa inayolima Pamba katika nchi hii. Kwa hiyo, tunapoongelea barabara hii ya Simiyu – Singida kuunganishwa kwa lami, tunaongelea uchumi wa nchi hii. Tunaongelea kuondoa changamoto za nchi hii. Kwa hiyo, naomba katika vipaumbele vya Wizara barabara hii ambayo ipo kwenye Ilani inayounganisha mikoa; hii sera ya kuunganisha mikoa ilianza tangu Awamu ya Nne, sisi bado hatujaunganishwa kati ya Mkoa wa Simiyu na Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba barabara hii iwekwe kwenye umuhimu wa kipaumbele, hii habari ya kusubiri, najua Mheshimiwa Waziri anaweza akaja na majibu mepesi tu, kwamba fedha ikipatikana; naomba aje na majibu yanayoeleweka katika barabara hii ili nasi tuondoke kwenye unyonge wa kutokuwa na lami. Kwa kuanzia basi, angalau kwa kipaumbele, hata zile kilometa 42 tu za kutoka Iguguno mpaka Makao Makuu ya Wilaya zipate lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Singida Wilaya pekee ya Mkalama ndiyo inayounganishwa na vumbi na Makao Makuu ya Mkoa. Hata kwenye Kamati pale nimesikia wanasema vipaumbele, Makao Makuu ya Wilaya, kuunganishwa na Mkoa kwa lami. Kwa hiyo, angalau hizi 42 basi zije kwa bajeti ya dharura angalau tupate kilometa 42 za lami kutoka Makao Makuu ya Wilaya mpaka Makao Makuu ya Mkoa, kwa kuanzia katika barabara hii ambayo ipo kwenye Ilani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami sitaruka sarakasi, lakini kwenye kushika shilingi nikipata nafasi kama hamjaja na maneno mazuri kuhusu barabara hii kwa kweli tutaungana na Mheshimiwa Flatei, yeye akiruka sarakasi mimi nagaragara chini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nirudi kwenye Jimbo langu. Lipo daraja linajengwa katika Mto Ndurumo, daraja la msingi; daraja lile linasuasua sana. Waziri sijui kama litaisha na ni muhimu sana, lakini kwa sababu daraja lile

linaendelea, pale kuna daraja la dharura la jeshi ambalo linatumika. Namwomba Mheshimiwa Waziri na Walinzi wa Ulinzi pia, daraja lile la jeshi ambalo lipo pale, baada ya daraja kubwa kukamilika, daraja lile liendelee kuhifadhiwa kwa udharura wake ndani ya Mkalama, lisiondoke kwa sababu lipo bonde kubwa la mto ambalo linatenganisha vijiji karibu vitatu; vya Yulansoni, Lelembwe na Mulumba ambapo wanakuwa kisiwani wakati wa masika na watoto wanakufa wakati wa kwenda shuleni kule Katani ambapo Kata ipo Kinyangire na bonde lile linatenganisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba daraja lile la jeshi liendelee kuhifadhiwa kwa udharura wake, lakini ndani ya Mkalama lipelekwe katika bonde hili la Yulansoni. Wananchi wa eneo lile wana uchumi mkubwa lakini barabara imekuwa ni shida na hatuna kivuko. Kwa hiyo, daraja lile la jeshi litakapokamilika daraja hili kubwa, libaki pale Mkalama katika eneo la Yulansoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye eneo pia la *TANROAD.* Najiuliza sana, *TANROAD* kila mkoa wapo na wanapata bajeti, lakini pale kwangu Mheshimiwa Flatei alikuwa analalamika kwamba barabara zake ni za vumbi, lakini mimi ninapotoka Mkalama naenda kwa jirani yangu Manyara, kwa Mheshimiwa Flatei; ninapotembea na barabara za vumbi za Mkoa wa Singida, unapofika tu, "Sasa unaingia Manyara," nakutana na utofauti kabisa wa barabara; za kwangu za *TANROAD* Singida zina mashimo, lakini ukiingia *TANROAD* Manyara unakuta nzuri. Kwa hiyo, nikaona hapa kuna uzembe katika suala la kusimamia Wakandarasi wanaokarabati hizi barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri mwangalie vizuri Meneja wa *TANROAD* Singida, ukarabati wa barabara za *TANROAD* mkoa wangu wa Singida zifanyike vizuri kwa fedha ndogo inayopatikana. Hata *timing* ya kutengeneza hizi barabara; unakuta barabara inatengenezwa wakati wa mvua. Bado hata Mkandarasi hajaondoka, ile iliyotengenezwa imeshabebwa na maji. Sasa sijui hizi *program* zao za utengenezaji zimekaaje! Naomba

ziangaliwe vizuri; na kile kidogo cha ukarabati kinachofanyika kiweze kudumu na wananchi wafurahie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ile imetengenezwa juzi tu pale, sasa hivi ni mashimo, lakini ukiingia Manyara unakuta barabara safi. Hii inaonyesha kabisa kuna uzembe katika suala la utendaji. Wengine wanafanya vizuri, fedha ni hiyo hiyo, usimamizi unakuwa mbovu. Naomba hili lifike na walisikie, najua watakuwa wameshalisikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuongelea jimbo sasa niuongelee mkoa wangu. Singida tuna uwanja wa ndege na kwa bahati nzuri katika hotuba ya Rais iliyopita uliongelewa ni katika viwanja 11 vitakavyojengwa. Nataka niombe, katika vile viwanja 11, Uwanja wa Mkoa wa Singida unatakiwa upewe kipaumbele cha pekee, kwa sababu ni uwanja ulio jirani na Makao Makuu ya Nchi. Uchukuliwe kama uwanja wa dharura, pale inapotokea tatizo katika Uwanja wa Makao Makuu ya Nchi, uwanja wa dharura ulio karibu unapaswa kuwa uwanja wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ikitokea tatizo, ndege inabidi irudi Dar es Salaam kilometa zaidi ya 500, wakati hapa Singida ni kilometa 240. Kwa hiyo, naomba Wizara iangalie uwanja wa Mkoa wa Singida kama uwanja wa dharura. Hii ni Makao Makuu ya Nchi, wanatua Mabalozi hapa, wanatua Marais wa nchi mbalimbali hapa; litakapotokea tatizo lolote la kianga, uwanja pekee wa dharura ni uwanja wa Singida.

Kwa hiyo, naomba uwanja huu katika vile viwanja 11 wenyewe utazamwe kwa jicho la tofauti kama uwanja wa *emergence* pale linapotokea tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nisisitize hilo katika suala la Mkoa wangu wa Singida. Nawashukuru sana, najua ujumbe umefika. Kama ambavyo nimesema, Mheshimiwa Flatei akiruka, mimi nitagaragara, namwomba Mheshimiwa Waziri aje na majibu ya kutosha katika maeneo haya ya Mkoa wangu wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Napata picha, itabidi tumwombe Mheshimiwa Waziri wakati wa kugaragara watu wakafanyie pale nje; itabidi mtoke naye mkamwonyeshe namna ya kugaragara hapo nje. Mheshimiwa Selemani Zedi atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka ajiandae. *(Kicheko)*

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia kwenye bajeti hii muhimu sana inayohusu barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema ikiwemo na wewe mwenyewe, kila mwaka wakati wa bajeti tunakuja hapa, tunajadili na kupitisha orodha ndefu ya barabara, lakini mwaka ukiisha unakuta hata robo ya hizo barabara hazijafanyiwa kazi. Hii imekuwa ni desturi ya miaka yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafikiri nishauri, tujaribu mwaka huu kwa sababu kuliko kuwa na orodha ya barabara 200 ambazo hatuna uwezo wa kuzishughulikia ni afadhali tukawa na barabara hata 50 tu kwa mwaka ambazo tunajua tuna uwezo halafu tukapanga *priority* tukaona ipi ianze na ipi ifuatie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo umesema, nashauri kwamba mwaka huu fedha tutakazozipitisha kwa ajili ya ujenzi wa barabara mwisho wa bajeti wakati tunapitisha sheria ya fedha ile *Finance Bill,* tuweke kipengele fulani cha kuzi-*ringfence* kwamba mwaka huu fedha zitakazotengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara lazima zote zitoke na zikafanye kazi ya kujenga barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mwaka huu wa fedha tulionao unaoisha mwezi ujao, tulipitisha shilingi

trilioni 1.5 kwa ajili ya barabara, lakini mpaka sasa fedha ambazo zimekwenda ni shilingi bilioni 900 tu. Kwa hiyo, kuna shilingi bilioni 600 ambazo hazikwenda kujenga barabara. Sasa hizi shilingi bilioni 600 ambazo hazikwenda kwa mujibu wa taarifa ya Kamati maana yake ni orodha ya barabara ambazo hazikushughulikiwa na ambazo wala hazitafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwangu kuna barabara ile ya Tabora – Mwambali – Bukene – Kagongwa, inaunganisha Mkoa wa Tabora na Kahama, mwaka huu wa fedha unaoisha mwezi ujao, tulitengewa fedha na ikasemwa kwamba itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Ukiwa umebaki mwezi mmoja, hakuna chochote kilichofanyika. Hakuna hata shilingi iliyopelekwa kwa ajili ya kufanya shughuli yoyote na mwaka huu nimepitia randama, barabara ile ile tena imetengewa fedha na maelezo ni yale yale kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama mwaka tunaoumalizia ilitengewa fedha, tukapitisha na hakuna chochote kilichochafanyika, nitaaminije kwamba hizi sasa zilizotengwa zitakwenda kufanya kazi? Kwa sababu yatakuwa yale yale!

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nashauri kwamba kuliko kuwa na orodha ya barabara nyingi na tunatenga fedha nyingi, lakini mwisho wa mwaka hakuna kinachofanyika, kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wengine waliotangulia, ni afadhali tuwe na barabara chache kwa kipaumbele maalum, ambapo tunajua tutaweza kuzi-*finance* ili ziweze kushughulikiwa badala ya kuwa tunapitisha bajeti, tunaondoka na matumaini makubwa, tunafika huko tunawapa matumaini wananchi wetu, lakini mwisho wa siku hakuna chochote ambacho kimefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara, kwamba kwa mfano kwenye hii barabara yangu, ukienda kuulizia *TANROAD* Tabora wanakwambia Wizara haijatupa kibali cha

kuajiri Mkandarasi au cha ku-*float tender.* Sasa fedha mwaka huu unaisha zimetengwa, bado mwezi mmoja, kwa mwaka ujao zimetengwa tena. Naiomba Wizara, safari hii toeni kibali kwa *TANROADS* Tabora ili iweze ku-*float tender*, kuitangaza ili tuweze kupata mkandarasi aweze kujenga barabara hii muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu shughuli ambazo zinahitajika kufanyika ni kulipa fidia kwa wananchi ambao wameshapimiwa muda mrefu ili wapishe ujenzi na gharama ya ku-*float tender*, kui-*engage* wakandarasi ili mkandarasi aweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyosema kwamba barabara kubwa haiwezi kufanya kazi bila zile *feeder road* zinazotoka vijijini, Jimbo langu nimekuwa nikisema mara nyingi, barabara zinazotoka ndani mashambani ambapo ndipo mazao yanapatikana kwa ajili ya biashara, ni mbovu, haziko vizuri. Kwa hiyo, hii nayo inapokuwa haifanyiwi kazi, basi hali inazidi kuwa mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara, barabara hii ndiyo ambayo inapita mahali ambapo mradi mkubwa wa kujenga *coating yard* kwa ajili ya mabomba yanayotoa mafuta Hoima - Uganda mpaka Tanga ndipo ile *yard* kubwa itajengwa pale. Kwa hiyo, barabara hii ndiyo itapitisha mabomba yote yatakayokwenda kupakwa ile rangi maalum ili yakifukiwa chini yasioze; mabomba yote ya kutoka Uganda mpaka Tanga, ile shughuli itafanyikia jimboni kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, barabara hii nashauri Wizara, mkae na Wizara ya Nishati, wale wenye *project* hii wana-*finance* baadhi ya huduma ambazo zinakuja pale, kwa mfano umeme unaokuja pale unakuwa *financed* na *project* hii, maji yanayokuja pale yanakuwa *financed* na *project* hii. Kwa hiyo, hata barabara kwa sababu hayo mabomba yakifika Nzega lazima yachepuke na yaende kama kilometa 40 ndani ya barabara hii ndiyo yafike kwenye hiyo *yard. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mnaweza kukaa na Wizara ya Nishati mkazungumza ili sehemu hiyo ya kilometa 40 kutoka Nzega Mjini mpaka kwenye hiyo *yard,* ili muweze kushirikiana na mwone namna gani mtaijenga kwa kutumia gharama za pamoja. Kwa hiyo huo ni ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na hotuba ya Wizara pamoja na hotuba ya Kamati kuhusu ujenzi wa *SGR* na kile kipande cha kutoka Tabora mpaka Isaka pale katikati kuna *station* kubwa sana ya Bukene ambayo siku zote imekuwa ni *station* kubwa na ndiyo inahudumia Wilaya nzima ya Nzega na Igunga. Kwa hiyo, pale ni lazima kuwe na *logistic* kubwa ya kushusha mizigo kwa ajili ya Nzega yote na Igunga yote kwenye huu mradi wa *SGR*. Sisi kwetu jambo hilo likifanyika maana yake ni ajira kwa wananchi na vijana wa maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. Hata hivyo, nashauri kwamba mwishoni wakati wa *Finance Bill* tuweke kipengele kwamba fedha zitakazotengwa kwa ajili ya barabara ziwe *ringfenced* na zote zipatikane ziende kwenye miradi ya barabara ili kwa mwaka huu tuangalie *effect* yake kwa mwaka mmoja, badala ya kutenga shilingi trilioni 1.5 halafu zinaenda shilingi milioni 900, halafu shilingi bilioni 600 zote hazijaenda na barabara zinakuwa hazijashughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe. atafuatiwa na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka na Mheshimiwa Yahaya Massare ajiandae.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kwa utangulizi nikushukuru sana wewe mwenyewe, Naibu Waziri wa Maji na Mheshimiwa Suma Fyandomo na Bahati kwa kwenda kuwaona wahanga wa mafuriko kule Ipinda. Wanawashukuru sana.

Mlichokifanya ni kitendo cha utu Mungu aendelee kuwabariki. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nikushukuru kwa utangulizi ulioanza nao na ninaomba hata katika hotuba yangu basi haya mambo yaingizwe moja kwa moja kwamba nami nayasema kama ulivyoyasema. Kitendo cha ugawanyaji rasilimali yetu, kufuatana na umuhimu wa sehemu ambapo barabara na sehemu za uchukuzi unaenda ni kitendo ambacho kinatakiwa kizingatiwe sana na Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejipanga nizungumzie mambo machache. La kwanza, ni suala la Serikali yetu kutimiza wajibu wake. Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi nataka nikiri inatimiza wajibu wake ipasavyo. Hata hivyo: Je, watendaji wetu wanafanya kazi zinazotakiwa? Hapana. Maana Serikali yetu inatoa fedha za matengenezo ya barabara kupitia Mfuko wa Barabara na kwa kweli zinatoka vizuri, lakini wenzetu wanaoenda kuzitumia hizi fedha wanafanya kazi ambayo kwa kweli wanaiaibisha taaluma ya Uhandisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo barabara nyingi, lakini nitatolea mfano barabara chache tu. Haiingii akilini, barabara inafanyiwa matengenezo, hapa kiraka kinachimbwa, wanatengeneza, lakini ukikaa siku mbili, ukirudi tena hapo hapo unakuta shimo. Naomba tujiulize, tatizo liko wapi? Haya yanapoteza rasilimali zetu sehemu moja kutengenezwa mara mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, utakuta sehemu iliyotengenezwa ni hiyo hiyo, sehemu inayofuata nayo inaharibika hakuna hata mita moja, sentimita mbili hapo hapo shimo linatokea. Hii barabara tunayoipita ya kutoka Dodoma kuelekea Iringa, kwa kweli wakati mwingine hatutakiwi kuwasimulia hata watoto wadogo, watatushangaa kabisa. Namwomba Mheshimiwa Dkt. Chamuriho, Waziri wetu haya matatizo myaangalie yasiendelee tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ni suala la ubora wa barabara zetu ambazo zinajengwa. Unashangaa kuna barabara zimejengwa hazina hata miaka kumi, lakini wameshaanza kuweka viraka. Tatizo liko wapi ndugu zangu? Tunapofeli ni wapi? Hivi ma-*engineer* wetu wako wapi? Tatizo kubwa tunaanza kusingizia eti Mkandarasi ndiye anafanya hivyo. Siyo kweli. Naomba hapa Bunge hili tuelewane vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, anayefanya barabara yetu idumu na iwe nzuri ijengwe kwa viwango siyo mkandarasi, ni msimamizi *(consultant)*. Hao wanaajiriwa na Serikali yetu na wanasimama upande wa Serikali. Sasa nani alaumiwe hapa? Naomba sana, kuanzia sasa nashauri tuwe na *standard* za ujenzi wa barabara za Tanzania*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunashindwa kuweka *standards* zetu basi tudese. Tufanye tutengeneze desa, nami hilo desa ninalo Mheshimiwa Waziri. Desa lenyewe ni barabara ya kutoka Uyole kwenda Kasumuru. Kwa nini tusichukue kama mfano? Kwa nini tusichukue nyaraka zao tukazitumia kama *standard* ya ujenzi wa barabara za Tanzania? Barabara ile ndugu zangu imejengwa mimi nina ndevu moja; ipo. Mpaka nimefikisha ndevu nne, naiona, miaka zaidi ya thelathini ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya kutoka Iringa kwenda Igawa sasa hivi ina vipara na haitadumu zaidi hata ya miaka kumi ijayo. Naomba tutengeneze *standard* zetu. Barabara ile ndugu zangu ya Uyole Kasumulu, ikitengenezwa vizuri, ikisimamiwa vizuri ina uwezo wa kuishi miaka mingine kumi. Walijenga *SOGEA* nina uhakika nyaraka za barabara ile zipo, twendeni tuzichukue, tutengeneze, tuziweke vizuri, iwe ni *reference* ya ujenzi wa barabara zetu, kila nchi duniani ina *reference* ya ujenzi wa barabara zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee masuala ambayo yanaharibu barabara, mojawapo ni matuta, matuta barabarani yanaharibu barabara zetu. Ndio maana hata ukiangalia matuta yenyewe hayana hata *standard,* mengine yamekaa kama vichuguu, mengine

yamekaa utafikiri ni matuta ya mbatata sasa, tuelewe lipi na ndio maana nataka niseme barabara zetu matuta yanaziharibu. Kwa nini tusifanye utaratibu mwingine? Matuta yana athari nyingi sana kwa uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, linapokuwepo tuta ni lazima mtu akamate breki, vipuri vile vya breki hatutengenezi hapa nchini vinatoka nje tunatumia pesa zetu kununua vitu nje ya nchi. Uchumi wetu unapungua. Kila unaposimama ukikanyaga breki unapoanza kuendesha gari, gari linakula mafuta mara ishirini ya lilivyokuwa linatembea. Mafuta hatuna hapa, lakini kitaalam ile lami haiwezi ikastahimili mzigo unaosimama, inastahimili mzigo unaodundadunda. Kwa hiyo, naomba hebu tuachane na haya tutafute njia nyingine ya kuweka hata *box cover* tu watu wapite chini barabara ipite juu haitasumbua hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba nisemee kidogo barabara moja ambayo inatoka Ibanda kwenda Itungi *Port.* Meli zimejengwa tunaishukuru Serikali, lakini mpaka sasa meli zinashindwa kupata hata mafuta. Tarehe 13 -17 Aprili, gari la kupeleka mafuta kwenye meli limeshindwa kupita, kwa sababu barabara ni mbovu na barabara hii tangu mwezi wa Disemba, 2019 iko mezani kwa Mtendaji Mkuu atoe kibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sasa hivi inaenda kutengenezwa, naomba niishukuru Serikali, lakini zaidi ya yote naomba pia Serikali itusaidie watu wanaotembea na vimulimuli wameweka kwenye magari mbele pale kama vile na wao ni *rider,* jamani tunashindwa kutembea vizuri barabarani, tunaomba Serikali itoe tamko katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri mimi sio mtaalam wa barabara, kwa maana ya kwamba sio Mhandisi, lakini hiyo barabara iliyotajwa ya Uyole - Kasumulu nadhani na nyie mmeshapita mara kadhaa, kuna kipande

cha Wilaya ya Rungwe hasa na Mbeya Vijijini mvua inanyesha, ni mwezi mmoja tu ndio mvua hainyeshi, inanyesha mvua mwaka mzima, lakini barabara ni nzima hakuna hata shimo. Mashimo pekee yaliyotaka kutokeza ni ya uchaguzi wa mwaka 2015, kuna watu walichoma sehemu na yenyewe barabara haikuharibika yote, bado inapitika. Sasa huku kwingine barabara inatengenezwaje na mvua haipo miaka yote, hasa hiki kipande hiki cha Dodoma – Iringa nadhani watumiaji wa hiyo barabara watakubaliana kabisa na huyu mchangiaji. *(Makofi)*

Sasa hivi imeshafumuliwa kabisa kuna eneo kubwa kabisa sijui ni kilomita ngapi, lakini imebidi ifumuliwe kwa sababu kila mahali kuna matobo. Nadhani ni jambo ambalo inabidi kulitazama kwa mapana yake kwa sababu, mnapotengeneza barabara maeneo mengine, naamini mnatilia maanani udongo wa hizo sehemu na mambo kama hayo, mvua iko kiasi gani. Mtusaidie kwenye hilo eneo ili tupunguze ukarabati, twende kwenye kutengeneza barabara ambazo hazijawahi kutengenezwa kabisa.

Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahya Massare na Mheshimiwa Festo Sanga, ajiandae.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba nzuri iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri. Nimpongeze kwa hotuba nzuri, nipongeze Manaibu Waziri pamoja na watendaji wote. Sina shaka na uzoefu wa Mheshimiwa Waziri kwa kuwa alikuwepo kwenye Wizara hii kama Mtendaji Mkuu, kwa hiyo, ninaimani mambo mengi ambayo ameyaeleza hapa anayafahamu vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuongea kwenye barabara, kwa kweli kwenye bajeti hii ambayo imesomwa leo, barabara yetu ya Mbeya - Chunya - Makongorosi zimetengwa takribani bilioni 13, lakini hizi bilioni 13 hizi zote, zitaenda kuishia kwenda kulipa madeni ya wakandarasi ambao wamefanya hii kazi. Barabara hii imekamilika kutoka

Mbeya mpaka Chunya na sasa hivi inaendelea Chunya – Makongorosi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipande cha Mbeya – Chunya kimeshakuwa na mashimo, tumeshakuwa na viraka. Mheshimiwa Waziri alikuja wiki mbili zilizopita alikuja akaona na nilimwambia kwamba, *standard* za barabara anazojenga inakuwaje na hii barabara toka imekamilika ina miaka karibu mitatu tu na hii bado iko chini ya uangalizi wa mkandarasi, lakini tayari imeshakuwa na viraka, sasa sijui miaka mitano mbele itakuwaje. Kwa kweli sisi watu wa Chunya tulihitaji sana hii barabara kwa kiwango cha lami, lakini kiwango ambacho kilijengwa mpaka sasa hivi tuna wasiwasi zaidi ya miaka mitano inayokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo na mimi nitoe ushauri *standard* za viwango vya barabara za *TANROADS* ziwe kimoja ile *layer* ya juu inayojengwa iwe moja kwa barabara zote za *TANROADS.* Sio barabara hii inawekwa tabaka hili na barabara nyingine inamwagwa tu lami na baadaye zinawekwa kokoto juu, kwa hiyo magari yakija kupita barabara zile zinakuwa na mashimo. Pia tujue kwamba barabara ya lami inapokuwa imetengenezwa eneo Fulani, maana yake matumizi ya ile barabara yanaongezeka, kama ilivyo kwa barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi. Barabara hii waliweka makadirio ya chini ya kupita magari, sasa hivi magari ni mengi mno ndio maana imeanza kuwa na viraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ujenzi wa barabara ya kuanzia Makongorosi – Rungwa – Mkiwa, hii imekuwa *story* sasa ya muda mrefu, kila siku inazungumzwa hii barabara, kila siku upembuzi yakinifu unaendelea. Kwenye bajeti hii zimetengwa hapa kuanzia Makongorosi – Rungwa wameonyesha hapa kilomita 50, lakini bado wanasema mpaka fedha zitakapopatikana! Pia kama hiyo haitoshi, hata upande wa kuanzia Ipole kuja mpaka Rungwa hivyo hivyo zimetengwa kiasi cha kilometa 56, lakini mpaka fedha zitakapopatikana. Kwa hiyo, kwa mtindo huu hatuwezi kwenda tukafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi barabara zimeahidiwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, tumeinadi Ilani hii kwa nguvu zote, tumewaaminisha na kuwaambia wananchi wetu. Kama fedha hazipatikani maana yake tutarudi kule kule kila siku. Sasa najiuliza hapa, sisi watu wa Mkoa wa Mbeya sisi tulikosea wapi? Maana yake barabara ya kuanzia Igawa - Mbeya Mjini mpaka Tunduma, hivyo hivyo fedha hakuna. Barabara za kuanzia Mbeya Mjini kwenda Makongorosi mpaka Rungwa, fedha hakuna. Vilevile ya Makongorosi, Mkwajuni mpaka Mbalizi, fedha hakuna na ndugu yangu Mheshimiwa Ally amezungumza ya kwenda mpaka Kasumulu kule, fedha hakuna. Sisi Mbeya kuna mradi gani wa barabara ambao fedha imetengwa kwa mwaka huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri, sisi watu wa Mbeya tuna shida sana ya hizi barabara. Naomba waangalie vizuri bajeti hii angalau na sisi watu wa Chunya kuanzia Makongorosi ili na sisi watu wa Tarafa ya Kipembawe kule nao waweze kuona lami kwa mara ya kwanza. Naomba sana Waziri akayafanyie kazi haya, atakapokuwa anahitimisha hoja yake tuweze kupata majibu mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumze kidogo kwenye upande wa kiwanja cha ndege. Nimeona hapa kwenye bajeti hii nzuri ambayo Mheshimiwa Waziri ameisema ina maneno mazuri sana. Kiwanja chetu cha Songwe kimekuwa kila mwaka kinaongelewa habari ya kuwekwa taa, kila mwaka inaongelewa habari ya kuweka tabaka la juu, kila mwaka inaongelewa habari ya jengo la abiria na mwaka huu pia takribani karibu bilioni tisa zimetengwa, hatuna uhakika kwa maelezo ya miaka ya nyuma, je, hizi fedha zitatoka?

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba, kwa kiwango hiki cha pesa ambacho kimetengwa, badala ya mambo mengi kufanyika kwenye kile Kiwanja cha Songwe, basi angalau mambo mawili tu yafanyike. Liboreshwe jengo la abiria, lakini pia ziweze kutengenezwa zile taa za kutua

ndege pale, hayo mambo mengine ya kutengeneza fensi na mambo ya matabaka mengine yatafuata baadaye, ili twende awamu kwa awamu, kuliko fedha hiyo kidogo ambayo inatolewa yote iende kufanya kazi pale haitaonekana nini ambacho kimefanyika. Hii iende pia kwenye viwanja vingine ambavyo vimetengewa fedha kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze kidogo upande wa bandari. Bandari yetu hii kuna uwekezaji mkubwa sana umefanyika na kama tunavyojua, bandari ni lango kubwa la uchumi. Geti Na.1 mpaka Na.7 limeweza kutengenezwa, kina kimeweza kuongezwa na sasa hivi tunaona geti la Na.7 na Na.8 yanaendelea na Geti Na. 12 na Na. 13 yanaendelea na usanifu wake. Hii ni kazi nzuri, tuipongeze Serikali kwa namna nzuri ambayo inafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyojua kwa kuwa bandari ndio lango kuu, linachangia kwenye uchumi lakini pia linachangia kuleta ajira, pale kwenye bandari kuna taasisi nyingi takribani zaidi ya 30 ambazo zinaizunguka bandari yetu hii. Kwa hiyo bandari inaweza ikaonekana kwamba ufanisi wake ni mdogo kwa sababu tu hizi taasisi nyingine hazina ofisi palepale bandarini. Kwa hiyo, nashauri hizi taasisi nyingine hizi ziweze kuweka ofisi zao palepale bandarini na ikiwezekana kuwe na dirisha dogo moja ambalo taasisi zote zitakuwepo pale. Hapo ndipo ufanisi wa hii bandari utaweza kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru Waziri Mkuu alikuja juzi pale na akawaambia watu wa *TRA* wawe na ofisi palepale bandarini, sio mtu anatoka pale chini bandarini mpaka apande juu kule, tena arudi chini, tunapoteza muda pasipokuwa na sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kwa kuwa hii bandari inatoa mizigo na nchi jirani pia, nitoe angalizo, wenzetu wa Zambia wametengeneza sheria, hii sheria inataka mizigo yote inayosafirishwa kwenda Zambia iweze kutolewa na makampuni ya Kizambia yaani zile *clearing and forwarding*

lazima ziombewe zikiwa Zambia, mana yake kampuni za Kizambia ndio ziweze kupata hizi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kana kwamba hiyo haitoshi mpaka makampuni ya usafirishaji pia yale ya *logistic* lazima na yenyewe ya kutoka Zambia yaweze kufanya hivyo. Maana yake sasa sisi hapa makampuni yetu ya *clearing and forwarding* hayataweza kupata kazi, lakini pia na makampuni ya *logistic* hayawezi kupata kazi, sisi tutabakia na barabara yetu kuharibika, makampuni yote yatafanya kazi huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kengele ya pili imegonga, mengine nitaandika kwa maandishi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yahaya Masare atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Sanga na Mheshimiwa Njau Felista ajiandae.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nichangie katika Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi. Mimi ni muhanga wa barabara, ninyi ni mashahidi, nikisimama hapa ni kulalamika. Pamoja na kuanza hivi vibaya, lakini nataka niipongeze Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa utendaji mzuri sana wa kazi ambazo zinaonekana na wananchi wanaziona. Miundombinu inayojengwa na Serikali iko bora na kwa kiwango kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze sana *Engineer* Chamuriho kwa kupata nafasi hii ya Uwaziri katika Wizara hii. Hata hivyo, nataka nimtahadharishe kwamba amekalia kaa ambalo kidogo lina moto mkali, akifanya vizuri kama Wizara ya Maji inawezekana mwakani bajeti yake nayo ikawa nafuu. Watu wa maji wewe ni shahidi umekuwepo hapa toka 2015, bajeti ya maji, ilikuwa ni miongoni mwa bajeti ngumu kupitisha ukikaa kwenye hicho kiti. Leo bajeti iliyopita ya maji imejipambanua na watu wa nishati wamefanya kazi ambazo zinaonekana. Niombe sana Mawaziri hawa walioko hapa Mheshimiwa Chamuriho na Manaibu Waziri wawili,

waone mifano ya Wizara nyingine, walisimama katika kuhakikisha kazi zinafanyika na zinafanyika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kwangu ambayo nataka niizungumzie ni Barabara ya Mkiwa – Itigi - Noranga inaenda mpaka Mitundu hadi Rungwa. Upande wa Singida ziko kilomita 219, lakini ukiiunga barabara hii kwenda Makongorosi ambako ndio mkandarasi anaishia kuna kilomita 412 kama si 413, ndio barabara pekee iliyobaki nchi hii ya kuunganisha mkoa na mkoa ambayo ni ndefu kuliko zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya zaidi barabara hii imefumbiwa macho. Barabara hii mwaka 2017 ilitangazwa na ikapata mkandarasi na mkandarasi alishafika *site* akataka kuanza ujenzi. Bahati nzuri...

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Massare kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Hussein Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mchangiaji kwamba si barabara hiyo tu katika nchi hii, hata Mkoa wa Geita, Mwanza na Shinyanga kupitia Wilaya ya Nyangh'wale hakuna lami kabisa. *(Makofi)*

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa yake, lakini kilomita nyingi...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa yake, lakini kilomita nyingi za barabara za kuunganisha mkoa mmoja na mkoa mwingine ziko katika barabara hii. Barabara hii kutoka Mbeya kwenda Arusha kama mtu anasafiri kama ingekuwa lami huwezi kupita Dodoma ni barabara fupi na ambayo kiuchumi itainua

uchumi wa nchi hii. Barabara hii ilipotangazwa mwaka 2017 na ikapata mkandarasi, Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alikuja pale akagundua kwamba, katika mchakato ule wa zabuni kulikuwa na upigaji, akazuia barabara hii isiendelee kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayati Magufuli akataka wakae wazungumze *TANROADS* na mkandarasi kilomita ziongezeke kwa pesa ile au pesa zipunguzwe kwa kilomita zilizopo. Mwisho walishindana sijui walifikia wapi, inawezekana watu walishachukua chao hakukuwa na namna, ile *tender* ikafutwa. Mwaka 2020 Mheshimiwa Rais alipokuja kuomba kura pale kwa niaba ya chama chetu na kuniombea kura mimi na Wabunge wa Mkoa wa Singida, Itigi alizungumzia barabara hii kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami lakini ataweka wakandarasi wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunavyozungumza hapa imeonyeshwa ukurasa wa 36, lakini ukurasa wa 171 katika hotuba ya kitabu cha Waziri, lakini kilomita zinazoenda kujengwa inaonekana ni zile 56.9, lakini kwenye kutangazwa nina mashaka zinaweza zikatangazwa chini ya hapo. Niwaombe sana Wizara hii ili na sisi tusije kuwa wapiga kelele na kushika shilingi ya mshahara wa Mheshimiwa Waziri, atoe nafasi ya kutangaza kilomita za kutosha. Barabara ina kilomita 412 kutoka Makongorosi, akitangaza kilomita 20 au 25 ni miaka mingapi atajenga barabara hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana katika vitu ambavyo Waziri azingatie, Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* yuko hapa, anaijua ile barabara, aone namna ya kufanya barabara ya Makongorosi kuja Mkiwa kuunga Mkoa wa Singida na Mkoa wa Mbeya, inawekewa lami. Angalau kilomita zitoshetoshe hamsini hizi na zingine hamsini hata zikianzia kule kufika Rungwa itaonyesha kwamba Wizara ina dhamira njema ya kutenda haki. Wananchi wa mikoa mingine wasije wakasononeka kwamba wengine wanapendelewa na wengine hawapendelewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapopiga kura tunapigia kura Wabunge wa CCM, mimi nimetumwa hapa, lakini walituma Wabunge wengi kama mimi kwenye Bunge hili na waliondolewa na sababu kubwa walinyimwa kura kwa sababu ya barabara hii. Naomba sasa Mheshimiwa Chamuriho alinde kura zangu za mwaka 2025. Kama asipojenga barabara hii maana yake sasa yeye ndio atakuwa sababu ya mimi kutoka katika Bunge hili na sitokubali katika bajeti ijayo, hii nitakuwa mpole kidogo, nitashika shilingi tu kidogo, lakini ijayo sijui kama tutapita na bajeti ya Waziri hapa, naamini ataendelea kuwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe sasa Mheshimiwa Waziri ukaangalie barabara hii lakini kuna barabara ambazo zinaanzia Handeni, Kibalashi, Kiteto, Chemba, Kwamtoro hadi Singida. Barabara hii ambayo inaambatana na lile bomba la mafuta nayo ni barabara muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni barabara ambayo itakuja kuchechemea uchumi kwa sababu ya mahusiano yatakayokuwepo baina ya mikoa hii mitatu. Mkoa wa Singida, Mkoa wa Dodoma na Manyara lakini na Mkoa wa Tanga mikoa minne ambayo inapitiwa na hili bomba la mafuta. Na ile mikoa ya kule Geita, Shinyanga na Mwanza kule ambayo ukijumlisha inakuwa mikoa kama nane au tisa ambayo uchumi wa Nchi hii utaenda kuongezeka na hata makusanyo ya kodi yatapatikana lakini kama barabara ni mbaya mtu badala ya kulipa kodi kubwa atalipa kidogo kwasababu anachelewa kufika mahali ambako anatakiwa afike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja ambalo nitalichangia haraka haraka la ving'amuzi vya mabasi. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Richard Festo Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhe. Felista Deogratius Njau, kama hawa watakuwa wamemaliza mapema tutamalizia na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza kabisa nianze kwa kupongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri hasa kwenye mambo ya ujenzi. Nianze kwa kuchangia kwa kuzingatia mambo mawili kwanza hotuba ya Rais lakini pia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na pia nikijikita kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Nitajikita zaidi kwenye jimbo langu la Makete kwasababu ndipo ambako tuna changamoto kubwa ya barabara hasa hasa kutokana na kwamba sisi ndio wilaya pekee Nchini tuna miezi minane ambayo mvua inanyesha bila ya kusimama. Kwa hiyo Makete ina uhitaji mkubwa wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza nataka nizungumzie barabara ya kutoka Isyonji – Makete kwa maana ya kupitia Kitulo ambayo ukisoma kwenye ripoti kwa maana ya hotuba ya waziri ipo kwenye ukurasa namba 148 lakini ukisoma kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi iko kwenye ukurusa namba 74. Hii barabara kwanza niseme ni barabara ambayo Mheshimimiwa Rais aliagiza alipofika Makete akawaahidi wananchi kwamba barabara hii itajengwa tena Rais mwenyewe ni huyu huyu Mama Samia Suluhu Hassan akasema barabara hii itajengwa. Na niwaombe Mheshimiwa Waziri, ninajua kwamba ipo katika mkakatati wa kutangazwa barabara hii ili iweze kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini ninaizungumzia barabara ya Makete kutoka Isyonjo kuja Makete kupitia Kituro ni kwa sababu moja barabara hii ndio *oxygen* ya uchumi wa Wilaya ya Makete. Ni *oxygen* kwa mantiki ipi ni kwamba barabara hii inapita kwenye mbuga ya Kituro, hifadhi pekee ya tofauti kabisa ndani la Bara la Afrika, hifadhi ya Kituro inategemea barabara hii ya kutoka Isyonji kuja Makete. Lakini pia nazungumzia barabara hii ni kwa sababu, barabara hii ndio inabeba uchumi mzima wa wafanyabiashara wa Makete na kwa zaidi ya miaka 30, 40, 50 ambayo tangu nimezaliwa barabara hii wananchi wangu wanateseka kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili barabara hii ndio inapeleka karibia wagonjwa wote wanaotokea Mkoa wa

Mbeya kwenye hospitali bora za Nyanda za Juu Kusini, Hospitali ya Ikonda. Wagonjwa wengi wanatoka Mbeya wanapita pale lakini wengi wanafia njiani kutokana na changamoto ya barabara hii. Barabara hii ni kitovu cha uchumi wa Wilaya ya Makete.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri; kwa uhitaji mkubwa tulionao barabara hii ni vyema tangazo likatoka mapema wananchi wakatangaziwa kwamba barabara hii inaanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nizungumzie barabara nyingine, barabara kutoka Chimara, Matamba, Kitulo; kwanza nizungumze jambo moja kwamba Waheshimiwa Mawaziri hasa hasa Wizara ya Ujenzi, ukiangalia Wabunge wengi hapa wana ahadi nyingi za viongozi ni vyema Wizara ya Ujenzi ikawa na benki ya ahadi za vongozi kwa wananchi wetu. Kwa sababu gani? Viongozi wakubwa wa Serikali wanapokuja kuahidi hizi barabara wanafanya wananchi waamini kwamba hizi barabara tayari zinakwenda kujengwa. Barabara ya Chimala, Kitulo, Matamba ambao ni kilometa 51 ni ahadi ya Waziri Mkuu Pinda hadi leo hii haijawahi kujengwa. Sasa wananchi wa Matamba, wananchi wa Makete wanaamini kabisa Waziri Mkuu akisema ndio tayari imeshatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema wizara ikaanda benki ya *statistics* takwimu za ahadi zote za viongozi zilizotolewa kwenye majimbo mbalimbali ili tukawasaidia, tukawasaidia Wabunge hawa barabara hizo zitengenezwe. Ahadi ya Rais ni utekelezaji; kwa hiyo, ni vyema Wizara ya ujenzi ikaamua kufanya hicho kitu kuandaa takwimu zile ili kwenye bajeti hapa muweze kubeba pia viongozi wetu wa kitaifa wasionekane walivyoviahidi haviweze kutekelezeka. Zaidi ya miaka 10 ninayoizungumzia toka Mheshimiwa Pinda alipokuwa Waziri Mkuu hadi leo barabara ya Chimala, Matamba, Kitulo kilometa 51 tu, hadi leo hii haijajengwa. Kwa hiyo. niwaombe ni vyema mkaingalia barabara ile kwa jicho la ukaribu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kitu kingine nizungumzie barabara ya kimkakati ambayo inatoka Songea inakuja Ludewa, inapita Lupila inakuja Ikonda, inakuja hadi Bulongwa kwa maana kupitia Ruvuma hii ni barabara ambayo inapita kwenye mpaka kati ya Tanzania na Malawi. Ni barabara ya kimkakati niiombe Serikali na hasa hasa nimpongeze Meneja wangu wa Mkoa wa *TANROADS* Injinia wetu Sharua ni mama ambaye anachapa kazi sana pale Mkoa wa Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana kwasababu gani, changamoto ya mvua yote tunayoizungumzia lakini barabara kama hii haijawahi kuhudumiwa mama yule anapambana na mfuko wa fedha ni mdogo kwa maana ya *TANROADS* lakini mama yule anapambana usiku na mchana kuhakikisha kwamba barabara hizi zinajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe wizara muiangalie Mkoa wa Njombe kwa jicho la karibu miezi nane mvua zinanyesha mkoa huu barabara huwa zinafungwa takribani miezi mitatu, minne watu hawafanyi shughuli za kiuchumi na wakati sisi ni wazalishaji wakubwa wa mbao, wazalishaji wakubwa wa parachichi, wazalishaji wakubwa wa viazi vya *chips* ambavyo mnavitumia, mngetukumbuka ili tuweze kutumia mkoa wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili kule Makete kuna mradi mkubwa ambao unakuja wa ujenzi wa bwawa la Lumakalya, ukitoka kwenye lile bwawa kuja kuitafuta Mbeya ambako kutakuwa na *power plan*t ni zaidi ya kilometa 200 lakini hapo hapo kwenye lile bwawa unaweza ukatengeneza barabara fupi ya kilometa angalau 17 tu ambayo toka kipindi hicho Waziri Profesa Mwandosya anaipigania barabara ya kutoka Madiyani - Lufliyo kuelekea Tukuyu ni barabara fupi sana ambayo ingeweza kusaidia hata huu mradi mkubwa wa kimkakati wa umeme ukajengwa ili iweze kusaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Ujenzi, mtusaidie barabara hizi zijengwe. Kuna sehemu nimesema viongozi wangu, hakuna heshima yoyote ile ya Ubunge, na heshima ya Ubunge wangu yoyote ile haitokani na tai au suti nzuri nilizovaa ni hii miradi kuona inatekelezwa ndio heshima yangu ya Ubunge. Heshima ya Waziri haitokani na kusoma vizuri bajeti ni utekelezaji wa bajeti hizi, watu wengi wanalalamika hapa, kuona kwenye Ilani zimo, kwenye kitabu cha Rais imo, lakini kwenye kitabu pia cha waziri mwenye imo lakini barabara hizi zinaishia kwenye makaratasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, heshima ya bajeti kama hizi ni kuona zinatekelezwa, fedha zinatoka. Watu wametoa mawazo hapa kujenga miradi mikubwa ya zege ya matrilioni kwa *own source* tunaiumiza Nchi labda tuache mfumo huo twende kwenye mfumo ambayo hizi fedha za *own source* ziweze kusaidia kujenga barabara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Mheshimiwa Waziri, heshima yako itatokana na utekelezaji wa Ilani, heshima yangu na Ubunge wangu 2025 utagemeaje na kwamba barabara ya kutoka Makete kwenda Kitulo hadi kufika Isyonja imetekelezwa ndio heshima ya Ubunge wangu, heshima ya Ubunge wangu sio uzuri wa tai niliyonayo ni kuona kazi inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mambo mengi lakini barabara za Makete naamini zitakumbukwa kwenye wizara hii. Mungu abariki sana. Ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Felista Njau, tutamalizia na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika**,** ahsante sana, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie kwenye wizara hii muhimu. Ninapozungumzia kwenye ujenzi na uchukuzi moja kwa moja tunaelekeza kwenye mambo ya miundombinu kama barabara, reli na

vitu vinginevyo. Katika sekta hii, imeonesha kukua mfululizo ndani ya miaka minne, imekuwa ikikuwa kwa asilimia 14.4 tangu 2016/2017, 2020/2021. Hii sekta inakua bila kigugumizi pamoja na janga la *corona* lakini imeiongezea Nchi pato la Taifa asilimia 14.8. Hii ni sekta ya pili kwa kuongezea Nchi pato la Taifa ukitoka kilimo lakini kwa kukua imeibuka kinara sekta hii ni muhimu inahitaji jicho la tatu kwa mustakabali wa Taifa na maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaposema hivi ninaona kuna changamoto chache ambazo tunaweza tukizimaliza hii sekta inayoenda kukua na kuwa kinara na pato la Taifa litakuwa zaidi na mwananchi mmoja mmoja ataweza kumiliki uchumi. Nikisema hivyo, ninaweza kusema wakandarasi walioingia mkataba, wakandarasi waliosajiriwa kwenye nchi yetu asilimia 10 tu ndio wageni kwa nchi za nje, asilimia 10. Asilimia nyingine ni wazawa lakini ukifanya upembuzi pale unakuta asilimia 60 ya miradi mikubwa inashikiliwa na asilimia 10 ya wakandarasi wageni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashindwa kuwa wazalendo kwasababu Wakandarasi wetu hawakidhi vigezo, kigezo cha kwanza hawana mitaji, hawana mitaji mizuri kwahiyo hawawezi ku-*afford* kuweza kushika hii miradi mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine hawana ujuzi wa kutosha, hawana ujuzi wa kutosha kwa hiyo mwisho wa siku tunatakiwa tukae chini tuweze kuwawezesha wakandarasi wetu wawe na ujuzi wa kutosha ili kuweza ku-*afford* ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni vifaa vya ujenzi havikai kwenye *level* moja bei zake zinapanda na kushuka na *sometimes* hazipo kabisa. Kwa hiyo, mwisho wa siku hawa wataalam wetu wanashindwa kwenda kwenye ushindani wa wakandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapoongea haya ninasema kwasababu Wakandarasi wetu wakiweza kushika hizi tenda uchumi wa mtu mmoja mmoja ndani ya nchi yetu

utakua, lakini pato la Taifa litaongeza kwa sababu watu wetu watakkuwa na fedha mfukoni. Niishauri Serikali katika hili, tunavyoona namna hii tuweze kuwawezesha Wakandarasi wetu waweze kumiliki hii miradi mikubwa ili tuweze kuona matunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninapotoka mahali hapo, ninaona kabisa barabara nyingi, vilio vingi vya Wabunge humu ndani wanalia juu ya barabara, hawatoki kwenye reli wanaingia kwenye reli ya barabara kwa sababu ndio kero inayomgusa mwananchi wa kawaida kule chini vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zinazounganisha mikoa kwa mfano barabara zinazounganisha mikoa kuja Dar es Salaam, barabara hizi ni mbovu za mikoa ya kimkakati mikoa ya kilimo. Mikoa ya Njombe, ya Iringa, Mikoa ya Singida barabara hii si salama kwa hiyo wananchi wa kawaida hawawezi kuleta mazao yao Dar es Salaam. Wakifika Dar es Salaam wanakutana na adha nyingine ya mafuriko, Dar es Salaam miundombinu ya mafuriko hakuna mifereji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wanatengeneza mkakati huo wa barabara waangalie mifereji kwasababu maji haya ya mifereji yamekuwa ndio chanzo cha kukata barabara katika Mkoa wa Dar es Salaam. Lakini mafuriko ukifika Jangwani eneo lile la mkutano kuelekea Kariakoo pale hapapitiki wakati wa mvua ni kwa sababu hakuna miundombinu ya mifereji ambayo ni imara. Ukija barabara ya Tegeta kuelekea Bunju, Boko, Basihaya mifereji hakuna barabara zimejengwa zipo vizuri lakini unakuta magari yame-*stuck* hayawezi kutembea kwa sababu maji yanajaa barabarani, barabara zinakatika kuisababishia Serikali kupata hasara. *(Makofi)*

Mhwahimiwa Naibu Spika, tuone namna gani bora wakati tunapokwenda kuweka miundombinu ya barabara tuona namna bora ya kutengeneza mifereji. Jiji la Dar es Salaam halina miundombinu rafiki, ukiangalia Jiji la Dar es Salaam watu wanasema kuna lami lakini ni asilimia 14 tu ya

Jiji la Dar es Salaam wananchi wake wameunganishwa kwenye maji machafu, maji taka asilimia 14. Asilimia nyingine tunachanganyika na maji hayo hayo tunakunywa, magonjwa ya mlipuko Dar es Salaam, wanaotoka mikoani wanakutana nayo, basi ni vurugu tupu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali, wanajua Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri mnajua, miundombinu ya Dar es Salaam si rafiki kila siku watu wanaugua vipindupindu, wanaugua *UTI*, wanaugua magonjwa kadha wa kadha kwasababu tu ya miundombinu, lakini sio adha nyingine. Niombe kwa sababu ni kitovu cha biashara, twende tukaitengeneze Dar es Salaam na mikoa yake inayounganishwa kuja Dar es Salaam ili tuweze kuimarisha uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoongea hapa kuna wananchi wangu wa Ununio hawana pa kukaa, barabara hazina mifereji, watu wapo pembezoni wamekaa wametulia hawana pa kwenda mbele wala kurudi nyuma, nyuma zinaelea. Ni Dar es Salaam hapo sio mikoani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikiangalia kiini naona ni mitaro niiombe Serikali chonde chonde kipindi kilichopita niliongelea juu ya mitaro pale Nyamachabisi alikuja waziri kipindi kile nafikiri waziri wangu anafahamu. Alikuja kipindi kile Nyamachabisi miundombinu ya mitaro hakuna watu wanaelea. Niombe, niombe Serikali hii ya Mama Samia Suluhu Serikali Sikivu na Mawaziri wake waweze kuweka mikakati mizuri ili wananchi waweze kufanya biashara zao*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoongelea miundombinu, ninaongelea viwanda huwezi kuwa na viwanda imara kama huna miundombinu. Ninavyoongelea mbiundombinu ninaongelea kilimo, huwezi kuuza mazao yako ya kilimo kama huna miundombinu. ninapoongelea hiyo miundombinu naongelea uwekezaji, wawekezaji wanaanglia miundombinu ndio wanakuja kwenye nchi yetu. Naomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge mimi mwenyewe nilikuwa nasikiliza kwa umakini sana, Mbunge kutoka Dar es Salaam atazungumza nini kuhusu miundombinu lakini naona mmesikia mchango, tatizo la Dar es Salaam ni tofauti na sehemu nyingine tunazozungumza hapa ndani. Kwa hiyo, umefanya vizuri sana Mheshimiwa Felista Njau. Nilikuwa nimeshamwita Mheshimiwa Boniventura Kiswaga. *(Makofi)*

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya miundombinu. Kuna lugha pale mbele nilitoa, nilikosea kidogo ni ulimi tu nadhani itafutwa kwenye *Hansard* siwezi kuchongea wizara hii kubwa na muhimu kwa Taifa letu. Najua sisi Kiswahili tulikijua shuleni hatukukijua kabisa nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Waziri na Naibu Waziri wa Uchukuzi kwa sababu tunajua kwamba kabla ya kuwa Waziri alikuwa alikuwa Katibu Mkuu kwenye Wizara hii, miradi yote ambayo ameisimamia ni miradi ya kielekezo. Kwa hiyo, tunaamini kwamba kwenye bajeti yake kadri alivyojipanga atafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tumpongeze Katibu Mkuu na yeye tunajua kwamba yuko vizuri katika wizara hii na atafanya kazi vizuri sana. Pamoja na wasaidizi wao anayesimamia reli Bwana Kadogosa, anayesimamia bandari Bwana Erick, anayesimamia *TEMESA* Bwana Masele, anayesimamia ndege Bwana Majingi na anayesimamia Ndugu yangu Mfugale naye yupo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wowote duniani ili ukue unategemea miundombinu, miundombinu ya reli, miundombinu ya barabara, miundombinu ya ndege na meli. Kwa hiyo, ujenzi wa reli ya *Standard Gauge* ulivyoanza Dar es Salaam na Morogoro – Makutupora na sasa Mwanza – Isaka kuna ulazima wa haraka sana kuanza ujenzi wa reli kutoka Makutupora – Tabora na Tabora - Isaka ili kuhakikisha

kwamba vipande hivi vinakuwa na maana ya kuleta uchumi kwenye taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tutakapokamilisha kutoka Dar es Salaam mpaka Makutupora, tukikamilisha Mwanza – Isaka, tukawa na *gape* hapa katikati hatutakuwa tumejenga uchumi unaostahili katika Taifa letu. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais wakati anahubia Bunge alisema vipange vyote hivi vianze. Sasa niombe waziri mshaurini Mheshimiwa Rais hata kama ni mapato ya ndani, hata kama ni kukopa kwa sababu deni letu ni himilivu tukope ili tuweze kuunganisha vipade hivi ili tuweze kuleta uchumi kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji ndege ya mizigo, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliahidi kwamba atanunua ndege za mizigo. Wanalalamika sana watu wa Kusini wanaolima matunda, tunalalamika sana sisi wa Kanda ya Ziwa tunaosafirisha Samaki na matunda pamoja na mbogamboga tunahitaji ndege ya mizigo ili kuhakikisha kwamba biashara zinafanyika kutoa mazao yetu hapa na kwenda Nchi za Nje. Kwa hiyo, naamini kwamba msimamizi wa Shirika la Ndege ajiweke vizuri, aishauri vizuri Serikali ili tuhakikishe kwamba tunanunua ndege hiyo mpya ya mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba tunayo mahitaji makubwa sana ya barabara zetu kama ambavyo wenzangu wamesema. Nina barabara ya Magu, Bukwimba, Ngudu ambayo ipo kwenye Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 74 na hii barabara inahitaji kujengwa tu kwa sasa. Lakini nimeona kwenye hotuba ni kwamba Serikali inatafuta fedha hata mwaka jana Serikali ilikuwa inatafuta fedha. Ina maana utafutaji wa fedha huu haukamiliki? Barabara hii ikaweza kujengwa? Mwaka jana mmetafuta fedha na mwaka huu mnatafuta fedha, maana na mwaka kesho mtatafuta fedha, tunakamilisha lini hii barabara! Kwa sababu tunaamini kwamba baada ya *standard gauge* kukamilika hii barabara ndiyo itakayosafirisha shehena za mizigo kupeleka Nairobi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Tabasam.

**TAARIFA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimweleza msemaji, ni kwamba barabara hii ya Magu, Ngudu – Kwimba hadi Hungumalwa imeahidiwa na Marais wanne haijawahi kutokea katika nchi hii. Ameahidi marehemu Mkapa ameahidi, ameahidi Mheshimiwa Kikwete, ameahidi Mheshimiwa Marehemu Magufuli na ikaahidikiwa na Mheshimiwa Samia, haijawahi kutokea sasa nafiriki labda tu ifutwe. Mheshimiwa Kiswaga. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Tabasam tunaifutaje barabara. Mheshimiwa Kiswaga endelea.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono kufuta, lakini naunga mkono kwamba imeahidiwa na Marais wanne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sasa tupate hizo fedha, Lakini kuna barabara ya Magu mpaka Mahaha, barabara hii inafungua uchumi kutoka Simiyu mpaka Magu Mwanza iliahidiwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli mwaka 2015. Waziri ninakuomba barabara hii uione kwa macho mawili ili uweze kuitengea fedha itekelezwe kwa lami kwa sababu ni barabara muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwamba *design* sasa inaendelea barabara ya daraja pale Sukuma itatusaidia pia kuendeleza barabara hii. Tuna barabara ya Kisamba – Sayata, Simiyu hii ni barabara ambayo ina sifa za kuingizwa kwenye *TANROADS,* lakini haijaingizwa kwenye *TANROADS* miaka yote tunaomba pamoja na ya Kabila Isolo, Isawida kule Itilima hizi niombe tu waziri kama itakupendeza uzikasimu zihudumiwe na *TANROADS* kwa sababu uwezo wa

*TARURA* ni mdogo sana kusimamia hizo barabara. Nikuombe sana hizi barabara ni barabara muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina barabara kutoka *Nyanguge Airport*, barabara hii inapunguza msongamano kwa sababu ni barabara ambayo inatokea Musoma inapita Nyanguge kwenda Kayenze mpaka *Airport* inapunguza msongamano wa Jiji la Mwanza. Nalo hili liko kwenye upembuzi yakinifu na ninaamini kwamba imeshakamilika kwa ajili ya kuwekewa lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Ilani ya CCM ukurasa 83, tumeahidi kwamba tutatengeneza kivuko cha Ijinga – Kahangala. Ninashukuru kwenye hotuba ninaona kuna maandalizi kivuko hiki ni muhimu sana kwa wananchi wangu wa Ijinga na Kahangala pamoja na visiwa vyote vya Ukerewe ambavyo vina vua samaki pamoja na mazao mengine itasadia sana kusaidia wananchi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna daraja la Simiyu, daraja la Simiyu lile linaunganisha Simiyu na Mwanza katika barabara kuu ya kutoka Nairobi, Mwanza mpaka Rwanda, kwa hiyo, hili ni daraja muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona hapa maelezo hayajaniingia vizuri kichwani labda uangalie Mheshimiwa Waziri uone namna ya kulijenga daraja hili la Simiyu ili kuondoa adha ambayo wakati wote wananchi wanaosafiri watanzania wanapata shida sana. Ni pamoja na kukijenga kipande cha kutoka Nyanguge kwenda Ramadi kimeharibika kabisa na wewe unakijua hebu tuona namna ambavyo tunaweza kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana na niunge mkono hoja. Nawapongeza wote katika Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa Sehemu ya Kwanza ya Bunge letu kwa siku ya leo. Nadhani Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri

na Watendaji wake wapo hapa wanapata picha ya changamoto ya miundombinu Nchi hii. Na namuona Mheshimiwa Kuchauka ananiangalia napata picha mchango wake unaokuja unafananaje. Lakini ushauri wa jumla tu, kwasababu Serikali ni moja na hapa Wabunge huwa wanawaomba sana Mawaziri na Manaibu Mawaziri kuambatana nao kwenye majimbo yao, pengine ifike sehemu wakati mnaambatana nao kwenye majimbo yenu mpite zile barabara ambazo huwa mnasema kuna kukwama. Itawarahisishia ili Waziri akikwama kule atajua kuja kumueleza Mheshimiwa hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Kama ambavyo nilikwenda kwenye msiba wa Mheshimiwa Atashasta Nditiye Mwenyezi Mungu amrehemu na nikapita barabara ya kutoka Kigoma kuelekea Mbeya ambayo unapita Katavi. Barabara kutoka Malagalasi mpaka ufike Mpanda kilometa 402 yaani nikakwama njiani, giza likanikuta, tukafika usiku wa manane ile barabara ukiambiwa malori yamekwama barabarani na hakuna pa kupita maana yake angepita Waziri pale halafu akwame ndio angeelewa kwamba kuna maeneo yanatakiwa kupelekwa angalau vipande vya hiyo barabara. *(Makofi)*

Hata kama sitoki huko lakini kitendo cha kupita ile barabara napata picha yaani mtu akisema ile barabara ni ya muhimu napata picha anamaanisha nini. Malori yana bidhaa nini yamekwama njiani na pale ndipo nilipokumbuka maana ya Zaburi ya 23 yaani Bonde la uvuli wa mauti ule usiku ule nikawa nimeelewa vizuri sana huo mstari. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa Kumi na Moja Kamili Jioni leo.

*(Saa 07.04 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

## HOJA ZA SERIKALI

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano na baadhi ya majina ambayo hayakupata nafasi ya kuchangia asubuhi watachangia mchana huu. Tutaanza na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, simwoni. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa... Aah, umekaa kwenye kiti siyo chako. Sasa sijui kama unaweza kuchangia hapo au ni mpaka urudi ili nimpe Mbunge mwingine nafasi.

Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, ajiandae.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi. Kwanza kabisa naomba niwapongeze viongozi wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya katika nchi yetu ya kutengeneza barabara. Wizara hii toka tupate uhuru imefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Marehemu mama yangu aliniambia, hapo zamani wanatoka Songea walikuwa wanatembea kwa mguu wakati anakwenda kusoma Shule ya Sekondari ya Loleza, wanatembea kwa mguu kutoka Songea mpaka Njombe wiki nzima, ndiyo wanapata usafiri kwenda Mbeya kusoma Sekondari ya Loleza. Ukitazama katika miaka hii, kazi kubwa imefanyika. Kwa hiyo, hatuna budi kuwapa pongezi wataalam na viongozi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, La pili, katika eneo ya barabara kuu zilizoingizwa katika Ilani yetu ya Uchaguzi ya

Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 73, pamoja na barabara mbili za kimkakati Kitaifa zipo katika Mkoa wetu wa Ruvuma ambazo zipo katika Wilaya ya Namtumbo; Barabara kutoka Mtwara – Pachani - Ligela – Lusewa – *Magazine* - Lingusanguse hadi Narasi Wilaya ya Tunduru. Barabara ya pili ni kutoka Lumecha – Hanga – Mputa – Kitanda – Londo – Malinyi – Lupilo hadi Ifakara Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara katika barabara hii ya Mtwara – Pachani na Rasi – Tunduru ambayo ina wakazi wengi sana zaidi ya 140,000 na ina vijiji visivyopungua 39 na mitaa 10 iliyopo katika Tarafa ya Sasawala au Kata ya Lusewa. Eneo hili lina uzalishaji mkubwa sana wa mazao ya chakula na biashara na ndiyo njia ya kwenda mpakani Msumbiji pia. Kwa hiyo, *strategically* pia liko kiusalama ili ukihitaji kupeleka *deployment* kwa haraka katika maeneo ya mpakani katika eneo hilo barabara hii pia inahusika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana, kwanza naishukuru Serikali, nimeona upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika. Nimeona katika hotuba ya Waziri ukurasa 41. Nawashukuru sana Serikali. Wisi wananchi wa Wilaya ya Namtumbo tunachoomba ni kufanyiwa ujenzi wa barabara hii haraka iwezekanavyo na tutashukuru sana ikianza kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara hii ya Lumecha – Londo – Malinyi – Lupilo – Ifakara Mkoani Morogoro nayo ni barabara ya kimkakati Kitaifa. Inafungua maeneo ya fursa zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Morogoro katika maeneo ya kilimo, utalii na usafiri. Barabara hii ukipitia njia ya kutoka Ruvuma kwenda Dar es Salaam kupitia Njombe mpaka Makambako na barabara hii ikikamilika inapunguza zaidi ya kilometa 350.

Kwa hiyo, itaifungua na kupunguza gharama ya mafuta kwa maana ya *kilometers* lakini itasaidia sana kwenye maeneo ya kiutalii na pia itafungua pia mazao mbalimbali kusafirishwa na kulima katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii mimi nilipata kuwa Mwenyekiti mwenza wa uratibu wa ujenzi wa ufunguzi wa barabara hii, wakati huo tunakata pori barabara hii na kujenga madaraja. Mwenyekiti mwenza mwenzangu alikuwa Mheshimiwa mzee wetu Dkt. Ngasongwa ambaye yeye alikuwa Mbunge wa Malinyi kipindi cha 2005 – 2010. Kwa hiyo, tulikuwa na Kamati ya uratibu wa barabara hii ambayo ilikuwa na Wajumbe Wakuu wa wilaya zote mbili; Ulanga na Namtumbo. Kulikuwa na Mameneja wa *TANROADS* Mkoa wa Ruvuma na Morogoro, pia kulikuwa na ma-*DED* wa Halmashauri zinazopita barabara hii na Mkuu wa iliyokuwa *Selous* kwa sababu barabara hii inapita katikati ya *Selous*. Sasa tulikuwa tunakata miti ya *Selous*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ile ilishauri na ilisimamia vizuri ujenzi wa madaraja kwa ukamilifu; Daraja la Mto Londo, Mto Mwatisi na Mto Fuluwa. Yalijengwa kwa ukamilifu na tumeifungua ile barabara, lakini Kamati ilishauri wakati ule na nilisahau Mjumbe mmoja alikuwa anatoka katika Wizara ya Ujenzi, *Eng.* Kilowoko. Kamati ya Uratibu wa Ufunguzi wa Barabara hii ilishauri pamoja na ufunguzi wa barabara hii, lakini *TANROADS* mikoa, Mameneja wa Mikoa wawe wanatenga fedha kwa ajili ya kuweka lami nyepesi katika maeneo korofi na ya miinuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mkoa wa Ruvuma, tulifanya hivyo katika eneo la Namtumbo. Tumekuwa tukiweka nusu kilometa au robo kilometa kwenye maeneo ya miinuko, yale korofi na maeneo ambayo yalikuwa hayapitiki kabisa. Imesaidia sana na katika kipindi hiki naweza kutoa ushuhuda hapo nyuma katika eneo linaloitwa Kata ya Hanga kwenda mpaka Kata ya Kitanga kupitia Mputa na Naikesi, wakati wa mvua barabara ilikuwa haipitiki kabisa, lakini baada ya kufanya utaratibu huo wa kuweka lami nyepesi katika vipande vidogo tu korofi imekuwa inapitia miaka yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali, unaweza ukakuta barabara ya kilometa 120 lakini sehemu korofi haziwezi kuzidi vipande vipande vya kilometa 20. Kwa

hiyo, tunaweza tukaanza kutenga fedha za kuweza lami nyepesi sehemu za miinuko nusu kilometa, sehemu hii labda kilometa moja, utakuta kwamba tunaondoa kabisa malalamiko ya wananchi, lakini pia barabara hizo zinapotika *throughout the year* wakati Serikali inajipanga kutengeneza barabara hizo kwa kiwango kamili cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndiyo ushauri wangu kwamba Serikali iwe inatenga sehemu kidogo kidogo ya kuweka lami nyepesi ili barabara ziweze kupitika moja kwa moja. Kama hii tuliyoifanya sisi ya kutoka Lumecha – Hanga – Mputa – Kitanda mpaka Londo kutokea Norogoro. CCM hoyee! Ah! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudi kwenye barabara ya Mtwara – Pachani...

**NAIBU SPIKA:** Jamani, mwacheni Mheshimiwa Vita Kawawa anawaza Uchaguzi wa Kigoma. *(Kicheko)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye barabara yetu hii ya Mtwara – Pachani ambayo inapita Ligela, inapita Lusewa - *Magazine* – Lingusanguse na mpaka Nalasi tuna mto unaoitwa Sasawala na katika kipindi hiki cha mvua mto huo daraja lake kubwa limekuwa *washed away* na mvua hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawashukuru *TANROADS* Mkoa wameenda kutuwekea kivuko tu kidogo cha kuweza watu kupita. Tunashukuru kazi ile wameifanya, lakini tunaiomba Serikali itutengee fedha ili kulikarabati lile daraja. Ndiyo daraja kubwa ambalo tunalitegemea katika Wilaya yetu ya Namtumbo na Tunduru. Naomba nikushukuru na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Tumaini Brycesen Magesa, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza, kama ilivyo ada nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kutoa mchango wangu. Kama ilivyo ada vile vile nitoe shukrani zangu na niwapongeze wahudumu wote wanaohudumu kwenye Wizara hii nikianzia na Waziri mwenye dhamana pamoja na Watendaji wote, Makatibu Wakuu na Naibu Mawaziri kwa kazi kubwa wanayoifanya na jukumu kubwa lililo mbele yao. Nawapongeza na kuwapa pole kwa sababu majukumu waliyonayo ni makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kuiomba tu Serikali, nchi yetu inaingia kwenye uchumi wa kati; na nchi yetu inasema kwamba yenyewe ni nchi ya viwanda. Ili tuweze kuingia kwenye viwanda tunategemea malighafi kutoka kwenye kilimo. Serikali hii ijaribu kuongea kwa Pamoja; Waziri wa Ujenzi ana vipaumbele vyake, ana barabara zake za kimkakati; ukiingia kwenye kilimo, wana mazao yao ya kimkakati; ukiingia kwenye viwanda, wana viwanda vyao vya kimkakati, lakini haya mambo ukiingia kwenye Serikali hayaendani pamoja. Leo tunazungumza zao la korosho, kahawa, katani, ni mazao ya kimkakati, lakini kwenye Wizara ya Ujenzi hatuyakuti hayo mazao. Hivi leo hii kama Waziri wa Ujenzi hajui korosho zitatokaje Liwale zikafika Lindi, zikafika sokoni, kuna sababu gani ya kusema kuna mazao ya kimkakati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo sasa tunataka tuwaambie nchi hii kwamba tujenge kiwanda cha korosho kule Liwale, Ndanda, kila mahali ambapo zao lipo. Mwenye shamba lake ajenge kiwanda hapo hapo. Kwa sababu kama kweli tulikuwa tunajua kwamba haya mazao ni ya kimkakati, lazima tuyatengenezee huo mkakati uonekane kwenye Serikali nzima, *chain* ile ionekane kwamba hili zao la korosho litatoka Liwale, litafika Lindi, litafika Dar es Salaam, litakwenda kwenye soko au litakwenda kwenye viwanda. Kama Serikali hatuunganishi hivi, hatuna maana ya kuwa na mazao ya Kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwenye upande huo huo wa barabara. *Lifetime* ya barabara zetu ni miaka 20, maana baada ya miaka 20 barabara zile zinatakiwa zifanyiwe *rehabilitation,* iondolewe lami iwekwe nyingine, lakini kwenye nchi kama hii unapoona wenzenu barabara ya zamani inaondolewa, wewe hata lami huijui, mimi napata wasiwasi kama tupo pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti, kuna barabara ya Dar – Chalinze inafanyiwa ukarabati, inaondolewa ile kwa sababu *lifetime* imeisha; kuna barabara ya Masasi – Mtwara inaondolewa; kuna barabara ya Dodoma – dar es Salaam, inaondolewa; na kuna barabara ya Arusha – Moshi, inaondolewa. Yaani hizi barabara *lifetime* yake imeisha, wanakwenda kuondoa hizo lami, waweke nyingine. Hata hivyo hizi barabara hazijawahi kulaza watu njiani, wala hazijawahi kusema kwamba kuna malori ya biashara yamekwama au malori ya mizigo yamekwama kwa sababu ya barabara mbovu, haiwezekani. Hizo barabara zinapitika masika na kiangazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ya Nangurukuru – Liwale, Nachingwea – Liwale, hazipitiki, nyakati za masika zinasimama. Mkoa wa Lindi hauna barabara za lami. Sasa wananchi wanaotoka Liwale na Lindi wanakwenda kutembelea Dar es Salaam, wanakuta lami zinakwanguliwa na kuwekwa nyingine, hivi wanajihesabu wako wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali, hebu tuongee kwa Pamoja, kama kweli tuna dhamira ya kuwahudumia wananchi wetu, lazima tuongee kwa pamoja. Kama hatutaongea kwa Pamoja, bado kuna maeneo yatabaki kuwa nyuma na maeneo mengine yataendelea kwa sababu leo mimi sioni sababu na wala haiingii akilini eti Dodoma – Chalinze wanaondoa lami wanaweka nyingine, mimi Nangurukuru sijawahi kuona lami, Nachingwea – Liwale sijawahi kuona, lami halafu nami napitisha hiyo bajeti, hii haiwezekani! Sitaeleweka! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali haka kakeki kalikopo tugawane sawa sawa. Wale ambao tayari wana lami, hebu tuwaache wapumzike kwanza. Sisi ambao hatuna, tupeni hizo lami, kwa sababu na sisi tunachangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine huko huko kwenye lami, kwenye ujenzi wa barabara zetu, kama hatuko tayari kuangalia *specifications* za barabara, haya mambo yataendelea kujitokeza, barabara hata miaka 15 haijafika, imeshafanyiwa upembuzi yakinifu na inafumuliwa. Kwa mfano, barabara ya Kibiti – Lindi haina miaka 20 lakini haifai. Inafumuliwa! Kuna barabara ya Wazo – Bagamoyo nayo haijafikisha miaka 15, nayo inafumuliwa. Ukiiangalia, kweli ina haki ya kufumuliwa kwa sababu barabara ni ya hovyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali, pamoja na kwamba tunahitaji wataalam wa ndani, lakini kama kweli tuna uchungu na fedha za nchi hii, barabara hizi ni lazima tuzisimamie ili ziweze kujengwa kwa kiwango kinachotakiwa na kiwe kama ni miaka 20 au 25, tuone barabara inadumu miaka 20. Ninyi wenyewe ni mashahidi mliopita barabara hii ya Dodoma, barabara kwenye kona na lami yenyewe inapiga kona. Kwenye tuta, na lami yenyewe inapiga tuta; wapi na wapi? Tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na mengi sana ya kusema, lakini napata kigugumizi. Nitakwenda kuwaambia nini Wana-Liwale kwamba mimi nimepitisha bajeti ambayo inaondoa lami za zamani na kuweka nyingine na mimi kule sina lami? Sitaweza kupitisha hili, nitakuwa nafanya dhambi. Hapa nami naendelea kufanya dhambi. Kuna mahali pengine barabara hazijaharibika, lakini wanajenga *bypass. Bypass* sijui ya Dodoma – Iringa. kuna *bypass* ya Dodoma, Songwe, Dar es Salaam, hizi *bypass* zinajengwa kwa sababu ni *wrong design.* Hivi unapitishaje malori kwenye barabara hii hapa ya Dodoma?

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, kuna Taarifa. Mheshimiwa Twaha Mpembenwe.

**TAARIFA**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimpe taarifa mzungumzaji, kigugumizi hicho hicho kinachompata yeye kupitisha bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi, ndiyo hicho hicho kinanipata mimi katika Jimbo la Kibiti. Barabara ile ya kutoka Nyamisati kuja Bungu jana nimepigiwa simu magari pale yamenasa na abiria pale wamelala.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Kicheko/ Makofi)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, lazima uulizwe kwanza kama unaipokea ama huipokei. Mbona unaipokea haraka haraka! Haya malizia mchango wako.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa. Sasa nafikiri hapo nimemaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kumalizia mchango wangu, naiomba Serikali kwanza kuhakikisha kulipa wakandarasi. Jambo hili linatupungizia sana ujenzi wa barabara zetu. Tunajenga barabara chache kwa sababu tunatumia fedha nyingi kujenga barabara chache; na tunatumia fedha nyingi kwa sababu ya riba inayolipwa kwa Wakandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wako Wakandarasi barabara imeisha miaka minne sasa bado Mkandarasi anadai na kwenye bajeti imo. Naiomba Serikali, hakuna

sababu ya kuendelea kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara mpya wakati kuna barabara tangu mwaka 2014 imeisha upembuzi yakinifu na hakuna kujengwa. Halafu ukiuliza kwenye vitabu, unaambiwa fedha hazipo. Sasa hizi fedha ni za aina gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie fedha hizi ambazo zinasubiriwa kwenye hizi barabara ambazo zimefanyiwa upembuzi yakinifu tangu mwaka 2014 hazijapatikana na hizi ambazo zinajenga barabara nyingine za mikoa mingine na sehemu nyingine ni pesa za aina gani? Yaani kuna pesa zina *label* kwamba, pesa hizi za Mkoa wa Lindi au pesa hizi ambazo tunasubiria sisi ni pesa gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kama ni fedha tunaona barabara nyingine zinajengwa, lakini sisi barabara zetu tunaambiwa fedha hazipo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele imeshagonga.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa shingo upande. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi na Mheshimiwa Daniel Sillo ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii ya kuweza kuchangia bajeti na hotuba ya Waziri wa Uchukuzi. Nimpongeze sana Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimebahatika kufika Dar-es-Salaam na miji mingine midogomidogo ambayo

inaendelea kukua Tanzania. Naomba tu niishauri Serikali nimeona pale Dar-es-Salaam tukiendelea kujenga barabara kwa ajili ya kupitisha mabasi ya mwendokasi. Nina mashaka sana kwa ongezeko la watu wale tukiendelea ku-*invest* kwenye mabasi yale inawezekana tusifanikiwe sana tunatakiwa twende kwenye *commuter train.* Tuwe na *train* ya umeme ambayo itakuwa inachukua watu wengi badala ya kuondoka basi moja na watu 65 au watu 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niishauri sana Serikali, iangalie pamoja na mipango iliyofanya katika miji yetu hii inayokua ianze kufikiria namna ya kuweka *commuter trains* ambazo ni za umeme ili ziweze kupeleka mabehewa 10. Tulifanya majaribio ya *train* pale inaitwa *train* ya Mwakyembe Dar-es-Salaam, ilikuwa inachukua watu wengi. Kwa hiyo, niseme wazi miji yote inayokua tuanze kwenda huko sasa tukiendelea tu kusema tutaendelea kuwa na barabara tutajikuta tunaingia *carpets, carpets* itakuwa *constant,* lakini *operation cost* ya kuendesha mabasi itakuwa kubwa na mwisho wa siku miradi hii itakuwa haiwezi kuizalishia nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye barabara. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri ameonesha wazi kwamba, mpaka Aprili Serikali ilishachangia asilimia 67.2 ya bajeti ya maendeleo ambayo ilikuwa imetolewa na Serikali. Kwa hiyo, ukurasa namba tisa unatuthibitishia kwamba, Serikali imeshatoa pesa asilimia 67.2, lakini ukurasa namba 11 kwenye utekelezaji wa miradi hii kwenye asilimia 67 iliyotolewa inaonesha wazi kwamba, wametekeleza miradi iliyokamilika kwa asilimia 30 tu. Kwa hiyo, 67 ambayo imeingia imeweza kufanikiwa kufanya kazi ya asilimia 30 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mahali hapa naona kabisa kutakuwa na shida ya usimamizi. Nilitegemea ilipoingia asilimia 67.2 tuone na miradi iliyokamilika iwe hata asilimia 50, sasa ni asilimia 30 ikionesha kabisa kuna hoja ya usimamizi hapa. Kwa hiyo, nimshauri Waziri, viongozi wetu walio kule ambao wanafanya kazi kwenye Serikali wahakikishe

kwamba, kile kinachoingia kwenye Wizara kinaweza kuwa kimetumika na wananchi wakaona mafanikio yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nihamie sasa jimboni kwangu. Kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inaoneshwa wazi kwamba, kuna barabara inajengwa kutoka Geita kupita Bukoli – Bulyanhulu hadi Kahama, uchambuzi yakinifu umekwishafanyika. Niwapongeze Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wanachangia asubuhi, walikuwa wanasema kuna uchambuzi yakinifu, kuna uchambuzi gani, kila aina ya uchambuzi umeshafanyika, lakini barabara hii bado haijajengwa na imewekewa loti tatu; kuna loti ya kwanza kilometa 54, kuna loti ya pili kilometa 61, loti ya tatu kilometa 64, lakini bado hakuna kinachokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu mvua imenyesha sana, pamoja na kwamba, iko kwenye mpango wa kujengewa lami, sasa imeharibika sana kiasi ambacho haipitiki, wananchi wanapata shida kupita pale. Niombe sana kama mipango hii ya Serikali bado iko mbali basi hii *periodic maintenance* ifanyike, ili wananchi waendelee kuitumia katika viwango vya kawaida wakati tukisubiri lami hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, naamini barabara hii anaifahamu na ni barabara muhimu kwenye eneo letu la kutoka Geita kuja Kahama na badaye kuja Dar-es-Salaam. ina mapato ya kutosha, tujengewe barabara hii ili wananchi wale waweze kuona matunda ya uhuru wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANROADS* kwa kawaida wanatakiwa kusimamia barabara zetu nyingi kwa sababu, *TARURA* tumethibitisha ndani ya Bunge hili kwamba, Mfuko wao wa ujenzi wa barabara ni mdogo na bahati mbaya sana barabara nyingi ziko *TARURA,* za vijiji. Sasa napendekeza barabara zote ambazo zimefikia viwango vya kupandishwa hadhi kwa namna ya mgawanyo huu ambao unaendelea kuwepo kati ya *TANROADS* na *TARURA* basi zirudi kule ili zipate *periodic maintenance* ambayo inatambulika kwa sababu,

sasa hatutabiri tena. Mvua imenyesha barabara zote zimekatika, tukiuliza *TANROADS* anatengeneza? Hapana, sio ya *TANROADS* hii, ya *TARURA* hiyo kwa hiyo, haitatengenezwa msimu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana Serikali iangalie, tunaomba mara nyingi kupandisha barabara zetu. Kwetu kule tuliomba barabara ya kutoka Katoro kupita Rwamgasa kupita Iseli kwenda mpaka Nyarugusu ipandishwe, wanasema vigezo bado havitoshi. Tumeomba barabara ya kutoka Katoro kupitia Igondo – Nyakamwaga kwenda Kamena, wanasema ni *feeder roads* bado vigezo haviridhishi. Hizi barabara zinakaa hadi miaka mitano bila kutengenezwa na hivyo zinakuwa hazipitiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo ziko ambazo zinatengenezwa kwenye *periodic maintenance.* Tunazo barabara ya Chibingo kwenda Bukondo *Port* inatakiwa ifanyiwe *periodic maintenance,* haijafanyiwa, kwa hiyo, imeanza kuharibika sana na wananchi wanapata shida kupita pale. Vile vile tunayo barabara ya Mgusu kwenda *port* ya Nungwe kwenda ziwani nayo imeanza kuharibika bado haijafanyiwa *periodic maintenance.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo pia barabara ya Katoro kwenda Ushirombo, imeanza kutengenezwa, lakini kasi yake ni ndogo. Ningeomba waongeze kasi sana ili wananchi wale sasa mvua hii inapopita barabara hizi ziendelee kupitika, kwa sababu ni *feeder roads* ambazo zikikatika tunashindwa kufanya zozote katika jimbo letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kama walivyosema wenzangu, kuna mipango mingi sana na watu wanasema pesa hazitoshi, lakini naamini kama Serikali imechangia tulichopanga mwaka jana asilimia 67, halafu sasa bado tunasema leo tuna mwezi mmoja bado mbele, kama itachangia asilimia 10 tutakwenda kwenye asilimia 77. 77, lazima ioneshe kitu ambacho kinaonekana kimetengezwa kwa asilimia 77, lakini utekelezaji wetu kama nilivyosema mwanzo ni asilimia 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana usimamizi kwa maana ya viongozi walioko kwenye wilaya zetu, walioko kwenye mikoa yetu wasimamie vizuri kuhakikisha kwamba miradi hii inakamilika. Ikiwezekana kama tutapata pesa asilimia 70 basi asilimia 70 iwe imefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Sillo na Mheshimiwa Aeshi Hilal ajiandae.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii. Kwanza kabla sijaendelea nitamke naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia kwenye maeneo kama manne kama muda utaniruhusu. Mwaka 2018 mwezi Septemba, ilitokea ajali ya kuzama kwa kivuko cha *MV Nyerere* pale Ukara ambacho kilipoteza maisha ya watu kama 228 hivi na Serikali ikaahidi kuleta kivuko kipya ambacho kitasaidia wananchi wa eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo faraja kutamka kwamba, Serikali imetimiza ahadi yake. Toka mwezi Oktoba mwaka jana kivuko hicho kilianza kufanya kazi. Kwa hiyo, kwa niaba ya wananchi wa Ukerewe naishukuru sana Serikali na kuipongeza sana kwa kutekeleza ahadi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hili ninayo mambo kama matatu ambayo ningetaka kushauri. La kwanza ni kuzingatia ratiba ya kivuko kile kwa sababu, toka kimeanza juzi hapa ratiba ya kivuko kile imebadilika, lakini msingi wa malalamiko kwenye kivuko cha kwanza ilikuwa ni ratiba ambazo hazikuwa sahihi na kwa maana hiyo kwenye safari moja kukawa na mlundikano mkubwa sana wa abiria. Niombe kama kilivyokuwa kimeanza kwa ratiba ya safari tatu kwa kila upande ningeshauri ratiba ile iendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko kwa mfano ya uchache wa abiria, namna pekee ambayo tunaweza tukadhibiti jambo hili ni kuboresha barabara ambazo zinasafirisha watu kuelekea kwenye kivuko kile. Kwa mfano Barabara ya kutoka Nansio – Bulamba mpaka Murutunguru kwenda Bugorola ikiboreshwa abiria watakuwepo wengi, lakini kutoka Bwisya mpaka Kome ikiboreshwa abiria wako wengi. Badala ya kupita kwenye mitumbwi watapita kwenye *route* ile na kufanya kivuko kile kuwa na abiria wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile baada ya ajali ile iliundwa tume kwa ajili ya kufanya uchunguzi chanzo cha ajali na watumishi waliokuwa wanafanya kazi kwenye kivuko kile walisimamishwa. Uchunguzi ulishafanyika, ripoti imekwishatolewa tayari, lakini watumishi waliosimamishwa wakati ule mpaka leo bado wako nje ya mfumo, jambo ambalo linasababisha kuwa katika mateso makubwa. Niishauri Serikali, maadam watumishi wale walionekana hawana hatia, baadhi yao, warudishwe kazini waendelee kufanya kazi, wajikimu na maisha yao badala ya kuendelea kuteseka kisaikolojia, lakini vilevile kimaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo ningependa kuchangia ni juu ya ujenzi wa vivuko vipya. Kwenye Ilani yetu ya Uchaguzi, ukurasa wa 84, Chama Cha Mapinduzi kimeelekeza Serikali kutengeneza vivuko vipya vitatu kwenye eneo la Ukerewe. Cha kwanza ni kutoka Bukondo kwenda Bwiro, kingine kutoka Murtanga kwenda Ilugwa na kingine ni kutoka Kakukulu kwenda Ghana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwenye bajeti hii Serikali imetenga pesa, milioni 180 kwa ajili ya kujenga magati kati ya Bukondo kwenda Bwiro, lakini vilevile imetengwa bilioni moja kwa ajili ya kutengeneza kivuko kwenye eneo hilo. Nashukuru sana, lakini niombe yale maeneo mengine mawili ni muhimu sana yakazingatiwa kwenye bajeti zinazokuja pesa zitengwe ili vivuko viweze kutengenezwa. Mazingira yetu Ukerewe ni mazingira ya usafiri wa majini, kwa hiyo,

tunapokuwa na changamoto ya usafiri, hasa kwenye vivuko, inakuwa ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kwenye eneo la Ilugwa. Kutoka Ilugwa kuja Kisiwa kikubwa cha Ukerewe inahitaji mtu apite majini a-*cross* maji saa nne. Kwa hiyo, kutokuwepo kwa kivuko ni jambo ambalo kidogo linasababisha watu ku-*risk* maisha yao. Kwa hiyo, kama nilivyosema niombe Serikali izingatie sana kutenga pesa kwa ajili ya kutengeneza vivuko hivi vingine vipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu, ambalo natamani niliongelee ni juu ya Barabara ya Nyamswa – Bunda – Kisolya na Kisolya – Nansio. Najua *lot one* na *lot two* tayari zimeanza kufanyiwa kazi, bado *lot three* ambayo inahusisha Daraja la Kisolya – Rugezi na kutoka Rugezi kwenda Nansio kilometa 14.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kwenye bajeti hii Serikali imetutengea bilioni mbili kwa ajili ya kutengeneza kivuko kipya kitakachofanya kazi kati ya Rugezi na Kisolya, lakini imetenga milioni 700 kwa ajili ya ukarabati wa Kivuko cha *MV Ujenzi.* Ni jambo jema, lakini wakati tukisubiri pesa za ujenzi wa Daraja kati ya Kisolya na Rugezi, kama ambavyo nimekuwa ninasema hapa ndani, Serikali ione umuhimu wa kujenga barabara ile kilometa 14.3 kutoka Rugezi kwenda Nansio Mjini. Ikiunganishwa barabara hii itaboresha sana mazingira ya usafiri, lakini hata kuimarisha uchumi wa wananchi wa Ukerewe. Kwa hiyo, niombe sana Serikali iweze kuzingatia jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la nne ambalo nataka kuchangia ni juu ya Bandari yetu ya Nansio kwenda Mwanza. Natambua Serikali imefanya juhudi kubwa na kutumia pesa nyingi kuboresha meli ya *MV Clarius* na *MV Butiama,* tayari *MV Butiama* inafanya kazi, *MV Clarius* bado inaendelea na matengenezo, lakini kumekuwa na shida kubwa sana ya usafiri hasa wa mizigo kwenye eneo hili. *MV Butiama* ikifanya kazi *at full capacity* ina uwezo wa kubeba mizigo tani mpaka 80, lakini hivi tunavyoongea meli ile ya *MV Butiama* haijawahi

kubeba mizigo tani 10 tokea imeanza kufanya kazi, jambo ambalo ni hasara kwa Serikali, lakini kwa nini imekuwa haibebi mizigo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mkanganyiko wa gharama zinazotozwa kwenye mizigo kwa tani kati ya *TPA* na *MSCL. TPA charge* yao ni kubwa sana, inafanya sasa watu wanaosafirisha mizigo kwenye kivuko hiki cha Serikali, wanatakiwa kulipa pesa nyingi sana na matokeo yake wana-*opt* kwenda kwenye vivuko binafsi, jambo ambalo linaleta hasara kwenye kivuko cha Serikali. Kwa hiyo, niombe Serikali ione namna ambavyo inaweza kufanya gharama hizi kushuka na zikishuka ishawishi sasa wasafirishaji waweze kutumia kivuko hiki cha Serikali kusafirisha mizigo na ile dhamira ya Serikali kutumia kivuko hiki kusafirisha abiria, lakini na kusafirisha mizigo iweze kufikiwa kwa gharama ya chini na hatimaye basi kiweze kuwa na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, Uwanja wa Ndege wa Mwanza ni uwanja ambao ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa hili hasa kwa Ukanda wetu ule wa Ziwa, unafanya kazi kubwa sana. Nashukuru sasa hivi uko kwenye matengenezo, lakini nishauri Serikali ione umuhimu wa kukamilisha ujenzi wa uwanja huu hasa jengo la abiria mapema kadiri inavyowezekana. Najua kwenye bajeti hii imetengwa karibu bilioni 6.3 kwa ajili ya kujenga jengo hili, lakini bado niendelee kushauri ni jambo la msingi sana uwanja huu ukakamilika mapema, ili kuweza kuchangia kwenye uchumi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, nikushukuru sana. Ahsanteni sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Daniel Sillo, atafuatiwa na Mheshimiwa Aeshi Hilal na Mheshimiwa Ahmed Shabiby ajiandae.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuchangia katika Wizara

hii ya Ujenzi na Uchukuzi. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa ujumla kwa kazi nzuri sana katika sekta mbalimbali hapa nchini, lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri wa Ujenzi, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kazi nzuri sana wanayoifanya katika Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi. Hii ni pamoja na hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri aliyowasilisha leo asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze pia Wizara kwa kazi nzuri ya kuunganisha mikoa ya nchini kwetu kwa mtandao wa lami ikiwepo na Mkoa wangu wa Manyara ambao leo hii unaunganisha Mikoa ya Arusha, Singida na Dodoma. Zamani kutoka Babati tu kuja Dodoma ilikuwa ni saa nne mpaka siku tatu, lakini leo hii ndani ya saa mbili hadi tatu unafika Makao Makuu ya nchi hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze pia Wizara kwa kuimarisha usafiri wa anga hapa nchini kwa ununuzi wa ndege nane na hivi karibuni tunatarajia ndege nyingine tatu, moja ikiwa ni ndege ya mizigo. Hii ni hatua nzuri sana, tunaipongeza sana Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niipongeze Wizara kwa kuimarisha usafiri wa majini ikiwa ni ujenzi wa meli za mizigo na abiria katika maziwa makuu hapa nchini. Ni kazi kubwa ambayo imefanywa na Wizara lazima tuipongeze sana. Hii inaenda sambamba na uboreshaji wa huduma za bandari katika Bandari ya Dar-es-Salaam, Tanga pamoja na Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kwenye Mkoa wa Manyara. Mkoa wa Manyara una barabara zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara *(TANROADS)* kwa kilometa 1,656. Kati ya hizo barabara kuu ina kilometa 207, lakini zilizobaki kilometa 1,449 ni barabara za mkoa ila kilometa ambazo zina lami ni kilometa 41 tu kwa mkoa mzima. Nadhani Kiteto kilometa sijui mbili, kule kwangu kilometa tisa, kwa hiyo, tuna kazi kubwa sana Wizara ya Ujenzi kuhakikisha kwamba, inajenga barabara za lami katika Mkoa wetu wa

Manyara ambao una miradi mingi ya maendeleo, ni mkoa wenye utalii, wakulima na wafugaji wa kutosha. Kwa hiyo, niombe sana Wizara iangalie sana Mkoa huu wa Manyara kwa jicho la pili kwa upande wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Jimbo la Babati Vijijini kuna barabara ambazo ziko kwenye Ilani ya Uchaguzi ambazo ni mkataba kati ya Serikali na wananchi wake. Barabara ya kwanza ni kutoka Dareda mpaka Dongobesh, kilometa 60. Bahati nzuri barabara hii upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umeshakamilika, alikiri Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akijibu swali langu la msingi, kwa hiyo, sina mashaka na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa utendaji mzuri wa Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi, naamini barabara hii kwenye bajeti ya 2021/2022, itatengewa fedha na itaanza kujengwa, sina mashaka na Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii inaunganisha wilaya mbili; Wilaya ya Mbulu na Wilaya ya Babati, lakini inapita kwenye kata ambazo zina uchumi mkubwa sana. Kuna wakulima kule wakubwa wa vitunguu maji, vitunguu saumu, mbaazi, ulezi na kadhalika. Kwa hiyo, naamini Mheshimiwa Waziri atakuwa ameipata hii vizuri, ili kuhakikisha kwamba, wananchi hao wanapata barabara hii kwa ajili ya manufaa makubwa, licha ya usafiri, lakini pia kwa ajili ya uchumi wa maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ya pili ni kutoka Mbuyu wa Mjerumani kwenda Wilaya ya Mbulu. Niipongeze sana Wizara imejenga daraja kubwa sana la bilioni 13, Daraja la Magara. Mheshimiwa Naibu Waziri alifika pale amejionea, lakini kinachosikitisha upande huu wa Mbuyu wa Mjerumani mpaka Darajani barabara ni mbovu mno na kutoka darajani kwenda upande wa Mbulu barabara ni mbovu mno, daraja limebaki kuwa la utalii wa ndani na umaarufu wa kupiga picha. Naomba sana Wizara itilie mkazo barabara hii ya Mbuyu wa Mjerumani mpaka Mbulu, ni ukanda mkubwa wa kilimo cha mpunga, waliofika pale Magugu wanajua mpunga ule unazalisha wali mtamu kweli kweli. Naomba sana Wizara iliangalie hili, tuna wakulima wa

mahindi, mbaazi na kadhalika, ni barabara ambayo ina manufaa makubwa sana kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutoka darajani kwenda upande wa Mbulu barabara ni mbovu mno daraja limebaki kuwa la utalii wa ndani na maharusi kupiga picha. Naomba sana Wizara itilie mkazo barabara hii ya Mbuyu wa Mjerumani mpaka Mbulu ni ukanda mkubwa wa kilimo cha Mpunga waliofika pale Magugu wanajua Mpunga wali mtamu kweli kweli, naomba sana Wizara iliangalie hili, tuna wakulima wa mahindi mbaazi nakadhalika ni barabara ambayo inamanufaa makubwa sana kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni barabara ya Babati inapita Galapo Orkesument mpaka Kibaya kule Kiketo ina kilometa 225 ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2025 niiombe sana Serikali iangalie barabara hizi kwa jicho la pili. Kuna muonekano mkubwa sana wa utalii lakini pia wakulima na wafugaji na itasaidia pia usafiri na usafirishaji wa wananchi wetu hawa kwa hiyo niiombe sana Wizara iangalie barabara hizi ambazo pia ni mkataba tumejiwekea sisi na wananchi wetu kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja wa ndege wa Manyara, Mkoa wetu wa Manyara kama mnavyoujua wengi ni Mkoa wa Utalii Mkoa mkubwa sana wa Kilimo, Ufugaji na kadhalika. Naomba sana Wizara ianze mchakato wa Ujenzi wa Uwanja wa ndege wa Mkoa wa Manyara ni Mkoa Mkubwa unafursa nyingi za kiuchumi. Kwa hiyo, ninaomba Wizara kwakweli ilichukulie suala hili kwa uzito maana tunauhitaji sana wa kuwa ujwanja huu wa ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo mimi nikushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aeshi Hilaly atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Ritta Kabati ajiandae.

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nipate nafasi ya kuchangia katika hii bajeti ya Wizara ya miundombinu, kwanza naomba niipongeze sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa kazi kubwa sana inayoifanya lakini la pili naomba nikipongeze Chama changu kwa ushindi mkubwa kwa Majimbo mawili kule Mkoani Kigoma, ambako kama Mbunge na Wabunge wenzangu tuliteuliwa kwenda kupambana kuhakikisha kwamba Majimbo yale mawili yanarudi kwa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo kama matano hivi ambayo ningeomba sana Mheshimiwa Waziri akirudi ili niweze kupata majibu. Huu ni mwaka wangu wa nne nimekuwa hapa nikipitisha bajeti ya kujenga uwanja wa ndege napiga makofi ninawaambia wananchi kule Sumbawanga kwamba uwanja unajengwa na hatimaye mpaka leo uwanja wa ndege wa Sumbawanga haujawahi kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu spika, nimeona kwenye bajeti mwaka huu tena kwamba tutajenga uwanja wa ndege mjini Sumbawanga sasa nilikuwa nataka nikuulize sisi tumekuwa tukipitisha bajeti kila siku na tunarudi kwa wananchi kule kuwaeleza kwamba tutajenga uwanja wa ndege muda fulani, leo ni mwaka wa nne ukienda kwenye *Hansard* kule utakuta tumepitisha bajeti na uwanja wa ndege haujawahi kujengwa na mwisho wa siku tumeshalipa fidia Mkandarasi yupo *site* tunaingia gharama lakini uwanja haujengwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikajaribu kuuliza nini tatizo kwanini uwanja wa ndege haujengwi? Nilichokijua mimi ni jambo la kushangaza viwanja vya ndege vile vinne au vitano pamoja na kiwanja cha Kigoma nafikiri na Tabora na maeneo mengine imekwamishwa kwa sababu ndogo sana viwanja vya ndege vinasimamiwa na mamlaka ya ndege Tanzania *TIA* lakini viwanja vinajengwa na *TANROADS* shida iliyopo kule wafadhili wamegoma kutoa fedha kwa sababu vilitakiwa

viwanja vile visimamiwe na *TIA* na sio *TANROADS* kujenga viwanja vya ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni jambo dogo mno kwanini tunavutana kwanini tusirudishe mamlaka ya viwanja vya ndege iende kwenye viwanja vya ndege *TANROADS* wajenge barabara kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikuombe sana jambo hili limechukua miaka minne na nimuombe Waziri akija kutujibu hapa kabla sijapitisha bajeti yake nijue tunakwenda kujenga kweli moja kwa moja mwaka huu au na yenyewe itakuwa ni histori ya kupitisha bajeti kila siku kila siku na mwisho wa siku wananchi wanatuchoka, tumekuwa tukiwaambia tunajenga uwanja na hatuwezi kuujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili mimi Mjumbe wa Kamati ya miundombinu tumepata barabara ya Ntendo Muzye tulipata *0.9-kilometer* hata kilometa moja haijafika kwenye bajeti hii nikamuuliza Waziri hivi kweli kumpata mkandarasi wa kuja kujenga 0.9 kilometa, hata kilometa moja haifiki utampata mkandarasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninaomba nishukuru baada ya mavutano kidogo Serikali imetusikiliza na hatimaye niipongeze Wizara imetupa kilometa 25. Lakini bado hoja yangu ipo pale pale barabara ya Ntendo-Muzye ndio barabara kubwa ambayo inailisha Mkoa wa Rukwa pamoja na Mbeya kule na Tanzania kwa ujumla. Kilometa kutoka Ntendo kwenda Muzye ni kilometa 35 lakini ukipeleka kilometa 25 tutakuja kwenye utata ule ule wa kilometa 10 nani atazimalizia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Wizara na nimuombe Waziri wetu wa miundombinu atuongezee baada ya kutupa kilometa 25 atupe kilometa 35 ili tuweze kumaliza barabara ile barabara ile ni kero Mheshimiwa Rais anaijua, Mheshimiwa Waziri Mkuu anaijua na Mawaziri wote wanaopita pale kutoka Ntendo kwenda Muzye barabara ile

haipitiki na watu wengi wanakufa. Lakini chakula chote kinatoka bondeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilitaka niombe kwa sababu nimekaa na Mbunge mwenzangu anatoka Kwela lengo kubwa sisi Wabunge mtusaidie ili barabara ile iweze kujengwa kwa kiwango cha lami hizo kilometa 10 tuwaombe Wizara iweze kutuongezea ili tuweze kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo barabara ya kutoka Matai kwenda Kasesha ina kilometa 51 ukiwapa kilometa 35 tutabakia na kilometa 20 nyingine kwa hasara, na Sumbawanga ni mbali hivi barabara ndogo ndogo hizi au fupi fupi zinazoweza kujenga Dar es salaam ni rahisi zaidi kwasababu wakandarasi wapo karibu na maeneo ambayo wanayapata lakini ukitoa kilometa 25 kwa Sumbawanga kumpata mkandarasi kutoka maeneo mengine ni shinda kubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri tunakuombe ili uweze kutusaidia, nazungumzia Bonde la Rukwa, bonde ambalo linakwenda mpaka Chunya mwisho wa siku linafika mpaka kule Mbeya barabara ile mbovu haipitiki, madaraja mabovu, nikuombe sana sisi tunaongea kama mkoa, mkoa wetu ulikuwa uko nyuma na sasa hivi umeanza kupiga hatua kubwa basi tunaomba Serikali na tumuombe Waziri aende akaangalie ile barabara ili iweze kupitika kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee *standards gauge* Wajumbe tulienda kutembelea reli ile iliyojengwa ya kisasa, nataka niseme nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali, Wabunge wote Wajumbe wote waliofika maeneo yale waliridhika kabisa na utendaji mkubwa wa Serikali wa inavyosimamia mradi ule. Kwa kweli ukiwa nje hawa wananchi ambao labda hawajatembea maeneo yale mkienda kutembelea Waheshimiwa Wabunge ni miujiza kwakweli reli imejengwa vizuri na sisi tuipongeze Serikali iweze kufanya sasa mambo mengine ili tuweze

kukamilisha barabara hii ya Reli iweze kufika Tabora, Kigoma, na kwenda Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya nirudie tena kumuomba Waziri MV Liemba *Lake Tanganyika* ziwa kubwa lenye watu wengi lakini leo ni mwaka wa tano meli haitembei watu wanakufa kila siku watu wanaangamia lakini kila tukifika Bungeni tunaambiwa kuna bajeti mwaka huu tunajenga meli, mwaka huu tunatengeneza MV Liemba mwaka huu tunatengeneza *MV* Mwongozo hakuna meli hata moja iliyotengenezwa.

Sasa mimi hoja yangu hapo ni kwamba tunapokuja kupitisha hizi bajeti na mwaka jana tumepitisha MV Liemba inajengwa mpaka leo haijaweza kukarabatiwa tufanye nini sisi Wabunge kwenda kuwaambia kule wananchi? Watupe majibu ili tukienda kule tuwaambie bwana hii meli tumeiondoa kwenye bajeti mpaka pale tutakapokuwa tumepata fedha ili tuweze kujenga meli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hatuna fedha tusiweze kutoa ahadi humu ndani kama tutajenga meli wakati fedha hatuna, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri mwaka huu, hiyo meli mpya sasa ikae pembeni tutengezeeni meli zetu zile ambazo tunazijua zianze kazi mpya itakuja baadaye. Lakini humu nimeona tuna Meli mpya mbili sijui tuna meli ya tani 3000 utapakia mzigo wa nani wa tani 300 *Lake Tanganyika*, kengele ya kwanza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ya pili Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa ninasikiliza kwa makini hapa namna ambavyo kilometa 25 zimeachwa hapo 10 nikawa nawaza kilometa 5 nilizopewa mimi kati ya kilometa 269 nikasema *Wallah*, Mheshimiwa Shabiby atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati Mheshimiwa George Mwenisongole ajiandae. *(Kicheko)*

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara yetu ya Ujenzi na Uchukuzi kwanza kabisa nianze kwa kusema kama sitopata haya majibu sahihi sitounga mkono hoja. La kwanza ni kuhusu barabara yangu ya Jimbo la Gairo ambayo inakwenda Jimbo la ndugu yangu Omari Kigua Kilindi. Ile barabara imekuwa na maslahi mapana kati ya Wilaya ya Kilindi, Gairo pamoja na Handeni na ni barabara nyepesi sana hata ya kutoka Dodoma kwenda Tanga, lakini ina kata nyingi sana za upande wa Gairo ziko ng'ambo ile ambayo inakaribiana na Wilaya ya Kilindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ina madaraja ya Chakwale na daraja la Nguyani viongozi wote wa Wizara ya Ujenzi mmefika pale Waziri kafika, Naibu Waziri kafika, Katibu Mkuu kafika mara mbili mbili, lakini hakuna matumaini ya aina yeyote na mwaka jana yameondoa magari zaidi ya tisa na imeleta vifo zaidi ya nane, lakini barabara hii siioni kwenye huu mpango kila siku upembuzi yakinifu sasa huu sijui mpaka lini utakwisha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninataka Mheshimiwa akija aniletee majibu ambayo ni sahihi, na kuna barabara ya kumalizia pale Gairo Mjini inayokwenda mpaka pale Halmashauri pamepakia kama kilometa 120 ya lami na sehemu nyingine ya kwenda kuunganisha na barabara kuu zimebakia kama mita 800 na ilipitishwa kwenye bajeti miaka minne lakini mpaka leo haijaguswa nataka na hiyo nayo nipate majibu ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni mfanyabiashara na nimfanyabiashara nyingi lakini mojawapo ni ya usafirishaji wa abiria leo nilikuwa nipo hapa na ndugu yangu Kiswaga hapa alishalizungumza kidogo hili suala baada ya kuja watu wa Kanda Ziwa na sehemu nyingine kutaka kuanzisha mgomo kama mliusikia kipindi cha nyuma kama miezi mitatu nyuma wa mabasi walitaka kugoma lakini migomo mingine wasije wakagoma wafanyabiashara wa mabasi alafu wakaonekana kwamba ni maadui wa Serikali, si kweli kuna mifumo ambayo imeanzishwa na Serikali na hizi mamlaka

ambazo zimepewa kwenye Serikali ya wizi na ya ajabu kabisa ambayo haitekelezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kwenye mabasi sheria inayoleta la *LATRA* sasa hivi unatakiwa ununue kwanza *possy* kile kimashine kile cha kuuzia kile, kila basi kile kimashine ni shilingi 1,000,000 mpaka shilingi 800,000 na kwenye ofisi zote kwa hiyo kama una mabasi 50 uwe na vile 50 na kama una ofisi 50 uwe na vile 50 kama huna kuna *vendor* anakukopesha unamlipa *percent* angalia wizi huo, halafu ukitaka kuuza kama una basi la abiria 57 unataka kumuuzia Mheshimiwa Kiswaga hapa tiketi kwanza ile mashine unahesabu abiria 57 labda 1,140,000 unaingiza kwenye ile mashine kwanza pesa, pesa yako wewe sio ya abiria, unakijaza kwanza fedha ya basi zima alafu ndio uanze kuuza hasa huoni kama ni kituko hicho? Halafu yaani bado ninadaiwa basi alafu tena kama nina mabasi 50 nitafute Milioni 57 za mtaji kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu ukishauza tiketi fedha haiji kwako inapita kwanza *database* inapita *TTCL,* inapita ... halafu wao ndio wanakupelekea benki, yaani fedha yangu, gari yangu halafu wewe unishikie fedha inatokea wapi hiyo. Hiyo biashara ya wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ukienda benki ile *statement* unapewa nauli 5,000, 10,000 lundo namna hii kwa hiyo, ukizubaa kuangalia utakuta haijaingia wiki fedha, nilimwambia Naibu Waziri kaenda Tanga akashuhudia kuna mtu milioni 23 haijaingia, mwenyewe millioni saba hazijaingia kuna wengine milioni 10 hazijaingia, sasa kwa hiyo na hauna *dashboard* ya kuangalia kila siku kwa hiyo kila siku uwe una re-*statement* kwanza biashara gani duniani? Nafanya vitu ninauza halafu fedha yangu sipati, hela yangu Serikali ndio ukaniwekee wewe benki?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshindwa kuweka hii jamani muangalie mifumo hii halafu mnasema leo wawekezaji wawepo, mwekezaji gani atakayefanya biasahra ya kipuuzi kama hii hapa, haiwezekani hata siku moja biashara ya namna hii! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nisingelisema hili alafu mimi ninafanya biashara ya mabasi na watu wote wa mabasi wanajua ...ya mabasi ningekuwa mnafi hiki kitu hakiwezekani tunajua sisi *EFD machine* peke yake mnataka leteni *EFD* mashine watu watumie *EFD* mashine huwezi ukawa na duka eti unapiga thamani ya mali za duka milioni 300 halafu unaingiza kwenye mashine ndio uanze kuuza duka inawezekana wapi? Halafu hapa katikati kuna ma-*vendor* wanakukata *two percent* haiwezekani huu utapeli ni utapeli wa hali ya juu sana, na wafanyabiashara siku ile walimvisia sana Mheshimiwa Hayati Dkt. Magufuli pale Ubungo wakati anafungua stendi lakini bahati mbaya walikosa nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walipiga kelele mzee mzee lakini hajawaona lakini kwakweli ilikuwa hatari kubwa sana hii, hii biashara haiwezekani kwa hiyo, wafanyabiashara wa mabasi hawawezi.

Mheshimiwa Naib Spika, kingine Waziri wa Uchukuzi...

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba wenye mabasi wakati mwingine basi linaweza kuharibika njiani abiria anatakiwa arudishiwe fedha, na fedha zipo kwa *vendor* atafanyaje huyu mfanyabiashara wa basi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shabiby.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ninaipokea kwa mikono miwili. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba haya mambo yafanyiwe kazi watu wasije wakagoma halafu baadaye watu wakaanza kulaumu

kingine, lakini na Waziri ulichukulie vizuri kwa sababu wakati linapitishwa wewe ulikuwa Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi kwa hiyo uwe nalo makini na nilipokuuliza ukasema ulikuwa haujui kama lipo hivi na bahati nzuri kulikuwa na Waheshimiwa wengine Wabunge na hata Mheshimiwa Katibu Mkuu wetu wa zamani mstaafu alilikemea sana hili akiwa Katibu wa CCM lakini lilishindikana wakasema huyo mwanasiasa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kingine stendi zinajengwa kweli za Serikali na zinatumia gharama nyingi ninazungumza hili kwa sababu Naibu Waziri wa Uchukuzi yupo hapa. Stendi ya Dodoma mwanafunzi anasoma chuo au shule anakuwa na nauli wakati mwingine hata mnamsaidia shilingi 20,000 mnaenda kumshusha nanenane halipii chochote halipi fedha ya mapato ya aina yoyote ya kuingia stendi lakini unamlazimisha ashuke akodishe bodaboda au taxi hilo lipo Dodoma lipo Songea, lipo Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, stendi ya Iringa kilometa 21 kutoka pale stendi wanaposhushwa abiria mpaka mjini na Halmashauri ile Manispaa haiingizi faida yeyote ila tu wanawaambia shule tu hapa basi liende tupu, basi linaenda huko huko mjini lakini haliruhusiwi kwenda na abiri ili umtese abiri ilimradi tu ashuke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilichogundua...

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ukiwa unazungumza taarifa ukishasema mara moja unasimama ili nijue uko wapi, ukishasema taarifa unasimama kimya halafu nikishakuona...

**MBUNGE FULANI:** Tatizo huyo mrefu sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa.

## TAARIFA

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba sio Dodoma peke yake hata Ruvuma ni Kilometa 25 Songea kituo cha mabasi kilipo na mpaka Makao Makuu ya Mji wa Songea ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shabiby unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndio hiyo nilikuwa ninaitaka, kwa hiyo Waziri wetu wa Ujenzi na Naibu wako hebu angalieni mnawatesa abiria kama mimi mwenye basi nimeamua kumchukua huyu abiria kumpeleka mpaka anapotaka wewe kinakuuma nini wewe ambaye huna hata basi nini kinakuuma? Na haupati fedha ya aina yeyote labda angekuwa anaingia ungesema unachukue ile shilingi 300 lakini anashuka ila tu unataka kwamba bodaboda sijui taxi wao unawaangalia wapo pale 60 lakini unatesa watu maskini wengine tumewapa mle lifti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ninataka nizungumzie bandari, bandari ya Dar es Salaam mambo mengi yamezungumzwa lakini ninataka niwaambie haitafanyakazi vizuri tusipoangalia hata siku moja, hapa maneno roho ya kuviziana vyeo, chuki ndizo zilizojaa kuna ule mfumo unaitwa *TANCIS* upo *slow* sana bandarini, upo *slow* sana kwa hiyo ubadilishwe au urekebishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, mimi hapa niliongea Bungeni, tulibishana sana wakati ule na akina Mheshimiwa Mwakyembe na wengine hadi tukafanikiwa kuipeleka ile bandari ya pale Vigwaza, inaitwa Bandari ya Kwala *(Dry Port).*

Nafikiri mimi ndio nilikuwa mtu wa kwanza kuzungumza baadaye nikawa nimeungana na Mheshimiwa Hawa Mchafu. Bahati nzuri bandari ile mpaka sasa hivi imeshajengwa, imebakia vitu vidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TPA,* bandari wamenunua vichwa vya treni viwili kwa ajili ya kutoa mizigo yote makontena yote kutoka bandarini yaje na ile reli ya kwenda Arusha, waje washushe Kwala, pale Vigwaza na ile bandari iko tayari, bado kumalizia tu ili malori yote yasiingie kule Dar es Salaam na ili foleni yote ya bandari hii isiwepo. Cha ajabu hii nchi mpaka leo, nendeni mkaangalie jamani, sisi watu wa Kamati ya Miundombinu tumeenda pale, ile bandari imekwisha, *TPA* wameshanunua treni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka pale bandarini treni inaweza kwa mara moja ikabeba kontena 60, 70 na zikiwa treni tatu au nne; na Kadogosa nimemwuliza, anasema yeye anazo treni, anaweza akaweka hata nne au tano pale. Kwa hiyo, kwa siku tunaweza tukatoa kontena zaidi ya 1000 bandarini kuja pale Kwala ili malori yasiende kule mjini. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Muda umeisha!

**NAIBU SPIKA:** Muda umeisha Mheshimiwa.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Dah, nilikuwa nataka niseme ya ndege. Haya, basi ahsante sana. Ila siungi hoja mkono mpaka nipate majibu ya kutosha. Bandari ya Kwala nataka nijue inaanza lini kazi; na barabara zangu. Pia ndege za Dodoma - Mwanza bado hamna hapa. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa George Mwenisongole na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, ajiandae.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Nianze na kumtanguliza Mwenyezi Mungu katika mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza na kuwapongeza sana Wizara ya Uchukuzi na Ujenzi. Tumetembelea miradi yao tukiwa na Kamati ya miundombinu, miradi ni mizuri sana, wameitendea haki nchi yetu na wametekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye Mkoa wangu wa Iringa na niende kwenye changamoto kubwa za barabara za kiuchumi zilizopo katika Mkoa wetu wa Iringa. Tunazo barabara ambazo kwa kweli tunaomba Serikali ingezichukua na kuanza kuzifanyia kazi kwa sababu Mkoa wetu wa Iringa unakosa uchumi kwasababu ya barabara ambazo ni mbovu, hazipitiki mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo barabara kwanza inayokwenda katika Mbuga za Wanyama. Hii barabara imeshasemewa na Wabunge karibu wote wa Iringa. Hii barabara inakwenda kwenye Mbuga ya Wanyama ambayo ni ya pili kwa ukubwa kwa Afrika. Tulikuwa tunategemea kama hii barabara ingeisha kwa wakati, basi wananchi wa Iringa wangeweza kujiajiri kupitia hata hii barabara kwa utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa inajengwa dakika mbili mbili…

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Napenda kumpa taarifa mzungumzaji anayezungumza kwamba barabara hiyo ya kwenda *Ruaha National Park* kilometa 104 ni barabara ambayo imeahidiwa na Hayati Rais wa Awamu ya Tatu, Rais wa Awamu ya Nne na Hayati Rais wa Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi kilometa zote kuanzia mwaka 2015 walikuwa katika upembuzi yakinifu na usanifu wa kina toka 2015. Kwa hiyo, ninapoona hivi, nataka kumpa taarifa kwamba hii hali ni mbaya na tumetengewa pesa ya kushika mfuko tu, shilingi milioni 1,500.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naipokea taarifa hiyo kwa sababu kwa kweli lazima Wabunge wote wa Iringa tuisemee kwa sababu inatusaidia wananchi wote wa Iringa. Naomba sasa Mheshimiwa Waziri aone umuhimu, kwa sababu tumeambiwa kwamba itakuwa kwenye *package* ya *World Bank*, lakini toka Mheshimiwa Marehemu yupo akiwa Waziri nilishawahi kuuliza swali na mpaka amekuwa Rais; naomba Mheshimwa Waziri hebu tupe kipaumbele kwenye hii barabara ambayo inakwenda kwenye Mbuga za Wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunazo barabara nyingine ambazo ni za kiuchumi zinahitaji sasa kupewa kipaumbele. Kuna barabara ile ya Nyololo - Mafinga kilomita 40.4. Hii barabara hata Mbunge wa Mafinga kila siku anaizungumza. Kuna Mgololo, kuna Igoole - Kasanga kilomita 54 lakini kuna Kinyanambo C - Usokami ambayo inakwenda mpaka Kisusa; kuna Kinyanambo A – Sadani – Madibila, hizi barabara na zenyewe zipatiwe kipaumbele kwa sababu ni za kiuchumi ambazo tuna imani kabisa Serikali ikizichukua, basi Iringa itakuwa ni moto kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunayo barabara nyingine ya Iringa - Idete hii barabara inaunganisha Jimbo la Iringa Mjini - Jimbo la Kilolo na kwa kweli hii barabara inakwenda Idete mpaka Mlangali mpaka inaenda kuunganisha Mlimba. Hii barabara itasaidia kutoboa, kwamba tutakuwa tunafika mpaka Morogoro na itakuwa mbadala kama kutakuwa kuna tatizo kwenye huu mlima wa Kitonga, hatutakuwa na haja ya kupita mlima wa Kitonga, tutatokea Morogoro kuja kufika mpaka Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna ile barabara ya Ilula, Mlafu, Mkalanga, Ipalamwa, Kising'a na Kilolo. Hizi barabara zote ni za kiuchumi. Tunaomba kwa kweli Serikali iziangalie ili uchumi uweze kufunguka. Kwa kweli hizi barabara mara nyingi hazipitiki hata Mbunge wa Kilolo juzi nilimsikia anaongelea. Kwa nini sasa kama alivyoshauri Mheshimiwa Kawawa, kuna maeneo korofi ambayo yanajulikana, ni kwa nini sasa yale maeneo korofi Serikali ingekuwa inaangalia kuliko kuanza kutengeneza kilomita labda mbili kutoka Iringa mjini, mbili kutoka Kilolo: ni kwanini sasa wasiangalie tu yale maeneo korofi halafu ndiyo waweke kipaumbele katika kutengeneza ili ziweze kupitika mwaka mzima? Kwa sababu zote zina maeneo korofi, siyo kwamba yote haipitiki, lakini tunachotaka ipitike mwaka mzima ili wananchi waweze kupitisha mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunayo barabara ile ya mchepuo ya Tumaini, kuchepusha yale magari mazito malori yasipite katikati ya barabara ambayo hata leo Mheshimiwa umesema kwamba ile barabara ya Tanzam malori yanapita mengi sana pale mjini kiasi kwamba kuna wakati itatokea ajali kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya zaidi Iringa pale hatuna sehemu ya kupaki magari, kwa hiyo, magari yakipaki pale barabarani yanaleta shida kwa sababu wafanyabiashara wanashindwa kufanya biashara zao, kwa sababu wakiweka tu magari *TANROAD* wanafunga yale magari na hapo hapo watu wanalipa karibu shilingi 150,000/= au shilingi 200,000/=, wafanyabiashara wanashindwa kufanya biashara. Sasa Serikali ione umuhimu hizi barabara zetu ziweze kujengwa kwa kiwango cha lami ili zipitike mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu mfuko ambao wanawake huwa wanasaidiwa. Wizara ilikuwa inatoa fedha ili iwasaidie Wakandarasi wanawake kuwajengea uwezo ili tuwe na wakandarasi wengi wanawake. Nampongeza Mheshimiwa Eng. Ulenge ambaye nakumbuka wakati ule alikuwa kwenye hiki kitengo, sasa sijajua;

changamoto kubwa ilikuwa ni ufinyu wa bajeti kwamba wanawake wengi hawajengewi uwezo. Sasa naomba hiki kitengo kitengwe fedha nyingi ili wanawake wengi waweze kuwa makandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo nampongeza binti mmoja katika barabara ile ya *Tanzanite Bridge,* tulikuta mtoto wa kike mdogo kabisa, yeye ndyo anasimamia ile barabara. Ni *Engineer;* kwa kweli alitu-*impress* sana sisi Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu na tukasema kwamba ipo haja sasa kwa watoto wetu wengi wa kike wajengewe uwezo. Tunakupongeza *Engineer* Mfugale lakini tunaomba weka wanawake wengi pengine hata ukiondoka waachie hawa akina dada; na unajua akina mama sasa wanaweza na huu ni wakati wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niendelee kupongeza mradi wa *SGR*; kwa kweli tumepita katika eneo lote kuanzia hapa mpaka Dar es Salaam na tumekuta asilimia 50 ya wataalam ni vijana wetu. Kwa hiyo, hiki ni kitu kizuri ambapo wanawajengea uwezo na uwe utaratibu mzuri kwamba hata hawa wataalam wa makampuni haya makubwa yakiondoka, vijana wetu wanakuwa wamejengewa uwezo. Kwa hiyo, hili lilitufanya na sisi tukapongeza sana kwamba vijana wengi sasa ma-*engineer* tutapata kutoka hapa hapa Tanzania na wanajengewa mradi mzuri. Pia kuna fursa nyingi sana kwenye huu mradi ambazo tuliziona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze sana pia ujenzi wa uwanja wa ndege uliopo Iringa na tuliambiwa kwamba mwaka huu, huu tutaenda kuzindua ule uwanja wetu na tunaimani sasa tutafanya biashara kupitia huu uwanja, lakini kama haitajengwa ile barabara, bado tutakuwa tunahitaji kwa kweli mfanye kazi nzuri. Vile vile tunapongeza kwamba wananchi wameshalipwa kabisa, hawadai kitu chochote. Kwa hiyo, tunaomba Waziri azingatie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nizungumzie kuhusu malipo ya Wakandarasi. Wakandarasi wengi bado wanadai.

Tulipokuwa kwenye Kikao cha *Road Board* cha Mkoa wa Iringa, walikuwa wana changamoto nyingi sana kwamba hawalipwi malipo yao, wanadaiwa pesa nyingi kwenye benki, wanadaiwa *TRA* na walikuwa wanaomba kujengewa uwezo. Tumekuwa na miradi mingi na tulisema kwamba Wakandarasi wa ndani wajengewe uwezo na ikiwezekana pengine hawa Wakandarasi wa nje wakija, pengine zile kazi ndogo ndogo wapatiwe Wakandarasi wetu wa ndani ili pia iwasaidie, pengine wanaweza wakaachiwa vifaa na pia wakapewa uwezo mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo nakushukuru, naomba Mheshimiwa Waziri, zingatia Mkoa wetu wa Iringa, una changamoto nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Mwenisongole atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya na Mheshimiwa Venant Daud ajiandae.

**MHE. GEROGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi. Kusema kweli ninaongea kwa uchungu sana kwa sisi watu wa Mkoa wa Songwe na kwa ujumla na mikoa hii ya kusini. Kiuhalisia niungane na Mbunge wa Newala ambaye ameongea kwa uchungu sana na ninashangaa kuona hata Wabunge wenzangu sijui mnaogopa nini kuongea ukweli katika hili jambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wabunge wa Mikoa hii ya Mbeya, Songwe, Liwale, Lindi tukiuliza hii barabara tunaambiwa barabara zenu zitajengwa kadri fedha zitakavyopatikana. Tukiuliza barabara, tunaambiwa barabara zenu Serikali inaendelea kutafuta fedha, lakini kuna baadhi ya mikoa hayo majibu hawayapati, wanaambiwa Mkandarasi amechelewa, barabara zenu hela ziko tayari, inakwenda kujengwa siku fulani. Sasa mimi nataka Waziri atuambie kuna kigezo gani mnatumia kugawa hizi fedha

kwenye mikoa? Kwa nini mikoa mingine Wabunge tunapewa majibu kama haya? Hata sisi tunalipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mambo ambayo amenifurahisha Mheshimiwa Rais Mama Samia, ni juzi alipofuta Sherehe za Muungano. Kwa mara ya kwanza aliamua kuzigawa zile hela za Muungano pasu kwa pasu; Bara na Visiwani. Sasa ninyi wasaidizi wake mjifunze kwamba hii keki ya Taifa hata mikoa yote igawanywe sawa. Ameshawapa somo! Sisi kwetu hii barabara ya Mloo - Utambalila mpaka Kamsamba upembuzi yakinifu uko tayari, usanifu wa kina uko tayari, nyaraka za tenda ziko tayari, lakini miaka yote kutenga fedha tenda itangazwe tunapigwa dana dana, lakini mikoa mingine barabara inatengewa usanifu wa kina, inatengenezwa kwa haraka kabisa. Hii siyo sawa mimi sioni kama sisi tunatendewa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hili naomba Waheshimiwa Wabunge tuungane, hii keki ya Taifa tugawane sawa mikoa yote. Hata huko nako kuna Watanzania. Kwako pale, kuna barabara ile ya Mbeya mpaka Tunduma tumeambiwa itajengwa njia nne za pembeni; ni stori tu, hakuna. Tusipoangalia mpaka 2025 haitajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge ambao mikoa yetu haipewi kipaumbele katika hii bajeti, tuungane tuhakikishe tunambana Waziri atuambie aje na majibu halisi, kwa sababu kule nako kuna Watanzania.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa. Nataka kumwongezea kaka yangu George anayeongea hapa...

**NAIBU SPIKA:** Subiri kwanza, huongei kabla hujatambuliwa na Kiti. Haya sasa unaweza kusimama. Mheshimiwa Condester Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. nataka kumwongezea taarifa Mheshimiwa

Mbunge wa Jimbo la Mbozi kwamba barabara pia anayoiongelea ya Mloo – Kamsamba – Chitete - Utambalila yenye kilometa 145.14 ni miongoni mwa barabara ya kimkakati kabisa katika mkoa wetu wa Songwe. Kwa hiyo, tunashangaa ni kwa nini Serikali haijatuingizia kwenye bajeti?

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni miongoni mwa barabara ambayo itatusaidia kuinua kipato sana kwenye mkoa wetu wa Songwe na ukitegemea ndiyo barabara ambayo inatoa mazao kupeleka nchi za jirani na kusambaza mkoa wote wa Songwe na sehemu nyingine.

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimwa George Mwenisongole unapokea taarifa hiyo?

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kichwa na miguu na mikono naipokea hii taarifa. Hii barabara ndiyo uhai wa mkoa wetu. Kahawa yote inayolimwa Mbozi inapita kwenye hii barabara. Mchele wote, mpunga wote wa Kamsamba unapita kwenye hii barabara na ni kiunganishi kati ya mkoa wetu, Mkoa wa Katavi mpaka Tabora. Kama hii barabara itawekewa lami, malori hayana haja ya kupita Iringa kwenda Dodoma au Tabora, yote yatakuwa yanapita njia ya huku.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nashindwa kuelewa, kila kitu kiko tayari; nyaraka za *tender* ziko tayari, usanifu wa kina uko tayari, upembuzi yakinifu uko tayari, shida nini Mheshimiwa Waziri kututengea fedha? Kwa kweli tunahitaji majibu katika hili suala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kusema hayo, mimi nikushukuru sana. Niungane na Mbunge wa Newala aliyesema anaunga hoja mkono kwa shingo upande, tusubiri majibu ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya atafuatiwa na Mheshimiwa Venant Daudi na Mheshimiwa Justine Lazaro Nyamoga, ajiandae.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nachukua nafasi hii kukushukuru sana wewe, nimshukuru kipekee kabisa Waziri, Mheshimiwa *Eng*. Dkt. Chamuliho na vile vile nawashukuru manaibu wake wawili. Nachukua nafasi hii niwashukuru sana ndugu zangu wa *TANROAD* Mkoa wa Singida, wamekuwa *proactive* sana tunapopata matatizo sisi Wilaya ya Manyoni hususan panapotokea matatizo ya kuharibika kwa barabara. Kwa kweli hili naomba niwashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hoja tatu ambazo zinaendana na ujenzi wa barabara, lakini vile vile nina hoja ambayo itahusiana na suala la ujenzi wa daraja na hoja nyingine ambayo nataka kuchangia inahusu Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi wa Magari *(One Stop Inspection Station)* ambacho kipo katika Jimbo la Manyoni Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natoka katika Jimbo la Manyoni Mashariki. Kwanza nichukue nafasi hii nimshukuru sana Waziri, katika bajeti hii ambayo ameiwasilisha kuna daraja ambalo linajulikana kama Daraja la Sanza ambalo limekuwepo ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa miaka 10. Nafurahi na namshukuru sana Waziri kwa sababu tayari upembuzi yakinifu ulishafanyika, tayari usanifu wa kina ulishafanyika na tayari zaidi ya 90% ya wananchi walishalipwa fidia zao. Namshukuru sana Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sanjari na hilo, kwa mwaka huu wa fedha, Waziri ametutengea takribani shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa hili daraja. Hoja yangu ya msingi, nataka kupata majibu haya wakati Waziri anakuja kuhitimisha kwa sababu hili daraja limekuwa likipangiwa hela kila mwaka lakini haliendi kutekelezeka. Nitapenda kusikia sasa kutoka kwa Waziri: Je, ni lini sasa huo ujenzi wa daraja utaanza? Wamejipangaje kuhakikisha kwamba wanatangaza hizo tenda ili Wakandarasi waanze hiyo kazi ya kujenga daraja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nina barabara ambayo Hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliiahidi alipokuja

wakati wa kuninadi wakati wa kampeni. Barabara ya kutoka Manyoni - Heka - Sanza ambayo inaenda mpaka Chaligongo barabara inaenda mpaka Mbabala - Bihawana inatokea Dodoma. Hii barabara ina umbali wa takriban kilomita 200. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara ina umuhimu mkubwa sana. Kwanza hii barabara inagusa Halmashauri nne. Inagusa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, inagusa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, inagusa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi na Halmashauri ya mji wa Dodoma. Kwa maana nyingine, hii barabara inaunganisha mikoa miwili; Mkoa wa Singida na Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi, hii barabara ni muhimu sana kwa ukuaji wa uchumi wa mikoa miwili hususan Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Singida. Tuna wakulima wengi sana ambao wapo katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki, Jimbo la Bahi na Jimbo la Dodoma Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hilo tuna *Game Reserve* ya Kizigo ambayo ni maalum kwa Utalii wa Uwindaji. Hiki ni kitega uchumi muhimu sana ambapo kwa kweli tunahitaji kuhakikisha hii barabara tunaiimarisha, nini hoja yangu? Ni muda muafaka sasa kwa sababu Rais Hayati John Pombe Joseph Magufuli alituahidi na tayari ipo ndani ya hii bajeti, lakini haijatengewa fedha. Sasa napenda kusikika kutoka kwa Waziri ni lini tunakuja kujipanga kufanya upembuzi yakinifu *(feasibility study),* lakini tunakuja kuanza kupanga na kuweka bajeti kwa ajili ya *detail design* na vile vile, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa hii barabara angalau kwa awamu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu Wabunge wengi wameeleza kilio chao cha barabara mbalimbali, wote tunatambua hizi barabara ambazo zinaunganisha zaidi ya halmashauri mbili, lakini barabara ambazo zinaunganisha mikoa zaidi ya miwili, ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu. Kubwa zaidi ndugu zangu wa kutoka kwenye haya majimbo manne wanapata huduma zao nyingi za

kiafya Dodoma, hususani katika hospitali ya Mkapa lakini hospitali ya Uhuru na hata Hospitali yetu ya *General* hapa Dodoma. Kwa hiyo, utaona ni kwa jinsi gani Serikali inahitaji ku-*invest* kwenye hii barabara ili tuweze kukuza uchumi wa maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni hiki Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi wa Magari ambacho kinajulikana kama *One Stop Inspection Station* na kipo katika Kijiji cha Muhalala. Hiki kituo kimefikia asilimia 50 ya ujenzi wake yaani *execution rate* na kwa mwaka huu tumetengewa milioni 120 kwa ajili ya ujenzi wa hiki kituo na tayari pale kuna magofu ya majumba zaidi ya miaka miwili yamekaa mradi ulikuwa umesimama. Hoja yangu ni nini? Kwanza nitapenda kujifunza kutoka kwa Waziri je, hii milioni 120 imewekwa kwa ajili ya vitu gani? Ningependa kupata *narrative* ya hii milioni 120 inaenda kukamilisha asilimia ngapi? Nasema hivi kwa sababu amesema kwamba ni asilimia 50 tu ambayo tayari tumeshakamilisha, bado asilimia 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya pili ningependa kujifunza kutoka kwa Waziri vilevile, atuambie kwamba, je, anategemea huu mradi utaenda kukamilika lini? kama umekaa miaka miwili Serikali haijapeleka fedha, *then* mwaka huu anatuwekea milioni 120 na tayari ni asilimia 50 tu ndiyo ambayo imeshakamilika, je, hiyo milioni 120 itaenda kukamilisha hiyo asilimia 50. Kwa hiyo, ningependa kupata majibu haya kutoka kwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nirudie tena kumshukuru sana Waziri, lakini vilevile, niwashukuru sana ndugu zangu wa *TANROADS* Mkoa wa Singida, wamekuwa na mchango mkubwa sana. Tuna barabara yetu ya kutoka Solya kwenda Londoni kwenda Ikungi kwa muda mrefu hii barabara ilikuwa haipitiki kipindi cha masika, lakini hawa ndugu zetu wa *TANROADS* wa Mkoa wa Singida kwa kweli walikuwa very *proactive,* tulikuwa tukiwapigia simu wanakuja kutoa ushirikiano mkubwa sana kwa ajili ya kutengeneza barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hii barabara ya kutoka Manyoni kwenda Heka kwenda Sanza kipindi cha masika ilikuwa haipitiki. Hawa ndugu zetu wa *TANROAD* wa Singinda walitusaidia sana, tulikuwa tunawakuta wamefika *site* wanakuja kurekebisha. Kilio chetu kikubwa ni hii barabara ya kutoka Manyoni kwenda Heka kwenda Sanza inakuja kutoka Mbambala inakuja kuingia Dodoma, Rais Hayati Magufuli alituahidi kuweka kiwango cha lami, nitapenda kusikia kutoka kwa Waziri anawaambia nini wananchi wa Manyoni sasa hii ahadi ambayo Rais wetu mpendwa hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba niishauri Wizara, kuna ahadi nyingi sana ambazo zimetolewa na viongozi wetu wakubwa, wengi wamesema kuna ahadi kuanzia Awamu ya Tatu, ya Nne na Tano. Ningeishauri Wizara wafanye *mapping* ya ahadi zote, unajua hawa wenzetu wakubwa wakishaahidi wananchi wetu wanakuwa na imani kubwa sana. Hivyo, ni vizuri tukatengeneza *mapping* na tukatengeneza *planning* ya jinsi gani kila mwaka wataenda kupunguza zile ahadi. Hawa ni viongozi wakubwa, wametumikia hili Taifa, tunahitaji kuwapa heshima, lakini tukumbuke ahadi ni deni. Mbaya zaidi...*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele imeshagonga.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Venant Daud, atafuatiwa na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga na Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, ajiandae.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi ambayo imewasilisha hotuba yake leo

asubuhi. Kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali na Wizara kwa ujumla kwa kujenga Barabara ya Chaya - Nyahua ambayo ilikuwa ni kero kwa wakazi wa Mkoa wa Tabora, lakini nishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuikamilisha kwa asilimia 100 ambayo ilikuwa katika Jimbo langu la Igalula, wananchi wa Igalula wanashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii imetoa fursa kwa watumia barabara hasa wa Mikoa ya Shinyanga, Simiyu na Mwanza badala ya kupita Igunga sasa wanapitia Jimbo la Igalula. Nitoe wito wanapopita katika Jimbo la Igalula tuna migahawa mizuri sana wakifika Tula pale kuna mama mmoja anaitwa mama Tausi, wakifika wapite pale kuna kuku wa kienyeji, anajua kuwapika vizuri. Vile vile wakipita Kizengi pale kuna mgahawa mmoja unaitwa Tula Mgahawa, basi mambo yanakuwa mazuri. Naibu Spika nawe karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani zangu hizo nirudi, mkandarasi amemaliza ujenzi wa barabara, Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi nilikwishamwandikia barua ya kumwomba majengo yale ya Kizengi. Naomba wakimaliza na wakakabidhi mradi, basi naomba yale majengo waikabidhi halmashauri yangu ili tuweze kufanyia utaratibu mwingine hasa tuweze kupata kituo cha afya kwa sababu Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi imetuelekeza tutajenga vituo vya afya kwa kila kata. Kwa hiyo, wakinikabidhi yale majengo nitayatumia kwa ujenzi wa kituo cha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nichangie baadhi ya mambo kidogo, pamoja na mazuri wanayoyafanya Serikali lakini bado tunachangamoto ya upatikanaji wa barabara. Kuna Kamati iliundwa ya Mapitio ya Barabara, sasa hii kamati ilivyoundwa ilikuwa inaenda kuzitambua barabara ambazo zinatekelezwa na *TARURA*, lakini mpaka leo kamati hii imekwishamaliza kazi, lakini hatujui hizi barabara ni lini zitaingizwa kwenye mfuko wa upatikanaji wa fedha wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kwangu kuna barabara ambazo ni uchumi, ni muhimu sana katika maeneo yangu, zinaunganisha wilaya na wilaya, lakini zingine zinaunganisha mkoa na wilaya nyingine ndani ya mkoa mwingine. Kwa mfano, kuna Barabara ya Makibo – Msololo – Goweko - Kamama mpaka Nyahua. Hii barabara ina zaidi ya kilometa 80, tunapoisema barabara hii ni muhimu sana kwa sababu inatoka katika Wilaya ya Sikonge inakuja katika Wilaya ya Uyui. Tukisema itekelezwe na *TARURA* haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni tulikuwa tumeweka utaratibu mzuri wa kuainisha hizi barabara, tunazipandisha hadhi *TANROAD* wanafanya utaratibu mzuri wa kuweza kuzitengeneza, lakini utaratibu ule Wizara waliukataa, wakasema hizi barabara zitekelezwe na *TARURA.* Leo wilaya yangu inapata bajeti ya *TARURA* 1.2 bilioni, ukisema utekeleze hii barabara yenye kilometa 80, tutakuwa tunawaonea *TARURA*. Niombe Serikali ni ile ile, *TARURA* ni ile ile, niombe Waziri atakapoongeza fedha kwenye Mfuko wa *TARURA* hata kwa *emergency,* basi atakuwa ameokoa wananchi wa Kata ya Jimbo la Igalula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Barabara ya Sikonge inakuja Igalula inatokea Goweko, nayo barabara ni nzuri sana kwa uchumi wa wananchi wa Sikonge na wananchi wa Jimbo la Igalula, Wilaya ya Uyui. Leo Mheshimiwa Kakunda akiwa anataka kwenda kufanya ziara kwenye kata moja inaitwa Makibo, lazima afike Tabora Mjini, baadaye arudi tena huku Makibo, ni kilometa nyingi sana anapoteza rasilimali mafuta, lakini angeweza kupita hii barabara basi angeokoa mafuta na hizo fedha zingine akaelekeza kwenye miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya barabara kila mahali ipo, lakini hizi barabara ambazo tunazozipigia kelele, Waziri anaweza kusema *TARURA* wanatekeleza kwa bajeti iliyopo kiuhalisia *TARURA* hawawezi kutekeleza bajeti hii. Nimwombe Waziri kupitia mafungu yake akipeleka *TARURA* fedha za dharura kule, basi wanaweza kuzifungua

barabara hizi na hatimaye zikafunguka na wananchi wakaweza kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye suala lingine ambalo ni kuhusu *TRC*, kwangu wananchi wanategemea sana uchumi kwa kupitia reli ya kati. Hata hivyo, tulikuwa tuna urekebishaji wa miundombinu ya reli ya kati ambayo walimtafuata mkandarasi akawa anatengeneza reli ya kutoka Manyoni kuja Tula, Malongwe ikaelekea Goweko mpaka Tabora Mjini. Sasa cha ajabu ninachokishangaa tulikuwa na miundombinu ya njia tatu katika *Station* ya Goweko, huyu mkandarasi badala ya kurekebisha reli akaanza kung'oa tena njia zingine, ameua njia zingine, zile reli hatujui amezipeleka wapi, sasa wananchi wa Kata ya Goweko wanauliza alikuwa anakuja kubomoa miundombinu au alikuja kurekebisha miundombinu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunategemea zile reli kwa kukuza uchumi wa wananchi wetu kwa kukata mabehewa na kupakia mizigo pale, lakini vile vile, *train* ikiwa inapita pale ikiweka njia mbili upishano wa *train* na *train* wananchi wetu wanapata biashara, lakini sasa leo imekuwa njia moja, *train* inasimama kwa dakika tano, wananchi hawafanyi biashara. Nimwombe Mheshimiwa Waziri tunataka kujua zile reli zimekwenda wapi? Wananchi wanahitaji pale reli ziwe za njia mbili *train* ipishane, mabehewa yakatwe, ili waweze kupata uchumi na pale sisi tunatengemea sana uchumi wa *train*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *station* ile pale tunategemea sana katika uchumi na abiria wapo wengi sana, lakini leo cha ajabu tangu shirika limeanza ile *station* hatuna choo cha abiria, abiria wakija pale wao wameshajisevia kutoka nyumbani wakifika pale hakuna huduma nyingine itakayoendelea. Kwa hiyo, tunaingiza fedha nyingi kupitia *station* ile, tunashindwa kujenga hata choo cha shilingi mbili na tuna kampeni nzuri ya choo bora, lakini *station* yetu kupitia Wizara yetu inashindwa kujenga choo. Niiombe Serikali yangu, Wizara yangu wakajenge choo

pale gharama yake ni ndogo sana ili wananchi na abiria wanaowasafirisha wapate huduma nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna changamoto nyingine, Serikali imeleta umeme ambao ni Sh.27,000/=, lakini *station* ile imekuwa giza miaka yote na umeme upo, lakini mpaka leo tunashangaa kwa nini *train* zikipita usiku wananchi wanapata adha, pale kuna uwizi unaotokea wakati wananchi wanasubiri abiria iweze kuja pale, giza limekuwa kubwa Sh.27,000 mimi Mbunge wao nitalipa wakafanye *wiring.*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, naam, muda umekwisha, jamani!

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, atafuatiwa na Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar na Mheshimiwa Benaya Kapinga, ajiandae.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu ya Ujenzi na nitajikita zaidi katika maeneo mbalimbali ya Jimbo la Kilolo jimbo ambalo ni pendwa sana kwa upande wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia kiundani nataka nitoe tu mlinganisho wa bei za vitu unaotokana na ubovu wa miundombinu katika eneo la Kilolo. Mfano, ubao wa mbili kwa nne unaouzwa Sh.6,000 Mafinga, Kilolo utauzwa kwa Sh.3,500 na hii ni kutokana na changamoto za miundombinu ya usafirishaji. Sasa Barabara hii ya kutoka Iringa Mjini kwenda Kilolo hadi Idete ni barabara

ambayo ni ahadi za Maraisi kadhaa kama zilivyo barabara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii kwa kiasi fulani nianze kuipongeza Wizara kwa kazi ambayo tayari inafanyika. Najua kuna kilometa 10 ambazo mkandarasi yupo kazini, amekuwa taratibu kidogo, huyu mkandarasi amefanya kazi pale kwa karibu miaka mitatu, nimepita hivi karibuni nimeona sasa angalau kazi inaendelea, inatia moyo. Nafahamu pia kwamba kuna kilometa tatu nyingine za kutoka kwenye daraja pale Ndiwili kuelekea mjini ambazo zimeshapata makandarasi, nalo pia ninalipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tutakuwa tumebakiza kama kilometa 13 hivi kufika Iringa Mjini, naomba, nimeona imetengwa shilingi 140, sijajua milioni 140 ni ya kilometa ngapi, lakini imeandikwa kwamba ni kuweka lami kwa hizo kilometa zilizobaki, basi naomba kama ambavyo barabara nyingine zina umuhimu, hii milioni 140 iongezewe ili ile barabara iweze kufika Iringa Mjini. Hiyo ndiyo wilaya peke yake kwenye Mkoa wa Iringa ambayo haijaunganishwa na barabara ya lami hadi kwenye Makao Makuu ya Mkoa. Kwa hiyo kama tutakamilisha hiyo, nitakuwa na sababu ya kupongeza na nitakuwa naunga mkono hoja zenu kwa moyo mkunjufu kwenye miaka ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia nizungumzie kuhusu hii barabara ambayo inatoka Ilula inapita Mlafu inaenda Ukwega - Kising'a - Mtitu na inakuja kutokea Kilolo ambayo uchumi wake ni mkubwa na tayari kutokana na athari za mvua barabara hii inapitika kwa shida sana.

Kwanza inatakiwa ifanyiwe *maintenance* ya kawaida kabla haijawekwa lami, lakini mapendekezo yangu, kwa sababu barabara hii inasumbua mara nyingi kwenye maeneo kadhaa na kwa sababu tayari Meneja wa *TANROADS* ameshafanya ubunifu wa kukata baadhi ya milima ili barabara ile iweze kupitika kwa urahisi jambo ambalo tunapongeza. Ningependa yale maeneo ambayo yana hali ngumu zaidi yanapitika kwa shida na yale maeneo mbayo

udongo wake ni shida hata ukiweka kokoto inazama yale yafikiriwe kuwekwa lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwe na mpango wa kuweka lami katika maeneo korofi, sisi hatusemi muweke yote, sisi tunasema waweke maeneo korofi, wakitupa kilometa mbili tutachagua sehemu ya kuweka, wakitupa kilometa tatu tutachagua sehemu ya kuweka, ili mradi magari yaweze kupita kwa muda wote. Kule sasa hivi kuna watu wengi ambao ni wazawa wanaoitwa wawekezaji, wanafanya kilimo cha maparachichi na tayari wameshaanza kuuza. Njombe bei ni kubwa kule sasa hivi wanauza kilo moja ni Sh.1,000, tatizo ni miundombinu ya barabara hiyo ambayo ni barabara inayokatisha kwenye eneo kubwa sana la Jimbo la Kilolo na ni barabara ya muhimu. Naomba barabara hii itiliwe mkazo hasa kwenye *maintenance* na kwenye kuweka lami kwenye maeneo korofi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kujielekeza, ni kuhusu utaratibu wa kupaki magari hasa Ilula na Ruaha Mbuyuni. Sasa hivi pale Ilula kimewekwa kituo nafikiri ni cha watu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, sasa wameweka banda pembeni ya barabara na magari sasa yanapaki pale yanaziba ile barabara kabisa. Nafikiria hizi sehemu kama Ilula ambapo kunahitajika ile barabara iwe wazi, basi kama kunawekwa kituo chochote cha kiserikali kitafute namna nzuri kama ilivyofanywa mizani. badala ya kuweka *stop* ambazo zinazuia barabara hasa kwenye haya maeneo. Tatizo hilo linaweza likawepo hata kwenye maeneo mengine, lakini kwa uchache nitayataja hayo maeneo mawili Ilula na Ruaha Mbuyuni ambayo nimepita na kuona na kuona kwamba ile ni changamoto kubwa na ningefikiria kwamba ingeweza kufanyiwa marekebisho ili magari yaweze kupita kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kutaja eneo lingine ambalo kama lingekarabatiwa vizuri lingetusaidia. Barabara hii kutoka pale Kidabaga kuna milima michache, kuna Mlima Msonza uko pale, wenyewe huko nyuma ulikuwa haupitiki kabisa, lakini baada ya ukarabati

ule mkubwa unapitika, lakini ile mifereji ile miundombinu yake kwa sababu milima ya kule inamomonyoka, Serikali inatumia fedha nyingi sana kuchimba ile milima, lakini kwa sababu hakuna namna yoyote inayowekwa ili kuzuia ile milima isimomonyoke ile milima inaendelea kumomonyoka na kuharibu tena barabara. Kwa hiyo kuna namna ya kutengeneza ile miundombinu ya mifereji ili barabara zile ziendelee kudumu kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zile sehemu zote pia hapo kwenye Mlima Msonza ukienda kama unaenda Idete kuna milima mingine kama miwili, ile nayo kwasababu ni milima ambayo ni sumbufu kwa muda mrefu na yenyewe ingeweza kufikiriwa kuwekwa lami. Tunapozungumzia lami hatuzungumzii, sisi hata ingewekwa kama hii ambayo ni ya kwenda Iringa iliyochanikachanika hata ikimwagiwa kokoto kokoto tu sisi hatuna tatizo ili mradi iweze kupitika mwaka wote. Kwa sababu sisi hatutajali sana ubora ili mradi ipitike tu mwaka mzima, nafikiri hapo hata bei itakuwa nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hizi milioni 60 walizotuwekea, milioni 140 wakiongeza tu kama milioni 300 hivi angalau tutapata kilometa saba au nane zitasaida katika yale maeneo ili wananchi waweze kupita kwa urahisi na waendelee vizuri na shughuli zao za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili niweze kuweka mkazo kwenye hizi barabara ambazo nimezitaja labda niendelee kuweka msisisitizo zaidi kwenye kipengele cha barabara nyingine ambazo zipo katika Mkoa wa Iringa na niza kiuchumi na kwa kweli tulikubaliana katika Mkoa wa Iringa kuendelea kuzitaja hasa zinazoingia kwenye mbuga za Wanyama. Na hapa nataka nikumbushe kwamba mbuga ya wanyama ya Udzungwa ambayo kwa kiwango kikubwa iko katika Wilaya ya Kilolo asilimia 80 lango lake la kuingilia liko Morogoro ambako ni asilimia 20 tu ya mbuga ndiko iliko na hii inatokana na tatizo la miundo mbinu la barabara inayotokea pale Mahenge na kuingia Udekwa ambapo kuna geti ambalo ndiko asilimia 80 ilipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na hii barabara ilishachimbwa kilomita 14 lakini haikutoboka kwa hiyo walianzia Udekwa wakachimba kilomita 14 wakaitengeneza tu vizuri kabisa lakini imebaki kilomita 7 kuingia kwenye lami. Sasa kule kunaota majani huku walikochimba kilomita 14 ni *useless* kwa sababu hakuna mtu anayepita kwenda asikofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningependekeza pia kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili ambako ndiko geti liliko lile geti la Udekwa waweze kwenda kuangalia kama ilikuwa ni halali kuchimba barabara na kuacha kilomita 7 kutoboa kwenye barabara ya lami halafu unaishia hapo halafu ile barabara inakuwa yakwenda porini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sasa hivi wanapita tu Ngedere Tumbili na wanyama wengine waliopo kule, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kuna mazingira mtu unapita unasema kweli hivi huyu injinia hamna kozi fupi yaani pengine Wabunge tukipitia hizo zitatusaidia kuelewa. Yaani kuna maeneo unaenda barabara imeanza kutengenezwa kijijini badala ya kuanzia mjini ambako lami iko ili ianze kuelekea kijijini yaani mnaanzia kijijini ndo mnakuja mjini sijajua nayo kama ni utaalam au ni vipi? *(Makofi)*

Kwa sababu mazingira hayo ndo hayo sasa ya hiyo barabara, mmeanzia kule ndani halafu huku barabarani hamjatokeza sasa kule ndani inafanya kazi gani sasa. Kwa hiyo, unaweza kuangalia yani sijui kama na lenyewe ni la kitaalam ni vipimo sijui lakini sielewagi barabara inaanzaje kutengenezwa kijijini ikielekea mjini yani uwa sielewi kabisa.

Labda kwa sababu sio mhandisi lakini ni mambo ya kuyatazama kwa sababu kama hapo maana yake fedha zimefukiwa sasa na hazifanyi kazi yoyote. Mheshimiwa Bakari Hamadi Bakari atafuatiwa na Mheshimiwa Benaya Kapinga Mheshimiwa Ng'awasi Damiani Kamani ajiandae.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii kuweza kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Tangia asubuhi leo hapa zinazungumzwa barabara tu hapa, lakini bahati nzuri nitahama kwenye eneo hilo la barabara nitakwenda kuchangia kuanzia haya ya 225 mpaka haya ya 227 ambapo inazungumzwa mamlaka ya hali ya hewa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge la kumi na moja lilipitisha Sheria Na. 2 ya mwaka 2019 Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, ni matarajio ya Bunge hili pamoja na Taifa kuona kwamba sheria ile inakwenda kuleta tija kwa Taifa lakini tija kwa mamlaka hii ya hali ya hewa Tanzania. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri tangia kupitishwa kwa sheria ile Sheria Na. 2 je ni mafanikiko gani yaliyopatikana kwa Taifa ama kwa mamlaka hii mpaka leo hii 2021? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza haya kwa sababu kwenye sheria ile Na. 2 wapo wadau mbalimbali ambao wametajwa kwenye sheria ile bandari ni mdau wa hali ya hewa *aviation* ni mdau wa hali ya hewa mazingira, viwanda watu wa nishati barabara majanga kilimo afya sayansi na teknolojia wote hawa ni wadau wa hali ya hewa hasa namuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie je wanaitumiaje wadau hawa sheria ili Na. 2 ya mamlaka hii ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba sheria haiwezi kutumika ipasavyo kama haijatengenezewa kanuni, lakini tangia mwaka huo ambapo sheria hii ilipitishwa lakini mpaka leo hakuna kanuni ambazo zinaiongoza kuifanya sheria ile iende ikatumike inavyopaswa. Sasa tunamuomba Mheshimwa Waziri atakapokuja atueleze je kanuni za Sheria Na. 2 ya mwaka 2019 imefikia wapi? imekwamwa wapi? tatizo ni nini kwamba mpaka leo kanuni zile hazijapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna bahati tumepata bahati ya kuwa na chuo kinachotoa taaluma ya hali ya hewa kwa nchi za Afrika ni nchi chache sana zenye

bahati zenye vyuo ambavyo vinatoa taalum hii. Kwa nchi za Afrika nchi za *SADC* na hasa nchi za Afrika Mashariki ni nchi chache sana tulitegemea sana kwamba chuo hiki kingeweza kuitangaza Tanzania, lakini kingeweza pia kuongeza mapato ya mamlaka lakini pia kuitangaza Tanzania kupitia taaluma hii ya hali ya hewa. Lakini hatuoni kwamba kuna mikakati ipi ya kukifanya chuo hiki kuwa tija na kuitangaza Tanzania kuongeza mapato ya nchi yetu lakini kuongezea mapato ya mamlaka ya hali Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo tutakiwezesha chuo hiki kimiundombinu naamini kwamba mapato ya mamlaka ya hali ya hewa yataboreka na maslahi yatakuwa mapana zaidi na tija kwa Taifa itakuwa pia itaongezeka. Namuomba waziri atakapokuja atuambie ni mikakati ipi aliyonayo kwenye kukiboresha chuo hiki cha mamlaka ya hali ya hewa ambapo kipo pale Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana nami kwamba kipindi hiki tulichonacho ni miaka ijayo ambapo majanga yanatokana na hali mbaya ya hewa taasisi hii ya mamlaka ya hali ya hewa ni taasisi muhimu sana kwa Taifa letu na kwa dunia. Umuhimu wa taasisi hii umeonekana zaidi hata hapa kipindi cha karibuni niipongeze sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niipongeze mamlaka hii kipindi cha jaribio cha kimbunga cha jobo walikuwa wanatuhabarisha mara kwa mara bila ya habari zile nchi ingekuwa ipo katika wasiwasi sana watu walikuwa na wasiwasi na mali zao lakini watu walikuwa na wasiwasi na maisha yao lakini kupitia mamlaka hii tulikuwa tunapata taarifa za mara kwa mara na ile presha ilikuwa inashuka kila *time* ambapo ilikuwa inakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamuomba sana Mheshimiwa Waziri atueleze ana mikakati gani ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi hili wafanyakazi wale waweze kufanya kazi zao kwa utulivu na moyo zaidi wa kujitolea. Sasa hivi kumekuwa na wafanyakazi wengi wa mamlaka hii wanatoroka kwa maana wanakimbia wanakimbilia sehemu

nyingine ambazo taasisi ambazo zina maslahi zaidi. Lakini pia kuna wafanyakazi ambao wamepewa barua za kupandishwa madaraja tangia 2016 mpaka leo hii 2021 barua zile zinabakia kuwa ni hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamuomba waziri atakapokuja atueleze ni kwa nini na lini maslahi ya wafanyakazi ni lini madaraja ya wafanyakazi pale ambao wana muda mrefu awajapandishwa madaraja ni lini sasa watapandishwa madaraja lakini ni lini barua zile zitajibiwa tangia 2016 mapaka leo 2021 watu wamepewa barua ya kupandishwa madaraja lakini hadi sasa hakuna kilichofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia tunafahamu taasisi hii ni taasisi ya muungano kama ilivyo sasa namuomba sana Mheshimiwa Waziri naiomba pia Serikali inapoajiri ajira hizi za taasisi ya muungano iangalie zaidi pande zote mbili, za muungano ile *ratio* ya 79 kwa 21 ianze kutekelezwa hasa kwenye taasisi hizo za muungano. Sasa hivi tunazungumza kwamba kuna *ratio* 79 kwa 21 maana zile ajira za muungano kwa Tanzania bara zitakuwa ni 79 asilimia lakini kwa Tanzania visiwani itakuwa ni asilimia 21 naomba sana tutakapo ajiri taasisi hizi za muungano basi tutumie hii *ratio* ili kuweza kuweka usawa kwenye ajira za taasisi zetu za muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya kusema hayo nikushukuru sana ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Benaya Kapinga atafuatiwa na Mheshimiwa Ng'wasi Damian Kamani, Mheshimiwa Sofia Mwakagenda ajiandae.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru awali ya yote niungane na wenzangu hasa Mbunge wa Jimbo la Mbozi kwa masikitiko makubwa kusema kwamba sisi wa mikoa ya Kusini hususani Jimbo la Mbinga tumesahaulika sana, wananchi wa Jimbo la Mbinga kwa muda mrefu tukitambua kwamba wao ndio wakulima

wakubwa nchi hii,wazalishaji wakubwa wa mahindi wazalishaji wakubwa wa kahawa lakini pia sisi ni wachimbaji wa madini mmesikia habari za mpepo mpepai ni wachimbaji wa madini sasa hivi tunachimba makaa ya mawe lakini kwa muda mrefu sana sana Mbinga imetengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hivi tu karibuni tumebahatika kupata barabara moja inayotoka *Mbambabay* inapitita Mbinga inaenda Songea sasa pale inagawika nyingine inaenda Mtwara na unaweza kuja makambako njombe na kuendelea kwa mara ya kwanza lakini tumesubiri tangu kupata uhuru nchi hii. Wananchi wa Mbinga ni watiifu sana katika nchi hii na tangu hapo hawajawahi teteleka wamebaki kuwa watiifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi wa kwanza niliuliza swali hapa kuhusiana na barabara ya kutoka Kitai hadi Lituhi, nikajibiwa hapa majibu vizuri sana, barabara hiyo tutuijenga kwa awamu kuanzia mwezi wa nne majibu yale wananchi wanayasikia nimeenda hivi karibuni hapa wananiuliza mbona kimya imekuwaje kwa bahati nzuri nimepata swali la nyongeza Bunge hili nikaambiwa wako kwenye utaratibu wa tenda tena sio kwa kiasi kidogo tunaitengeneza hii barabara yote kuanzia Kitai mpaka Lituhi ikipitia Rwanda Ndongosi, na maeneo mengine. Lakini sasa lini tunaanza kuitengeneza hii barabara ilikuwa mwezi wa nne hamna kitu hii ni mwezi wa tano tunaenda na humu kwenye bajeti nashukuru nimeona kidogo kwa nini nasema kidogo nimeona hii barabara ina kilometa 90. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapa nimeona bilioni 11 na milioni 500 lakini maelezo yanasema kuna vipande vipande vya kwenda kulipa madeni kumlipa mkandarasi aliyekamilisha barabara ile ya kutoka Mbinga Mbambabay sijui ni kiasi gani. Lakini inaenda kulipa kipande cha Namtumbo sijui ni kiasi gani inaenda kulipa tena kipande kingine kule juu Masasi sijui sasa najiuliza na nashangaa, ni kiasi gani kinaenda kujenga hizi kilometa 90. Mambo haya ni ya ukweli au ndio yaleyale tunayosema sisi wa kusini sasa tusubirie wenzetu wamalize kujengewa hizo barabara zao

kwa kweli kwa mtindo huu naungana na Mbunge wa Mbozi tuko tayari kufanya kitu hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani kwani sisi sio watanzania sisi ni watanzania tunalipa kodi na tunazalisha sana kwa nini tusijengewe na sisi barabara kama huko zinakofumuliwa hizo nyingine.

Kwa hiyo, ndugu yangu Mbunge wa Mbozi mimi niko tayari kukuunga mkono kichwa miguu kila kitu tukubaliane hapa na sisi tujengewe barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi wa kwanza pia nimeuliza hapa swali Rais wa nchi hii alipokuwa anapita kuomba kura alitoa ahadi ya kujenga barabara kwa kiwango cha lami, kuanzia Mbinga kwenda Litembo. Litembo ndiko sisi tunakotibiwa kuna hospitali ya misheni kule miaka yote tangu uhuru ndio inayotusaidia sisi, namna ya kufika hapo Litembo ni shughuli kubwa. Naibu Waziri *Engineer* Kasekenya anafahamu lakini pia hata Naibu Waziri wa TAMISEMI nilienda nae mpaka Litembo alishika mikono kichwani kwamba ehh hivi mnapitajepitaje huku tulimpeleka hivyo kwa hiyo yale uliyosema kwamba tuwapeleke.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilijaribu kumpeleka Naibu Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Silinde, halishika mikono kichwani na tulimchangulia kinjia fulani cha kujipenyeza angalau lakini tungempitisha zile njia tunazopita sisi nadhani angemwambia dereva arudishe uongo, ukweli yule pale anasema kweli hali ni mbaya sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa bahati nzuri barabara ile kabla ya awamu hii alifika Rais wa Awamu ya Nne baada ya kuona matatizo kwenye ile barabara akatoa ahadi ya kujenga kwa kiwango cha nini cha lami. Miaka kumi ile imepita tumefika Awamu ya Tano ikatolewa ahadi imepita na bahati nzuri Awamu hii ilikuwa ya Tano imeingiliana hivi Rais wa sasa hivi ndiye aliyepita kule alienda akaja akatupa ahadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeuliza swali hapa majibu yale hayaeleweki mpaka sasa hivi sijui nitawaambia nini wananchi wa Mbinga kwamba lini ile barabara itaanza kujengwa na naomba sasa ile ni ahadi ya Rais wa nchi hii. Naomba kupata ufafanuzi lini ahadi ile inaenda kutelezwa ni pamoja na barabara ya kutoka Kigonsera kwenda hadi Matili lakini hiyo barabara inaenda mpaka Hinda kwa Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya na yenyewe ipo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliuliza swali hapa hiyo ni ahadi ya Rais kwamba tunakwenda kujenga barabara hizi kwa kiwango cha lami Mheshimiwa...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana muda umeisha Mheshimiwa kengele imeshagonga.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Sio ya kwanza?

**NAIBU SPIKA:** Ni ya pili!

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, basi kwa shida sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ng'wasi Damian Kamani atafuatiwa na Mheshimiwa Sofia Mwakagenda Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ajiandae.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii ya kuchangia katika wizara hii, kwanza kabisa nianze kwa kuipongeza wizara hii na watendaji wake wote kwa hatua hii ya utendaji ambayo imefikia lakini pili niungane na Mheshimiwa Eshi kukipongeza Chama changu Cha Mapinduzi kwa ushindi mkubwa kilichopata kule mkoa ni Kigoma katika jimbo la Mwihambwe na Bwihigwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto ya ajira tuliyonayo vijana katika nchi hii, sehemu ya kandarasi ni moja ya sehemu ambazo vijana wengi wamejikita katika

kutatua changamoto hii ya ajira. Lakini bado pamoja na juhudi hii wanayoifanya kujiingiza katika sehemu hii wanachangamoto nyingi na changamoto kuu ambayo tunakutana nayo ni ukosefu wa mitaji na ujuzi wa kutosha kujiingiza katika kazi hizi za ukandarasi hasa ukandarasi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inanifanya nijiulize ni lini hasa au Serikali inadhani ni lini hasa tutaendelea kutoa asilimia zaidi ya 70 ya kazi zote ambazo zinazofanyika katika nchi hii kwenda katika makampuni ya kigeni ili hali asilimia kumi tu ya makampuni yaliyosajiliwa ndio ya kigeni hii ni aibu sana. Nadhani ni wakati sasa Serikali ijihoji kwamba tuna mkakati gani wa miaka 2, 3, 4, 5, 10 au hata 50 kwa kuhakikisha kwamba na sisi itafika wakati wakandarasi wa kitanzania watafanya kazi zetu za hapa ndani kwa asilimia 70 na wakandarasi wa nje wafanye kwa asilimia 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ilani yetu ya uchaguzi tuliyotumia kuomba kura zaidi ya asilimia 90 ya Wabunge tulioko katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 72 ni kushirikisha kikamilifu vikundi vya wanakijiiji na wananchi pamoja na makandarasi wadogo katika kazi za matengenezo madogo ya barabara kama vile kufyeka nyasi kuzibua mifereji mitaro ya barabara na kufanya usafi wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, "pili, kuendelea kuwajengea uwezo wakandarasi wazalengo ikiwemo kuwapatia kazi nyingi zaidi za fedha za mifuko ya barabara na kuwawezesha kupata mikopo ili kushiriki kikamilifu kwenye kazi kubwa za ujenzi wa barabara, madaraja na majengo." Maana yake tuliwaahidi vijana, hasa wakandarasi, kwamba kazi yetu ndani ya miaka hii mitano itakuwa ni kuhakikisha tunawajengea uwezo wa kushiriki katika kandarasi, hasa kandarasi kubwa, lakini pia kuwasaidia ili waweze kukopesheka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika changamoto hii ya mitaji, kwa kiasi kikubwa imechangiwa na Serikali yenyewe. Tunatambua kwamba kazi hizi ni kazi ambazo zinahitaji mitaji mikubwa na labda wengi wetu hatuna, lakini Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha inatubeba sisi vijana na kutuwezesha hivyo hivyo kushiriki katika kazi hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi yao wamejitahidi, wametuafuta hela huku na huku ikiwemo kukopa katika benki za kibiashara kuingia katika kazi hizi, lakini shida inakuja kwenye vipaumbele vya kulipwa. Kwa vile wageni katika kampuni zao wanakuwa wana-*raise invoice* kila baada ya mwezi na kudai *interest* katika *invoice* zile zisipolipwa kwa muda, Serikali yetu inawalipa wao kama kipaumbele kuliko kuwalipa wazawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo imekuwa changamoto zaidi ya kuua mitaji ya vijana hawa. Huyu mtu kakopa kwenye benki ya kibiashara, anatajiwa riba kila anavyozidi kuchelewesha malipo; na imefikia hatua mikataba wanayopewa Wakandarasi wetu wa ndani haiaminiki tena kwenye benki zetu na taasisi za fedha. Mtu hawezi kupeleka mkataba ule akapewa pesa ya mkopo ili aje afanyie kazi. Kwa nini? Kwa sababu Serikali haiwalipi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta mtu hana hata pesa ya kula, lakini anakwambia anadai Serikalini shilingi milioni 500. Ni kitu cha aibu sana. Wakati makampuni ya nje tunayalipa kwa wakati, wazawa tunawaacha pembeni, inatia mashaka kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili suala la kuhakikisha kwamba tunawashirikisha…

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer.* Mwanaisha Ulenge.

**TAARIFA**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji, Mheshimiwa Ng'wasi kwamba anachosema ni kitu sahihi. Siyo tu kwamba Wakandarasi hawa wazawa wa ndani wanachelewa kulipwa, lakini pia Wakandarasi wazawa wa ndani hawana jeuri ya kumwomba *client interest.* Ile 14.7 *billion* aliyoisema *CAG,* ile ni ya Wakandarasi wa nje. Wakandarasi wazawa wanaogopa kudai hata *interest* kwa sababu wanaogopa kukosa kazi kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa hiyo. Naomba niendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ambayo inapatikana kwenye kushirikisha hivi vikundi vidogo vidogo vya wananchi kwenye kazi hizi, hasa kazi ndogo ndogo ni kwamba, kwanza hakuna mikataba inayoeleweka wanayopewa watu hawa kabla ya kupewa kazi hizi na wengi wanaishia kukimbiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naongea na baadhi ya Wabunge wa Majimbo, pesa nyingi wanaishia kulipwa wao kwa sababu wale Wakandarasi wanawapa kazi hizi ndogo ndogo, wanaishia kuwakimbia. Kwa hiyo, nashauri Serikali iangalie utaratibu wa kuweza kuvilinda vikundi hivi vidogo vidogo vinapokuwa vinapewa kazi na wakandarasi wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye *bidding process;* tunatambua kwamba tenda hizi zinatolewa kwa uwazi, watu wanakuwa na uhuru wa ku-*bid freely,* lakini

tukiangalia Wakandarasi wetu wa ndani na wa nje, wa kwetu wako kwenye *disadvantage* kubwa kuliko wa nje. Kwa sababu wa nje kwanza kabisa wanapewa *support* kubwa sana na Serikali zao, kitu ambacho hakipo katika kandarasi zetu za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha pili, watu hawa wana-*bid* kwa bei ya chini wakiwa wameshajua kwamba upungufu wa ulipaji uliopo kwenye mifumo yetu ikoje na wanategemea faida wataitengeneza kwenye *interest,* kitu ambacho Mtanzania hana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri ni wakati Serikali iangalie namna gani inafanya juhudi ya makusudi kutekeleza yale tuliyoahidi kwenye ilani yetu kwa kuwapa *support,* kuwawezesha Wakandarasi wa ndani, kuhakikisha wanawapa kipaumbele kwenye malipo ili waweze kukua na mwisho wa siku basi tuone asilimia za Wakandarasi wanaofanya kazi zetu za ndani ni watu wetu wa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, tumeahidi kwenye ilani kwamba tutazidi kuwawezesha kuwapa kazi nyingi zaidi. Hapa kwenye hili, naomba Serikali kuangalia kwa umakini sana tunavyokwenda na hili suala. Sekta binafsi ni ya msingi sana kwenye maendeleo ya Taifa lolote lile, lakini sasa baada ya kuwa kandarasi nyingi za ndani zinasumbua kwenye ufanyaji wa kazi ikiwa ni pamoja na kazi kuishia njiani kwa sababu hawana pesa au wamecheleweshewa pesa, Serikali sasa ime-*resort* kwenye kutumia taasisi zake binafsi kufanya kazi hizi. Hilo ni jambo jema, kwa sababu najua Serikali haicheleweshi malipo kwenye taasisi zake zenyewe, lakini hii inakwenda kuua wakandarasi binafsi, inaua sekta binafsi ya wakandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, badala ya kuwanyang'anya kazi na kuzipa kazi taasisi za Serikali kama *TBA,* SUMA JKT, basi tuangalie namna gani ya kuwasaidia kuondoa changamoto walizonazo, ili basi tuendelee kuwakuza na sekta binafsi ikue zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kuna huu mfuko wa kudhamini Wakandarasi wadogo ambao ndiyo Serikali iliuanzisha kwa ajili ya kuwakomboa kwenye suala zima la mtaji, lakini Mheshimiwa Waziri amesema kwamba mfuko huu una shilingi bilioni 3.9 pekee mpaka sasa tangu uanzishwe na Wakandarasi walio ndani yake ni 1,167. Haitoshi kabisa kuwapa mtaji Wakandarasi hawa kufanya hizo kazi. Kwa hiyo, pia tunaomba Serikali iangalie katika bajeti hii namna gani inaongeza pesa katika mfuko huu ili Wakandarasi wa ndani wengi zaidi wapate kunufaika nao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwenye hizi kazi; tunashukuru Serikali imefanya kazi nzuri ya kuhakikisha wazawa wanaajiriwa zaidi kwenye kazi hizi za ukandarasi, lakini basi tunaomba iangalie namna gani wahusika wa eneo husika waweze kuwa wanufaika wa kwanza wa zile kazi zinazofanyika kwenye maeneo yao. Kwa mfano, tuna reli ambayo sasa hivi inatakiwa kujengwa kutoka Mwanza kwenda Isaka. Basi watu wa Mwanza na wa kanda ile wawe wanufaika wa kwanza wa tenda na kazi zinazopatikana kutoka katika reli ile, sambamba na maeneo mengine yote. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na mengi ya kusema, nitayachangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wa siku, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu na Mheshimiwa Boniphace Butondo, ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nitaanza na suala la *TAZARA.* Toka waasisi wa nchi yetu na nchi ya Zambia waunde *TAZARA* ni zaidi ya miaka 46 sasa. Waliunda kwa Sheria Na. 23 ya mwaka 1975.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TAZARA* imekuwa na matatizo ya kifedha kwa muda mrefu sana. Imeshindwa hata wakati mwingine kutoa mishahara na kwa wanaostaafu kwa wakati. Ninaiomba Serikali iweze kuwekeza fedha zake kwa watu wa *TAZARA* ili iweze kujiendesha. Tunajua kabisa *TAZARA* – na kama ulivyosema hapo awali, inasaidia Nyanda za Juu Kusini ambao sisi ndio tunaozalisha mali nyingi, na hasa chakula katika Taifa hili. Sasa tukiwekeza kwenye reli hii itasaidia sana upatikanaji wa chakula hata kwa Dar es Salaam na kwenda huko huko Zambia ambako tunapeleka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, natoa ushauri; kwa sasa tunajua kabisa barabara zetu zinaharibika kwa sababu ya shaba inayobeba toka Zambia kuja kwenye Bandari ya Dar es Salaam. Sasa iwekwe sheria kama ikibidi, watu wa Zambia wapitishe shaba hiyo kwa kutumia reli hii ili iweze kupata fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, wenzetu wa *TAZARA* ya Zambia wameacha na kuweka nguvu zaidi kwenye reli hii, wametuachia sisi wenyewe. Hivyo basi, tunaomba tuisaidie reli hii iweze kufanikiwa na hasa kupata fedha ya kulipa mishahara na kujiendesha mpaka hapo itakaposimama yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua *TAZARA* ina majengo katika stesheni zote, ina majengo pale *TAZARA* Makao Makuu, lakini bado wanashindwa hata kuweza kuitengeneza. Tunahitaji tuipatie fedha zaidi. Kama tuna miradi mipya ya *SGR* tumeanzisha, tunaweza tukawekeza katika *TAZARA* nayo ikaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie *TANROADS.* Kwenye ripoti ya *CAG;* wamesema *TANROADS* ilishindwa

kutoza tozo ambayo ilikuwa ni zaidi ya shilingi bilioni tano kwa watu wa Sanzali ambayo ilikuwa ni barabara ya kilometa 50. Sasa hili ni tatizo. Kama tunashindwa kufanya tozo, tunawezaje kupata mapato kama Taifa? Kwa hiyo, nawakumbusha watu wa *TANROADS* kuwa makini kusimamia shughuli ambazo tunawapatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Daraja la Kigogo na Busisi lilianzishwa kabla ya cheti cha kuangalia madhara ya kimazingira. Walianza ujenzi kabla ya kupata kile cheti. Tunawaomba sana wasifanye chochote mpaka wawe wametimiza haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tumezungumzia daraja lile la Jangwani, bado mpaka leo hii wanasema kwamba wanaendelea kuangalia upembuzi yakinifu na mambo kama hayo. Tunaomba wafanye haraka ili Jangwani isiendelee kuzama na watu waendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna shida ya pesa ya maendeleo. Tunapitisha sisi kama Bunge, tunasema tunatoa fedha hizi, lakini mwisho wa siku bado fedha hizo haziendi kwenye Wizara husika. Leo hii Kamati imetoa maoni pale, kwamba miezi minne imebaki fedha ziwe zimekwisha, lakini bado hawajaletewa fedha zote. Tumeona nyingine ni asilimia 30, nyingine asilimia 50; hatuwezi kufanikiwa kama hatutoi fedha na maendeleo yakaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba ujenzi wa viwanja vya ndege vile vya kimkakati. Kwa mfano, Viwanja vya Ndege vya Songwe, Moshi, Manyara na Iringa, hivi vimewekwa kwa ajili ya utalii, lakini bado havijaanza kuwekewa mkazo wa kujengewa pale. Tukija Uwanja wa Ndege wa Songwe, mpaka leo taa hazipo kwa hiyo, ndege haiwezi kuondoka usiku. Kwa hiyo, tunaomba waziweke hizo taa, maana ni muda mrefu tumekuwa tukilizingumzia suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ya wananchi ambao wamepisha ujenzi wa viwanja vya ndege, tunaomba

walipwe kwa wakati. Tunaomba tafadhali kwa sababu wananchi wanajitolea kwa ajili ya kuweza kusaidia maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia barabara za mikoa zinazounganisha vipaumbele kwa ajili ya maendeleo mbalimbali, kwa mfano, Kyela kuna barabara ambayo inaunganisha Kyela na Ileje, ile ni barabara muhimu sana. Tunafahamu Ileje kwa kupitia Mbeya ni mbali lakini wakijenga ile barabara ya Ileje kuelekea Kyela itatusaidia sana kufanya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado ninajua kwamba kuna shida ya vibali *TRA.* Pale barabara zinapojengwa *TRA* wamekuwa wakichelewa kutoa ule msamaha wa kodi na hiyo husababisha barabara zinapojengwa zinakuwa zinachelewa na kuleta deni kwenye Serikali yetu. Ninaomba waweze kusimamia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba niishie hapo na huo ndiyo mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Butondo na Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niongelee tu kwa ujumla sekta hii ya usafirishaji, kwanza sifa zake mahususi kiulimwengu ili sekta hii ionekane iwe bora. Sifa ya kwanza, ni lazima kuwe na mifumo mizuri iliyotengenezwa ya usafirishaji kwenye miji au tunasema *well designed inter-city systems.* Sifa nyingine ni ku-*avoid unnecessary traffic flows* au tunasema ni kuepuka ile misongamano isiyokuwa ya muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sifa nyingine ni kuhakikisha kwamba mifumo ya usafirishaji inapunguza gharama. Sifa nyingine ni kuhakikisha mifumo ya usafirishaji wetu inakuwa salama na ya uhakika. Nyingine ni kuhakikisha kwamba tunaweka mifumo mizuri ya usimamizi ya miundombinu yetu ya usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichangie pale kwenye kuweka mifumo mizuri ya usafirishaji kwenye miji yetu. Ndugu zetu hawa wa Wizara ya Ujenzi wao ni wataalam na bahati nzuri sana Waziri tuliyenaye alikuwa Katibu wa Wizara hii. Napenda kushauri jambo moja kwenye Wizara hii. Kwanza, kuangalia mifumo ya usafirishaji kwenye miji yetu. Ipo miji imekuwa sasa kama ni vigogo vya usafirishaji kwenye mazao yanayotoka kwenye mikoa mbalimbali na yanayotoka kwenye vijiji vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, umeongea kuhusu Mji wa Mbeya asubuhi, lakini mimi nitaongea kuhusu Mji wa Iringa pia. Miji ile inapita au ipo katikati ambapo barabara kubwa zinapita katikati ya ile miji. Tunafahamu katikati ya miji mikubwa kama ile, kuna shughuli nyingi za kibinadamu zinafanyika. Sasa wenzetu hawa ni wataalam, walipokuwa wanajenga miundombinu ya barabara hizi, wakifungua mikoa mingine walijua kabisa geti kubwa litakuja kuwa ni Iringa; walijua barabara kubwa itakayosafirisha magari makubwa yote kutoka kwenye mikoa sita inayotegemewa kulisha nchi hii kwenda kaskazini na Kanda ya Ziwa mikoa sita itapita katikati ya Mji wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walijua kabisa kwamba nchi zile ambazo ni *landlocked countries,* kwa mfano Zimbwabwe, zinapita katikati ya Jiji la Mbeya. Kwa hiyo, ilitakiwa wenzetu hawa watusaidie kutengeneza miundombinu ya kufungua yale majiji yasiwe *barrier*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii viazi vinatoka Songwe vinaozea Mbeya, au vinaanza kuungua Mbeya; vikifika Iringa vinataka kupita vije Dodoma viende Mwanza, vinafia Iringa. Kwa sababu miji haipitiki. Ni sawa na umetengeneza

barabara ya njia sita halafu unakwenda kuipitisha kwenye daraja la mita moja, lazima uvunje lile daraja; na ndicho kinachofanyika kwenye miji yetu. Mle kwenye miji ndiyo maana sasa kumekuwa na matatizo. Sisi Wabunge tumeongezewa kazi nyingine nje ya ilani kwenda kuanza kuzuia migomo inayotokea katikati ya vyombo vinavyopita kwenye miji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umeongelea mgomo uliotokea Mbeya; wiki iliyopita sisi Iringa tulikuwa tuna mgomo wa watu wa barabara, bajaji na bodaboda. Sasa hivi ninavyoongea, kuna vijana wengine pia wamegoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunafahamu, nami nawaomba Waheshimiwa Wabunge, mchawi bwana mkabidhi mtoto akulelee. Mimi nafikiri sasa *TARURA* tuwakabidhi hawa hawa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, iwe chini yao na wawe na *full mandate* ya kui-*control TARURA* ili sasa kule kulaumiana kwamba hapa alitakiwa atengeneze *TARURA,* kusiwepo. Wasimamie wenyewe kuanzia juu mpaka chini ili wanapofika kwenye mji ule waweze kuwasiliana na wenzao wa *TARURA* waangalie ni namna gani sasa mji huu tunaufungua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Iringa tuna *bypass.* Tunapoongelea miji hii mikubwa, kwa mfano pia Songea kuna *bypass,* Mbeya kuna *bypass.* Sasa hizi *bypass* waliziweka kabisa kitaalam, wamelipa fidia, wamefanya kila kitu, yaani kinachotakiwa ni kuzijenga. Kwa mfano, Iringa tuna kilometa 7.3, ili tuchepushe yale magari makubwa yapite pembezoni *activities* nyingine katikati ya mji ziendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo tunakuja kwenye ile sifa nyingine ya kupunguza *unnecessary traffic flows* kwenye miji. Hizo ni *unnecessary,* tungekuwa tumejenga zile *bypass* tusingekuwa na sababu ya magari kuja pale. Njegere za akina mama zinaozea kwenye barabara, viazi vya vijana wetu...

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Twaha Mpembenwe.

**TAARIFA**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimpe taarifa mzungumzaji kwamba tatizo hilo la kutoweza kuzijenga barabara kwa wakati kama mifano tunayopewa ya barabara ya kutoka Mbeya kwenda Tunduma na barabara nyingine za Iringa, barabara ya Kibiti mpaka Mloka, hii yote ni kutokana na sababu ya mambo ya utelezi. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msambatavangu, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili. Niseme kwamba huu utelezi ndiyo tunataka utolewe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *bypass* zijengwe kwenye miji yetu. Kwa nini tunasema *bypass* zijengwe? Kwa sababu mijini ndipo huduma za jamii zinakopatikana, watu wetu wanakwenda kupata huduma kule. Watu wanafia barabarani. Pia mijini ndiko kwenye masoko. Wewe umefikisha bidhaa mpaka stendi inashindwa kufika sokoni kwa sababu tu ya *traffic jam.* Sasa uangalie, huo ndiyo utelezi tunasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, angalia Mji kama Iringa, kwanza barabara yenyewe ya Tanzam inapita iko kwenye mlima, malori makubwa yote yanakwama pale. Lori likianguka katikati pale, Iringa haipitiki kwenda chini, kwenda juu; na malori ya dagaa zilizotoka Mwanza zinaozea pale. Tunawaomba wenzetu waangalie haya, tunaomba sana watusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ninachotaka kuongea hapa, sisi tumepitisha hapa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Sasa inaonekana kama Mpango tunaoupitisha hauendani na mipango ya Wizara nyingine. Nilimsikiliza Katibu Mkuu Kiongozi wakati anaapa, alisema kazi yake ni ku-*coordinate* hizi Wizara. Tunaomba kupitia Bunge hili aka-*coordinate* mambo ili Mpango wetu wa Miaka Mitano uende sambamba na mipango ya hizi Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunataka sekta ya utalii ichangie watalii wafike milioni tano ifikapo 2025, na *share* kubwa tunategemea kupata kwenye utalii wa *Southern Zone.* Leo tumeiwekea barabara inayokwenda *National Park* kujenga kwa usawa wa kilometa 1.5, barabara ya kilometa 104, hivi tunapomaliza huu Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2020 - 2025 ni kweli tutakuwa tumefikisha sisi kuchangia pato hilo la Taifa, kufika dola bilioni 6.0? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine tunajiuliza hii mipango tumeweka Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano halafu bado tunaongelea kuunganisha madaraja tu hatuongelei barabara zile zinazokwenda kwenye *strategic areas*. Tunaongelea kilometa mbili, kilometa tano kwenda kwenye miradi ile ya kimikakati ya kutuongezea pato la Taifa. Je, tupo *serious*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana ndugu zangu tuwaangalie Watanzania kwa jicho la huruma, tuwaangalie hawa vijana wetu wa bajaji, wa bodaboda waliopo mijini kwa jicho la huruma. Askari wanafanya kazi kubwa yaani mpaka wanashindwa sasa. Leo *TARURA* inapewa fedha ya *maintenance* tu, asilimia 80 mpaka 90, lakini kwa maana ya miradi ya maendeleo wanapewa asilimia 10 mpaka 20. Miji yetu inakua, Waheshimiwa Wabunge tunaposema *maintenance* maana yake unapewa fedha za kutunza barabara tu zilizokuwepo, hawapewi pesa ya kuongeza mtandao wa barabara. Miji yetu sisi inakua, Iringa *TARURA* haijapewa fedha ya miradi ya maendeleo na mji unakua wale watu kule wanafuatwa vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi bajaji sijui bodaboda zinafikaje kule kwenye makazi ya watu? Kama watu wanapewa fedha ya kutunza barabara ambazo hazipo, mtoto huyu akabidhiwe wenyewe, wakabidhiwe hawa Ujenzi na Uchukuzi wamchukue *TARURA* wakae nae ili yanapotokea matatizo tusilaumu kwamba huyu yupo TAMISEMI, tujue ni wenyewe Uchukuzi asilimia mia wamefeli hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba *TARURA* wapewe, nashukuru wamenipatia milioni 120 kwenye barabara yangu inayopita Kleruu, nayo inatakiwa itengenezwe kwa kiwango cha kokoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kiwango cha kokoto si kiwango. Sasa nashukuru kwa ajili ya hilo lakini niwaombe sana tujaribu ku-*coordinate* mpango wetu na mambo yetu tuliyoyapanga lakini tujaribu kuangalia hizi by pass kwenye majiji zifunguliwe ili huduma zingine za kiuchumi ziendelee. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Butondo atafuatiwa na Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti na Mheshimiwa Assa Makanika ajiandae.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi iliniweze kuchangia katika Wizara hii muhimu inayoshughulikia masuala ya miundombinu na hasa barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba niwapongeze Mawaziri; kwa maana ya Waziri pamoja na Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote katika Wizara hii. Kazi wanayoifanya ni kubwa lakini kusema kweli changamoto bado ni nyingi. Tunahitaji kuongeza nguvu zaidi kuhakikisha kwamba barabara zinapitika kwa sababu msingi wa uchumi wetu unahitaji sana kuimairisha miundombinu na hasa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kama Tanzania hii tumeamua kusimama na kuamua Tanzania yetu iwe ni Tanzania ya viwanda. Viwanda hivi bila kuwa na barabara nzuri, uhakika wa viwanda vyetu kuzalisha na kuwa na ufanisi bado utaendelea kuwa ni hadithi. Pia tunafahamu kwamba bila barabara nchi yetu inategemea kilimo na kilimo ndiyo uti wa mgongo, wakulima wetu wataendelea kupata shida ya kusafirisha mazao na hivyo na wao wataendelea kutokupata tija katika shughuli yao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla shughuli zote za kijamii, ziwe huduma za afya na maeneo mengine kama hatujajipanga vizuri katika eneo hili la miundombinu bado Tanzania tutaendelea kusuakusua kwenda mbele katika shughuli za kimaendeleo. Kwa hiyo eneo hili ni eneo muhimu sana, hivyo Serikali nchi nzima bila kujali eneo fulani ama maeneo ya mijini, iwe vijijini ni lazima igawanye sawa hii keki kama Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambavyo wamechangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nizungumzie katika bajeti ya hii ambayo tunaijadili, kusema ukweli katika eneo langu na hasa Kishapu unaweza ukaona ni kana kwamba hakuna barabara yoyote mpya ambayo imeweza kuwekewa fedha hapa. Kuna barabara ambayo hapa imeainishwa ni Barabara ya Kolandoto yenye urefu wa kilometa 62.4. Barabara hii ya kutoka Kolandoto ambayo inakwenda mpaka Mwanuzi hizi kilometa 62 sote ni mashahidi ni kilometa nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukaona labda ni fedha ambazo zimewekwa kwa ajili ya kushika kifungu ni bilioni mbili, bilioni mbili hizi zinakwenda kutengeneza kilometa ngapi? Ni mambo ambayo unaweza ukashangaa. Barabara hii ni barabara ambayo imekuwepo hata katika Ilani ya mwaka 2015 - 2020, lakini barabara hii haikuweza kutengewa fedha, lakini katika kipindi hiki imetengewa peke yake, jumla ya shilingi bilioni mbili peke yake. Fedha hizi ni kwa ajili ya kufanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine wananchi wetu wanaweza kufika mahali wakasema hii ni habari ya utani. Walikuwa wanataka majibu sawasawa katika hatua ile ya majumuisho ya mwisho ya Mheshimiwa Waziri kwamba nini mpango wa Serikali kwa sababu fedha hizi ni fedha za ndani lakini kama pengine kuna mikakati ya kupata fedha za nje nataka nipate majibu sawasawa na vinginevyo naweza nikaona kwamba wananchi wetu wanaendelea kuvunjika imani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, aliyekuwa Rais wetu Marehemu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alisema kwamba barabara hii ni lazima tuitekeleze na akawakumbusha wananchi tuliweka kwenye mpango katika kipindi kilichopita hatukutekeleza tunawahakikishieni tunakwenda kuitekeleza. Kwa hiyo hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, lakini kwa sababu imo kwenye Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ni lazima tujipange tuhakikishe kwamba barabara hii tunaitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukaona katika barabara nyingine ya Mwigumbi kwenda Maswa, hii ni barabara ya lami ambayo ipo tayari. Kitu ambacho kinasikitisha pengine labda nipate majibu katika, ukiangalia kwenye bajeti hii barabara hii imetengewa bilioni 50.3, sasa bilioni 50.3 hizi sijajua ni kwa ajili ya nini kwa sababu barabara hii ilishakamilika na kuna maeneo ambayo yalikuwa mabovu yalishafanyiwa matengenezo. Kwa nini fedha hizi zisingepelekwa kwenye barabara hii ya kutoka Kolandoto kwenda Mwanuzi kuja Kishapu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya ni mambo ambayo pengine nataka nijue hizi bilioni 50 ni kwa ajili ya kufanya nini? Kwa sababu tunaendelea kutoa pesa nyingi tunazipeleka kwenye barabara ambayo tayari ilishatengenezwa. Wakati mwingine inaweza ikaleta tafsiri ni mianya rahisi ya kuweza kutumia fedha bila kuwa na maswali mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilitaka nataka nizungumze hili, nipate majibu mazuri kwamba hii bilioni 50 kwa barabara hii ya Mwigumbi kwenda Maswa ni kwa ajili ya nini wakati barabara hii imekamilika. Juzi ilipata matatizo ikafanyiwa *maintenance,* lakini bado imewekewa fedha nyingi huku barabara ya Kolandoto kwenda Kishapu imewekewa bilioni mbili, nataka tafsiri na maelezo kuhusiana na hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka nizungumzie ni suala zima la uwanja wa ndege wa Shinyanga. Mkoa wa Shinyanga tuna shughuli za madini pale Mwadui, lakini tuna wachimbaji wadogo katika Mji wetu wa Maganzo pamoja na eneo lingine, eneo lote linalozunguka maeneo ya Maganzo na wananchi wanazo fedha, lakini Shinyanga tunalima pamba, habari ya fedha kwetu siyo tatizo. Kwa hiyo, habari ya usafiri wa ndege wala hata sisi kwetu siyo habari mpya kwa sababu ni watu ambao tunazo fedha bwana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwanja wa Ndege wa Shinyanga imekuwa ni hadithi, hadithi. Kila mwaka kipindi kilichopita ilikuwemo kwenye Ilani, ilikuwemo sijui kwenye bajeti mbalimbali, uwanja wa Shinyanga unaenda kukarabatiwa, kila mwaka ni habari ya hadithi hizi. Jamani katika Wizara hii kuna matatizo gani? Uwanja huu mimi niwaambieni hata kipindi kile ambacho kiwanja hiki kilikuwa kinafanya kazi, kati ya viwanja ambavyo vilikuwa na abiria wengi sana kipindi cha nyuma, kimojawapo ni Kiwanja cha Shinyanga. Sasa sijajua kama wanapiga hesabu ama tunaendelea kujenga viwanja vingine tu bila kuangalia uhalisia na historia ya viwanja vipi ambavyo vinakuwa na wateja wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nipate majibu mazuri kwamba kiwanja hiki kinakwenda kutengenezwa kweli? Unaweza ukaangalia fedha zilizowekwa peke yake ni bilioni 3.6, naziona ni fedha kidogo na kiwanja kile tumekiacha kwa muda mrefu, kilikuwa na uharibu mdogo,

lakini viwanja vya aina hii vimeendelea kuharibika, kwa rafiki yangu kule Mhata kule...

**MHE. ESTHER N. MATIKO**: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Butondo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO**: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa mzungumzaji kwamba ni kweli kabisa nakubaliana naye kwamba Serikali haiangalii viwanja ambavyo vina; mosi, vinakuwa vina historia lakini pia vinaweza kuchangia pato kubwa kwenye uchumi wa Taifa, mfano uwanja wa ndege wa Musoma ambapo anatoka Baba wa Taifa, tuna madini kule, tuna ziwa, tuna Mbuga za Wanyama na vitega uchumi kibao lakini mpaka sasa hivi unasua sua tu, nilikuwa naomba nikupe hiyo taarifa Mheshimiwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Butondo unapokea taarifa hiyo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kwa sababu hoja ya Mheshimiwa Matiko ni ya maslahi mapana kabisa ya Taifa letu nimeipokea taarifa yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka nizungumzie kwa Mheshimiwa Mhata, Kiwanja kile cha Masasi ni aibu, ni moja kati ya maeneo ambayo nilitaka nizungumze kwa uwazi. Kiwanja kile kilifikia hatua mbaya, hata kile kipindi tunakwenda kumhifadhi cha mzee wetu, ilifanyika kazi ya kuchoma nyasi zile, ndiyo ile helikopta ikatua pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavisahau viwanja vikongwe na viwanja ambavyo tumekuwa tukisema mwaka kila baada ya mwaka kwamba vitakwenda kukarabatiwa. Hii ndiyo habari ambayo wanazungumza wenzangu, Mheshimiwa Mwenisongole amezungumza kwamba keki hii

ni lazima tuigawanye katika usawa. Kwa hiyo nataka niiombe sana Wizara, tusije tukajenga tafsiri ya kwamba kwa kweli kuna baadhi ya maeneo watu wengine wanapendelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika hotuba hii maeneo mengine tusingependa kuyafungua na kuzungumza, baadhi ya maeneo yamepewa fedha tena fedha nyingi, lakini baadhi ya maeneo mengine hatuna fedha, pengine inaweza ikaleta tafsiri nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka hili nilizungumze naikumbusha Wizara kwamba iwe makini kuhakikisha kwamba maeneo yote hasa ya msingi yanatazamwa na fedha zinapelekwa kwa ajili ya kusaidia wananchi katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka nilizungumzie, ni kuhusiana na daraja. Lipo daraja moja ambalo limejengwa katika Jimbo langu la Kishapu. Daraja la Buzinza, Kishapu - Buzinza na daraja lile linaunganisha pia Wilaya ya Igunga. Daraja hili limejengwa kwa thamani ya shilingi bilioni 2.3, lakini tangu daraja hili litengenezwe leo ni zaidi ya miaka mitatu daraja hili limekamilika, lipo katika Mto Manonga, lakini baada ya kukamilika daraja hili halifanyi kazi kwa sababu nyakati za masika kushoto na kulia yaani unapokuwa unavuka na unapokuwa unavuka upande mwingine mto ule unatakiwa ujengelee sasa barabara. Kivuko cha kutoka huku na kivuko cha kutoka huku, kwa sababu ule ni mto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni sawa na kwamba Serikali imekwenda kutupia zile fedha halafu barabara hiyo haina maana yoyote. Niombe sana Wilaya ya Igunga na Wilaya ya Kishapu iunganishwe kupitia daraja hili vinginevyo ni sawa na kwamba tumezimwaga zile fedha na hakuna maana yoyote ya kupeleka hizo fedha. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imegonga.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa ya kwanza.

**NAIBU SPIKA:** Imeshagonga ya pili, ahsante sana.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Alexender Pastor Mnyeti, atafuatiwa na Mheshimiwa Assa Makanika.

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Nitazungumzia mambo matatu. Jambo la Kwanza, mwaka 2010 wananchi waliokuwa wanaishi karibu na ile Barabara ya kutoka Geita kwenda Usagara walilipwa fidia zao, lakini wananchi kama tisa hivi wakasalia wakidai jumla ya shilingi milioni 30. Tangu mwaka 2010 mpaka leo wananchi hao wanadai milioni 30, wanaidai Serikali, haya ni mambo ya aibu, milioni 30 kudaiwa na wananchi maskini, waliowanyang'anya maeneo yao wakapitisha barabara. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri hilo alichukue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kule Misungwi tuna hili Daraja la Kigongo kwenda Sengerema, daraja hili wale wakandarasi walipewa *tender* hiyo na sasa wanaendelea vizuri na ujenzi, lakini cha kusikitisha wamevamia milima ya wananchi wanaponda kokoto wanachukua bila utaratibu bila malipo ya aina yoyote. Mheshimiwa Rais alivyopita pale jambo hili liliibuliwa na wananchi na Mheshimiwa Rais akaagiza twende tukalishughulike. Tumekwenda kushughulika na jambo hilo tukaonyeshwa dharau ya juu, akaja Mheshimiwa Waziri tukamweleza jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kumjulisha kwamba tangu ameondoka hakuna kilichofanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Waziri, yeye ndiye Waziri wa Ujenzi, anakuja pale anatoa maelekezo kwa wakandarasi aliowapa *tender* mwenyewe lakini bado watu hao hawafuati alichowaagiza. Hii nayo ni aibu kubwa. Nitoe ushauri kwa Mheshimiwa Waziri, tupunguze sana kutoa *tender* hizi za ujenzi kwa wakandarasi wa Kichina wana dharau sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunashindwa kutengeneza wakandarasi wetu wenye nguvu ndani ya nchi yetu, tunashindwa nini kuwawezesha watu wetu wa ndani ili waweze kujenga barabara zetu na miradi mingine. Pale kwenye ule Mradi wa Kigongo – Busisi wale Wachina wanatengeneza, lakini hakuna mkandarasi mwenza wa Tanzania anayeangalia nini kinajengwa ili keshokutwa tujenge na sisi wenyewe madaraja yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumewaacha wale Wachina, wanajenga wanavyotaka wenyewe, wakijenga chini ya kiwango hakuna anayejua, wakiweka mawe badala ya *cement* hakuna anayejua, mwisho wa siku tunakabidhiwa vitu hivi vikija kuanza kuharibika hakuna anayeweza kuvikarabati mpaka tuwatafute Wachina wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama kweli tupo *serious, otherwise* nataka nitoe mfano mmoja, waulizeni Wazambia walifanywa nini na Wachina. Waliamua kukabidhi nchi yao kwa Wachina, leo tunavyozungumza kila kitu kimekamatwa na Wachina. Sasa na sisi tunarudi kulekule, madaraja yote Wachina, barabara zote Wachina, makalvati Wachina, majengo yote Wachina, kila kona Wachina, kila mtu Mchina sasa tunafanya nini? Hivi kweli hatuna, bahati nzuri Mheshimiwa Waziri alikuwa Mwalimu wa Chuo Kikuu pale, hivi hajafundishwa mainjia vijana wetu wa Kitanzania wanaoweza kujenga madaraja. Sasa kama hajafundisha maana yake tunapotezeana muda sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hilo Waziri aliangalie, lakini hapo hapo kwenye hilo daraja kuna vijana wetu wameomba kazi, wanaozunguka maeneo hayo,

wanaoishi katika maeneo hayo, mpaka kesho hakuna hata mmoja anayepewa kazi pale. Wale Wachina wana watu wao, tunaambiwa kwamba ile kampuni ya Kichina imeingia hapo miaka ya 70 au 60 kwa hiyo wana watu wao sijui wanawatoa wapi kuja kufanya kazi pale Misungwi, lakini wale watu wa Kigongo *Ferry* pale hawapati kazi, hata ndogo ndogo zile hawapewi. Mheshimiwa Waziri alikuja Misungwi nikamwambia jambo hili, lakini tangu ameondoka hakuna kilichofanyika. Sasa kama ni mambo ya porojo, basi tuendelee kupiga porojo, mwisho wa siku hakuna kinachofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, nizungumzie kuhusu Shirika la Ndege. Sisi kule Mwanza unaingia kwenye mtandao unafanya *booking,* tunaipongeza Serikali kwa kununua ndege nyingi za kutosha, lakini unaingia unafanya *booking* unaambiwa ndege imejaa. Wakala anakwambia hebu subiri nikufanyie sarakasi upate tiketi ya kwenda Dar es Salaam, anafanya sarakasi yaani wakala wa tiketi naye amekuwa bosi sasa hivi, anafanya sarakasi unapata tiketi ya bahati nasibu, ukiingia kwenye ndege hakuna watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani tunahujumiana sisi wenyewe kwa wenyewe na huu mchezo Mheshimiwa Waziri nataka nimwambie, huu mchezo upo kwenye Wizara yake. Unafanya *booking* hakuna nafasi, ukiingia kwenye ndege ukibahatisha hukuti watu kwenye ndege *bombardier* ile inasafiri na watu 15 watu 20, lakini kwenye kutafuta unaambiwa tiketi zimejaa, tafuta usafiri mwingine. Hapa tunamkomesha nani? Ni nani tunamkomesha, tunajikaanga kwa mafuta yetu wenyewe Watanzania, ndege hizi mwisho wa siku zitakuwa ni za kupigia picha, watu wanatafuta tiketi, tiketi hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hilo hilo, ukifanya *booking* kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam unaambiwa tiketi laki tano. Ukiangalia kwenye ile ndege nyingine sitaki kuitaja jina hapa unakutana na tiketi ya laki mbili, halafu ukilipa hiyo laki tano ukiingia kwenye ndege hakuna watu, kwa nini Waziri asiweke bei *reasonable* ili watu wengi wa

kawaida wapande ndege na ndege zetu zijae. Tunamhujumu nani? Tunahujumiana sisi wenyewe Watanzania, mwisho wa siku hizi ndege zitakuwa ni ya kupigia picha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANROADS* Mwanza unaweza ukazunguka nchi nzima ukitoka Dodoma hapa utaenda vizuri, utaenda vizuri ukishaona kibao kinasema, sasa unaingia Mkoa wa Mwanza unaanza kukutana na sarakasi za mabonde, viraka, mabarabara yasiyoeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, maeneo mengine wanataka lami na sisi tunataka hayo hayo mabonde yadhibitiwe *TANROADS* Mwanza kuna shida gani? Kwa nini ukifika Mwanza tu ndio unakutana na mabonde kuinama unaingia kwenye majaluba mule mule kwenye lami kuna majaluba mule mule kuna matuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri hebu iangalie vizuri Mwanza kuna shida gani Mwanza ni mkoa mkubwa huo ndio ukweli, haya mabonde mabonde ni aibu tunatiana aibu. Kama hatuwezi kutengeneza barabara basi tuseme hatuwezi kutengeneza barabara, lakini sio kila siku tunaziba viraka mara kiraka hiki kimepasuka hapa, mara kinazibwa hapa. Hizo gharama mara mia tano zikatengeneze mabarabara mapya huko Kusini kama hamuwezi, kwa sababu imeonekana kama ni *deal.* Kila mwaka mnatengeneza mabarabara hii ni *deal* ya watu kila siku mnaziba viraka, kwa sababu ya *deal* kila siku *deal.* Pale Wilayani kwangu Misungwi kuna kilometa karibia 20 kila mwaka *TANROADS* wanatengeneza barabara kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu naona huu ni usanii na tunaiba pesa za watu. Jambo la mwisho limesemwa hapa kwamba, daraja la Busisi lisiendelee kujengwa mpaka ipatikane *certificate* ya mazingira. Yaani unaaga kwa mumeo kwamba nakwenda kazini kuja kusema kitu kama hicho kwamba, daraja lisijengwe eti kwa sababu hakuna *certificate* ya mazingira! Sisi tunasema hivi mazingira ni ya kwetu, daraja ni la kwetu, ziwa ni la kwetu, kila kitu ni cha

kwetu tunahitaji daraja lijengwe na kwa wakati na likamilike na tunahitaji kwa muda mfupi. Naomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge. Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe tena kufuatia mchango huu hasa eneo la hawa Wachina, nadhani limetajwa mahususi kwa ajili ya huyo mkandarasi ambaye anajenga hilo daraja la Kigongo - Busisi. Na nadhani wizara ikaangalie hayo mazingira ya pale. Lakini nilishawahi kuzungumza humu Katiba yetu inavyotutaka na mahusiano yetu sisi kama nchi na nchi nyingine, namna tunavyoweza kuisema nchi nyingine humu ndani ni kwa namna ile ambayo tunataka kuiga kitu fulani bora kutoka kwenye nchi hiyo. *(Makofi)*

Lakini, kama kuna mapungufu yoyote kuhusu nchi yoyote hatuwezi kuyazungumza humu ndani kana kwamba Bunge sasa linataka kuijadili nchi fulani na mapungufu yake. Kwa hiyo, hata hawa ile mifano ya kwamba wamefanya hivi kule wamefanya vile kwenye nchi ile, Bunge letu halikubali kwa mujibu wa kanuni zetu sisi wenyewe tulizojiwekea. Ni kwa ajili ya kulinda kwanza diplomasia ya Taifa letu na mataifa mengine lakini pia, hii nchi mahususi ambayo imetajwa hapa ni washirika wetu wakubwa sana kwenye mambo mengi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa namna yoyote ile kama ambavyo nchi nyingine zote huwa tunakataza kujadiliwa kwa namna ambayo, inazifanya aidha ziwe duni au kwamba kuna jambo halifanywi sawa sawa na hizo nchi. Kwa muktadha huo huo mchango huu sehemu ambayo inazungumza kuhusu nchi hiyo na nchi nyingine jirani unaondoka kwenye taarifa rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Lakini pia, ukiacha hiyo sehemu mahususi ya Kigongo – Busisi ambayo Mheshimiwa Waziri nadhani umepewa hayo mazingira yake na Wizara yako mtafuatilia mchango mwingine kuhusu nchi hii unaondoka kwenye taarifa rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Assa Makanika atamalizia huyo siku ya leo.

**MHE. ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kufunga dimba la leo. kKabla ya yote nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameweza kutupa salamu za pongezi kwa ushindi tulioupata wa kishindo kwa majimbo mawili ya Mkoani Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunajadili Wizara hii ya Ujenzi ambayo ni Wizara muhimu sana katika nchi yetu ya Tanzania na Wizara hii inamgusa kila Mtanzania na inagusa maisha ya kila masikini wa nchi hii. Miundombinu ndio uti wa mgongo wa nchi hii na ni moyo hasa, kulingana na rejea ya hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Rais wa nchi hii tarehe 22 Aprili, 2021. Lakini ukiangalia bado kuna changamoto nyingi sana, na changamoto hizi zinazopatikana kutokana na Wizara hii, kwa kweli zinaonyesha kabisa kwenye hali ya uchumi wa nchi hii bado kuna shida kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi wa kwanza tarehe 8 Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje bwana *Wang'* alitembelea nchi yetu ya Tanzania. Alizungumza kauli moja sana na kauli ile Wachina wengi sana wanaipenda na waliitumia kipindi wako kwenye taratibu za kukomboa nchi yao kiuchumi. Alisema ukitaka kumkomboa mtu mnyonge wa nchi yoyote ile mpelekee muundombinu kwa sababu, mkulima yeyote akilima anataka aweze *ku-exchange* mazao yake na pesa. Anaweza kufanyaje hivyo ni lazima awe na muundombinu wa kupeleka zao lile alilolima sokoni, atawezaje kama muundombinu hauridhishi au haumfikishi sokoni? Matokeo yake muundombinu ukiwa uko hohehahe hawezi kutoka kwenye hali aliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, niiombe Wizara hii iweze kuweka mpango wake madhubuti. Ukiangalia mfumo wa kibajeti tulionao, ni tofauti kidogo na mifumo ya nchi zingine kama nchi za Marekani. Nchi za Marekani wanatumia *federal reserve* lakini sisi tunatumia *basket fund,* ambapo

masikini wa Kigoma analima shamba lake anatoa kodi ambayo kodi hiyo isiporudi kumpelekea muundombinu, inakwenda kujenga muundombinu wa mkoa mwingine. Na hii inatokea endapo tunakuwa hatujaweka mgawanyo sawa wa rasilimali hii ambayo ndio keki ya Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sasa Wizara kwa kupitia mfumo huu wa kibajeti tulionao, iweze kuangalia namna ambavyo inagawanya haka ka keki kadogo. Kwa sababu inaweza ikachukua pesa kutoka sehemu nyingine ikaenda kuwahudumia watu wengine. Huenda hata hayo *ma-fly over* tunayoyasema huenda na kodi pia ya mtu wa Kigoma amejenga yeye kila siku anapitia kwenye matope haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu wa kijijini ameenda kujenga miji yeye bado yuko kwenye hali ya chini, na hii inatokana kulingana na mgawanyo mdogo ambao hauna usawa hata kidogo haumrudii mtu wa kijijini katika kujiletea maendeleo. Nitoe mfano mdogo tu, huku Kigoma kwetu mpaka dakika ya sasa mkoa wetu mnafahamu bado haujaunganishwa na mikoa mingine kwa lami. Sehemu kubwa sana ukiangalia njia ya Kaliua hii mpaka kuja Tabora bado kuna zaidi ya kilometa 90 na kitu hazijaunganishwa kwa lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija njia hii ya Kasulu bado haijaunganishwa kwa lami. Pamoja na kwamba tunashukuru ndio mkandarasi yupo, tuombe sana Serikali iendelee kuongeza nguvu sana, ili na mkoa wetu na mikoa jirani hii iweze kuunganishwa kwa lami. Lakini, imekuwa ni jambo la kusikitisha sana juzi nimesikitika sana, Mbunge wa Kakonko anaomba kilometa 3 za lami ndani ya mji tena ndio mjini. Lakini wapo Wabunge ambao wanaomba zaidi ya kilometa 15 tena pembezoni mwa mji, hii sio sawa na Wizara isikie. Hiki tunachokifanya ni kitu ambacho tunafanya tuamshe hisia za watanzania wengine, huku tunakwenda kuwanufaisha watanzania wengine na huku wengine, wataamsha hisia za hasira na tunaweza tukafika mahala ambapo sio pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niiombe Wizara iweze kugawa sungura huyu kwa kuangalia uwiano sahihi kabisa, ili watanzania wote waweze kuona ya kwamba na *waji-feel proud* ya kwamba ni sehemu ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, itakupa mifano michache tu pale kwetu Kigoma, kuna baadhi ya wananchi mpaka sasa toka tunaupata uhuru hawajawahi kuona gari! Toka uhuru ukienda Kata ya Kagunga, ukienda Kata ya Mwamgongo, ukija na Kata ya Ziwani zaidi ya wananchi 70,000 gari haifiki. Barabara yetu ya kuanzia Mwandiga kupita mpaka Chankere kwenda mpaka Mwamgongo na kufika mpaka bandari ya Kagunga haijawahi toboka mpaka dakika ya sasa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kwenda kuwatembelea wananchi wetu hawa lazima upite nchi jirani ya Burundi. Mheshimiwa Waziri alikuja Kigoma, ameshindwa kufika kuwatembelea wananchi wetu na hiyo yote ni kwa kuwa hakuna barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Wizara iweze kuangalia iwezekanavyo iwapelekee wananchi na hawa wajione ni sehemu ya nchi hii. Waweze kuona ya kwamba na wao wanachangia kuijenga nchi ambayo na wao wanapata haki sawa. Ukiangalia bajeti nilikuwa napitia na nimepitia nikiwa safarini natokea Kigoma, wametengewa ile barabara milioni 200 barabara ambayo inahitaji zaidi ya bilioni 23. Unakwenda kutenga milioni 200 itatoboka lini? Itamalizika lini hii barabara? Na hii barabara iko kwenye Ilani ukurasa wa 74 wa Ilani ya Chama chetu Cha Mapinduzi, umeisema hii barabara kilometa 60 lakini ukiangalia pesa zinazotengwa zinasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, niiombe Wizara nitakuwa na machache sana na msingi wangu ni kwenye hii barabara. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, shida umeiona, utakapokuja *ku-wind up* hapa uje utuambie ya kwamba ni lini wananchi hawa watakuja kupata uhuru kama wananchi wa sehemu zingine? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema machache hayo naomba kuunga hoja mkono, lakini Waziri utuambie ya kwamba barabara hii ya kutokea Mwandiga mpaka kwenda bandari ya Kagunga ambapo Serikali imewekeza mabilioni ya pesa kwenye bandari ile ya Kagunga. Lakini hayana manufaa yoyote, ili yaweze kuwa na manufaa na bandari ile ifanye vizuri lazima tupate muunganiko wa barabara hii ya Kagunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho kabisa kuna barabara ya Mwandiga – Manyovu imeanza ujenzi mwaka 2008. Barabara ile imejengwa lakini kuna wahanga wa barabara ile ambao walibomolewa majumba yao walipoteza na baadhi ya maeneo yao. Hawajalipwa fidia mpaka sasa, nikuombe Waziri ikiwezekana uweze kufika uzungumze nao, imekuwa ni muda mrefu hawajalipwa fidia za nyumba zao zilizobomolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya machache hayo niweze kuunga hoja mkono, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. HUSEIN N. AMAR:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge niwashukuru kwa michango yenu iliyotolewa hapa na tumefika mwisho wa mchango wetu wa mchana na bajeti hii kama mnavyofahamu itaendelea kesho. Mheshimiwa Waziri, Wabunge wanapochangia kwa hisia hapa wanafahamu kwamba, Ilani utekelezaji wake utachukua miaka mitano sio kwamba tutatekeleza kila kitu katika mwaka huu. Lakini mwaka huu ndio unaoweka msingi mzuri wa utekelezaji wa Ilani. Kwa hiyo, michango inayotolewa ni dhahiri mingine itatakiwa majibu kesho lakini tunafahamu itakuwa ni miaka mitano. *(Makofi)*

Sasa michango hii inaashiria kwamba katika hii miaka mitano kila mahali ambapo utataka kugusa, basi isiwe kwa namna ya *ku-beep* kama simu. Kama unafanya jambo basi ufanye jambo ili lionekane jambo limefanyika, nadhani hilo litakuwa limekaa sawa. Muda wetu umeenda sana lakini

Mheshimiwa Amar anataka kusema kuna jambo limefanyika hapa ambalo haliko sawa sawa. Mheshimiwa Amar.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. HUSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninaomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 76, kuna jambo ambalo linaendelea humu ndani nilikuwa nataka nipate Mwongozo wako. Kuna baadhi ya wachangiaji ambao tayari wanaonesha kana kwamba nchi hii sasa inaenda kugawanyika vipande vipande. Kuna wachangiaji wamesema mbona sisi sasa wananchi wa Mkoa wa Songwe, Mbeya, Iringa, sijui wapi huko kusini inaonekana kama vile tumetengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Michango kama hii inaleta hisia si nzuri kwa mikoa mingine. Mfano, kuna mchangiaji mmoja amefikia kuthubutu kusema kwamba lile daraja la Kigongo – Busisi lisimame kujengwa kwa sababu, kibali cha *NEMC* hakijatoka. Na yeye huyu mchangiaji ni wa huko huko Kusini je, sisi watu wa Kanda ya Ziwa tuanze kutafakari vipi michango hiyo? Kuna nini ndani yake? Hili usipoliangalia vizuri linaweza likaleta uchangiaji ambao unaweza kuleta mtafaruku au taharuki kwa wananchi wetu naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge amesimama Mheshimiwa Amar kwa ajili ya muda sitarejea alichokisema, lakini kanuni yetu ya 76 inataka ukisimama kuomba mwongozo useme hilo jambo je, linaruhusiwa? Ama haliruhusiwi? Waheshimiwa Wabunge pamoja na mambo mengine Kiti, kazi yake kusimamia kanuni kama zimefuatwa ama hazijafuatwa. Na mara nyingi huwa najaribu kuweka mambo sawa hapa kama mtu ametoka nje ya kanuni kidogo.

Lakini michango iliyotolewa ni ya ujumla sana, kila mtu anajaribu kueleza changamoto zilizoko katika eneo lake la uwakilishi, hakuna mtu anayejaribu kuashiria kwamba labda kuna kipande kitaondoka nchi hii kihamie nchi nyingine. Kila Mbunge amejaribu kuonesha namna ambavyo kwake kuna

changamoto na angetamani zifanyiwe kazi hilo ndiyo lengo lake haswa hakuna Mbunge ambaye ameenda nje ya utaratibu. *(Makofi)*

Lakini sasa ametaja mahsusi maeneo haya mawili kwa maana ya kwamba Mheshimiwa aliyesema kwanza, hajasema daraja lisimame mimi hapa huwa nasikiliza kila neno linalosemwa. Mbunge huyu wakati anachangia Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, hajasema daraja lisimame kujengwa. Wakati wa mchango wake ametoa kama mfano kwamba daraja lile lilianza kujengwa kabla ya kibali cha mazingira kitu kama hicho. Na taarifa hizi Waheshimiwa Wabunge ninyi ndiyo mnaofanya kazi kwenye kamati mimi na Mheshimiwa Spika hatushikiri kwenye kamati. *(Makofi)*

Ni dhahiri taarifa hizi nataka kuamini, taarifa hizi lazima wamezitoa upande wa Serikali kwao, na kama hili haliko hivyo basi Mheshimiwa Waziri atapata fursa ya kulieleza kesho kama kibali kilikuwa kimetoka kabla au baada. Kama kanuni ingekuwa imevunjwa ningeshasema hapa kwamba mchango huu haujaenda sawasawa. Lakini pia Wabunge wengine ambao wameeleza mambo fulani upande wao hakuna Mbunge aliyevunja kanuni. Kila mtu anaeleza kwenye eneo lake na ndiyo maana wengi wamejizuia, nimeona wengi wamejizuia kutaja maeneo mahususi kwamba kwa mfano sehemu fulani wamependelewa sana. Lakini kimsingi siyo kupendelewa kimsingi ni kwamba kila mtu anataka kazi ifanyike kwenye jimbo lake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, lugha ya mawasilisho inaweza ikatofautiana kutoka kwa mtu mmoja na mwingine, lakini hakuna jambo lolote linalotaka kuanzishwa hapa ndani. Na ninyi mtakuwa mashahidi hata mimi nimesema leo kuhusu Mbeya Mjini, Mbeya Mjini haiendi popote ule ni mkoa upo na unahitaji huduma kama mikoa mingine tu.

Kwa hiyo, hakuna hisia zinazotaka kujengwa kwamba pengine kwingine kusijengwe, kujengwe sana huku hapana. *(Makofi)*

Mbunge wa Liwale amesimama kueleza mazingira kwake hawajawahi kuona lami. Kwa hiyo, mtu kama huyo akisimama kueleza kwamba na yeye apelekewe lami, huwezi kusema kwamba anataka kuonyesha watu wa Liwale labda wapo namna fulani. Anajaribu kuweka zile hisia za wananchi wake humu ndani maana ndiyo anaowawakilisha na wao pia wanataka hizo huduma. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama nilivyoweka mwongozo kabla sijaombwa mwongozo wa Kiti na Mheshimiwa Amar, nilieleza hapa upande wa Wizara maana Wabunge tunachangia kwa hisia. Lakini tunafahamu kwamba utekelezaji wa mambo yote tunayoyasema utachukua hii miaka mitano. Sasa tunaweka msingi ili mwaka huu aliyekosa basi mwakani, aweze kukaa vizuri na yeye watu wake wajue wana mwakilishi humu ndani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu Kamili asubuhi.

*(Saa 02.00 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 18 Mei, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*